MASOMO YA BIBLIA

KARAMA ZA ROHONI

Sehemu ya Kwanza

Na; - Mr. & Mrs. S. G. Mwakatwila

KARAMA ZA ROHONI (SEHEMU YA KWANZA)

UTANGULIZI

Tunatoa Shukurani zetu nyingi kwa Mungu, kwa upendo wake mkubwa kwetu, kwa kutupatia wokovu na baraka zake nyingi sana, pia tunatoa salamu zetu nyingi sana kwa watoto wa Mungu wote.Ambao wako pande zote za nchi, pia tunawashukuru watu wote wanao tuombea na hata kujitoa kwa hali na mali ili kutuwezesha katika kufanikisha kazi hii ya Bwana. Pia tunamshukuru sana Roho Mtakatifu ambaye yeye ndiye aliye tufundisha somo hili, na aliyetuwezesha kuliandika somo hili la Karama za rohoni sehemu ya kwanza, na ni matumaini yetu na maombi yetu Roho Mtakatifu pia atakufundisha wewe ndugu mpendwa kwa kupitia ujumbe huu.

MAMBO MUHIMU.

Kabla hujaanza kujifunza somo hili, kuna mambo ya muhimu unayotakiwa uyafanye, nayo ni kama ifuatavyo:-

1. Unatakiwa utulie au ukae sehemu ya utulivu, ambayo utasoma somo hili pasipo kubughudhiwa.
2. Umwombe Mungu kupitia Jina la Bwana Yesu Kristo amtume Roho wake Mtakatifu akufundishe vema.
3. Uwe na Biblia yako na karamu na daftari lako.
4. Pia lolote lile ulilofundishwa unatakiwa ulitendee kazi na uwafundishe na wengine.

Fungua kitabu cha (**1 Kor 12:1 – 3) "Basi, ndugu zangu kwa habari ya karama za Roho, sitaki mkose kufahamu. Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa mataifa, mlichulikuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa. Kwa hiyo nawaalifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema Yesu amelaaniwa, wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu".** Mtume Paulo kabla hajaanza kuwafundisha Wakorintho somo la Karama za Rohoni, kwanza alianza kuwafundisha hao Wakorintho somo la namna hao ndugu walivyokuwa wanaabudu, kabla ya kupata Imani katika Yesu Kristo

Fahamu Paulo alianza kwa kuwakumbusha kuwa kabla hawa ndugu hawajaokolewa kutoka katika hali yao ya umataifa au hali yao ya kipagani, walikuwa ni watu walio kuwa wanaabudu sanamu zisizonena, Paulo alilifahamu jambo hilo, na akawafundisha hao Wakorintho kuwa zamani walikuwa ni watu wasio na Mungu wa kweli, tena aliye hai, bali walikuwa wanaabudu vitu visivyo hai, tena visivyosema na kutenda, Paulo aliwaambia hao ndugu ya kuwa, mtu yeyote yule asiye na Roho wa Mungu hawezi mtu huyo kumkiri Yesu kuwa ni Bwana, pia mtu yeyote yule ambaye ana Roho wa Mungu hawezi kumlaani Bwana Yesu Kristo.

Unaweza ukajiuliza swali kwa nini Paulo alianza kufundisha somo la Karama za Rohoni kwa kusema maneno hayo? Fahamu Paulo alianza kufundisha somo hili kwa namna hiyo kwa sababu hii, ili hao ndugu wapate kulielewa somo hili la Karama za Roho, ilitakiwa kwanza hao ndugu wapate kufahamu wametokea wapi katika mambo ya kuabudu kwao, na sasa hivi wao ni kina nani baada ya kumwamini Yesu kristo, fahamu ndugu yangu bila ya kufahamu kwa upana ushirika wao hao ndugu na Mungu, na jinsi walivyo baada ya

kutoka katika Imani ya kipagani, hao watu wasingeliweza kabisa kufahamu habari za Karama za rohoni.

Pia hata wewe leo hii ili upate kufahamu kwa uzuri somo hili la Karama za Roho, unatakiwa kwanza ujijue kuwa wewe ni nani? Na unamwabudu Mungu yupi, itakuwa ni rahisi sana kwako kufahamu habari za karama za Roho.

KUTOKUWA NA UFAHAMU

Watoto wa Mungu wengi sana, wamekuwa na tatizo la kutofahamu kuwa baada ya kumwamini Yesu Kristo na kumpokea ndipo walipoanza kumwabudu Mungu aliye hai, ambaye anasema, anatembea, ana nguvu nyingi, ana uweza na mamlaka yote, mwenye kufanya maajabu na miujiza ya kushangaza kabisa, mwenye kuabudiwa na kusifiwa Mbinguni na duniani mwote, mwenye kuogofya na mwenye kusujudiwa n.k.

Watoto wengi sana wa Mungu au watu waliookoka hawafahamu kwa upana jambo hili, wengi wanakiri kwa vinywa vyao kuwa Mungu ana nguvu, maajabu, anasema n.k, lakini vitu hivi wengi huwa wanavisema mdomoni tu, lakini kwa ujumla wengi hawafahamu kabisa mambo hayo, na sababu kubwa ya kutofahamu ni hii, wengi hawasomi maandiko, na matokeo yake wamekuwa ni watoto katika maisha yao ya wokovu.

Sasa hebu leo hii upate ufahamu huu, wa kuwa mimi na wewe kabla hatujaokolewa tulikuwa tukiabudu Miungu mingine, yaani tulikuwa watu wasio na Mungu wa kweli, lakini baada ya kuokolewa na kumpokea Bwana Yesu Kristo mioyoni mwetu kuwa ni Bwana na Mwokozi wetu, siku hiyo tulifanyika makao ya Mungu aliye hai. hebu pata ufahamu hapo wa neno "Makao" neno Makao lina maana nyingi sana, makao ni Mji, au ni Nyumba ama ni mahali pa kuishi, sasa neno la Mungu linasema hivi **"Yesu akajibu, akamwambia mtu akinipenda, atalishika neno langu na Baba atampenda, nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake" (Yohana 14:23)**

Ukiyaangalia maneno hayo kwa makini, utaona ya kuwa Bwana alikuwa anatufundisha kuwa, mtu yeyote yule atakayempenda Mungu na kushika Maneno ya Mungu basi Mungu pamoja na Yesu Kristo watakuja kuishi ndani ya huyo mtu. Watafanya makao yao ndani ya huyo mtu. Sasa hebu fahamu Mungu huyo, ni Mungu aliye hai, kwa maana nyingine ni Mungu anaeishi, anayesema, anayefahamu, anayesikia, kumbuka Mungu huyo ndio mwenye nguvu za kutisha, ambaye anaweza kufanya jambo lolote hakuna linalomshida, n.k.

Neno linasema kuwa Mungu huyo ndiye atakayefanya makao yake ndani ya watu wote wampendao Yesu Kristo. Watu wampendao Bwana Yesu ni wale waliompokea na kumwamini au kwa lugha inayoeleweka wale waliookoka. Ikiwa wewe ni miongoni mwa watu hao fahamu kabisa kuwa unamwabudu Mungu aliye hai, si Mungu aliye sanamu, tena fahamu Mungu huyo hayuko mbali bali yuko karibu na wewe kweli. Lazima uelewe hivyo.

Tatizo lililoko kwa watoto wa Mungu wengi wanafikiri kuwa Mungu yuko mbali nao ndio maana wengi mpaka sasa hivi wanamashaka mioyoni mwao, wakifikiri Mungu yuko kwa watu Fulani tu, au yuko kwenye dhehebu Fulani ama faragha Fulani au kwenye Ministry Fulani, na mashaka hayo ndiyo yanayowasababisha watu hao kutangatanga hovyo na

kutafuta kwa Juhudi kutaka kumwabudu Mungu aliye hai, hebu fahamu ndugu Mungu aliye hai ambaye ndiye anayepaswa kuabudiwa yuko ndani yako tokea dakika ile uliyoamini na kumpokea Yesu Kristo kuwa ni Bwana na Mwokozi wako. hebu soma maneno haya ya Mungu yanavyoema

"Kwa ajili ya hayo kumbukeni ya kwamba zamani ninyi, mlio watu wa mataifa kwa jinsi ya mwili, mnaoitwa wasiotahiriwa na wale wanaoitwa waliotahiriwa, yaani tohara ya mwili iliyofanyika wa mkono, kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani lakini sasa, katika damu yake Kristo kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi tuliokuwa wawili kuwa mmoja akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake, ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba. Akaja akahubiri amani kwenu nyinyi mliokuwa mbali, na amani kwa wale waliokuwa karibu. Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja. Basi tangu sasa nyinyi si wageni wala wapitaji bali nyinyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la Pembeni katika yeye jengo lote linaunganishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.Katika yeye ninyi nanyi mmejengwa pamoja kuwa masikani ya Mungu katika Roho". (Efe 2:11-22)

Elewa kuwa baada ya kuokolewa tu, Mungu ameurudisha ushirikiano ule ambao wanadamu tulikuwa tumeupoteza baada ya kumwasi au kutenda dhambi, sasa hivi, ushirika kati yako na Mungu umekuwa ni mkubwa sana, upo karibu sana na Mungu kuliko vile unavyoamini, watoto wa Mungu wengi sana wamekuwa na mawazo ya kuwa wako karibu sana na shetani kuliko kuwa karibu ya Mungu. Fahamu baada ya kumwamini Bwana Yesu, Mungu alimtuma Roho wa mwanae ndani yako **" na kwa kuwa nyinyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa mwanawe mioyoni mwetu, aliye Aba, yaani Baba kama ni hivyo wewe si mtumwa tena bali umwana; na kama u mwana basi umrithi kwa Mungu".** (**Gal 4:6**) Fahamu wewe si mtumwa bali ni mwana, ambaye unaurithi kwa Mungu. Lazima uelewe wazi ya kuwa wewe si mtumwa bali ni mwana, ikiwa wewe ni mwana basi unaoushirikiano kamili na Mungu, na ikiwa unaushirikiano kamili na Bwana basi fahamu kuna vitu vingi vya Mungu atakupatia au atakushirikisha, kama vile tabia yake uwezo wake, nguvu zake, baraka zake n.k. fahamu ndugu yangu kuwa Mungu yumo ndani yako na ni Mungu anayesema, si sanamu isiyo na uhai, bali ni Mungu wa kweli aliye hai.

Mungu huyu ndiye anayepaswa kuabudiwa na kuogopewa na hata kusujudiwa, elewa Mungu huyo ndiye aliye ndani yako, na Mungu huyo ndiye anayekuwezesha wewe kumkiri Yesu kuwa ni Bwana, ndugu yangu kipimo cha kukuthibitisha kuwa unaye Mungu wa kweli ndani yako ni hiki, cha kumtukuza Bwana Yesu na kumkiri Bwana Yesu Kristo. kitendo cha kumtambua Yesu kuwa ni Bwana wako na ukaanza kumtukuza au kumbariki huwa mwanadamu anawezeshwa na Mungu tu. hebu ona mifano hii katika Biblia **"Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria – filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, watu hunena mwana wa Adamu kuwa ni nani? Wakasema wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii,**

akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema, wewe ndiwe Kristo, mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akawaambia Heri wewe Simoni Bar-yona ; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni (MATHAYO 16:13-17) ukiyasoma maneno hayo utagundua hapo ya kuwa kitendo cha Petro kumkiri Yesu kuwa ni mwana wa Mungu hakikutokana na ufahamu wa Petro, bali ni kwa uwezo wa Mungu. Mungu ndiye aliyemfunulia Petro jambo hilo, na ndiye aliyemwezesha Petro kusema maneno hayo.

Ndugu yangu ikiwa wewe ndani ya moyo unamwamini, Yesu kuwa ni mwana wa Mungu pia unamkiri kwa kinywa chako, fahamu si kwa uwezo wako bali ni kwa nguvu za Mungu zilizo ndani yako, ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu tu.kwa hiyo ndugu fahamu ya kuwa Mungu yumo ndani yako usiwe na hofu kabisa, pia ukiangalia neno la Mungu kutoka **(Yohana 16:13-14) " lakini yeye atakpokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hata nena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa yaliyo yangu na kuwapasha habari".**

Ndugu yangu ikiwa rohoni mwako wewe una mtukuza Yesu, basi fahamu kuwa si kwa uwezo wako, bali Roho wa Mungu ndiye akupaye uwezo huo wa kumtukuza Bwana Yesu, hebu ona jinsi watu wengi wanavyoshindwa kusema Bwana Yesu asifiwe!! Wengi wanatamani kusema neno hilo, lakini hawawezi kulisema wazi kwa sababu Mungu hayumo ndani yao, lazima ufahamu ndugu yangu kuwa, Mungu ndiye aliyetuumba watu wote, kwa hiyo hapa duniani watu wote ni wake Mungu, pia neno linasema kuwa wapo pia wana wa Mungu kati ya watu wa Mungu, na wana hao wa Mungu ndio hao waliaminilo Jina la mwana wa Mungu yaani Yesu Kristo, pia hao wana wamempokea huyo Yesu Kristo mioyoni mwao kwa hiyo lazima ufahamu kuwa si watu wa Mungu wanaoweza kumtukuza Yesu Kristo kwa moyo wa Ukweli na vinywani mwao, bali wana peke yao, kwani Roho Mtakatifu yumo ndani yao. Na Roho huyo ndiye pekee amtukuzaye Yesu Kristo

Kwa hiyo ndugu yangu pata leo ufahamu huu kuwa Mungu Mkuu yumo ndani yako, na huabudu sanamu, bali una mwabudu Mungu aliye hai mwenye uweza.

BAADAYA KUOKOLEWA.

Baada ya kuokolewa tumekuwa masikani ya Mungu, au makao yake Mungu, pia tumekuwa nyumba yake Mungu au Hekalu la Mungu. Tu - nyumba ya Mungu. Hatuabudu kitu kingine bali tunamwabudu Mungu aliye hai. Neno linasema hivi **" Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mlipewa na Mungu (1Kor 6:19)** wewe ni hekalu la Mungu na unamwabudu Mungu aliye hai, angalia maneno haya katika kitabu cha **(Habakuki 2:18-20)** "**Sanamu ya kuchora yafaa nini, hata yeye aliyeifanya ameichora? Sanamu ya kuyeyuka, nayo ni mwalimu wa uongo, yafaa nini, hata yeye aliye ifanya aiwekee tumaini lake, na kufanya sanamu zisizoweza kusema? Ole wake yeye awaambiaye mti. Amka; aliambiaye Jiwe lisiloweza kusema, ondoka! Je! Kitu hicho kitafundisha? Tazama, kimefunikwa kwa dhahabu na fedha, wala hamna pumzi ndani yake kabisa. Lakini Bwana yumo ndani ya hekalu lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele zake".**

Zamani kabla haujaokoka ulikuwa unaongozwa na sanamu, neno sanamu kibliblia ni mawazo yako, soma, **(Kol 3:5) "basi vifisheni viongo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya na kutamani, ndiyo Ibada ya sanamu".** Zamani ulikuwa ni mtu mwenye tabia hiyo lakini baada ya Mungu kuingia ndani yako tabia hiyo mbaya iliondoka. Mungu yumo katika hekalu lake ambalo ni wewe ndio maana leo hii unakataa tamaa mbaya au mawazo mabaya, yakikujia unayakataa basi fahamu Mungu yumo ndani yako, na hauabudu sanamu tena, bali Mungu aliye hai, ambaye anaishi ndani yako

TATIZO LILILOPO KWA WANA WA MUNGU

Siku moja nilikuwa katika maombi, na nilikuwa na maombi ya kuliombea Kanisa yaani, watu waliookoka, na baada ya maombi yale, Bwana akanionyesha Ono ambalo lilinisikitisha sana, na nikamuomba Mungu anifafanulie maana ya ono hilo.

Niliona hivi **"nilichukuliwa na kuonyeshwa Jumba moja kubwa sana, ambalo lilikuwa ni Kanisa, na nikachukuliwa na kuingizwa mle ndani ya hilo Kanisa, nikaona katikati ya Kanisa hilo kuna mtu amekaa, nikaenda mpaka pale alipoketi mtu huyo, na nilipomkaribia, nikaona ni Yesu Kristo, lakini nilipofika karibu yake, nikagundua kumbe ilikuwa ni sanamu ya Yesu, hakuwa Yesu halisi, baada ya kuona hivyo nikaondolewa mle ndani, na ndipo nilipofika nje nikaona juu, mtu, mwenye mamlaka, na aliye hai, mkononi mwake akiwa ameshika kichana cha zabibu zilizoiva na nzuri na nilipomkaribia, alikuwa ni Yesu akiwa hai, na anasema, tofauti na yule niliyemkuta mle ndani ya jumba lile, yule wa ndani mle alikuwa sanamu, hasemi wala hana uhai, hatembei ila ana sura ya Bwana Yesu, huyu wa pili aliye juu nilimkuta akiwa hai, ana mamlaka na nguvu anasema na anatembea na mkononi ameshika zabibu nzuri sana**" Ono liliishia hapo, nilipoona hivyo nilianza kumwomba Mungu anifundishe maana ya maono hayo, na siku moja Bwana alinifundisha somo hili la ajabu sana.

Bwana Mungu kwa kupitia Roho wake Mtakatifu alianza kunifundisha kuwa, lile Jumba nililoliona ni Kanisa lake yaani watu wale waliookoka, waliopo duniani na wana hao wamempokea Yesu Kristo mioyoni mwao, na yumo kweli ndani yao, lakini Yesu aliye ndani yao ni kama sanamu, hasemi, hatendi, yumo ndani kakaa tu kama sanamu, na Bwana akanifundisha kuwa yeye Yesu si sanamu bali yu hai, anasema anatenda kazi ana nguvu, na mamlaka n.k. lakini watoto wake baada ya kumpokea Yesu Kristo mioyoni mwao, pasipo wao kufahamu kuwa Yesu yu hai anatenda kazi anasema, ana nguvu ni Yesu yule yule aliyefanya miujiza, aliyekuwa na Hekima na ufahamu na maarifa ya ajabu, aliyepambambanua roho mbalimbali aliye ponya wagonjwa kwa ajabu, kabisa aliyetenda miujiza, na ishara za ajabu kabisa, aliyekesha na kuomba kwa ajabu sana n.k. ndiye aliyeingia ndani ya mioyo yao kwa watu wote wamwaminio yaani Kanisa lake.

Ndipo Bwana alipoanza kunifundisha somo hili la Karama za Rohoni ndugu yangu zamani kabla hujaokoka ulikuwa ndio unaabudu sanamu, na yamkini ni sanamu ya Yesu lakini baada ya kuokoka au baada ya kumpokea Yesu Yesu aliingia ndani yako, Yesu aliye ndani yako si sanamu bali ni Yesu halisi anatakiwa atende kazi, aseme azidhihilishe nguvu zake katika maisha yako wewe na hata watu wengine wapate kuziona kazi zake hizo, hebu yakumbuke maneno yake Yesu mwenyewe aliyoyasema kabla hajaenda Mbinguni

juu. **(YOHANA 14:11-24) " mnisadiki, ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa kazi zenyewe. Amin Amin nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya mwana. Mkiniomba neno lolote kwa jina langu, nitalifanya. Mkinipenda mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba naye atawapa msaidizi mwingine ili akae nanyi hata milele ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea kwa kuwa haumwoni wala haumtambui, bali ninyi mnamtambua, maana anakaa ndani kwenu, naye atakuwa ndani yenu, sitawacha ninyi yatima; naja kwenu bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona. Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai. Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu. Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu nami nitampenda na kujidhihirisha kwake. Yuda (siye Iskariote), akamwambia Bwana, imekuwaje ya kwamba watakakujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu? Yesu akajibu, akamwambia mtu akinipenda, atalishka neno langu na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake mtu asiyenipenda yeye hayashiki maneno yangu nalo Neno mnalolisikia silo langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka"**

Maneno hayo ya kuhusia ndio aliyoyasema Bwana Yesu Kristo siku chache kabla, hajafa na siku ya tatu akafufuka na kupaa Mbinguni, Yesu alisema mambo mazito sana siku ile ya kitufundisha sisi wanafunzi wake, jambo la kwanza ni kwamba alitutaka watoto wake tusadiki au tuamini kabisa kuwa Yesu na Baba ni Umoja, yaani Yesu yuko ndani ya Baba na Baba yuko ndani ya Yesu huwezi kuwa tofautisha na wala huwezi kuwatenganisha kamwe, pia Bwana Yesu anasema kuwa, ikiwa husadiki kuwa Yesu na Mungu ni kitu kimoja, au Yesu ni Mungu, basi sadiki kazi alizozifanya, kwani kazi alizozifanya Yesu awezaye kufanya hizo ni Mungu aliye hai peke yake, awezaye kufufua wafu, pia ndiye aliyefufuka kutoka kwa wafu, ndiye aliye yaumba macho ya vipofu, alikuwa na uweza hata juu ya vitu navyo vilimtii, kama maji n.k, awezaye kuzifanya kazi hizo ni Mungu tu, na Yesu alitenda hizo kazi ili watu wapate kusadiki kuwa Mungu yu ndani ya Yesu. Sasa Yesu anasema jambo lingine kubwa na la kutisha sana kuwa, kwa kuwa yeye anakwenda Mbinguni na ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba, basi kazi zile alizokuwa anazitenda yeye, sasa, watakao kuwa wanazitenda ni watu wote watakao mwamini yeye Yesu. Tena anasema kazi watakazozitenda hao wamwaminio zitakuwa kubwa kuliko zile Bwana Yesu alizozitenda alipokuwapo hapa Duniani! Umesikia maneno hayo mpendwa?

Umewahi jiuliza swali ni kwanini Bwana alisema maneno hayo? Jibu liko wazi ni kwa sababu baada ya yeye kwenda mbinguni aliahidi kurudi tena, alisema wazi kuwa atakuja tena hapa ulimwenguni, na atakuja na Baba Mungu ambaye ni wa moja na Yesu na wataingia na kuishi ndani ya waaminio, yaani watu wale wote wanaomsadiki Yesu Kristo. fahamu Yesu Kristo, alirudi tena duniani kwa kupitia Roho Mtakatifu. hebu angalia **(Gal 4:6) "Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa mwanawe mioyoni mwetu aliye Aba yaani Baba"** fahamu Roho Mtakatifu ndiye Roho wa mwana wa Mungu, yaani Yesu Kristo. Yesu alisema maneno yale kuwa mtu yeyote amwaminiye Yesu Kristo atakuwa akizitenda kazi zile alizokuwa akizitenda, na tena atazitenda kubwa kuliko zile alizokuwa akizitenda wakati ule alipokuwepo katika hali ya mwili huu wakibinadamu.alikuwa anajua kuwa ataludi na kukaa ndani ya watu wote

watakaomwamini, Fahamu Yesu yule aliyekwenda Mbinguni na mwili wa nyama na damu, ndiye yule yule aliye rudi kwa mwili wa Roho Mtakatifu, na aliingia ndani yako. Siku ile uliomwamini na kumpokea, tatizo tulilonalo watoto wake ni hili, wengi wana Yesu, lakini hayuko hai, ni sanamu, kwa nini? Ni kwa sababu ya kutofahamu habari za karama za roho ambazo kila mwamini amepewa ili Yesu afanye kazi zake kwa kupitia wewe ambaye ni mtoto wake au mwana wake!, au niseme kwa jamii yote ya watu waliookoka ambao wamempokea Yesu mioyoni mwao

KARAMA ZA ROHONI

(1 KOR 12:1) "Basi ndugu zangu kwa habari ya karama za roho sitaki mkose kufahamu" basi ndugu zangu kwa kuwa tayari umekwisha kupata ufahamu, kuwa wewe ndio Kanisa la Mungu, na Roho Mtakatifu anakaa ndani yako, basi Mungu anataka watoto wake hao wote lazima wapate kufahamu habari za karama za roho ambazo Mungu amemgawia kila aaminiye, ili Mungu apate kutenda kazi zake kupitia wewe, au kwa lugha nyingine kwa kupitia watoto wake.

Ndugu yangu baada ya wewe na mimi kuokoka, Mungu Roho Mtakatifu aliingia ndani yetu na siku ile alipoingia ndani yako alikuja na karama mbalimbali, ambazo alikuletea, ili upate kuzitenda kazi za Mungu unaweza ukajiuliza swali hili, hivi karama maana yake nini?

Neno karama maana yake ni **"KIPAWA**" na neno kipawa maana yake ni: **"Zawadi"** Mungu Yesu Kristo anapenda mimi na wewe tuliookoka lazima tupate kufahamu zawadi zetu mbalimbali tulizopewa rohoni mwetu, na zawadi hizo ni zile zilizo katika mambo ya rohoni, au mambo ya Kiungu, Mpango wa Mungu kwa watoto wake ni kwamba anataka tufanikiwe katika mambo yote, **" Mzee kwa Gayo mpenzi nimpendaye katika kweli. Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yako yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo" (3YOHANA 1:1-2)** Mungu anataka watoto wake tufanikiwe katika afya zetu yaani kiuchumi, kielemu n.k, pia anataka tufanikiwe katika mambo ya Kiroho, sasa ndio maana neno la Bwana linasema kwa habari za karama au zawadi za rohoni ni lazima tuzifahamu, na tukizifahamu, itakuwa ni rahisi kwetu sisi kuya fanya mambo yafuatayo:-

1. Kuzihitaji
2. Kuzitendea kazi (au kumruhusu Roho Mtakatifu atende kazi) ndani yetu.

Unajua ni kwanini Mungu alinionyesha sanamu ya Yesu ndani ya Kanisa? Ni kwa sababu watoto wake hawajafahamu bado zawadi zao ambazo Mungu kawapa, Nini maana ya zabibu nzuri zilizokuwa mkononi mwa Yesu? Fahamu zabibu zile maana yake ni zawadi, au karama, ambazo Mungu yuko tayari kumpa mtoto wake yeyote yule atakaye zitaka!, kwa sababu ya kutozifahamu, watoto wake Yesu wengi hawamwombi hizo karama ili awape. Na kosa hilo ndilo linapelekea Yesu kutofanya kazi kubwa amabazo anataka leo azifanye kwa kupitia wewe unayemwamini!

Ndugu yangu mpendwa Mungu alipomtuma Roho wa Yesu ndani yako alikuja na karama nyingi sana za rohoni, hebu sikiliza maneno haya ya Bwana yasemavyo **" atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo" (Efe 1:3).** Mungu ametubariki sana rohoni mwetu, kuna baraka nyingi sana tulizopewa na Bwana katika ulimwengu wa roho

na baraka hizo Mungu anataka watoto wake tusikose kuzifahamu. Na tukizifahamu, hatuta kuwa na Yesu aliye sanamu ndani mwetu, bali tutakuwa na Yesu aliye hai, na Mungu atazitenda hizo kazi kupitia hizo karama alizoziweka ndani yako na Mungu atatembea katikati yako ka udhihilisho wa waziwazi, na Mungu atatukuzwa na watu wote ambao wataziona kazi za Mungu azitndazo kupitia karama za rohoni alizo ziweka ndani yako!.

Karama au zawadi hizo tumepewa bure, hatulipii kitu chochote ila ni zawadi tunayopewa na Bwana Mungu. Watu wengi wanafikiri ili wawe na karama Fulani, basi lazima wawe watu wa umri Fulani, au wa Elimu Fulani n.k, fahamu karama ni zawadi ambazo tumepewa bure, yaani kitu ambacho hatujakifanyia kazi, ni kwa "Neema" tu, tumepewa. karama ni udhihirisho wa ki-Mungu kwa Kanisa lake na kwa watu mbalimbali, natumaini mpaka hapa umeelewa kuhusu mpango wa Mungu wa kujidhihirisha akiwa ndani ya watu wote wamwaminio na kuzitenda kazi zake kwa kuwatumia hao watoto wake yaani Kanisa.

TOFAUTI YA KARAMA NA HUDUMA

Kabla hatujaendelea mbele katika somo hili, hebu tangalie kwanza kuhusu huduma na Karama, watoto wa Mungu wengi sana huwa wanachanganya haya mambo mawili, wengi unapozungumzia habari za karama za rohoni huwa wanachanganya na huduma za kiutendaji katika Kanisa la Mungu.

Fahamu kuna tofauti ya huduma au (ofisi) na karama za roho, Neno la Mungu linatufundisha kuwa katika kulijenga Kanisa la Mungu, Mungu alizitengeneza Idara tano za kiutumishi, Idara hizi ndizo ziitwazo huduma, hebu sikiliza maneno haya ya Bwana yanavyo tufundisha **" naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwa kamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" (Efe 4:11- 12)** Bwana amezitengeneza huduma au ofisi hizo tano ili Kanisa lake lijengwe, Watumishi wa Mungu wapo wa aina hizo tano, ambao ni wachungaji, waalimu wainjilisti, manabii na mitume, sasa utaona kuna tofauti kati ya Karama, na huduma hebu soma, **(1Kor 12:4-5) : basi pana tofauti za karama, bali roho ni yeye yule tena pana tofauti za huduma, Bwana ni yeye yule"** ili ulielewe kwa uzuri somo hili ndugu yangu lazima utofautishe kati ya neno Huduma (Ofisi) na Karama.

KARAMA NI VITENDEA KAZI.

Karama ni vitendea kazi ambavyo vitamsaidia Mtumishi wa Mungu aliye Mchungaji, Mwalimu, Nabii, Mitume, na wainjilisti ili waifanye kazi ya Mungu kwa uzuri wakiwa pamoja na Mungu, labda niseme hivi **" Karama ni sawa na jembe ambalo ni kifaa cha kumsaidia mkulima ili alilime vema shamba lake."**

Mungu amewaweka watumishi wake shambani mwake ambao ni hao waalimu, wachungaji, wainjilisti, manabii, na mitume, sasa ili hao watumishi wapate kuifanya kazi ya Mungu vizuri, Mungu akawaletea hao watumishi wake vifaa (karama) mbalimbali vya kuwawezesha kuifanya hiyo kazi ya Mungu kwa uzuri sana, pia karama hizo Mungu huwa anazitumia kulidhibitisha neno la Mungu, pia kuwadhihirisha watumishi wake hao mbele za watu kuwa kweli Mungu amewatuma. Neno la Mungu linasema hivi **"Basi Bwana**

Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu Mbinguni akaketi mkono wa kuume wa Mungu. Nao wale wakatoka wakahubiri, kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo" (Marko 16:19-20)

Mungu Roho Mtakatifu anatufundisha katika maneno hayo kuwa Mungu alitumia karama ya miujiza n.k. ili kulithibitisha neno hilo kuwa limetoka kwa Mungu, fahamu ishara mbalimbali Mungu alizitumia kulidhibitisha neno lake, Paulo anasema katika (**1Kor 2:4-5**) **"na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu. Ili Imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu"** Paulo anasema hakufanya mahubiri ya maneno ya Mungu tu kama Mtumishi mwinjilisti, bali kulikuwa na udhibitisho uliothibitisha maneno hayo, na uthibitisho huo ulitolewa na Roho Mtakatifu ambaye alilithibitisha neno lililosemwa na Paulo kwa dalili za nguvu, fahamu ndugu yangu kuwa katika hizo karama za rohoni zipo karama ambazo zinathihilisha "nguvu" za Mungu kwa dalili zote za uwepo wa Mungu. elewa hivi, karama za rohoni ni vitendea kazi ambavyo Mungu amevitoa kwa watumishi wake ili waitende kazi ya Mungu wakiwa pamoja na Bwana, na Bwana akithibitisha kwa karama zake maneno yaliyotolewa katika vinywa vya watumishi wake.

Ebu angalia tena maneno haya ya Bwana yasemavyo **"Mungu akishuhudia pamoja nao kwa ishara, na ajabu na nguvu za namna nyingi na kwa magawanyo ya Roho mtakatifu kama alivyopenda mwenyewe (Ebr 2:4)** Mungu yeye hushuhudia pamoja na watumishi wake kwa kutumia hizo karama zake alizowapatia watumishi wake.au huthibitia uwepo wake mbele za watu wote kuwa yupo katikati yao

Ebu elewa sasa tofauti ya Karama na utumishi (Huduma). Mtumishi anatakiwa apeleke ujumbe au neno la Mungu, na Mungu pia huwa anakwenda kulithibitisha hilo neno lake, sasa Mungu hulithibitisha neno hilo kwa kutumia karama mbalimbali alizowapatia hao watumishi wake.

Mungu pi hutumia hizo karama kwa kuwadhihilisha watumishi wake, neno la Mungu linasema hivi **"Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya; Yesu wa Nazaleti mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na maajabu na Ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; (MDO 2:22)** Mungu huwa anawadhihirisha watumishi wake, na huwa wakati mwingine anawadhihilisha kwa kutumia miujiza ishara na maajabu na ukiangalia hapo utaona kuwa Mungu huwadhibitisha watumishi wake kwa kuzitumia Karama zile alizowapatia hao watumishi wake, Yesu alidhihilishwa mbele ya watu wote kuwa kweli ndiye aliyetumwa na Mungu kwa miujiza yake ya kuponya, kupambanua roho, kutembea juu ya maji, kutengeneza mikate n.k. sasa watumishi wa Yesu Kristo tuliye mbeba Yesu Kristo ndani mwetu, tunatakiwa tumwombe sana Mungu apate kumdhihilisha Kristo aliye ndani mwetu, kwa kila dalili za nguvu na ishara ili mwili wa kristo ujengwe. kama kweli tunataka Mungu amdhihilishe Yesu aliye ndani yetu, na ayadhibitisha maneno yake yote tunayo yahubiri au kuyafundisha, basi ni lazima tusikose kufahamu habari zote za Karama za rohoni ambazo Mungu huwapatia Watumishi wake.

MAMBO YA MSINGI YA KUYAFAHAMU

Katika somo hili tutajifunza aina za Karama, na namna zinavyofanya kazi, unaweza kuwa katika (ofisi) au huduma ya mchungaji, mwinjilisti, mwalimu, nabii au mtume, na pia ukawa na Karama ya aina Fulani, kwa ajili ya kukusaidia katika utendaji wa kazi yako. Pia inawezekana kabisa ukawa huna ofisi yeyote ile kati ya hizo lakini Mungu akakupa karama fulani hayo ni mambo ya msingi sana unayotakiwa uyajue.

Neno la Mungu linatufundisha kuwa kila mtu aliye mwamini Yesu Kristo ndiye mtumishi wa Mungu. Neno la Bwana linasema kuwa siku moja wayahudi walimuuliza Bwana Yesu kuwa wafanyeje ili wapate kuwa watumishi wa Mungu. Yesu aliwajibu hivi "**Yesu akajibu, akawaambia hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye" (Yohana 6:28-29**) kwa hiyo ndugu yangu mpendwa fahamu kuwa, kila mtu aliyempokea Yesu moyoni mwake, na kumwamini huyo mtu mbele za Mungu anahesabika kuwa ni mtenda kazi wa Mungu, au ni Mtumishi wa Mungu na neno la Bwana linasema wazi kuwa baada ya sisi kukombolewa kwa kununuliwa kwa damu ya Yesu Kristo, tumefanywa kuwa Makuhani wa Mungu soma kitabu cha(**Ufu 5:9-10**), na kuhani ni Mtumishi wa Mungu, wewe uliyeokoka ni kuhani au mtumishi wa Mungu. Na ikiwa wewe ni Mtumishi basi lazima usikose kufahamu kuhusu habari za karama za roho ambazo Mungu amekupatia wewe ili uwe kama anavyotaka na kukusaidia katika kuifanya kazi ya Mungu pia kukujenga wewe binafsi.

KILA ALIYEOKOKA ANATAKIWA ASIPUNGUKIWE NA KARAMA YEYOTE

"namshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu; kwa kuwa katika kila jambo mlitajirika katika yeye katika maneno yote na maarifa yote, kama ushuhuda wa Kristo ulivyothibitika kwenu; hata hamkupungukiwa na Karama yoyote, mkikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo" (1Kor 1:4-7)

Neno la Mungu linatufundisha kuwa kila mtu aliye ndani ya Yesu Kristo, amepewa utajiri sana na Mungu, na utajiri huo kumbuka upo katika sehemu mbili, baraka zilizo ndani rohoni na baraka zilizo nje ya roho, yaani kuwa na fedha, wanyama, mali mbalimbali, neno la Bwana linasema kuwa kila mtu aliye ndani ya Yesu Kristo hakupungukiwa na Karama yeyote. Ndio maana Paulo anatusisitizia kuwa kila mtu aliye mwamini Yesu Kristo asikose kufahamu habari za Karama za roho, kwa sababu kila mtu aliye ndani ya Bwana Yesu Kristo Neno linasema hajapungukiwa Karama yeyote.

Ngoja nikuulize swali je! Una Karama gani? Watoto wa Mungu wengi sana ukiwauliza swali hili huwa wanajibu hatufahamu lakini neno la Mungu linasema tukiwa katika Yesu Kristo hatujapungukiwa na Karama, watoto wa Mungu wengi sana hawafahamu habari za Karama zao walizopewa na Bwana Mungu, fahamu hujapungukiwa Karama toka kwa Mungu, tatizo hujazifahamu habari hizi za Karama, na Mungu Roho Mtakatifu naamini atakufundisha habari hizo kwa uzuri na utafahamu kabisa kuwa una Karama gani uliyopewa na Bwana.Tatizo la kutofahamu kuwa una Karama ya aina gani ndilo linalosababisha Bwana asionekane katika huduma yako, na katika maisha yako ya wokovu, kwa sababu huifahamu Karama uliyopewa basi huwezi kuichochea, utakaa kimya tu. Mungu anakutaka uifahamu Karama uliyopewa na uichochee. Paulo alimwagiza Timotheo kuwa inatakiwa aichochee Karama aliyopewa **(2Timo 1:6) " kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee Karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu".**

Ukisoma maneno haya utaona ya kuwa Timotheo hakupungukiwa Karama, alikuwa nayo hiyo Karama ya Mungu ndani yake na aliifahamu ndio maana Paulo alimwagiza aichochee, Kama angelikuwa haifahamu sidhani kama Paulo angelimwagiza aichochee, Mungu anataka ikiwa unaifahamu Karama uliyopewa basi uichochee, kama uifahamu, basi anataka ufahamu, na ukiwa na nia ya kuifahamu basi bila shaka atakufahamisha utakapomwomba akufahamishe.

KILA MWAMINI (ALIYEMPOKEA YESU) ANAWEZA KUPOKEA ZAWADI HIZI AU KARAMA HIZI ZA ROHO

Fungua (1Kor 12:6-11) " lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa Neno la hekima; na mwingine neno la Maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine Imani katika Roho yeye yule na mwingine Karama za kuponya katika Roho yule mmoja na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja yeye yule akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye" ukiyasoma maneno hayo utaona ya kuwa Roho Mtakatifu anaweza kumpatia Karama yeyote ile, mtu yeyote yule amwaminiye Yesu Kristo.

Mara nyingi watoto wa Mungu wamefikilia kuwa Karama hizi za rohoni, Mungu amewawekea watu Fulani Fulani tu na wengine wanafikiri kuwa Karama hizo za rohoni huwa zinapatikana katika faragha Fulani, au katika dhehebu Fulani tu. Fahamu, Roho Mtakatifu peke yake ndiye agawaye Karama hizi, na anaweza kumpa mtu yeyote yule kama apendavyo yeye, hivyo ndugu hakuna mtu yeyote yule awezaye kumlazimisha Roho Mtakatifu ampe Karama Fulani, bali Roho Mtakatifu hutoa zawadi hizi kama atakavyo yeye. Pia fahamu kuwa anaweza kumpa mtu yeyote yule, hata wewe anaweza akakupa Karama yeyote ile akipenda kukupatia

Pia fahamu ya kuwa katika suala hili la Karama za rohoni Mungu huwa anawagawia watoto wake mbalimbali, Karama mbalimbali humpa huyu Karama ya aina Fulani na huyu ya aina Fulani huwa hazifanani, hutofautiana tofautiana. Neno la Bwana linasema hivi **" kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu aliyeko kwenu asinie makuu kupita ilivyompasa kunia; bali awe na nia ya kiasi kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha Imani. Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja; tuna viungo vingi. Wala viungo vyote havitendi kazi moja; vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo kila mmoja kwa mwenzake. Basi kwa kuwa tuna Karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya Imani (Rum 12:3-6)**

Mungu amemgawia kila mmoja Karama. Na Karama hizo huwa hazifanani ni za aina mbalimbali, fahamu hatakatika utendaji wake pia huwa haufanani hutofautiana Neno linasema hivi **"Basi panatofauti za Karama; bali Roho ni yeye yule. Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote" (1Kor 12:4-6);** kila mtu Mungu humgawia Karama kama Mungu anavyotaka, pia katika utendaji kazi wa hizo Karama haufanani, fahamu wote mnaweza mkawa na Karama ya kunena kwa lugha, lakini katika utendaji wenyewe wa kunena mkatofautiana sana, hata Karama ya miujiza, usifikirie mtumishi Fulani anaweza kufanana kiutendaji na mtumishi Fulani, lazima ufahamu kuwa kuna kuwa na tofauti kubwa ya kutenda, ila Roho ni yule

yule mmoja, aliyempatia Karama huyo wa kwanza na pia ndiye aliyempatia Karama huyo wa pili, hata katika utendaji Roho aliyemwezesha huyo wa kwanza na ndiye anayemwezesha huyo wa pili.

Mara nyingi watoto wa Mungu wamekuwa na mashaka na baadhi ya watumishi kuwa katika kutenda kwake kazi hakufanani na jinsi walivyowaona watumishi wengine wakitenda, fahamu ndugu yangu kuwa kila mmoja Mungu humpa Karama kama anavyotaka Mungu na katika utendaji pia fahamu kila mtu hutenda kama Mungu alivyomjalia. Kunaweza kukawa na tofauti sana ya kiutendaji. Ona mfano wa watumishi hawa wafuatao, Samson na Eliya.Ukisoma hao watumishi wawili na jinsi walivyokuwa wanafanya huduma zao zilikuwa tofauti kabisa, hata utendaji kazi wa Yohana mbatizaji na Elisha, ulikuwa tofauti kabisa, Yohana hakufanya muujiza hata mmoja. Lakini Elisha alifanya miujiza mingi tu lakini fahamu wote hao walikuwa ni watumishi wa Mungu. Kwa hiyo ndugu yangu fahamu, Mungu anaweza kumpa mtu yeyote yule karama, na pia katika utendaji kazi wa hizo karama huwa haufanani, mambo hayo mawili ukiyafahamu, kwa uzuri, naamini kuwa hutataka kwa wivu Karama aliyopewa mwenzio, pia utaichochea Karama uliyopewa wewe kwa sababu hakuna mtu mwingine aliyepewa karama hiyo zaidi yako, tumepewa karama hizo mbalimbali kwa ajili ya kufaidiana, sasa usitake kuwa kama Fulan, pia usiwe na shaka na mwenzio eti kwa kuwa haneni au afanyi miujiza kama wewe.au kwa sababu mwenzio ana fanya miujiza tofauti na wewe

Kila mtu aliyempokea Bwana Yesu Kristo anaweza kutumiwa na Mungu katika huduma zake, pia Mungu anaweza kukupa karama yeyote ile akipenda, kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa upate ufahamu moyoni mwako kuwa Mungu anaweza kukutumia na kukupatia karama yoyote ile wewe. Mara nyingi watoto wa Mungu katika suala hili huwa wanakosea, huwa wanaona kuwa watu Fulani ndiyo wanaostahili kutumiwa na Mungu katika kazi zake na kupewa karama hizo za rohoni, Neno linasema kila mtu aaminiye, anatakiwa asikose kufahamu habari za karama za rohoni, kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa Mungu anataka umtumikie na pia yuko tayari kukupatia karama hizo za rohoni, na yamkini amekupatia ila hufahamu kuwa umepewa karama ya aina fulani, na haufahamu namna ya kuitumia hiyo karama uliyopewa na Mungu, basi katika somo hili tulilopewa naamini Bwana atakwenda kukufahamisha karama uliyopewa na pia kukufundisha namna ya kuitumia.

NAMNA KARAMA ZINAVYOFANYA KAZI.

Karama ni utendaji kazi wa ki Mungu moja kwa moja kupitia mtumishi wake. yaani Mtumishi huyo anafanya kazi ya Mungu ili kujenga Kanisa la Mungu pasipo mtu huyo kupanga kuwa sasa nafanya hivi, bali ni nguvu ya Mungu itakayotenda kazi moja kwa moja kutoka ndani ya huyo mtumishi wa Mungu, ni pale Mungu anapoamua kufanya jambo Fulani kupitia mtu Fulani na baada ya hiyo kazi mtu huyo anabaki kuwa ni mtu wa kawaida tu. Kwa maana hiyo kitendo kile cha ki Mungu kinapotendeka ndiyo kinachoitwa karama

Utendaji kazi wa Karama huwa haupangiliwi au kuamuliwa na mwanadamu, bali Mungu ndiye anayepangilia. Na ndiye muamuzi wa kazi hiyo anayotaka kuitenda. Fahamu utendaji kazi wa karama ni tofauti na uzoefu wa utendaji kazi za Mungu. Utendaji kazi wa karama huwa ni pale Mungu anapoamua kufanya kazi yake Fulani, basi huifanya yeye mwenyewe kwa kumtumia mtu yule aliyemchagua, baada ya hiyo kazi mtu huyo

huwa hawezi kuifanya tena kazi hiyo, kwani aliyeifanya ni Mungu. Itabidi asubiri tena mpaka Mungu atakapoamua kufanya kazi ingine tena kwa kumtumia huyo mtu. Pia lazima ufahamu kuwa karama huwa haikui. Kama vile watu wengi wanavyofikiri kuwa karama inaweza kukua, fahamu unapewa karama hiyo na Mungu na itakuwa hivyo hivyo kwa kiasi kile Bwana alichokujalia kukupa. Neno la Mungu linatufundhisha kuwa tunatakiwa tuzichochee Karama zile tulizopewa, na tunatakiwa tuzichochee kwa njia mbili, moja ni kuomba na pili kwa kuwa watendaji wa kuifanyia kazi. Paulo alimwagiza Timotheo maagizo **haya "Usiache kuitumia Karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa kuwekea mikono ya wazee" (Timotheo 4:14)** utaona hapo Paulo anamwagiza Timotheo asiache kuitumia karama ile aliyopewa na Bwana maana yake awe mtendaji pia anaagizwa kuwa anatakiwa aombewe ili kuichochea karama ile iliyo ndani yake" kwa kuwekewa mikono.

Kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa utendaji wa karama ni tofauti na utendaji kazi ule wa uzoefu wa kumtumikia Mungu walio nao watumishi wa Mungu wengi, utendaji kazi wa karama ni pale Mungu anapoamua kufanya kazi Fulani katika wakati anaoutaka, na kazi hiyo ataifanya kwa kumtumia mtu yule aliye mchagua, na baada ya hiyo kazi mtumishi huyo anabaki na hali ya kawaida tu, wala hawezi kuitenda tena kazi hiyo. hebu ona mfano wa utendaji kazi wa moja wapo ya karama tuiangalie karama ya Imani.

Fungua (1kor 12:9) "mwingine Imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho mmoja" hapo neno la Mungu linatueleza kuwa kuna karama ya Imani. Karama hii ya Imani ni tofauti na Imani ya kawaida **(Efe 2:8) "kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya Imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu ni kipawa cha Mungu!** Mungu amemgawia kila mtu aliyeokoka Imani, neno kipawa maana yake ni zawadi, sasa Mungu amemgawia kila mtu aliyeokoka zawadi hii ya imani, kwa sababu pasipo Imani hatuwezi kuokoka, na Imani hii ya kutookoa kila mtu amepewa kwa kiasi kile Mungu alichomjalia, neno la Bwana linasema hivi **" kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu aliyeko kwenu asinie makuu kupita ilivyompasa kunia; bali awe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha Imani (Rumi 12:3)** kila mtu aliyeokoka amepewa kiasi cha Imani, tunatakiwa tuishi kwa Imani hiyo.

Na Imani hii ya kawaida huja kwa njia moja, nayo ni kusikia Neno la Kristo **(Rum 10:17) " basi Imani, chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo"** Imani hii ya kawaida ambayo ndani yake kuna wokovu, huja kwa njia ya kulisikia neno la Yesu Kristo, na neno la Mungu tunalipata katika Biblia takatifu, na tunaweza kulisikia kwa kusoma, na kwa kufundishwa na waalimu pia kwa kuhubiriwa na wainjilisti, na pale unapolisikia ndipo Imani hii inapozaliwa na pale unapolishika neno hilo na kulitendea kazi ndipo Imani hiyo inapokua, kwani tumetakiwa na Bwana tuzikuze Imani zetu **(Rum 1:17) " kwa maana haki ya Mungu inadhihiriswha ndani yake, toka Imani hata Imani, kama ilivyoandikwa mwenye haki ataishi kwa Imani,**

Fahamu Imani hii ya kawaida inatakiwa ikue, itoke chini kwenda juu. Na ukitaka kuikuza Imani hii ya kawaida basi unatakiwa uweke bidii ya kusikia neno la Kristo na kulitendea kazi Imani hiyo itakaa ndani yako milele.

TOFAUTI YA KARAMA YA IMANI NA IMANI YA KAWAIDA

Karama ya Imani humjia mtu aliyeteuliwa na Mungu na kufanya kazi ya Mungu ambayo ilitakiwa ifanyike kwa Imani yaani pale wapendwa wote walipo kata tamaa na Imani zao za kawaida zilipofikia ukomo wake, ndipo Mungu hushuka na kumtumia mtu yule aliyemteua kwa kumpatia Imani maalumu au Iamni kubwa ili kazi yake ifanyike, na Baada ya kazi hiyo kwisha mtu huyo aliyetumiwa na Bwana, ana baki na Imani yake ileile ya kawaida. Kama alikuwa hajaikuza basi itabakia hiyo hiyo kidogo. Hawezi kuamini hata kitu kidogo. Hawezi kuamini hata kitu kidogo tu cha Mungu mpaka asikie neno la Kristo ndio Imani yake hiyo ya kawaida itaongezeka. Na kuanza kuamini kile alichotakiwa aamini

ONA MFANO WA UTENDAJI KAZI WA KARAMA YA IMANI

Fungua (1 Fal 18:36-40) " Ikawa, wakati wa kutoa dhabihu ya jioni Eliya Nabii akakaribia, akasema, Ee Bwana Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli, naya kuwa mimi ni Mtumishi wako, naya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako. Unisikie ee Bwana unisikie ili watu hawa wajue ya kuwa wewe, Bwana, ndiwe Mungu na ya kuwa wewe umewageuza moyo wakurudie. Ndipo moto wa Bwana ukashuka ukaiteketeza sadaka ya kuteketezwa na kuni na mawe, na mavumbi, ukayaramba yale maji yaliyokuwamo katika mfereji. Na watu wote walipoona, wakaanguka kifudifudi; wakasema, Bwana ndiye Mungu, Bwana, ndiye Mungu. Eliya akawaambia, wakamateni hao manabii wa baali, asiokoke hata mmoja. Wakamateni; na Eliya akawachukua mpaka kijito cha kishoni, akawaua huko"

Ukisoma maneno hayo utagundua kuwa Eliya, alikuwa na Imani kubwa sana, ambayo ilitumika siku ile, Eliya ali kuwa na Imani kubwa sana kiasi ambacho alimuendea mfalme na kumuambia maneno magumu sana ya kwamba mvua haitanyesha miaka mitatu na nusu kwa neno la Bwana. Na pia alikuwa na Imani kubwa ya kukusanya watu wote wa Israeli pia kuwaambia watumishi wa baali na waite moto toka kwa Mungu wao na yeye atamwomba Mungu anayemwabudu ashushe moto toka Mbinguni ili ushuke na kuiteketeza sadaka iliyokuwa madhabahuni pale. Eliya alikuwa na Imani kubwa kweli saa ile kwa Mungu wake, na alikuwa na Imani kuwa Mungu wa wale manabii hakuwa Mungu wa kweli, na kweli Mungu wa Eliya, ndiye aliyejibu kwa moto na Eliya akiwa na Imani kubwa sana aliwakamata manabii mianne wa baali na kuwauwa.

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Imani aliyokuwa nayo Eliya siku ile, kwa kweli haikuwa ya kawaida ambayo ndiyo ilifanya mambo yote yale, kwa nini nasema Imani hiyo ilikuwa ni Imani maalum? Ni kwa sababu baada ya tukio hilo ambalo Eliya alilifanya siku ile mbele za watu wote wa Israeli. Yezebeli ambaye alikuwa ni mke wa mfalme, na ndiye aliyekuwa Kiongozi wa watu wote waliokuwa wanamwabudu Mungu wa uongo baali, alisikia habari kuwa, Eliya, amewaua manabii wote wa baali, Yezebeli alikasirika sana, na kumtisha Eliya kuwa kwa kuwa amewaua manabii wa baali, basi na yeye atauwawa, basi Eliya, baada ya kitisho hicho alitetemeka sana, na kuogopa sana, na akakimbia akamsahau hata mtumishi wake.

Soma **(1 Falm 19:1-4) " basi Ahabu akamwambia Yezebeli habari ya mambo yote aliyoyafanya Eliya, na jinsi alivyowaua manabii wote kwa upanga. Ndipo Yezebeli akampelekea Eliya mjumbe, kusema Miungu wanifanyie hivyo na kuzidi nisipokufanya roho yako kesho, panapo wakati huu kama roho mmojawapo wa hao.**

Naye alipoona hayo aliondoka, akaenda aihifadhi roho yake, akafika Beer-sheba, mji wa Yuda, akamwacha Mtumishi wake huko.

Eliya yule aliyekuwa na Imani kubwa sana ya kumwomba Mungu na kushusha moto, pia aliyekuwa na ujasiri wa kuwauwa manabii mia nne wa baali, baada ya kutishwa tu, Tena na mwanamke, anapata woga na kukimbia bila hata mtumishi wake, na huko alikokimbilia neno la Bwana linasema kuwa alikwenda huko na kujiombea kufa. hebu fikiri kwa nini Eliya alipata woga huo ghafla?Jibu lake ni hili, Eliya wakati ule wa kwanza, alikuwa na Imani maalum iliyoambatana na Karama ya miujiza, yaani Mungu alitaka kujidhihilisha kupitia mtumishi wake Eliya kwa wana wa Israeli, baada ya huduma ile, Eliya akabaki na Imani ya kawaida, ambayo haikustahimili vitisho vya Yezebeli!Hivyo ndiyo karama ya imani inavyofanya kazi, Mungu humpatia mtu yule amchaguaye imani maalum ili kazi yake Mungu anayotaka ifanyike kwa kutumia imani ipate kutendeka kwa ufanisi, na baada ya kazi hiyo kutendeka imani hiyo maalum huondoka na mtu huyo anabaki na imani ya kawaida inayoweza kukua kwa kulisikia neno la Kristo. na imani ndugu yangu umeelewa jinsi karama zinavyo fanya kazi.

DHUMUNI KUU LA MUNGU KUTUPATIA KARAMA ZAKE

Fungua **(1Kor 14:1-15) "ufuateni upendo na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu. Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake. Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo.yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake, bali ahutubuye hulijenga kanisa. "Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini zaidi sana mpate kuhutubu; maana yeye ahutubuye ni Mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa"**

Lengo kubwa la Mungu kutupatia Karama hizi ni kwa kusudi la kulijenga Kanisa lake Bwana Yesu Kristo, na Ujenzi wa Kanisa la Mungu umesimama katika nguzo nne **(Mdo 9:31) "Basi Kanisa likapata raha katika Uyahudi wote na Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana na faraja ya Roho m takatifu"**

Mungu anataka Kanisa lake lipate raha, pia lipate kufarijiwa, na liendelee, na kuongezeka, mambo hayo manne ndiyo ambayo Mungu anayataka yatendeke katika Kanisa lake, si mpango wa Mungu Kanisa lake lisiwe na raha, Mungu anataka Kanisa lake lipate raha, si kweli kuwa Mungu anataka watu wake, waumwe, wawe masikini n.k, Mungu anataka kanisa lake liongezeke, yaani jamii ya waaminio iongezeke sana, kwani mtu mmoja anapompokea Yesu kuwa Bwana na mwokozi wake na kumwamini ndipo Kanisa la Bwana linapokuwa limeongezeka, pia Mungu anataka watu hao waaminio wawe na maendeleo, wakue katika maisha ya wokovu, na pia wawe na maendeleo katika roho zao na katika uchumi wao, pia Mungu anataka Kanisa lake lipate faraja katika Roho mtakatifu ambaye yeye ndiye faraja ya Kanisa, hayo mambo manne yakijengwe katika Kanisa la Mungu. Kanisa hilo litakuwa limekamilishwa. Fahamu Kanisa maana yake jamii ya watu waliomwamini Yesu Kristo na kumpokea haijalishi ni kabila gani au ni wa umri gani, au wa dhehebu gani hilo ndilo Kanisa la Bwana Yesu Kristo. Dhumuni kuu la Mungu kutupatia Karama hizo ni hilo yaani kuujenga mwili wa Kristo au Kanisa. Mungu aliona kuwa atupatie zawadi hizo ili mwili wa Kristo ujengwe na kwa kweli

kabisa, ikiwa watumishi wa Mungu, watazipokea Karama hizo, na kuzichochea kwa uaminifu, basi mwili wa Kristo utajengwa kwa urahisi na kwa mafanikio makubwa. hebu fikiria karama ya miujiza, ikiwepo na ifanye kazi yake kisawasawa, ni watu wangapi watakao mwogopa Mungu wetu? Na kumrudia?

Kumbuka karama hii ilivyofanya kazi siku ile Eliya alipokuwa katika huduma ya kuwatoa wana wa Israeli katika uasi mkubwa waliokuwa nao, matunda yake yalionekana baada ya moto ule kushuka, ndipo watu wote walipomrudia Mungu na kuuwawa manabii wa uongo. Fikiri karama hii ikitumika miaka hii ya leo ambayo watu wameelimika sana kwa sayansi na teknolojia na watu wa leo hii hawataki hadithi au maneno mengi ya kuwahubiria, bali wanataka kuona na tayari wameona vitu vingi sana vilivyotengenezwa na mwanadamu kama kompyuta, roboti na mashine nyingi sana zifanyazo mambo ya ajabu, fahamu kama watumishi wa Mungu watakuwa na karama hii ya miujiza naamini kweli watu wengi wenye Elimu watamwona Mungu wetu na kumwamini kuwa yeye ni zaidi ya kompyuta. kama watumishi wa Mungu watazitumia ipasavyo karama hizi za Mungu kama ya kinabii, basi fahamu hata ndani ya jamii ya watu waaminio hakuna atakayeingia na uchafu au kwa kujificha kama ilivyo leo hii ndani ya Kanisa.Ebu kumbuka Mfalme Daudi alipofanya dhambi sirini na kujificha sana, Mungu alimtumia Daudi ujumbe kwa kumtumia nabii, ambaye alipewa taarifa yote ya mambo ya sirini aliyoyafanya Daudi na Daudi alitubu na kuendelea akiwa ndani ya Bwana.Hiyo ni mifano michache tu iko mifano mingi sana ambayo inaelezea wazi kuwa kama watumishi wa Mungu watazifahamu habari za Karama za rohoni na kuzitaka kwa Bwana na kuzipokea pia wakizichochea basi mwili wa Kristo utajengwa kwa haraka sana na kwa mafanikio makubwa sana.

TATIZO

Kwanini watumishi wa Mungu wameshindwa kuzipata na hata kuzitumia Karama hizi za Mungu? Hapo kuna majibu mazuri mawili. Jibu la kwanza, ni kwa sababu hawazijui sana habari hizi za Karama za rohoni kwani watumishi wengi wa Mungu kwa sababu ya kutozijua habari hizi wamekuwa waoga sana wanaposikia au kuona Karama hizi zifanyapo kazi kutoka kwa watumishi wengine wa Mungu waliozijua habari za Karama za rohoni. Nimewaona wengi na kuwasikia wengi wakiwa na mashaka sana na hata kutokuwaamini watumishi wenzao walio na karama mbalimbali kama, miujiza, uponyaji, neno la maarifa n.k watumishi wengi na hata viongozi wa Kanisa wawaonapo watumishi walio na Karama hizi huwa hawawaamini hufikia hata kuwatenga na hata kutowapa vipindi vya kuhudumu, kwani uhisi watumishi hao kuwa hawana roho nzuri. Si kosa lao, kwani wengelizifahamu habari hizi za karama za roho wasingelikuwa na wasiwasi na watumishi wenzao.

Sababu ya pili ya watumishi wengi wa Mungu kutopokea Karama hizi za Mungu ni kutokuwa na sifa zile azitakazo Mungu. Tatizo lipo kwa watumishi wenyewe wala halipo kwa Mungu. Roho Mtakatifu anatufundisha kupitia neno la Mungu kuwa, karama hizo zinatakiwa zitumike kwa kujenga Kanisa la Mungu, lakini utaona watumishi wengi wa Mungu hawako hivyo. Watumishi wengi wa Mungu mpaka sasa hivi hawajui Kanisa la Mungu ni nini? Na liko wapi? Wengi wanajua Kanisa la Mungu ni dhehebu lao, au ni Ministry yao, au ni faragha yao tu. Hilo ndilo tatizo linalosababisha Mungu kutowapatia Watumishi hao Karama zake. Kwani ikiwa watazipata Karama hizo, badala ya kuujenga mwili wa Kristo watazitumia kwa kujenga Ministry zao, au madhehebu yao ama faragha

zao.Hivi hujawaona au kuwasikia watumishi ambao wamepewa karama za Mungu na wakazitumia vibaya kwa kujenga madhehebu yao na kuacha kuujenga mwili wa Kristo yaani Kanisa? Hilo ndilo tatizo linalosababisha Mungu kutowapa watumishi wake karama hizo za rohoni. Mpaka watakapofunguka akili zao kwa kuufahamu mwili wa Kristo ulivyo na wakiufahamu tu Mungu atawapa karama hizo, ili Kanisa lake Bwana liendelee na kuongezeka n.k.Sababu nyingine inayosababisha watumishi wa Mungu wengi kutokupewa Karama hizi za rohoni Nikutokuwa na Upendo wa dhati mioyoni mwao. Neno la Bwana linasema hivi **" ufuateni upendo na kutaka sana Karama za rohoni……" (1 Kor 14:1)** kabla hatujazitaka karama hizi za rohoni kutoka kwa Mungu tumeagizwa kwanza tuufuate upendo, au tuwe na moyo wa upendo sababu kubwa inayowazuia watumishi wengi sana wa Mungu kutopewa karama hizi za rohoni ni hii ya kutokuwa na Upendo. Watumishi wengi wa Mungu wanakiri katika vinywa vyao kuwa wanaupendo, lakini mioyoni mwao hawana Upendo, Neno la Bwana linatuonya watoto wa Mungu wote kutoshindana. **(Flp 2:3-5) "Msitende Neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe bali kila mtu aangalie mambo yawengine. Iweni na nia hiyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu."**

Fahamu Upendo hauna mashindano au majivuno, wala hauna ubinafsi, upendo unaunyenyekevu, na unaheshimu wengine ndivyo Mungu anavyotaka watumishi wake wote tuwe, na kama utakuwa na sifa hiyo ni rahisi sana Mungu kukupatia Karama zake. Tatizo linalosababisha Mungu asiwapatie watumishi wake karama hizi za rohoni ni pale anapowaona wengi mioyo yao haijatengenezwa vyema, mioyo iliyojaa husuda, mashindano, majivuno, ubinafsi, kutaka kuonekana n.k. Mungu hawezi kukupatia karama zake ikiwa wewe umejaa kiburi na dharau kwa watu wengine. Watu wengine wanamuomba Mungu awapatie karama za rohoni, lakini wamejikuta hawapati kwa sababu moja nayo ni hii "**tamaa zao". (Yakobo 4:2-3)** hayo ndiyo matatizo yanayozuia watumishi wengi wa Mungu kutopewa, karama hizi za rohoni.

Mfano hebu angalia leo hii jinsi watumishi wengi wa Mungu walivyo, utaona wengi sana baada ya kuinuliwa kidogo tu na Bwana katika huduma zao wamekuwa na kiburi kweli hawataki kushauriwa na wamekuwa ni watu wa kutafuta zaidi mambo yao na kutaka kuonekana na kushindana na watumishi wengine. Wengi wao wametumia nafasi hii kujianzishia ministry zao au madhehebu kwa ajili ya tamaa zao, fahamu ikiwa wewe mtumishi wa Mungu una tabia ya namna hii Mungu hawezi kukupatia Karama yake yoyote ile na ikiwa ulipewa Karama yake ya namna yeyote ile na ukaanza kuitumia vibaya kwa kutaka utukufu au kwa kuitumia kama biashara ya kukuingizia pesa, fahamu ni kitu kidogo Mungu kukuondolea katika huduma yako vipawa vyake alivyokupatia, pia hata kukufuta kabisa katika orodha ya watumishi wake.Ebu ona mfano wa Balaamu, Mungu alimwondoa Balaamu katika orodha ya watumishi wake kwa sababu ya tabia yake mbaya ya kupenda mali kwa kutumia vipawa alivyopewa na Bwana, neno linasema Baalamu baada ya kufanya huduma ile aliyoitiwa na Balaki, aliuawa kwa kupigwa kwa upanga **(Hesabu 31:7-8) "Nao wakapigana na midiani kama Bwana alivyomwagiza Musa; nao wakamuua kila mume nao wafalme wa midiani wakawaua pamoja na watu wengine waliouawa, Evi na Rekemu, Suri na Huri na Reba, hao wafalme watano wa Midiani, Balaamu mwana wa Beori naye wakamwua kwa upanga"**

Fahamu ndugu yangu kuwa Mungu anataka kila mtumishi wake awe na Karama hizi za rohoni lakini hawezi kumpatia karama hizo mtumishi yeyote yule asiye na nia njema ndani ya moyo wake unatakiwa kabla haujaenda kumuomba Mungu akupatie Karama hizo za rohoni uwe na malengo maalumu ya kulijenga kanisa lake. Pia uhakikishe kuwa una mtukuza na utazidi kumtukuza Bwana kwa kukupatia karama zake hizo za rohoni, siyo utukufu wake uuchukue wewe, fahamu Mungu hatakupatia hizo karama zake za rohoni ukiwa na tabia hiyo mbaya. hebu mwombe Mungu ashughulikie kwanza tatizo ulilonalo la dharau ubinafsi, wivu, kiburi kutosamehe, uongo kutoamini n.k. ndipo uende mbele zake na umwombe akupatie karama hizo za rohoni, Mungu hawezi kukupatia karama hizo za rohoni ikiwa moyoni mwako umeshindwa kuwasamehe watu wale waliokukosea. Watumishi wengi wameshindwa kupokea karama hizi za rohoni kwa sababu ya kutosamehe wamekuwa na uchungu mioyoni mwao na chuki nyingi sana ndani yao kwa sababu ya watu Fulani waliowakosea, ikiwa wewe umeshindwa kusamehe, Mungu hawezi kukusikia umuombapo akupe karama zake za rohoni neno linasema hivi **(Marko 11:25) " nanyi kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili baba yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi makosa yenu lakini kama ninyi hamsamehi wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu".** Inatakiwa uwe mtu wa namna hiyo kama unataka Bwana akupatia karama zake za rohoni, ikiwa wewe hujawasamehe hao waliokukosea huwezi kupata kitu kutoka kwa Mungu. Watumishi wengi walikolofishana kwenye madhehebu yao, na wakatoka na kwenda kuanzisha vikundi vyao au madhehebu yao na wengi wao wanamuomba kila siku Mungu awapatie karama zake ili wazitumie katika huduma zao ili Kanisa la Bwana lijengwe lakini wamejikuta hawapewi unajua ni kwanini? Kwa sababu ndani ya mioyo yao hawajawasamehe hao waliowakorofisha. Hebu jifunze kusamehe, na wapende adui zako na Mungu atakupatia hizo karama zake.

Pia wako baadhi ya watumishi wanamuomba Mungu awapatie karama za rohoni wakati ndani ya mioyo yao wanashuhudiwa wazi kuwa wameachana na Mungu kwa sababu ya dhambi zao walizozitenda na hawataki kutengeneza (kutubu) eti kwa sababu wao ni watumishi, wanaona aibu kusimama mbele za watu na kuombewa sala ya toba kwa upya, fahamu hauwezi kupewa karama yeyote toka kwa Mungu mpaka utakapotubu. Yesu anasema **" lakini nina neno juu yako ya kuwamba umeacha Upendo wako wa kwanza basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu ukayafanye matendo ya kwanza lakini usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahari pake, usipotubu" (Ufu 2:4-5)** basi ikiwa unataka kupewa karama hizi za rohoni unatakiwa utubu, na utengeneze ndipo umwombe Mungu akupatie Karama hizo zake, kumbuka, Samsoni alipoanguka na kupoteza karama aliyopewa ya miujiza, siku moja alimkumbuka Mungu na kutubu na kuomba Bwana amlejeshee karama ile ya miujiza aliyokuwa nayo. Na bwana alimrudishia na akafanya mauaji makubwa kwa wale watu waliokuwa adui za Mungu yaani wafiristi. Basi kumbuka ni wapi ulipoanguka ukatubu na mwombe Mungu akurudishie au akupatie karama zake za rohoni. Ili upewe karama hizi jifunze kuishi maisha matakatifu. Achana na dhambi kabisa mche Mungu na utendee kazi kila neno lake Bwana alilokuagiza ulifanye kwa kufanya hivyo itakuwa ni rahisi Bwana kukupatia karama zake hakikisha unakuwa na Upendo ndani ya moyo wako kumpenda Mungu pia kuwapenda watoto wa Mungu na watumishi wake wote. Hapo Mungu atakaa ndani yako na kukupatia karama zake kama apendavyo (**1 Yoh 23-24) "na hii ndiyo amri yake, kwamba tuliamini Jina la mwana wake Yesu Kristo na kupendana sisi kwa sisi, kama alivyotupa amri naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo roho**

aliyetupa" ili Mungu akae ndani yako unatakiwa uyafanye mambo hayo mawili, uwe na Imani kwa Bwana Yesu Kristo na pia uwe na Upendo kwa watu wote.

Fanya maombi mara kwa mara ili Mungu akupatie pendo lake moyoni mwako neno linasema **"Heri walio masikini"** umasikini maana yake ni (Uhitaji) sasa kila siku mwombe Mungu akupatie hitaji lako la upendo ndani yako, pia unatakiwa uuchochee kwa kutendea kazi neno lake alilokuagiza la Upendo.

KARAMA SI TIKETI YA KUONYESHA KUWA UMEKUA SANA KIROHO NA UTAFIKA MBINGUNI

Watu wengi sana baada ya kupokea Karama kutoka kwa Mungu ya aina yeyote ile, wanafikiri kuwa wamekua Kiroho sana ama wengine wanafikiri kuwa kwa kuwa una karama hizo za Mungu basi hata Mbinguni wataingia watu wengi wamefikiri kwa kuwa wana karama ya kunena kwa lugha basi wao ni bora kuliko hao wasionena kwa lugha, wengine wamefikiri kwa kuwa wao wana karama ya miujiza basi wao ni bora kuliko wengine, pia wako watu wengine ambao bado hawajapewe karama ya aina yeyote ile wamekuwa na fikra kuwa huenda wao wokovu wao ni mdogo kuliko hao watu walio na karama mbalimbali.Pia wako watu wengine, kwa sababu wao hawana Karama ya aina yeyote ile, basi wao wanajiona kuwa ni bora kuliko hao walio na Karama ya kunena au ya kinabii, hivi ndivyo watu wengi walio wakristo walivyo, ikiwa umepewa Karama ya aina yeyote ile na Bwana Mungu, usifikiri kwa kuwa una Karama hiyo basi ndio umekuwa na tiketi ya kwenda Mbinguni. Ukisoma maneno ya Mungu kutoka kitabu cha **(Mathayo 7:22-23) "wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana hatukufanya unabii kwa jina lako na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo ntawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu"**

Maneno hayo ya Bwana yanatufundisha kuwa, kumbe siku ile ya mwisho wapo watu wengi ambao wana Karama za miujiza, unabii n.k, hawataingia uzimani, kwa maneno hayo ya Bwana Yesu Kristo tunapata fundisho hapo ya kuwa mtu kuwa na karama ya aina yeyote ile si tiketi ya kuurithi uzima wa milele. kilamtumishi wa Mungu ikiwa anatenda maovu, na kujipa matumaini ya kufika mbinguni eti kwa sababu ana waombea wagonjwa na wagonjwa hao wakapona au kwa sababu wana Karama ya uongozi basi ndio wafanye mambo yasiyompendeza Mungu nakujipa matumaini ya kwenda mbinguni fahamu huko ni kujidanya kabisa.

Yesu anasema atawafukuza watumishi wa namna hiyo, tena anasema hata kuwafahamu hawafahamu kabisa watumishi hao, atawaambia ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu. inawezekana kabisa ukawa na Karama mfano ya kunena kwa lugha halafu wakati huo huo ukawa mzinzi, pia, inawezekana kabisa ukawa na Karama ya miujiza halafu ukawa mzinzi, hebu mwangalie Samsoni alikuwa na Karama ya miujiza lakini alikuwa na tabia (uovu) wa uzinzi, hebu sikiliza maneno haya **"Samsoni akaenda Gaza akaona mwanamke Kahaba, akaingia kwake. Watu wa Gaza wakaambiwa, ya kwamba huyo Samsoni amekuja huku wakamzingira, wakamvizia usiku kucha penye lango la mji, wakanyamaza kimya usiku kucha wakisema na tungoje mpaka mapambazuko, ndipo tutamwua. Basi Samsoni akalala hata usiku wa manane, akaondoka katikati ya usiku, akaishika milango ya lango la mji, na miimo yake miwili akaing'oa pamoja na komeo lake, akajitwika mabegani, akavichukua hata kilele cha mlima ule**

unaokabili Hebroni. Ikiwa baada ya hapo akampenda mwanamke mmoja katika bonde la soreki Jina lake akiitwa Delila". (WAAMUZI16:1-4)

Ukiyasoma maneno hayo utagundua tabia mbaya aliyokuwa nayo Samsoni, ambaye alikuwa na Karama ya miujiza aliyopewa na Bwana, Samsoni alikuwa na tabia hiyo ya uzinzi, uzinzi ni chukizo kwa Mungu, kumbuka maneno ya Bwana Yesu anayosema wazi kuwa siku ile ya mwisho atawafukuza watumishi wale wote watendao maovu, kwa hiyo kila mtu aliye na Karama za rohoni anatakiwa afahamu wazi kuwa hataingia mbinguni eti kwa sababu ana Karama ya aina yeyote ile. Tutaingia mbinguni kwa sababu tunayatenda mapenzi ya Mungu na kuukataa uovu wa aina yeyote ile. Pia unaweza usiwe na Karama yeyote ile lakini ikiwa unayatenda mapenzi ya Mungu fahamu Mungu yuko pamoja na wewe, na umeokoka kabisa, usiwe na hofu kuwa kwa sababu hauna Karama yeyote ile basi wewe haujaokoka au hautaupata ufalme wa Mbinguni, ikiwa umemkiri Yesu Kristo kwa kinywa chako na kumwamini na umempokea Moyoni mwako, Mungu yumo moyoni mwako na ukiwa kila siku unayatenda mapenzi yake na kuukataa uovu fahamu kuwa utaurithi uzima wa milele. Pia inawezekana kabisa ukawa hauna Karama yeyote ile na ukawa unawaona wale watu walio na karama za rohoni kuwa wamepotea, kwa sababu huenda yale matendo ya zile Karama wewe hubarikiwi nazo kwa sababu zako binafsi au za faragha yako au za dhehebu lako, au ministry yako, ukiwa wewe ni mtu wa namna hiyo fahamu hautakuwa unayafanya mapenzi ya Mungu. Wako watu wengine waliookoka na kumwamini Yesu Kristo lakini wao hawana Karama ya kunena au ya miujiza n.k, huwa wakiona watu walio na Karama ya kunena kwa lugha au ya miujiza n.k huwa wanawapinga na hata kuwatenga ama kuwa dharau. Fahamu mbele za Mungu utakuwa umemtendea uovu mkubwa sana, kwani utakuwa unampinga Mungu wala humpingi huyo mtu mwenye hiyo Karama. Neno linasema hivi **"wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao" (2Tim 3:5)**

Wapo watu waliowa mfano huu wengi sana, katika jamii ya waaminio, wanaamini kuwa Yesu ana nguvu na uweza, lakini Yesu akianza kuzidhihilisha nguvu zake na uweza wake kwa kupitia watumishi wake ambao ni wale wamwaminio, huanza kumpinga na hata kumuita pepo na wengine husema ana nguvu za giza huyo, n.k. fahamu ndugu yangu ambaye hauna Karama yeyote ile, ukiwa una waona hao watu walio na Karama za Mungu kuwa wana mapepo au nguvu za giza utakuwa unamkosea Mungu.

Ona mfano huu, siku moja Bwana Yesu akiwa amejaa Roho Mtakatifu na akiwa na karama ya miujiza na uponyaji alimponya na kumfungua mtu aliye kuwa na pepo mbaya na baada ya ile huduma, jamii ile ya Wayahudi wamwaminio Mungu na ambao walisimuliwa na kuziona nguvu za Mungu katika maisha yao hawakuziamini nguvu hizo za Bwana Yesu Kristo, Wakasema kuwa ana Belzeburi, yaani mkuu wa mapepo, fahamu baada ya wale watu kusema maneno hayo, Bwana Yesu Kristo aliwaambia kuwa hawajamkufuru yeye bali wamemkufuru Roho Mtakatifu wa Mungu. Hebu soma **(Math 12: 22-37).** Ukiyasoma maneno hayo utaelewa kuwa kumbe unaweza ukawa huna karama ya aina yeyote ile na ukawa unawadharau watu walio na karama za Mungu na kuwaona kuwa wana mapepo utakuwa una mkufuru Mungu Roho Mtakatifu, unatakiwa leo hii uachane na tabia hii mbaya, Mungu anatutaka watu wake tusizipinge nguvu zake, na nguvu zake Mungu tunazipata kupitia karama zake mbalimbali. Basi tubu na kuanzia sasa fahamu kuwa, kuwa na karama za rohoni na kutokuwa na karama hizi za rohoni hakumfanyi mtu kuwa mtakatifu, au ndio tiketi ya kwenda mbinguni, na imani ndugu yangu umeelewa kwa uzuri kuhusu sehemu hii muhimu sana.

EBU TUANZE KUZIANGALIA KARAMA ZENYEWE ZA ROHONI

Katika siku hizi za mwisho Roho Mtakatifu anafanya kazi kubwa ya kuliamsha Kanisa kutoka katika hali ya kulala usingizi kwa kuliletea mafundisho mengi mazuri ili kazi ya Mungu ya kulijenga Kanisa lake isonge mbele kwa nguvu sana. Na katika somo hili Roho Mtakatifu naamini atakwenda kutufundisha na kutufunulia mambo yote tuliyokirimiwa na Mungu, kama neno la Mungu **linavyosema " lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho maana Roho huchunguzaa yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila Roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokiriwa na Mungu nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni (1Kor 2:10-12)**

Hivyo ndivyo neno la Mungu linavyotufundisha kuwa mambo yote yaliyo ya Mungu, Roho Mtakatifu peke yake ndiye mwenye uweza wa kutufundisha. Kwa hiyo hata suala hili la Karama za rohoni mwenye uwezo wa kutufundisha ni Roho mtakatifu, kwani, fahamu habari zenyewe tunazotaka tuzifahamu ni za roho, na kwa hiyo Roho Mtakatifu anatupatia maneno yake mazuri na kutufasiria kwa uzuri maneno yake hayo ya rohoni yatokayo katika kitabu chake kitakatifu yaani Biblia.

Neno la Bwana linasema **"Basi ndugu zangu, kwa habari ya Karama za roho, sitaki mkose kufahamu" (1Kor 12:1)** maneno hayo ambayo Roho Mtakatifu anayasisitiza kwetu kuwa "kwa habari za karama za rohoni Mungu anataka watoto wake wote lazima tusikose kuzijua. Katika siku hizi za mwisho Mungu Roho Mtakatifu anataka watoto wake tuzijue baraka zote alizotukirimia zilizo rohoni, kwa hiyo ndio maana leo hii Mungu ametupatia somo hili la Karama za rohoni.

AINA ZA KARAMA ZA ROHONI.

Ukisoma maandiko matakatifu utaona kuwa kuna aina nyingi za Karama ambazo Mungu ametupatia watoto wake. ukisoma kitabu cha **(1kor 12:4-11) " basi, pana tofauti ya karama; bali Roho ni yule yule. Kisha panatofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote. Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, ependavyo Roho yeye yule; mwingine Imani katika Roho yeye yule; na mwingine Karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye"**

Ukiyatazama maneno hayo na ukiyasoma kwa makini utagundua kuwa karama ambazo Mungu anazotaka tuzijue zipo za aina nyingi sana, ukiangalia na kuzihesabu ziko karama

tisa za rohoni zilizoandikwa hapo. Lakini ndani ya Biblia kuna karama nyingi sana ambazo Mungu ametupatia watoto wake. zaidi ya hizi tisa zilizo katika Wakorintho 12. hebu fungua Biblia yako kitabu cha **(Mhubiri 5:19) "tazama kwa habari za kila mwanadamu ambaye Mungu amempa mali na ukwasi, akamwezesha kula katika hizo na kuipokea sehemu yake, na kuifurahia mali yake, hiyo ndiyo karama ya Mungu."**

Mungu ametupa Karama nyingi sana mojawapo ni hiyo ya kupewa mali na utajiri pamoja na kula vizuri, watoto wa Mungu wengi hawafahamu kuwa kula vizuri ni karama toka kwa Mungu, wengi wanazifahamu karama tisa tu. Fahamu kuna karama zaidi ya tisa ambazo Mungu anataka tusikose kuzifahamu. Ukisoma kitabu cha **(Mhu 3:13) "tena ni karama ya Mungu kila mtu apate kula na kunywa na kujiburudhisha kwa mema katika kazi yake yote**". Kitendo cha kula vizuri, kunywa vizuri kama soda, maziwa, asali na kufanikiwa katika kazi zako zote fahamu hiyo pia ni karama toka kwa Mungu, watoto wa Mungu wengi sana huwa awamwombi Mungu awapatie Karama hii wengi wamezifikiria karama tisa tu zilizopo kwenye wakorintho sura 12. Fahamu leo kuwa kuna aina nyingi sana za karama toka kwa Bwana. Karama hizi zimegawanywa katika makundi mawili (1) Kundi la karama za rohoni zinazoonekana. Yaani, kuwa na mali, kama nyumba, mashamba, fedha na kula chakula kizuri, kuwa na mavazi na afya njema nk (2) pia kuna karama za rohoni ambazo hazionekani kwa macho haya ya kibinadamu. Zipo rohoni, katika ulimwengu wa roho na utambulikana kwa jinsi ya rohoni. Mtu asiye wa rohoni hawezi kuzitambua. Nazo ndio hizo karama tisa. Zilizotajwa katika kitabu cha wakorintho sura ya kumi na mbili.

Pia ukiendelea kuyaanglia maandiko utaona ya kuwa kuna karama zingine zimetajwa katika Kitabu cha **(1kor 12:28) "na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza Mitume, wa pili manabii, watatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa na masaidinao na aina za lugha"** ona hapo tunakuta katika sehemu hii zimetajwa karama za rohoni ambazo ni **"masaidiano na maongozi"** na karama hizi tunatakiwa tuzijue, hebu jiulize swali, kwa nini leo hii Kanisa la Mungu limekuwa na matatizo sana ya kutokuwa na Viongozi walio na upako au Karama ya kuongoza? Jibu ni kwamba watoto wa Mungu wengi hawajui kuwa Mungu amewapatia baadhi ya watu Karama ya kuongoza Kanisa lake. Kwa kweli leo hii ukiwauliza viongozi wengi wa kanisa kuwa Je! Unayo karama gani? Wengi watakwambia hawafahamu au wengi watasema nina Karama ya lugha au ya uponyaji n.k. lakini Karama hii ya maongozi wengi hawaifahamu na hawajijui kuwa wanayo au hawana.

Pia hata watoto wa Mungu wengi wafanyapo chaguzi zao, hawaangalii karama hii ya maongozi, wengi huwaangalia watu walio na karama za miujiza, uponyaji au za lugha na kinabii, na pia huwaangalia watu walio na huduma ya kiinjilisti au kiuchungaji na ualimu n.k. na kuwapa uongozi, na matokeo yake Kanisa linakuwa na Kiongozi asiye na Karama hii ya maongozi, matokeo yake ndio hayo magomvi na migawanyiko mingi iliyopo ndani ya Kanisa. Mungu amewapa baadhi ya watu Karama ya maongozi na kama watoto wa Mungu tutaifhamu vema Karama hii, tutamwomba Mungu vizuri sana, ili atupatiye viongozi bora mwenye Upako wa kuongoza Kanisa lake, siyo kama ilivyo leo hii, watoto wa Mungu huwachagua watu ili wawe viongozi kwa sababu wamewaona wanahubiri sana au ni kwa sababu wanawaona kuwa wanafedha, au wana Elimu Fulani.Kwa hiyo fahamu ndugu yangu kuwa kuna Karama nyingi za rohoni ambazo hazikutajwa katika

Wakorintho sura ile ya kumi na mbili.Na katika somo hili tutajifunza sana habari za Karama hizo tisa, zilizo katika Wakorintho sura ya kumi na mbili.

KARAMA TISA ZA ROHONI

Kama tulivyojifunza tokea mwanzo wa somo hili ya kuwa Karama maana yake ni zawadi, na utendaji wa Karama hizo ni udhihilisho wa Mungu kwa watu wake kwa kupitia mtu yule ambaye Mungu amependa yeye kumtumia katika kazi aitakayo Mungu ifanyike, na lazima ufahamu kuwa si kwa uwezo wa mtu huyo ndio karama hizo zitafanya kazi, bali ni kwa uweza wa Mungu tu.

Sasa basi hebu tuziangalie hizo Karama tisa ambazo Baba Mungu anataka watoto wake tupate kuzifahamu jinsi zilivyo na namna zinavyofanya kazi na faida zake kwa Kanisa la Mungu. Fungua (**1kor 12:7-11) "lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa apendavyo roho yeye yule; mwingine Imani katika Roho yeye yule na mwingine Karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii, na mwingine kupambanua roho; na mwingine aina za lugha na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda roho huyo mmoja yeye yule akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye."** Mungu ameligawia Kanisa lake hizo Karama zake zipatazo tisa, na ameziumba katika makundi matatu. Zipo karama zifanyazo kazi zikiwa ndani ya moyo au nafsi ya mwanadamu. na zipo karama zifanyazo kazi zikiwa katika ulimi au sauti ya mwanadamu pia zipo zingine zifanyazo kazi zikitumika kupitia mwili wa mwanadamu. na katika kila kundi zipo karama tatu tatu yaani zile zitendazo kazi kwa kupitia katika ulimi wa mwanadamu zipo karama tatu na zile zitendazo kazi kwa kupitia katika mwili wa mwanadamu zipo tatu, na zile zitendazyo kazi ndani ya moyo wa mwanadamu pia ziko tatu. Hivyo ndivyo Mungu alivyoziweka hizo Karama zake na ndivyo tunavyotakiwa kama watoto wa Mungu tufahamu, kama neno la Mungu linavyotuagiza watoto wake kuwa kwa habari za Karama za rohoni tusikose kufahamu. zipo Karama tisa za rohoni, na zipo katika makundi hayo matatu hebu tuone katika kila kundi kuna karama gani.

KARAMA TATU ZILIZOKO NDANI YA MWILI, YAANI MOYONI MWA MWANADAMU

Karama ambazo Mungu anaweza kuziweka ndani ya moyo;
(1) KARAMA YA NENO LA MAARIFA.
(2) KARAMA YA HEKIMA
(3) KUPAMBANUA ROHO

KARAMA TATU ZILIZO KATIKA KINYWA CHA MWANADAMU

Karama tatu ambazo Mungu anaweza kuziweka kinywani mwako ni:-
(1) KARAMA YA AINA ZA LUGHA
(2) KARAMA YA KUTAFSIRI LUGHA
(3) KARAMA YA UNABII
Hilo ndilo fungu la pili kati ya makundi hayo matatu

KARAMA TATU ZILIZOKO MWILINI

Karama tatu ambazo Mungu anaweza kuziweka katika mwili wako ni.
(1) KARAMA YA IMANI
(2) KARAMA YA MATENDO YA MIUJIZA
(3) KARAMA YA UPONYAJI

Karama hizi tatu Mungu anaweza kuziweka katika mwili wako na hili ni fungu la tatu kati ya makundi hayo matatu. Na tumaini ndugu umeelewa vema namna Mungu alivyozigawa hizo karama tisa. Katika mafungu matatu maalum. Mungu aliamua kuzigawa Karama hizo katika mafungu hayo matatu ili kwa kupitia sehemu zote za mwili wa mwanadamu Mungu apate kujidhihirisha kwa wanadamu. Mungu anataka watumishi wake tufahamu kuwa anaweza kutenda kazi zake kwa kupitia hizo Karama zake ambazo katupatia, katika Akili yaani ndani mioyo yetu, katika ndimi zetu, pia katika miili yetu.

Ukiangalia kundi lile la Karama zilizo ndani, yaani Neno la maarifa, hekima na kupambanua roho, ikiwa watumishi wake Mungu watakuwa nazo hizo Karama na kuzitumia vema, fahamu ujenzi wa Kanisa la Mungu utakwenda kwa mafanikio sana. Na pia watumishi wake Mungu lazima wafahamu kuwa Mungu anataka usipungukiwe na Karama yeyote ile, katika sehemu hizo tatu. Mpango wake Mungu kila Mtumishi wake asikose kuwa na Karama Fulani ndani yake ulimini mwake au mwilini mwake. Hivyo ndivyo Bwana anavyotaka tuwe, sijui ndugu yangu katika hizo Karama tisa umebahatika kuwa na Karama iliyo katika kundi gani?

Inawezekana ukawa na karama mbili zilizo katika makundi mawili tofauti au ukawa na karama mbili zilizo katika kundi moja pia unaweza ukawa na karama tatu yaani moja moja kutoka katika kundi jingine, au unazo zote tatu zilizo katika kundi moja, ukisoma maandiko matakatifu utaweza kuwaona watumishi waliona karama zote tatu zilizo katika kundi moja. Eliya alikuwa na karama tatu zilizo katika kundi moja la Karama zilizo katika mwili yaani karama ya uponyaji, miujiza na Imani, ukisoma maandiko utaona Eliya alikuwa na Karama hizo zote tatu.

Fungua **(1 Falme 17:17-24) " Ikawa, baada ya hayo, mwana wake yule mwanamke, bibi wa nyumba ile akaugua; ugonjwa wake ukazidi akawa hana pumzi tena akamwambia Eliya, ninanini nawe, Ee mtu wa Mungu? Je! Umenijia ili dhambi yangu ikumbukwe, ukamwue mwanangu, akamwambia nipe mwanao akamtoa katika kifua chake akamchukua juu chumbani mle alimokaa mwenyewe, akamlaza kitandani pake. Akamwomba Bwana akanena Ee Bwana Mungu wangu Je! Umemtenda mabaya mjane huyu ninayekaa kwake hata kumfisha mwanawe. Akajinyosha juu ya mtoto mara tatu, akamwomba Bwana, akanena, Ee bwana Mungu wangu, nakusihi roho ya mtoto huyu imrudie ndani yake tena. Bwana akaisikia sauti ya Eliya na roho ya mtoto ikamludia, akafufuka, Eliya akamtwaa mtoto akamchukua toka orofani mpaka chini ya nyumba ile, akampa mama yake Eliya akanena, Tazama mwanao yu hai, mwanamke akamwambia Eliya, sasa najua ya kuwa wewe ndiwe mtu wa Mungu naya kuwa neno la Bwana kinywani mwako ni kweli"**

Katika maneno hayo tunapata mafundisho kuwa Eliya mtumishi wa Mungu alikuwa na Karama ya uponyaji na karama ya Imani na karama ya miujiza, fahamu mtoto yule alikuwa ni mgonjwa sana, na alikufa, sasa ili mgonjwa huyo apone pia afufuke fahamu Imani aliyokuwa nayo Eliya siku ile haikuwa Imani ya kawaida, bali alikuwa na Imani maalumu itokayo kwa Mungu yaani Karama ya Imani, pia kitendo cha mtoto yule

kufufuka toka kwa wafu si tendo la kawaida ni jambo la kustaajabisha kabisa. Kwa tendo hilo tunaona muujiza mkubwa alioufanya Bwana pia kumbuka mtoto yule alikuwa anaumwa sana, baada ya huduma ile mtoto huyo neno la Mungu halituambii kuwa aliendelea kuumwa bali alipona na kumrudia mama yake akiwa na afya njema, kwa hiyo utaona hapo ya kuwa siku ile karama ya uponyaji ilitenda kazi.

Kwa hiyo ndugu fahamu Eliya alikuwa na Karama zote tatu zilizo katika kundi moja kumbuka ofisi yake au huduma yake alikuwa ni Nabii, **" ikawa wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya nabii akakaribia…….. (1Fal 18:36)** Eliya alikuwa ni Nabii na pia alikuwa na Karama au vitendea kazi VITATU kwa wakati mmoja. unaweza ukawa na Karama zote tatu zilizo katika kundi moja. Pia unaweza ukawanazo na zingine moja moja zilizoko kwenye makundi mengine. Ona kwa mfano Eliya pia alikuwa na Karama ya neno la maarifa. Ukisoma kitabu chote cha wafalme sura ya 17 utaona jinsi Karama ya neno la maarifa lilivyofanya kazi, fahamu Eliya alipewa neno hilo la maarifa au kwa lugha itakayoeleweka vema neno la ufahamu. Neno hili la ufahamu alilopewa Eliya toka kwa Mungu lilikuwa ni la mvua kutokuwepo kwa kipindi cha miaka mitatu. Neno hilo halikuanzishwa na Eliya, bali Bwana ndiye aliyemtuma Eliya kama Eliya mwenyewe anavyokiri kwa kinywa chake hivi **"ikawa wakati wa kutoa dhabihu ya jioni Eliya nabii akakaribia, akasema ee Bwana Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Israeli na ljulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli naya kuwa mimi ni mtumishi wako na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako" (1Fal 18:36)** fahamu kipindi kile wana wa Israeli walimwasi Mungu na Mungu akapanga namna ya kuwarudisha hao wanawe. Akapata maarifa ya kutokuwapa mvua hao wanawe kwa muda wa miaka mitatu na nusu na maarifa hayo ya kuwageuza wana wa Israeli Mungu alimjulisha Eliya. Na Eliya akaenda mbele za Ahabu mfalme wa Israeli, na kumwambia maneno hayo aliyopewa na Bwana, wakati njaa imekuwa kali, Mungu alimpatia Eliya maarifa ya namna ya kupata chakula, wala hayakuwa maarifa ya Eliya bali "Karama ya neno la maarifa toka kwa Bwana ndiyo iliyotenda kazi siku ile. Neno la Mungu linasema hivi **"Neno la Bwana likamjia kusema ondoka hapa, geuka, uende upande wa mashariki, ujifiche huko. Basi akaenda akafanya kama alivyosema Bwana;kwa kuwa akaenda akakaa karibu na kijito cha keriethi, kinachokabili Yordani. Kunguru wakamletea mkate na nyama asubuhi na mkate na nyama jioni, akanywa maji ya kile kijito. Ikawa, baada ya siku kupita, kile kijito kikakauka, kwa sababu mvua haikunya katika nchi. Neno la Bwana likamjia kusema, ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni ukae huko, Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe" (1 Fal 17:2-9)**

Hapo tunasoma maneno mazuri ya Mungu yakitufundisha kuwa maarifa ya kupata chakula wakati ule mgumu, Eliya aliyapata kutoka kwa Mungu, hayakuwa maarifa ya kawaida, ya akili za kibinadamu. Bali yalikuwa ni maarifa ya Mungu aliyompatia Mtumishi wake Eliya ili apate chakula. Na maarifa hayo maalumu ndiyo yaitwayo karama ya neno la maarifa; na hapo tunapata fundisho zuri kuwa Eliya alikuwa pia na Karama nyingine iliyo katika kundi tofauti na Karama zile za miujiza na Imani na uponyaji. Kwa maana hiyo basi, unaweza ukawa na Karama moja moja kutoka katika kila kundi, au unaweza ukawa na karama moja iliyo katika kundi mojawapo kati ya hayo matatu. Pia unaweza ukawa na Karama zote zilizo katika kundi moja na nyingine kutoka katika makundi mbalimbali. Katika Biblia hii mtu aliyekuwa na Karama zote tisa aliyezitumia zote kwa uzuri sana ni Bwana Yesu kristo alikuwa na Karama zote tisa.Katika Kanisa la leo Mungu anataka watumishi wake tusipungukiwe na Karama ya aina yeyote

ile, ikiwa leo hii tutakuwa na Karama hizi na zikatumika kwa kila mmoja aliyepewa kwa uzuri basi mwili wa Kristo utajengwa vizuri, Kwa hiyo basi, hebu jiangalie, mtumishi umejaliwa kuwa na karama gani? Je! Umejitambua kuwa wewe ndiwe uliyekusudiwa na Mungu kupewa hizo Karama? Ikiwa wewe ni mtumishi uliyempokea Bwana na una ushuhuda wa Kristo na umeshuhudiwa vema na watu waliokuzunguka na wewe mwenyewe unajishuhudia kuwa Yesu yumo moyoni mwako na umekubaliwa naye umejihakikisha hivyo basi ni lazima ufahamu kuwa Mungu hataki upungukiwe na karama mojawapo katika makundi hayo matatu. Mwombe Mungu naye atakupatia, Karama zake kama apendavyo. Usiogope, Karama hizi za Bwana hazina majuto kama wengi wanavyofikiri, neno linasema **"kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake" (Rum 11:29)** usiogope kupewa Karama yeyote ile toka kwa Bwana. Mwombe akupatie, amini, pokea, kwa kushukuru mwamini Mungu atakupatia karama yoyote ile kama apendavyo.

Ni matumaini yangu kuwa Roho Mtakatifu amekupatia ufahamu ndani ya akili yako kwa kukufahamisha jinsi Karama zake zilivyo katika makundi matatu na jinsi Mungu alivyokusudia kufanya kazi zake kwa kututumia sisi wanadamu kwa kutuwekea karama zake katika akili zetu, katika ulimi wetu na katika miili yetu. Pia kwa kutufundisha namna tunavyoweza kuwa na Karama mbalimbali tunamshukuru Mungu kwa kutufunulia hayo.

Tusonge mbele na tuanze kuangalia Karama hizi moja moja jinsi ilivyo na inavyofanya kazi yake. Tuanze na fungu la Karama zilizo kwenye ulimi au sauti.

KARAMA YA LUGHA NA KUFASIRI LUGHA NA UNABII

Tumefundishwa na Mungu Roho Mtakatifu kuwa, Mungu amezigawa Karama zake katika mafungu matatu, na kundi mojawapo ni hili la Karama zilizo katika vinywa vyetu.

Na kazi kubwa ya Karama hizi fahamu ni ile ile ya kulijenga Kanisa la Mungu. Pia kazi nyingine ambazo Karama hizi zinafanya ni kuliweka Kanisa katika hali njema ya kumwabudu Mungu, pia kuliweka Kanisa katika hali ya Utakatifu na kulifahamisha au kulijulisha Kanisa mapenzi ya Mungu, na pia kulifariji na kulitia amani Kanisa lake Bwana Yesu Kristo hayo ndiyo mapenzi ya Mungu aliyokusudia kwa kutuletea Karama hizi za rohoni na kuziweka katika ndimi za watoto wake wale wampendao na walio watumishi wake, fahamu Karama hizi zilizo katika ndimi zetu si kuwa zipo kama mapambo tu, au Ishara ya kuwaonyesha watu kuwa Yesu yumo ndani yako tu, fahamu Mungu kwa kutupatia Karama hizo ana lengo maalum, nalo ni la kulijenga Kanisa lake, watu wengi hawafahamu hili, wengi waliopewa na wanaohitaji Karama hizi za kunena kwa lugha, unabii, na kufasiri lugha, wengi wanafikiri kuwa Karama hizi wamepewa kwa sababu wao ni watakatifu sana, au kwa ajili yao binafsi, n.k. fahamu karama hizi Mungu ametupatia kwa ajili ya kulijenga Kanisa lake. Si kwa ajili yako binafsi n.k. fahamu karama hizi Mungu ametupatia kwa ajili ya kulijenga Kanisa lake. Si kwa ajili yako binafsi bali ni kwa ajili ya jamii nzima imwaminio Yesu Kristo, yaani Kanisa, na Kanisa ni wewe na kila mtu aliyempokea Yesu Kristo. Basi fahamu leo hii kuwa kusudi la Mungu kutupatia watumishi wake karama hizi ni kwa ajili ya kulijenga Kanisa lake. Na ikiwa unayo Karama yeyote ile au utakuwa na uhitaji wa Karama yeyote ile toka kwa Mungu iliyo katika kundi hili, basi unatakiwa uitumie Karama hiyo kwa kulijenga Kanisa lake Bwana na fahamu ukiwa na nia hiyo ndani ya moyo wako, Mungu atakupatia Karama yeyote ile iliyo katika kundi hili la Karama zilizo katika ulimi au sauti ya mwanadamu.

KARAMA YA LUGHA

Karama hii ya lugha, au kunena kwa lugha mpya, Mungu aliiahidi kuwapa wana wake tokea zamani sana. **(Isaya 28:11) "la bali kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa"** Mungu aliyasema maneno hayo kupitia kinywa cha nabii Isaya, kuwa kuna siku atakapo sema yeye Mungu na watu wake kwa lugha nyingine mpya kabisa, na fahamu atakaye kuwa anasema ni Mungu, naye, atasema kwa kupitia mtu. Yule atakaye mchagua, kwa hiyo basi Mungu leo hii anasema kwa lugha mpya kabisa masikioni mwa wale wasikiao na hata kwa hao waliotumiwa na Mungu katika kuyanena maneno hayo, pia kwao maneno hayohuwa ni mageni kabisa, huwa hawayafahamu yanakuja tu kinywani mwao na waowanayatamka, lakini kwao huwa ni maneno mapya kabisa.

Pia Bwana Yesu Kristo alisema kuwa watu wale watakao mwamini watapewa Karama hii ya kusema au kunena kwa lugha mpya **(Marko 16:17) "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo watasema kwa lugha mpya"** maneno hayo aliyasema Bwana wetu Yesu Kristo kuwa watu wale wamwaminio watapewa ishara, na ishara zenyewe ziko nyingi, na mojawapo ya ishara ni hii ya kusema kwa lugha mpya. Fahamu katika suala hili la ishara si wote watakuwa na Karama ya aina moja unaweza ukawa hauneni kwa lugha lakini ukatoa pepo hiyo ni ishara unaweza ukawa hauneni kwa lugha lakini ukawawekea wagonjwa mikono waumwapo nao wakapata afya, hiyo pia ni ishara kuwa unamwamini Bwana Yesu Kristo.

Kwa hiyo basi tendo hili la kusema kwa lugha mpya ni tendo la kimungu kabisa, si tendo la kuiga au kujifanyisha au kujitungia bali ni tendo ambalo Roho Mtakatifu analifanya kupitia sauti au kinywa cha mtu yule amwaminiye Bwana, na kumuwezesha aseme maneno ambayo ni mageni kabisa kwake, yaani Roho Mtakatifu aliye ndani ya mtu yule amwaminiye Yesu Kristo, anao uwezo wa kumpatia mwamini yoyote yule maneno mapya kabisa ambayo huyo mwamini hayafahamu. Na tendo hilo ndilo linaloitwa Karama ya kunena kwa lugha. Yaani ni zawadi tuliyopewa na Mungu ya kusema kwa lugha tusiyoifahamu kwa kuwezeshwa na Roho Mtakatifu.

Fahamu Karama hii au zawadi hii Mungu amewagawia watu wale wote wamwaminio, walio sehemu yoyote, aijalishi umri wao, au nyadhifa zao, au dhehebu lao, bali ni kwa kila mtu amwaminiye Yesu na kumpokea, watu wengi wamefikiria vibaya kuwa Karama hii ni ya watu waliopo katika dhehebu Fulani tu fahamu hiyo sio kweli, Mungu anao uwezo wa kumpatia Karama hii mtu yeyote yule aliyemwamini Bwana Yesu Kristo, aliyepo katika dhehebu lolote, na haijalishi amempokea Yesu kipindi kirefu au kifupi.

Nimemwona Bwana akiwapatia Karama hii watu wa madhehebu mbalimbali, ili mradi tu wamemwamini Bwana Yesu Kristo.

LUGHA ZA AINA MBALIMBALI

Pia fahamu Roho Mtakatifu anao uweza wa kukupatia Lugha za aina mbalimbali. Anaweza kukuletea kinywani mwako lugha za kibinadamu usizozifahamu au anaweza kukuletea lugha za Mbinguni za malaika, neno la Bwana linasema **"nijaposema kwa lugha za za wanadamu na za malaika ... (1Kor 13:1)** Paulo alikuwa anazungumzia

hapo kuwa ikiwa mtu atakuwa na Karama ya kusema kwa lugha na ikiwa mtu huyo pia ana karama ya kinabii kama mtu huyo hana upendo ni bure kabisa. Sasa ukiangalia sehemu hiyo ya kunena kwa lugha, anasema hapo habari za lugha za aina mbili kuna lugha za wanadamu, pia kuna lugha za malaika. Kwa hiyo basi ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa kwa kupitia karama hii ya lugha Roho Mtakatifu anaweza kukuwezesha ukanena kwa lugha za wanadamu, pia akakuwezesha unene kwa lugha za malaika. Lugha za kibinadamu zipo nyingi sana na inawezekana nyingine tokea umezaliwa haujawahi kuzisikia na fahamu Roho Mtakatifu anaweza kuzisema zote hizo na akakuletea uzinene katika kinywa chako, pia hata lugha za malaika anazifahamu, na anaweza akakuwezesha uziseme pia.

Kwa hiyo fahamu Karama hii ya kunena kwa lugha inaitwa hivyo kwa sababu mtu aliyepewa Karama hii, anasema kwa lugha mpya, asiyo ifahamu kabisa katika maisha yake. Nimewahi kuwaona watu wengi wakinena kwa lugha, ambazo wao hawazifahamu kabisa, lakini mimi nilikuwa nazifahamu hizo lugha, kuwa hiki ni kiingereza, kiganda n.k. lakini watu hao ukiwaambia waongee kiingereza walikuwa hawawezi kabisa, lakiniRoho Mtakatifu alipowashukia juu yao walinena kwa lugha hizo wasizozifahamu kabisa. Kwa hiyo fahamu ndugu, Roho Mtakatifu anao uwezo wa kukuwezesha wewe unene kwa lugha mpya kabisa. Mfano kina Petro baada ya kupokea Karama hii walinena kwa lugha mpya kabisa za wanadamu siku ile ya Pentekosti **(Mdo 2:5-12) "na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila Taifa chini ya Mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa Makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote wakastaajabu wakiambiana, Tazama hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Warparth na wamedi na waelami nao wakaao Mesopotamia, Uhayudi na kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia Karibu na kirene na wageni watokao Rumi, wayahudi na waongofu, wakrete na waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana maana yake nini mambo haya? Wengine walidhihaki, wakisema, wamelewa kwa mvinyo mpya".**

Siku ile Mungu Roho Mtakatifu aliwapatia Mitume Karama hii ya kunena kwa lugha, na fahamu siku ile lugha walizozinena hao mitume zilikuwa ni za wanadamu, maandiko yanatufundisha kuwa watu wa makabila mbalimbali walikuwepo Yerusalemu siku ile, na waliwasikia mitume wakisema maneno kwa lugha ambazo hao wageni walizielewa, kwani zilikuwa ni lugha walizozifahamu kabisa, la kushangaza lilikuwa ni hili, waliokuwa wananena maneno hayo walikuwa ni "**Wagalilaya**" watu ambao walikuwa hawafahamu lugha nyingine zaidi ya lugha zao, sasa jambo hili lilikuwa ni la kushangaza sana kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa, Mungu akikupatia Karama hii anaweza kukuwezesha unene kwa lugha yoyote ile ya kibinadamu, pia anaweza akakuwezesha wewe unene kwa lugha ya malaika.

Watu wengine wamekuwa na hofu sana na Karama hii, wengi hufikiria kunena kwa lugha ni tendo walilopewa mitume tu, na watu wa Kanisa la sasa hawawezi kuwa na Karama hii.fahamu hiyo si kweli kabisa, na mara nyingi watu waliopewa kipawa hiki miaka hii ya leo huwa wanadharauliwa na pia kutengwa na Wakristo wenzao. na wengine huonekana kama ni watu waasi walioeta mambo mapya yasiyokubalika ndani ya Kanisa. Fahamu ndugu yangu kuwa, kunena kwa lugha ni Karama ambayo Mungu humpa mtu yeyote yule

amwaminiye Yesu Kristo, ukisoma maandiko matakatifu utaona kuwa, tendo hili la kunena kwa lugha liliendelea tokea siku ile waliopewa mitume Karama hii mpaka siku hii ya leo, ukisoma maandiko matakatifu katika kitabu cha **(Mdo 10:44-47) " Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliosikia lile neno, na wale waliotahiriwa walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha na kumwadhimisha Mungu. Petro akajibu ninani awezaye kukata maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho mtakatifu vilevile kama sisi?**

Maneno hayo yanatufundisha wazi kuwa Karama hii ya kunena kwa lugha haikukomea kwa mitume tu, Mungu aliendelea kuwapatia watu wengine walioamini neno la Mungu yaani watu waliomwamini Yesu Kristo kuwa ndiye mwokozi na kuwa alikufa na kufufuka, na ndiye masihi mwana wa Mungu watu wale walioliamini neno la Mungu, Mungu bila upendeleo aliwapatia Karama hii ya kunena kwa lugha tena lazima ufahamu kuwa hata wamataifa ni watu wale wasio wayahudi kwa asili, pia Mungu aliwapatia Karama hii, ili mradi tu, wameliamini neno la Mungu. Kornelio hakuwa myahudi, lakini yeye na nyumba yake walipmwamini Yesu tu walipokea Karama hii ya kunena kwa lugha, jambo hili liliwashangaza sana watu wale waliojiona kuwa wao tu ndio wanaostahili Karama hii, yaani wayahudi waliotahiriwa. Neno la Bwana linasema kuwa walishangaa na kustaajabu kwani waliwasikia hao ndugu wakinena kwa lugha mpya, na kumwadhimisha Mungu. Tena fahamu watu walipokea Karama hii kabla hata hawajabatizwa kwa maji kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa Karama hii ya kunena kwa lugha, Mungu anaouwezo wa kumpa mtu yeyote amwaminiye Yesu Kristo sasa hivi, si kwamba Karama hii walipewa Mitume tu, pia fahamu Mungu anaouweza wa kumpa mtu yeyote Yule Karama hii ikiwa ataliamini neno la Mungu na kumpokea Yesu Kristo hata kabla hajabatizwa ubatizo wa maji, kwa staili ya aina yeyote ile.

Watu wengi sana walio wakristo yaani waliookoka wamekuwa na maswali mengi sana juu ya Karama hii, hasa wawasikiapo watu wale ambao wao wanawaona kuwa hawajabatizwa kwa maji au watu wasiostahili wakinena kwa lugha mpya, na wengi wamewaona hao watu kuwa hawaneni katika Roho Mtakatifu, bali ni pepo wachafu wanaonena ndani ya hao watu, kwa sababu hao watu hawajabatizwa kwa maji kama wao walivyobatizwa kwa maji, ndivyo watoto wengi sana wa Mungu wanavyowaza mioyoni mwao na wengi ndivyo wanavyokiri kinywani mwao.

Fahamu ndugu yangu kuwa, Mungu anaweza kumpatia Karama hii mtu yeyote aliyemwamini Yesu Kristo kuwa ni mwokozi wake, hata kama hajabatizwa kwa maji kama ulivyobatizwa wewe. Fahamu kuwa tatizo hili la watu kujihesabia kuwa wao tu ndio wenye haki ya kupokea Karama hii ya kunena kwa lugha halikuanza leo, lilianza tokea zamani, kwani siku ile Petro alipofanya huduma nyumbani kwa Kornelio, habari ziliwafikia Wakristo waliokuwa Yerusalemu. Kuwa Petro kaenda kuwagawia Karama hii watu wasiostahili fungua **(MDO 11: 1-18) "Basi mitume na ndugu waliokuwako katika uyahudi wakapata habari ya kwamba watu wa mataifa nao wamelipokea neno la Mungu**. Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale walio wa tohara wakashindana naye, wakisema, uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao. Petro akaanza kuwaeleza kwa taratibu, akisema, nalikuwa katika yafa, nikiomba roho yangu ikazimia, nikaona maono, chombo kinashuka kama nguo kubwa inateremshwa kutoka mbinguni kwa pembe zake nne, kikanifikilia. Nikakitazama sana, nikifikiri, nikaona wanyama wanchi wenye

miguu minne; na wanyama wa mwituni, nao watambaao na ndege wa angani. Nikasikia na sauti ikiniambia ondoka Petro ukachinje ule. Nikasema, Hasha, Bwana, kwa maana kitu kilichokichafu na kilichonajisi hakijaingia kabisa kinywani mwangu, sauti ikanijibu mara ya pili kutoka mbinguni, alivyovitakasa Mungu usivinene wewe najisi. Jambo hili likatendeka mara tatu, kisha vitu vyote vikavutwa tena juu Mbinguni. Na tazama mara hiyo watu watatu wakasimama mbele ya nyumba tuliyokuwamo waliotumwa kwangu kutoka Kaisaria. Roho akaniambia nifuatane nao, nisione tashwishi. Ndugu hawa sita nao wakaenda pamoja nami. Tukaingia katika nyumba ya mtu yule akatueleza jinsi alivyomwona malaika aliyesimama nyumbani mwake na kumwambia, tuma watu kwenda yafa ukamwite Simoni aitwaye Petro, atakayekuambia maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo. Nikalikumbuka neno lile la Bwana, jinsi alivyo sema Yohana alibatiza kwa maji kweli, bali ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Basi ikiwa mwenyezi Mungu amewapa wao Karama ile ile aliyotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu kristo, mimi ni nani nani niweze kumpinga Mungu? Waliposikia maneno hayo wakanyamaza, wakamtukuza Mungu wakisema, basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima"

Petro aliitwa kwenye kesi nzito ya kwa nini aliwaendea watu wasio wayahudi na kuwaambia maneno ya wokovu watu hao, na kosa kubwa aliloshitakiwa Petro, lilikuwa ni kwanini amewagawia hao watu Roho mtakatifu watu hao na wakanena kwa lugha Na Petro aliwaambia kuwa si yeye aliyewapelekea hao ndugu Karama hiyo bali yeye aliwapelekea hao ndugu neno liwezalo kuokoa na huduma hiyo ndiyo aliyoifanya, Petro aliwaeleza kuwa Mungu ndiye aliyemtuma aende kuifanya na si yeye Petro aliyewapatia hao ndugu Karama hiyo bali ni Mungu aliyewapatia Karama ile ile kama alivyowapatia kina wao na Mitume wengine na baada ya maelezo hayo ya Petro kesi iliisha hapo hapo.

Leo hii ndugu Mungu anataka ufahamu habari za karama zake, kuwa anao uwezo wa kumpatia mtu yeyote yule aliaminiye neno la wokovu kama alivyoamini Kornelio na ondoa mashaka kuwa mimi sijabatizwa kwa maji na si myahudi au si wa dhehebu Fulani kwa hiyo siwezi kupata Karama hii ya kunena kwa lugha mpaka nikabatizwe kwa maji au niamie dhehebu Fulani ndio nitapokea Karama hii ya kunena kwa lugha, fahamu sifa kuu ya wewe upokee Karama hii ya lugha ni hii Pokea neno la Mungu liwezalo kukuokoa wewe na nyumba yako na neno hilo ni Yesu Kristo, ukifanya hivyo fahamu Mungu atakupatia Karama hii ya lugha katika saa na wakati ule atakao utaka yeye.

USHIRIKA NA KARAMA NYINGINE

Karama hii ya lugha pia inaushirika mkubwa na Karama nyingine zilizo katika kundi lake, yaani Karama zile zilizowekwa kwenye sauti au ulimi wa mwanadamu, Karama hii huwa inafanya kazi na Karama ya kufasili lugha, neno la Bwana linasema hivi **"kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri (1 Kor 14:13).**

Neno la Bwana linatufundisha wazi hapo kuwa, Karama ya kunena kwa lugha huwa ina shirikiana na Karama ya kufasili lugha. Kwa hiyo utaona hapo ya kuwa kama mtu anayo Karama ya kunena kwa lugha basi inatakiwa awe pia na karama ya kufasili hiyo lugha. Kwa hiyo utaona wazi kuwa karama hii inaushirikiano mkubwa na karama nyingine, watu wengi walio na karama hii ya kunena kwa lugha huwa hawafahamu kuwa wanatakiwa

pia wawe na karama ya kufasili lugha pia kuna wengine wanayo karama hii ya kufasiri ila hawajijui kuwa wanayo karama hii ya kufasiri lugha, kwani hawajui namna karama hii ya kufasiri lugha inavyofanya kazi, fahamu ndugu kuwa kuna ushirikiano mkubwa kati ya karama hii ya kufasiri lugha na karama ya lugha.

Pia Karama hii ya kunena kwa lugha ina ushrikiano mkubwa sana na karama ya unabii, fahamu unabii ni neno lililotoka moja kwa moja kutoka kwa Bwana si neno la mtu, bali ni lile neno lililotoka moja kwa moja toka kwa Bwana, akisema jambo kwa wakati huo, sasa ushirikiano wa karama hii ya lugha na Karama ya kufasiri lugha zikifanya kazi pamoja ndipo unabii unapopatikana. Kwani **Karama ya Lugha + Karama ya kufasili lugha = UNABII**. Tutajifunza zaidi huko mbeleni tukianza kuziangalia Karama hizo za kufasili lugha na Karama za kinabii zilivyo na zinavyofanya kazi, kwa sasa hebu tuendelee na Karama hii ya lugha jinsi inavyoshirikiana na Karama nyingine. Fahamu pia ya kuwa Karama hii ya lugha inafanya kazi na Karama isiyo katika kundi la Karama zilizo kwenye ulimi, nayo ni Karama ya Imani, Mungu mara nyingi huwa anatutumia Karama hii ya Imani au Imani maalumu, pale anapoanza kunena kwa lugha na kufasiri hiyo lugha.

Kwa sababu Mungu anatufahamu sana sisi watoto wake kuwa wengi wana Imani haba, ndipo anapotuma Imani hii maalumu ili kumsaidia mnenaji asiwe na shaka na kile anachokinena, hasa siku zile za kwanza za kunena kwa lugha. Kwani watu wengi kwa kuwa walizoea kunena kwa lugha walizozaliwa nazo na zile walizofundishwa, waanzapo kunena kwa lugha nyingine ngeni tena ghafla huwa wanaingiwa na mashaka, na hapo Mungu ndipo anapowatumia Imani maalumu yaani Karama ya Imani ili wasiwe na shaka waendelee kunena kwa hizo lugha mpya mpaka pale Imani zao za kawaida zitakapoongezeka au kukua, kwa kufundishwa somo linalohusu kunena kwao kwa lugha. Ikiwa wataelewa na kupokea mafundisho hayo katika neno la Bwana Yesu Kristo, basi Mungu hatakuwa na haja tena ya kuwatumia hao watu Karama hiyo ya Imani, kwani atakuwa amewaona kuwa Imani zao za kawaida zimekua na watu hao wamekuwa na uhakika kuwa Roho Mtakatifu ndiye anayewajalia waseme lugha hizo bila shaka. Hivyo ndivyo ilivyo Karama hii ya lugha inashirikiana pia na Karama nyingine kwa maana hiyo fahamu mtu aliye na Karama hii ya kunena kwa lugha pia huwa na Karama zingine pia, kama ya kufasiri lugha naya unabii pia ya Imani, ndiyo maana Bwana asema watoto wake hawajapungukiwa Karama yeyote ila tatizo lililopo ni hili la kutokujua habari hizi za karama za rohoni.

NAMNA UNAVYOTAKIWA UICHOCHEE KARAMA HII

Fahamu ndugu yangu kuwa, Mungu akisha kukupatia Karama hii ya kunena kwa lugha. Usifikiri kuwa atakaye ichochea ni Mungu. Fahamu ni wewe mwenyewe Neno la bwana linasema hivi **"kwa sababu hiyo nakumbusha uichochee Karama ya Mungu iliyo ndani yako…." (2Tim 1:6)** fahamu hata Karama hii ya lugha ni zinginezote anayetakiwa aichochee ni wewe uliyepewa Karama hiyo. Unatakiwa usijizuie au, usiaje kunena kwa lugha, watoto wa Mungu wengi sana hushindwa kuichochea Karama hii kwa sababu ya kuogopa, na kushindwa kufahamu kuwa wao ndio wanaotakiwa waliendeleze tendo hilo la kunena alilolianzisha Roho Mtakatifu ndani yao. Watoto wa Mungu wengi sana husubiri mpaka Mikutano ya Injili ije ndipo waanze kunena kwa lugha. Neno linasema kuwa unatakiwa uichochee Karama hii ya kunena kwa lugha, na fahamu ukiwa umejaa Roho Mtakatifu fahamu kila saa utakayo wewe unene kwa lugha utanena tu. Pia watu wengi wameshindwa kuyaelewa mafundisho ya Paulo katika kitabu cha **1 Kor 14**

yote; wengi wanafikiri Mtume Pulo alikuwa anakataza watu wasinene kwa lugha, bali alikuwa anatoa mwongozo mzuri wa namna watoto wa Mungu tunapokuwa wengi kwa wakati mmoja yatupasa tufanyeje! Neno la Bwana linasema hivi "**Basi ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja kila mmoja ana zaburi, ana fundisho ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri, mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga. Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri", (1 Kor 14:26-27)**

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Paulo alikuwa anafundisha namna watu wanavyotakiwa wanene wanapokuwa wamekutana pamoja. Na fahamu ndugu ya kuwa Paulo alikuwa hawazuii watu wengine wasinene bali alikuwa anatoa utaratibu wa namna watu wanapokuwa wamekutana pamoja basi wafanye kila jambo kwa utaratibu yaani wapangilie Ibada hiyo itakavyo kuwa. hebu ona mfano ikiwa leo umeingia sehemu umewakuta watu wengi wengine wananena kwa lugha, wengine humo humo wanaimba zaburi na wengine wanaimba tenzi na wengine wanafasiri na wengine wanafundisha wakati huo huo mmoja Je! Watu hao watakuwa wanajengana Kiroho kweli? Jibu ni hapana, bali kutakuwa ni vurugu tu ndio maana Mungu akaamua kuwafundisha hao ndugu kuwa wawe na utaratibu mzuri wa kusikilizana, yaani wakinena watu wawili au watatu wengine wasikilize na hao wanaosikiliza si kwamba hawana uwezo wa kunena, wanao, ila itawabidi watulie ili wawasikilize wenzao waliochaguliwa ili wanene. Zamu kwa zamu huo ndio utaratibu ambao Paulo aliwafundisha hao ndugu, kwani utagundua hao ndugu walikuwa na mashindano na kushindwa kuvitumia vizuri vipawa walivyopewa kwa kufaidiana. Paulo anasema katika **(1Kor 14:39) " kwa ajili ya hayo, ndugu takeni sana kuhutubu wala msizuie kunena kwa lugha".**

Neno linatufundisha tusijizuie au tusizuie watu kunena kwa lugha, kwa hiyo ndugu yangu unaouwezo wa kujizuia kunena na pia unao uwezo wa kujiachia unene hebu angalia upo sehemu gain, ni kwenye Ibada ambayo inatakiwa utulivu sana, na kuna utaratibu umewekwa wawatu wanene wawili tu, basi usinene kwa lugha. Basi hebu jiachie kwa kunena ndani kwa ndani inawezekana, kwani hata kusema unaweza ukaamua useme kwa kutoa sauti, au hata unaweza ukasema na mtu yoyote asisikie na sauti yako isitoe neno unalolisema, lakini wewe ukajua unasema nini. Pia hebu ukiwa peke yako kama ni nyumbani kwako, shambani n.k. ujiachie kwa sauti yako nena kila siku. Chochea hivyo Karama hii ya kunena kwa lugha. Kwa kufanya hivyo, pia fahamu Paulo alikuwa anasema mnene kwa utaratibu, hakuwa na maana kwa kutotoa sauti kubwa, alikuwa anataka watu wawe na mpangilio mzuri wa namna wanavyoweza kunena na kusikiliza mafundisho na mambo mengine wakiwa wamekusanyika pamoja. Watu wengine wamefikiri kuwa mtu anaponena ni lazima anene kwa kutokutoa sauti. Siyo hivyo ona mifano hii katika Biblia inavyosema.

Fungua (**MDO 10:45) " na wale waliotahiliwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu:.**

Fahamu watu hao siku ile walipopokea Karama hii ya kunena kwa lugha walinena kwa sauti, kwani watu wengine waliwasikia wakiyatamka yale maneno mapya toka vinywani mwao, kwa hiyo si kwamba unenapo usitoe sauti. Bali unatakiwa usikike. Ila itategemea upo katika mazingira gani. Siyo upo Polisi unaanza kunena kwa sauti kubwa, bali ukiwa

katika eneo kama hilo nena kwa ndani Mungu atasikia tu. Neno linasema hivi **"na itakuwa ya kwamba kabla hawajaomba nitajibu; na wakiwa katika kunena, nitasikia" (Isaya 65:24).**

Mungu anauweza wa kukujibu hata kabla haujanena. Kwa hiyo fahamu Mungu anataka pia unene kwa kutoa sauti yako ili aisikie, kumbuka kina Petro pia siku ile ya Pentekosti neno linasema wote walinena kwa lugha hakukuwa na utaratibu wa kunena sawasawa nailivyotokea siku ile kwa Kornelio wote walinena, kwa hiyo kimsingi inategemea mazingira uliyopo ni ya namna gani. Je! Yanakuruhusu unene au umsikilize mwenzio anene, na fahamu pia lugha hizi zinatofautiana, zipo lugha mpya za ibada na kuna lugha za maombi, sasa ikiwa wote tumeambiwa tuombe basi usiogope kuomba kwa lugha. Nena kwa sauti kwani wakati huo ni wakati wa kuomba na wote kwa pamoja tumepatana kuomba, basi ukiwa katika mazingira hayo basi usiache kuomba kwa kunena kwa lugha. Mungu akusaidie katika kuichochea Karama hii

KUIJENGA NAFSI YAKO

Watu wengi wamekuwa na mawazo kuwa neno linasema kuwa **"maana yeye ahutubuye ni Mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha isipokuwa afasiri, ili kusudi Kanisa lipate kujengwa" (1 Kor 14:5B)** ndivyo neno la Mungu linavyosema, ya kwamba tunatakiwa sana kama watumishi wa Mungu tupate kuwambia watu maneno ya Mungu, kwa lugha inayoeleweka, ili wapate kujengwa. Na watumishi wengi sana wa Mungu kwa kuwa neno limesema hivyo huwa wana idharau sana Karama hii na wengi wametafuta sana kuhutubu kuliko kunena kwa lugha, ni vizuri kwani neno linasisitiza sana kuwa tunatakiwa tutake sana kuhutubu. **"kwa ajili ya hayo ndugu, takeni sana kuhutubu …." (1Kor 14:39).**

Neno la Mungu linatuhimiza tutake sana tuhutubu na watumishi wengi sana wamelishika sana neno hili wako tayari kwenda sehemu yeyote ile saa yoyote ile wakahutubu na wengi hawaoni haja ya kutaka pia Karama hii ya lugha. Fahamu mambo haya mawili lazima yaende pamoja, watumishi wengi hawaumalizii mstari huo wa 39 unasema hivi **"wala msizuie kunena kwa lugha" (1Kor 14:39)**

Fahamu ndugu yangu ya kuwa Mungu anakutaka wewe uende ukalijenge kanisa lake lakini fahamu kabla hajakutuma uende ukalijenge Kanisa lake anataka akujenge wewe kwanza nafsini mwako, au moyoni mwako. Watumishi wengi sana wapo kwenye hatari hii, wengi wanajituma sana kuwajenga wengine ila wao wamejisahau kuwa Mungu anataka kuwajenga pia. Tena wao ndio wanatakiwa wajengwe kwanza ndipo waende kujenga wengine

Neno la Bwana linasema hivi **"maana yeye anenaye kwa lugha hasemi na watu, bali husema na Mungu, maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri ya Roho yake. Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga Kanisa" (1Kor 14:2-4)**

Neno la Bwana linatufundisha kuwa, mtu anenaye kwa lugha **"anajijenga nafsi yake"** fahamu ndugu yangu kuwa Mungu aliona jinsi nafsi nyingi za watumishi wake zilivyo na matatizo mengi sana, na ya kuwa tangu ujana wa mwanadamu nafsi au moyo wa mwanadamu kuna mawazo mengi mabaya na tena ndani ya moyo wa mwanadamu mara

nyingi sana huwa kuna ugonjwa wa kufisha. **(Yeremia 17:9-10) "moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Mimi Bwana, nauchunguza moyo, navijaribu viono hata kumpa kila mtu kiasi cha njia zake, kiasi cha matunda ya matendo yake"**

Mungu anatufundisha kuwa mioyo ya watu wake wengi inamatatizo mabaya ya kuwaza na kuenenda katika njia mbaya zisizo mpendeza Mungu na mwisho wake ni kuangukia katika hukumu mbaya ya mauti. Fahamu ndugu kuwa ndani ya moyo au kwa lugha nyingine nafsi ndiko kunakotoka mambo yote yaliyo mabaya, Bwana Yesu anatufundisha kutoka kitabu cha **(Mathayo 15:19) "kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wivu, ushuhuda wa uongo na matukano.**

Katika nafsi ya mwanadamu ndimo mambo hayo maovu yanakotokea, ambayo ndiyo machukizo kwa Mungu. hebu angalia jinsi watoto na watumishi wa Mungu wengi walivyo utagundua wengi sana nafsi zao bado hazijajengwa vizuri ndio maana wengine wamekuwa na tabia ambazo ni mbaya mno wanaushuhuda wa uongo wazinzi, waizi yaani (hawatoi zaka) wanawaziana mabaya wao kwa wao, hawana Upendo wa kweli, wengi wametengana na wakristo wenzao kwa sababu za udanganyifu wa mioyo yao, kwa kweli nafsi isipojengwa vizuri na Bwana hata huduma uliyonayo itakuwa na unajisi mwingi sana, haitakubalika mbele za watu hata mbele za Mungu, mara nyingi utahudumu kwa akili zako na utatoka tu kwenye mipango ya Mungu aliyoipanga katika huduma yako.

Mungu aliliona tatizo hilo tulilonalo, ndio maana akaamua kutuletea Karama hii ya kunena kwa lugha ili apate kutujenga nafsini mwetu. Sasa kwa sababu watumishi wengi hawafahamu habari hizi za Karama za rohoni wengi wamekimbilia sana kuhutubu wakati kwanza walitakiwa wajengwe ndani ya nafsi zao ndipo waende kuhutubu.

Fahamu bila kujengwa nafsini mwako na Bwana ni rahisi sana kufanya huduma iliyojaa mapokeo yaani maagizo ya wanadamu na pia ukafundisha mafundisho yasiyopatana na neno la Mungu. Mfalme Daudi alilifahamu jambo hili, akamwomba sana Mungu amjenge ndani ya nafsi yake, Soma. **(ZAB 119:25) "Nafsi yangu imeambatana na mavumbi, Unihuishe sawasawa na neno lako".Soma na, (ZAB 199:28-29) nafsi yangu imeyeyuka kwa uzito, unitie nguvu sawasawa na neno lako. Uniondolee njia ya uongo, unineemeshe kwa sheria yako.**

Mfalme Daudi alifahamu wazi kuwa nafsi yake imeambatana na mavumbi yaani mwili, na kumbuka mambo ya mwili ni yaleyote yaliyo maovu, kama uchafu, uchawi, uzinzi, matukano mawazo mabaya, wivu, husuda, uchoyo, matukano, hasira uongo n.k. mfalme Daudi aliafhamu kuwa ni rahisi sana kwake kuiamini njia ya uongo kuliko ya kweli, ndio maana akaamua kufanya maombi maalum kwa Mungu ili apate kumjenga nafsini mwake, fahamu ili nafsi ijengwe lazima neno la Mungu liingie ndani yako hapo ndipo nafsi ya mtu yoyote ile itakuwa imejengwa.

Sasa basi ndugu kumbe ili ukajenge Kanisa au kuliongoza vema ni lazima nafsi yako ijengwe kisawasawa, ishibe neno la Mungu kweli, ndipo hapo Mungu atakutuma uende kuhutubu. Fahamu mfalme Daudi alifahamu kuwa nafsi yake ilikuwa imeyeyuka kwa uzito, au ilikata tamaa kwa magumu mbalimbali, akaenda kwa Mungu na kumwomba aitiye nguvu ili asikate tamaa, sasa ukiwatazama watu wengi waliookoka nafsi zao zimechoka

sana, kwa sababu ya magumu mengi wanayokutana nayo ndio maana maombi yao ya siku za nyuma na sasa hivi hayako sawa, sasa hivi wanachoka haraka, hata nguvu ya kukataa dhambi ya sasa ni tofauti na zamani, hawana nguvu, nafsi zao zimeyeyuka, kabisa. Sasa Mungu ili atujenge ndani ya nafsi zetu, ndio maana akaamua kutuletea Karama hii ya lugha ili kila siku apate kutuhuisha na kutujenga ndani yetu ili tupate kulielewa neno lake pia na kuyajua mapenzi yake yote aliyotukusudia na kututenga na njia za uongo. Fahamu ikiwa unataka kuhutubu vizuri basi itake Karama hii kwa Mungu kama unayo basi ichochee wewe mwenyewe kwa kunena mara kwa mara.

Fahamu ukiwa unanena mara kwa mara ndipo Mungu anapokujenga vizuri ndani yako, na kukutengenezea ndani yako kiu ya kulisoma neno lake pia hata kukuwezesha kulielewa na kulishika neno la Bwana, fahamu Neno la Bwana linatufundisha kuwa **" Awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, kwa Yesu kristo;utukufu una yeye milele na milele, Amina" (EBR 13:21).**

Mungu yeye ndiye anayetufanya tuwe wakamilifu, wala siyo sisi tunaojifanya kuwa wakamilifu, kwa hiyo basi Mungu ili atufanye sisi kuwa wakamilifu ndio maana akatuletea karama hiiya kunena kwa lugha ili apate kutukamilisha au kutujenga ndani ya nafsi zetu, Kwa hiyo ndugu uliyepewa karama hii usifikilie kuwa umepewa karama hii kama pambo la wokovu tu, bali Mungu kakupatia karama hii ili apate kukujenga ndani ya nafsi yako, ambako uko kuna Hisia, Akili, na Utashi, sasa ili akili zako zipate kujengwa katika Bwana vizuri unatakiwa uitumie vema karama hii, au uweke bidii katika kunena kwa lugha, ukiichochea na ukiitumia vizuri fahamu Mungu atazijenga Hisia zako na fikira zako kila wakati zitafikili kama Mungu anavyotaka zifikili, pia Utashi wako utayafanya mambo ya Roho kwa uzuri sana. Kwa hiyo ndugu yangu fahamu kwa kupitia karama hii ya kunena kwa lugha, unaweza kupata faida nyingi sana kiroho, moja ya faida hizo ni hii ya kujengwa wewe mwenyewe ndani ya nafsi yako na Bwana,

Kwa hiyo basi, kama unataka huduma yako ya kuhutubu iwe nzuri unatakiwa kama mtumishi wa Mungu ujengwe wewe mwenyewe kwanza vizuri ndani ya nafsi yako, ndipo uende kuhudumia watoto wa Mungu, kwa kuwahubilia au kuwafundisha pia kuwa chunga kwa uzuri kabisa.Mungu anataka kuwajenga watoto wake ndani ya nafsi zao ili wawe na nafsi nzuri sana, lakini, watoto wake wengi hawazijui mbinu ambazo Mungu ana zitumia katika kuwajenga, na ndio maana wengi wao walipopewa karama hii ya lugha huwa hawaitumii vizuri, ndio maana hawaichochei karama hii, wengi baada ya kupokea karama hii wameitumia kwa kujionyesha kuwa wao wamekuwa kiroho kwa kuwa tambia wenzao ambao bado hawaja pokea karama hii ya kunena kwa lugha, pia wengi huwa hawaneni mara kwa mara, huwa wanasubiri mapaka ije mikutano ya lnjili na ndipo wanene kwa lugha au mpaka siku za maombi kwenye vikundi vyao vya maombi, fahamu neno hili ndugu yangu kuwa unatakiwa unene kwa lugha mara kwa mara, uwapo nyumbani kwako, hata ofisini kwako, unaposafiri nk, Unaweza kunena ndani kwa ndani hata mtu asikusikie hata kufahamu kuwa unanena kwa lugha, jizoeze kila mara kunena bila kutoa sauti, fahamu Mungu atakujenga kila mara ndani ya nafsi yako, na utaona mabadiliko makubwa katika maisha yako ya kiroho.Pia wako watoto wengine wa Mungu hawana haja ya kuwa na karama hii, wameridhika na hari waliyo nayo, fahamu ndugu yangu kuwa Mungu ana taka kukujenga vizuri ndani ya nafsi yako tokea siku ile ulipookoka, ana nia ya kukujenga mpaka ufikie ukamilifu ule au takao yeye, kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa uwe na kiu au haja ya kuihitaji karama hii, Neno la Bwana lina sema hivi, **"Ufuateni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, …" (1KOR 12:1).**

Weka bidii ya kuitaka sana karama hii ya kunena kwa lugha ili Mungu apate kukujenga vema ndani ya nafsi au moyo wako, tafuta sana kuhutubu, pia tafuta sana kujengwa wewe kwaza na Bwana kabla ya kwenda kuhutubu, Ukifanya hivyo fahamu huduma yako itakuwa ni ya mafanikio sana. Ichochee karama hii kwa kunena mara kwa mara, ikiwa huna karama hii usichoke kumuomba Bwana ili akupatie.

SABABU NYINGINE YA MUNGU KUTULETEA KARAMA HII YA LUGHA

Baada ya kujifunza kwa sehemu jinsi karama hii ya lugha inavyotumika katika kutujenga ndani ya nafsi zetu pia kunafaida nyingine nyingi nzuri ambazo tunazipata katika karama hii ya kunena kwa lugha, Ebu, tuziangalie faida hizo.

Neno la Mungu linatufundisha kuwa karama hii ya lugha licha ya kutumika katika kutusaidia kwa kutujenga ndani ya nafsi zetu, pia karama hii ya lugha ina tusaidia sisi kwa kuyafanya kwa uzuri mambo mengine mawili muhimu yafuatayo,

Jambo la kwanza: Jambo la kwanza ambalo karama hii ya lugha ina shughulika nalo ni Kutuwezesha sisi watoto wa Mungu kumuabudu Mungu na kumwadhimisha au kumsifu na kumshukuru kwa uzuri sana.

Jambo la pili: Jambo la pili ambalo karama hii ya lugha ina shughulika nalo ni kutuwezesha kumuomba Mungu kwa uzuri tena bila ya kuchoka.

Mambo hayo mawili muhimu ndiyo tunayapata ndani ya karama hii ya kunena kwa lugha, Baba Mungu ametupatia karama hii ya lugha ili kutuwezesha kumwomba Mungu kwa uzuri pia katupatia karama hii ili tupate kumwadhimisha au kwa lugha nyingine kumtukuza Mungu wetu kwa uzuri sana, kama ilivyoandikwa kuwa tunapaswa kumuomba Mungu bila kukoma na tunatakiwa tumtukuze Mungu na kumwabudu yeye peke yake, basi ili tuyafanye mambo hayo mawili kwa uzuri Mungu akaamua kutuletea karama hii ya lugha ili kutusaidia katika maombi yetu kwa Mungu, na kutusaidia katika kumtukuza Mungu wetu siku zote za maisha yetu, hebu tujifunze kwa upana jinsi karama hii inavyofanya kazi katika sehemu hizi mbili, tuanzie na sehemu ya kumwadhimisha Mungu na kumwabudu kwa uzuri.

SEHEMU YA LUGHA ZA IBADA NA SIFA

Fahamu mimi na wewe kama watoto wa Mungu tumeumbwa na Mungu ili tupate kumwabudu na kumtukuza yeye peke yake, Bwana wetu Yesu Kristo ana tufundisha katika neno lake hivi **" Yesu akajibu akamwambia, Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, Umwabudu yeye peke yake" (LUKA 4:8);** Bwana Yesu ana tufundisha hapo kuwa tunatakiwa katika maisha yetu yote tumwabudu Mungu na kumsujudia yeye peke yake, na hayo ndiyo mapenzi ya Mungu ambayo anataka watoto wake tuyafanye, fahamu tumeumbwa na Mungu ili tupate kumwabudu na tumtukuze, na huo ndio mpango wake mkubwa wa kutuumba sisi wanadamu, neno la Bwana linasema hivi **"Akaniambia; Wewe ni mtumishi wangu, Israeli, ambaye katika wewe nitatukuzwa" (ISAYA 49:3)**

Fahamu ndugu yangu kuwa Mungu anachotafuta kwa watoto wake ni kutukuzwa, ikiwa wewe ni mtoto wa Mungu ambaye umeokoka na kumpa Yesu Maisha yako, Mungu

anataka atukuzwe kupitia wewe, kuna namna nyingi sana za kumtukuza Mungu, tunatakiwa tumtukuze Mungu wetu kwa kumwimbia, kwa kumtukuza kwa kuyasema matendo makuu ya Mungu, kuwa watu waushuhuda mzuri mbele za watu wengine, kwa kumchezea na kumshangilia, pia kwa kumwabudu, nk, Bwana anatafuta watu wanamna hiyo, watu wanao mwabudu Mungu katika roho na kweli, **"Lakini saa inakuja, nayo ipo, ambayo waabuduo harisi watamwabudu Mungu katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu"(YOHANA 4:23),**

Fahamu Mungu alituumba kwa kusudi hilo la sisi tupate kumwabudu yeye, na Mungu leo hii anawatafuta watu kama hao, wale ambao wana mwabudu katika roho na kwa ukweli kabisa au kwa lugha nyingine kwa uaminifu kabisa, na fahamu leo hii watu wanamna hiyo wapo, Bwana Yesu ana sema **"Lakini saa inakuja nayo ipo, ambayo waabudio harisi watamwabudu Mungu katika roho na kweli" Bwana alisema saa itakuja, na sasa ipo ambayo watu watamwabudu Mungu kwa uzuri kabisa ndani ya roho zao, na saa hiyo ilianzia siku ile ya Pentekosti, siku ambayo wanafunzi wa Yesu Kristo walipompokea Roho mtakatifu na karama zake, na moja ya karama waliyoipokea siku ile ilikuwa ni hii ya kumwabudu Mungu kwa uharisi na kumwadhimisha Mungu kwa kunena kwa lugha, neno la Bwana linasema hivi "Na walikuwako Yerusalemu wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe.wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, wote wasemao si Wagalilaya?Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Warparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na pamfilia, Misri na pande za Libia karibu na kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu; tuna wasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu. Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, maana yake nini mambo haya?"(MDO 2:5-12).**

Siku ile wanafunzi walipompokea Roho mtakatifu walikuwa wananena kwa lugha ambazo zilisikika kwa watu wa mataifa mbalimbali waliokuwa Yerusalemu siku ile, na waliyokuwa wanayasema hao wanafunzi ni matendo makuu au sifa za Mungu, karama hii ilikuwa ikiwawezesha wanafunzi wa Yesu siku ile kumtukuza Mungu pasipo hata wanafunzi kujua wanachokifanya, siku ile Mungu alilidhibitisha neno alilolitabiri Bwana Yesu kuwa saa ina kuja ambayo waabudio harisi watamwabudu Mungu katika roho zao, sasa wanafunzi siku ile, roho zao zilimwadhimisha Mungu na kumtukuza walipokuwa wananena kwa lugha. Na maneno yao yalikuwa si ya kumwomba Mungu, bali yalikuwa ni ya kumtukuza Mungu, kwa hiyo utaona kuwa karama hii ya lugha Mungu ametupatia ili roho zetu zipate kumwabudu Mungu kwa uharisi, kama atakavyo yeye Bwana.

Fahamu tendo hili la kumwabudu na kumwadhimisha Mungu kwa lugha si tendo la kawaida, ni tendo la Kimungu, yaani Roho mtakatifu ndiye anayeiwezesha roho ya mtu katika kumwabudu na kumsifu Mungu, wala si kwa ujuzi wa huyo mtu au akili zake, bali ni kwa uweza wa Roho mtakatifu ambao anakuwa ameuweka katika ulimi wa huyo mtu ili apate kumtukuza Mungu, kwa hiyo ndugu unatakiwa ufahamu kuwa unaponena kwa lugha wakati mwingine huwa una mtukuza na kumshukuru Mungu pasipo hata wewe kujua kuwa unamtukuza Mungu, Wakristo wengi hawalifahamu hili, wengi wana changanya mambo, wanafikili tendo la kunena kwa lugha ni la kumwomba Mungu tu, fahamu wakati mwingine karama hii inatumika katika kumwabudu Mungu kwa kumsifu na kumshukuru

kwa sifa zake zote, na anayetuwezesha katika kumtukuza Mungu ni Roho mtakatifu, na atakusaidia kwa kukuletea yeye sifa harisi za Mungu kuliko sifa zile akili zako zinazozijua, na fahamu roho yako ndiyo inayo mwabudu Mungu, na hizi zinaitwa karama za rohoni, yaani ni zawadi ambazo roho yako imepewa na Mungu katika mambo ya rohoni, na karama hii ya lugha ni zawadi tuyopewa na Mungu ili kuzisaidia roho zetu katika kumwabudu Mungu kwa uharisi kabisa,

Una weza ukajiuliza je! Kulikuwa na haja gani ya Mungu kutusaidia sisi katika suala hili la kumsifu yeye Mungu? Fahamu Mungu siku ya kwanza kabisa aliyomuumba mwanadamu alimuumba mwanadamu akiwa mkamilifu kabisa, na alimuumba kwa kusudi la mwanadamu apate kumwabudu na kumtukuza Mungu, sasa dhambi ilipo mwingia mwanadamu ile hali ya kumwabudu Mungu kwa kweli na kwa uharisi ilimtoka mwanadamu, na roho ya mwanadamu ilishindwa kumwabudu Mungu na kumtukuza kama ilivyokuwa mwanzo wa kuumbwa kwake, na fahamu baada ya Bwana Yesu kuja alisema wazi kuwa saa inakuja ambayo watu watamwabudu Mungu tena kwa uzuri, na saa yenyewe ilitimia pale Bwana wetuYesu kristo alipo tukomboa kwa damu yake ya dhamani ambayo ilituondolea ule uadui tuliokuwa nao na Mungu, na kutulejeshea tena uwezo ule tulioupoteza wa kumwabudu Mungu ambao roho zetu ziliupoteza, kwani neno la Bwana linasema wazi kuwa **"Kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu:" (RUM 3:23)**

Dhambi ilipotuingia wanadamu utukufu wote wa Mungu aliotutia ulipunguka, yaani ule wasisi kumwabudu Mungu, na ule Mungu aliotutukuza sisi, na baada ya ukombozi tulioupata kupitia Bwana Yesu Kristo Mungu aliamua kuturudishia ule utukufu, na ndipo alipoamua kutulete hata zawadi hii ya kutusaidia sisi katika kumtukuza Mungu, Kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa Mungu ametulea karama hii ili kutusaidia katika kumtukuza Mungu, kwani kwa akili zetu hatuwezi kutukuza ipasavyo, kwa msaada wake katika karama hii ya lugha za ibada wanadamu tunakuwa tunamwabudu na kumtukuza Mungu kwa uharisi kabisa, Watoto wa Mungu wengi sana wanapokuwa wananena kwa Lugha na kumtukuza Mungu, huwa hawabarikiwi sana, kwa kuwa akili zao hazifahamu kitu katika maneno wanayo yatamka, na wengi huwa wanayakata maneno hayo na kuanza kumtukuza Mungu kwa lugha wanayoifahamu. wakiona kuwa kwa kufanya hivyo ndiyo bora zaidi kuliko kunena kwa lugha mpya, Sikia ndugu yangu mpendwa kwa ujumla akili zetu sisi wanadamu Mungu amezikataa, **" Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, Na akili zao wenye akili nitazikataa" (1KOR 1:19).**

Akili zetu zinapo mtukuza Mungu na kumwadhimisha ni tofauti na karama ya Lugha inapotumika katika kumtukuza na kumwadhimisha Mungu, **"Nakumbuka Nilipookoka nilikuwa na kawaida ya kumtukuza Mungu kila siku kwa kumwimbia na kuyasema matendo yake ya ajabu, na kwa ujumla kila siku nilikuwa na imba nyimbo zilezile na kusema matendo makuu ya Mungu yaleyale, sasa siku Mungu aliponipatia karama hii ya lugha na kunifundisha kuhusu karama hii ya lugha inavyo fanya kazi hasa katika sehemu hii ya Lugha za ibada na kumsifu Mungu, nilianza kumsifu Mungu kwa kunena kwa Lugha mara kwa mara, pia nilipomwomba Mungu anipatie kipawa chake cha kufasiri hiyo lugha, ndipo nilipogundua tofauti kubwa ya kumtukuza Mungu kwa akil ina kumtukuza Mungu kwa lugha, kwani nilipo fasiriwa niliona au nilipataufahamu kuwa siku hiyonilimsifu Mungu kwa sifa amabazo akili zangu haziku fahamu kabisa, tena niliimba nyimbo nyingi sana ambazo maneno**

yake yalikuwa yana upako na mazuri zaidi ya yale yaliyo katika nyimbo zile nilizozizoea kuziimba kwa akili, Tokea siku ile nikajifunza kuwa kwa akili zangu siwezi kumtukuza na kumsifu Mungu kwa uharisi, bali kwa roho ndipo ninapo mtukuza Mungu kwa uharisi zaidi",

Kwa kuwa Mungu anapenda tumtukuze kwa uzuri zaidi ndi omaana akatuletea watoto wake karama hii ya lugha, na anachotaka ni kutuona sisi watoto wake tulioipokea karama hii tukiichoche na kuitumia kwa uzuri sana, na wale wasio na karama hii waende kwake na kumwomba awapatie, ili **wamwabudu** Mungu kwa uharisi zaidi.

KUIMBA KWA LUGHA

Fahamu ukiwa na karama hii unaweza kila saa kumtukuza Mungu kwa uzuri sana, una weza kila saa kumvuta Mungu iliawepamoja na wewe kila wakati, Bwana Yesu ana tufundisha wazi kuwa Mungu huwatafuta watu wamwabuduo katika roho, sasa hebu ichochee karama hii kwa kuziimba nyimbo za kumwabudu Mungu kwa roho, au kwa lugha ambayo Roho mtakatifu amekujaria uitamke ili umwabudu Mungu, imba kila wakati kwa lugha utaona badiliko kubwa sana ndani ya moyo wako, na kila wakati Mungu atakutafuta wala si wewe utakae mtafuta, kwani Mungu huwatafuta watu wanaomwabudu kwa roho, watu waliowaaminifu, Mtume Paulo ana sema kuwa ataimba kwa roho yaani kwa lugha na ataimba kwa akili yaani hali ya kawaida baada ya kufasiri yale aliyoyaimba kwa roho, hebu soma (**1KOR 14:13-15**); **" Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri.maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili"**

Sasa ili upate kumwimbia Mungu kwa uzuri unatakiwa uimbe kwa roho mara kwa mara, na inawezekana kabisa kila wakati ukiamua wewe kumwimbia Mungu kwa lugha unaweza kumuimbia, unaweza ukaimba nyumbani kwako au katika safari yako au hata ofisini kwako nk, unaweza ukaimba kwa kutoa sauti ya chini, unaweza ukaimba kwa kutoa sauti ya kati au ya juu sana, pia unaweza ukaimba kwa kutokutoa sauti kabisa, yaani ukaimba ndani kwa ndani humo moyoni mwako, na Mungu akakusikia kabisa, na baada ya kuimba kwa roho hebu mwombe roho mtakatifu akupe kufasiri, utashangaa utakapoanza kuimba kwa akili utaona jinsi ulivyo mwimbia Mungu nyimbo zilizo nzuri sana na za kupendeza sana, tena nyimbo mpya kabisa usizo zifahamu, unachotakiwa ukifanye ni kuondoa mashaka tu, hebu anza kuimba tamka maneno hayo atakayokupatia bila hofu, sikiliza ana taka useme maneno au anataka uimbe, ikiwa anakuletea kwa mtililiko wa kuimba basi pokea, anza kuimba, imba kwa mtililiko anaoutaka anayo kuletea anza kuimba pole pole kama mwanafunzi, na ukiisha ufahamu huo wimbo imba kwa uhakika bila hofu, na baada ya kuimba kwa roho omba upewe kufasiri, na Bwana atakupatia karama hii ya kufasiri lugha na hapo ndipo utakapopata ufahamu wa namna ulivyo mtukuza Mungu wako katika nyimbo ulizokuwa unaziimba kwa lugha, au kwa maneno yote uliyomwadhimisha Mungu katika roho.

Karama hii inatusaidia sana wakati tuwapo katika wakati wa kumwimbia Mungu nyimbo za kumwabudu, watoto wa Mungu wengi sana ndani ya nafsi zao au mioyoni mwao wanapokuwa wamezama katika kumwabudu Mungu kwa akili zao huwa wanapata shida sana ya kuendelea kumwabudu Mungu, na sababu kubwa inayo wafanya washindwe kumwabudu Mungu ni pale nafsi zao zinapo anza kupiga kelele, kwa kuwa kumbusha

shida zao au magumu mengi waliyonayo au dhambi zao walizozitenda zamani na tena walizitubia zamani lakini wawapo kwenye sehemu hiyo ya utulivu na hukuwakiwa wanamwabudu Mungu kwa kumwimbia hapo ndipo wengi akili zao huanza kukumbuka mambo hayo yote, na matokeo yake ni kushindwa kuendelea kuimba na wengi huanza kulia au kutubu dhambi ambazo walizitubia zamani, na Bwana aliwasamehe kabisa na alizisahau kabisa, hivyo ndivyo watoto wa Mungu wengi walivyo, Bwana Mungu analifahamu sana tatizo hili ulilonalo wewe mtoto wake, ndio maana akamua kutuletea msaada kwa kutuwezesha sisi tumwabudu pasipo hofu yoyote ile mioyoni mwetu kwa kutuletea karama hii ya lugha, kwani mtu yeyote yule anenaye kwa lugha anapokuwa anamwabudu Mungu akili yake huwa haielewi kitu chochote kile, huwa nivigumu sana kutolewa nje ya tendo la kumwabudu Mungu mtu akiwa ana mwabudu Mungu kwa lugha mpya, labda mtu huyo asijue kuwa anayoyasema ni maneno mazuri ya kumwadhimisha na kumtukuza Mungu, watoto wa Mungu wengi kwa sababu ya hofu tu ndio huwa wana nena kidogo tu na kuacha, sikia Bwana anataka tumwabudu pasipo hofu kabisa. Neno la Mungu lina sema katika **(LUKA 2:73-75) " Uapo aliomwapia Ibrahimu, baba yetu, Ya kwamba atatujalia sisi, Tuokoke mikononi mwa adui zetu, Nakumwabudu pasipo hofu, kwa utakatifu na kwa haki mbele zake siku zetu zote".**

Huo ndio uapo ambao Mungu aliuapa wa kutuwezesha watoto wake tupate kumwabudu yeye kwa utakatifu tena bila kuwa na hofu katika maisha yetu yote ya kiroho, huo ndio mpango wa Mungu kwa watoto wake wote, yaani watu wale waliookoka, Mungu hapendi tumwabudu kwa hofu, anataka watoto wake tuwapo katika kumsifu na kumtukuza tumtukuze na tumwimbie nyimbo za kumwabudu pasipo hofu kabisa, na ili uapo huo apate kuutimiza ndio maana akatuletea karama hii ili tupate kumsifu na tumwimbie Mungu kwa lugha za mbinguni yaani za Malaika na za kibinadamu ili akili zetu zisiwe na kitu chochote chakutuchomekea kwa kutukumbusha mambo yale ya kutuletea hofu, nakutufanya tuache kumwabudu Mungu na kutuingiza kulia pasipo sababu, kwa hiyo ndugu yangu hebu weka bidii ya kumwimbia Mungu kwa lugha, na usiogope kabisa, akili yako inaweza kufikili kuwa kwa kufanya hivyo una kuwa unakosea na kukuletea mawazo ya kukutaka umwabudu Mungu kwa akili, hebu usiisikilize akil iyako, hebu jikabidhi katika mikono ya Roho Mtakatifu, na endelea kusema au kuimba kwa lugha hiyo anayokuletea Roho Mtakatifu na endelea kumwabudu Mungu bila hofu yeyote ile, usiogope kabisa, kumbuka tunao ujasili wa kuingia patakatifu pa Mungu kwa Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo Neno la Bwana lina sema hivi.

"Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani mwili wake; na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyuziwa mioyo tuache dhamiri mbaya; tumeoshwa miili kwa maji safi".(EBR 10;19-22). Hivyo ndivyo tunavyo takiwa tumkaribie Mungu wetu, kwa ujasiri kabisa kwani damu yake ndiyo inayo tusafisha na kutuondolea dhambi zetu na makosa yetu yote, na tunatakiwa tuwe na imani yaani uhakika kabisa ya kuwa tumesamehewa na tunakibari cha kumkaribia Mungu, na pia tunatakiwa tuache dhamri au nia mbaya, na tuwena nia njema na ukiwa msafi mwilini na moyoni, fahamu ukiyafanya hayo huna haja ya kuogopa kitu chochote kile, Bwana yuko karibu na wewe mwabudu acha kufikilia shida zako mfikirie yeye kuwa anazijua shida zako kuliko wewe unavyozijua mwabudu na msifu na mtukuze pia mshukuru kwa roho yaani kwa lugha, ndipo atakapokusikia na kukutimizia mahitaji yako yote, kwani utakuwa umemfurahisha kwa kumwadhimisha mno.

Kumbuka karama ni utendaji kazi wa Mungu kupitia mtu yule ambaye amechaguliwa na Mungu, ni tendo lile ambalo Mungu anakuwa anafanya kazi furani moja kwa moja tokea mbinguni akimtumia huyo mtu, tendo hilo ndilo liitwalo karama, na hata karama hii ya kunena kwa lugha Mungu ndiye anayeimba akiwa ndani ya mtu huyo, Neno la Bwana **lina tufundisha kuwa Yesu yupo pamoja na watoto wa Mungu ili apate kumsifu Mungu (EBR 2 :9-13) " Ila twamuona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu. Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja, kwa ajilihii haoni haya kuwaita ndugu zake; akisema Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu;katikati ya kanisa nitakuimbia sifa Na tena Nitakuwa nimemtumaini yeye Na tena, Tazama, mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu"**

Fahamu ndugu yangu kuwa Bwana Yesu yuko katikati ya kanisa yaani ndani ya mioyo ya watoto wa Mungu, na fahamu akiwa katikati ya watoto wa Mungu huwa anamsifu Mungu, na leo hii Yesu ndiye anayemtukuza Mungu akiwa ndani Yetu kwa kutumia hiyo karama ya lugha, kwani si kwa akili zetu ndio tunainena hiyo lugha, bali ni kwa nguvu za Roho Mtakatifu tu. Fahamu Yesu kila siku ana nia hiyo ya kumwimbia Mungu, sasa anakutegemea wewe ndugu umpatie nafasi, na nipale unapo kuwa una mwimbia Mungu kwa lugha na kumwadhimisha Mungu kwa lugha fahamu unakuwa unashilikiana kabisa na Bwana Yesu katika kumwimbia Mungu na kumtukuza Mungu, hebu pata kiu hii ya kushirikiana na Bwana Yesu Kristo katika kumwimbia na kumtukuza Mungu, fahamu wewe ni sawa na redio, ambayo mtangazaji yuko mbali sana, ila mawimbi ya sauti yake huingia redioni ukiifunguli tu, sauti yake usikika, fahamu sisi ni sawa na redio, Yesu yuko hewani akimtukuza Mungu, anachokitaka ni wewe ufungue kinywa chako ili sauti ya maneno ya kumsifu Mungu yatokayo kwa Roho Mtakatifu yasikike kinywani mwako, na hilo ndilo analolihitaji Mungu ulifanye kila siku katika maisha yako yote. Kama huna karama hii basi mwombe Mungu akupatie, ukiwa unayo basi hebu ichochee kwa kunena kwa lugha mara kwa mara.

Neno la Bwana linatufundisha kuwa Mfalme Daudi alikuwa hodari sana wa kuimba na kutunga nyimbo za kumtukuza na kumwabudu Mungu, lakini ukusoma maandiko matakatifu ya Mungu utagundua kuwa Mfalme Daudi alikuwa na karama maalumu aliyopewa na Bwana, Mfalme Daudi anasema hivi **"Basi haya ndiyo maneno ya mwisho ya Daudi, mwana wa Yese, anena, Anena huyo mtu aliyeinuliwa juu, Yeye, masihi* wake Mungu wa Yakobo, Mtungaji wa nyimbo za Israeli mwenye kupendeza; Roho ya Bwana ilinena ndani yangu, Na neno lake likawa ulimini mwangu"(2 SAMWELI 23: 1-2).** Maneno hayo ya Bwana yanatufundisha kuwa Mfalme Daudi alikuwa akiziimba nyimbo katika ulimi wake ambazo Roho Mtakatifu alikuwa akizinena ndani yake, kazi aliyokuwa anaifanya Mfalme Daudi ilikuwa ni kuyanena yale maneno yaliyo semwa katika ulimi wake, pia kazi nyingine aliyokuwa anaifanya ilikuwa ni kuziandika hizo nyimbo alizokuwa anazipokea kutoka kwa Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani yake, Sasa ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Mfalme Daudi alikuwa na karama au kitu maalumu toka kwa Mungu kilichomuwezesha kumwimbia na kutunga nyimbo za kumwabudu na kumsifu Mungu, Kwa leo hii tunaona kuwa hiyo ilikuwa ni

karama iliyowekwa katika ulimi, nayo ni karama hii ya lugha, ambayo ndani yake kuna huduma ya kumwadhimisha Mungu.

Leo hii watoto wa Mungu wengi sana wanapenda sana kumwimbia Mungu, na wengine wanapenda sana kuwa watunzi wazuri wa nyimbo, na wengi wamekwenda katika vyuo vya uimbaji ili wakajifunze namna ya kutunga na kuimba vizuri, kufanya hivyo si kufanya vibaya, lakini hebu jiulize swali hili hivi! Mfalme Daudi alikwenda katika chuo gani cha kujifunzia kuimba na kutunga nyimbo alizokuwa akiziimba? Jibu lipo katika maneno yake Mfalme Daudi mwenyewe, anasema **" Roho wa Bwana alinena ndani yangu, Na neno lake likawa ulimini mwangu."** Mwalimu wake alikuwa ni Roho wa Mungu, huyo ndiye aliyemfundisha na kumwezesha Mfalme Daudi kuimba na kutunga nyimbo za kumwadhimisha Mungu wetu mkuu mno, Fahamu ikiwa unamwomba Mungu akujarie uwe mwimbaji mzuri na mtungaji mzuri wa nyimbo za kumwadhimisha Mungu zilizo na upako kutoka mbinguni zisizo tungwa kwa akili za kibinadamu, basi fahamu Mungu atakacho kupa ni karama hii ya lugha, ambayo Roho Mtakatifu akiwa ndani yako atakuletea maneno yake na kuyaweka kinywani mwako na ukiyaimba na kuyasema, na ukiomba kufasiri, na ukafasiri fahamu, utakuwa na utunzi mzuri mno, na uimbaji wako utabadirika kabisa,

Watu wengi wamepewa karama hii lakini hawaichochei, na hawaichochei kwa sababu hawafahamu kabisa habari za karama za rohoni, Neno la Bwana leo hii linatuambia, **"Basi, ndugu zangu, kwa habari za karama za roho, sitaki mkose kufahamu." (1KOR 12:1)**, Ili uwe mwimbaji mzuri ni lazima uhakikishe unazifahamu habari za karama za rohoni, ambazo kama kila Mkristo angelizifahamu, waimbaji wengi wasingeliimba nyimbo za kumsifu Mungu kwa kuiga, na kwa ovyoovyo, pia nyimbo hizo zingekuwa na upako, na Mungu kila mara angelikuwa anashuka na kuwatafuta watoto wake mahari pale walipo, leo hii ukiangalia kwaya nyingi na vikundi vingi jinsi vilivyo utagundu jambo hili ninalo lisema, wengi wanajitahidi kutunga na kuimba lakini lakini wengi hawana maarifa, hawajui kumtumia Roho Mtakatifu vizuri, ili awawezeshe kuimba na kutunga nyimbo vizuri, nyimbo zitakazomgusa Mungu katika kiti chake cha enzi na kumfanya ashuke aje kuzisikiliza na kuzifurahia,

Fahamu ndugu yangu ukiwa na karama hii ya kunena kwa lugha na ukajua kuitumia vizuri uwapo katika maombi yako kila mara, ukimtukuza Mungu kwa lugha kabla ya kuanza kumwomba haja yako, ukiitumia vema karama hii Mungu atashuka na kukutimizia hitaji lako kabla hata ya wewe kumwomba, Mungu anawatafuta watu wa mwabuduo kwa roho, sasa ukimwabudu kwa roho, kabla hujamuomba atakuwa amekutafuta na kukutimizia shida yako kabisa, wakumbuke kina Paulo na Sila walipokuwa gelezani, walimwadhimisha Mungu na kumshukuru Mungu, kwa masaa mengi, Bwana alishuka na kuwafungua pingu zao walizo kuwa nazo, sasa hebu jiangalie wewe unapingu gain? Ina wezekana ni ndoa yako, kazini kwako, au kukataliwa nk, hebu leo jifunze kumwadhimisha Mungu, nena kwa lugha sifa zake Mungu, Mwambie Roho Mtakatifu hitajilako kuwa unataka kumwadhimisha Mungu kwa Lugha, na anzakuyasema maneno yote atakayo kuletea kinywani mwako kwa imani, na jitahidi kwa bidii usikome kuyanena maneno hayo, na fahamu Mungu atashuka na kukufungulia hicho kifungo chako, fanya hivyo mara kwa mara utaona badiliko kubwa sana katika maombi yako, mara kwa mara yatakuwa na majibu mazuri toka kwa Bwana, Neno la Bwana lina sema hivi **"Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu" (EFE 5:19);** Tunatakiwa tuhakikishe tunamwimbia Mungu wetu kila siku, tena kwa

nyimbo za rohoni ndani ya mioyo yetu, na tenzi hizo ni za rohoni, fahamu, ukimwimbia Mungu kwa lugha, roho yako ndiyo inayo imba, kwa hiyo, ebu, kila siku mwimbie Mungu wako kwa roho, yaani kwa lugha.

Basi ndugu yangu unatakiwa leo hii uichochee karama hii ya kunena kwa lugha kwa kumsifu Mungu, unaweza ukawa unafanya hivi, ikiwa unataka umtukuze Mungu kwa lugha mwambie hitaji lako Roho Mtakatifu kuwa sasa nataka kumwadhimisha Mungu kwa lugha, na yeye atakuletea lugha hiyo kwa mtililiko huohuo wa kumwadhimisha Mungu, kwani neno lina sema hivi **"Nami nawaambia, ombeni nanyi mtapewa;tafuteni, nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona;naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (LUKA 11:9-13)**

Mungu ni Baba aliye mwaminifu sana, fahamu atakupa kitu sawasawna hitaji lako, na sehemu nyingine amesema wazi kuwa tukimuomba sawasawa na mapenzi yake atatupatia mahitaji yetu, na ana sema wazi **kuwa " Na huu ndio ujasiri tuliopewa kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba" (1YOHANA 5:14-15).** Kwa maneno hayo ndugu yangu unatakiwa uwena ujasiri kabisa wa kumwomba Mungu Roho Mtakatifu akuletee kinywanai Mwako maneno ya kumwadhimisha Mungu, na kumwabudu Mungu, kwani Mungu huwatafuta watu kama hao, wanaomwabudu katika roho na kweli, kwa hiyo utakuwa unamwomba kitu anacho kipenda Mungu, fanya hivyo, mwombe atakupa, na ukipewa fanya, yatamke maneno hayo na Bwana atakusikia na kukufurahia sana, Mungu akusaidiye na kukubariki sana katika maisha yako ya kiroho.

SEHEMU YA KUOMBA KWA LUGHA

Kama tulivyojifunza mwanzo wa somo hili katika sehemu hii ya karama ya lugha kuwa inaweza kutuwezesha kufanya mambo mawili, jambo la kwanza tayari tumekwisha kuiona nayo ni ya lugha za ibada, pia karama hii ya lugha hutumika katika maombi, na watoto wengi wa Mungu wanafahamu kuwa karama hii ya kunena kwa Lugha hutumika kwa kumuomba Mungu, Fahamu kuwa ndani ya karama hii ya lugha Mungu ameweka vitu viwili, cha kwanza ni lugha maalum inayotumika katika kumwadhimisha Mungu, na sehemu ya pili ni lugha inayotumika katika kumwomba Mungu.

Neno la Mungu linatufundisha kuwa **"Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina Matunda. Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia;……" (1KOR 14;14-15);** Ukiya soma maneno hayo ya Mungu tunapata fundisho zuri kuwa, karama hii ya lugha inatumika pia katika kumwomba Mungu, Paulo anasema wazi kuwa yeye katika maisha yake ya kiroho atakuwa anafanya mambo mawili katika maombi yake, jambola kwanza anasema atakuwa akimwomba Mungu kwa Akili zake, yaani kwa "kawaida" na jambo la pili atakuwa akimwomba Mungu kwa kunena kwa lugha, yaani yaani **"Maombi maalum"**

Kila mtoto wa Mungu ameagizwa na Bwana kuwa asikome kuomba, **"Ombeni bila kukoma;" (1THE 5:17), Pia ukisoma maneno ya Mungu katika kitabu cha (ISAYA 1:1A); Unasema hivi " Haya, njooni, tusemezane, asema Bwana."** Bwana ametuagiza sisi watoto wake tuhakikishe katika maisha yetu yote hatukomi kumwomba, pia Bwana ametoa agizo kwa watoto wake twende mbele zake na kusemanae, Hivyo ndivyo tulivyo agizwa na Bwana, Bwana anapenda sana ushirikano na sisi watoto wake, pia anapenda sana watoto wake tumtegemee yeye tu, na pale tunapokuwa na mahitaji yetu Bwana anatutaka sisi watoto wake tumuombe yeye tu, pia fahamu Bwana anataka kila mara watoto wake tupate kusema naye, yaani tuzungumze naye, ana sema wazi katika neno lake kuwa, **"Unikumbushe; na tuhojiane; eleza mambo yako, upate kupewa haki yako." (ISAYA 43:26).**

Fahamu Bwana Mungu ametupatia kibari cha kuhojiana naye, pia kumkaribia na kuzungumza naye, na tunazungumza naye na kuhojiana naye tukiwapo katika maombi yetu, ya mara kwa mara, hivyo ndivyo Bwana wetu anavyo panda tufanye kila siku ya maisha yetu, tuwe watu wa maombi, Sasa basi kwa kuwa sisi watoto wake ni wa dhaifu hatujui kuomba itupasavyo kama neno lake Mungu linavyo sema katika (RUM 8:26-27); **"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo;lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombe watakatifu kama apendavyo Mungu."** Fahamu wazi ndugu yangu kuwa mimi na wewe na huyo mtu unaye mfikiria na kumwomba kila siku akuombee, hatujui kuomba itupasavyo, ni wadhaifu kabisa, Mungu analifahamu suala hili vizuri sana, kuwa watoto wake hatujui kuomba, akaamua kutusaidia huo udhaifu wetu kwa kumtuma Roho wake Mtakatifu ili akaendani yetu na kutusaidia kuomba kwa lugha ambayo hatuijui kabisa, hata kuitamka tu inaitaji neema toka kwa Mungu, fahamu Roho Mtakatifu ndiye anaye tupatia karama hii ya kuomba, yaani Roho Mtakatifu anatusaidia na kutuwezesha kuomba kwa uzuri zaidi mbele za Mungu wetu, na fahamu anapokuwa anatusaidia kuomba huwa anatuletea hiyo lugha au maneno yale anayo tuombea katika ulimi wetu na maneno hayo huwa ni mageni kabisa katika ndimi zetu na tunapo yatamka ndio hapo tunapo shirikiana naye katika tendo la ajabu kabisa la kusema na Mungu moja kwa moja akiwa katika kiti chake cha enzi.

UNAPO NENA KWA LUGHA HUWA UNASEMA NA MUNGU:

Fahamu ndugu yangu kuwa mtu akiwa ananena kwa lugha huwa ana sema na Mungu, **"Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake" (1KOR 14:2),** Watoto wa Mungu wengi wanapenda kusema na Mungu lakini hawa fahamu namna ya Kusema na Mungu, fahamu, neno la Mungu lina sema kuwa mtu anaye nena kwa lugha anasema na Mungu, tena anasema naye moja kwa moja, hakuna mtuanayesikia, wala shetani hasikii na kuyafahamu mazungumzo hayo kati ya mtu huyo na Mungu, pa hata akili za kimwili za mtu huyo anenaye huwa zinakuwa hazijui kitu chochote kinacho zungumzwa kwani lugha inayo tumika katika mazungumzo hayo akili ya mtu huyo inakuwa haiifahamu, Bali Mungu tu ndiye anaye kuwa anafahamu nini kinachozungumzwa, Naipenda karama hii kwani ndiyo inayotusaidia sisi watoto wa Mungu kusema na Mungu, pia kuombewa na Roho mtakatifu kwa uzuri sana, Neno la Bwana lina sema Yesu amekaa mkono wa kuume wa Mungu akituombea, **"Ni nani atakaye wahukumia adhabu? Kristo**

Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea." (RUM 8:34)

Bwana Yesu alipopaa kwenda mbinguni kazi kubwa mojawapo anazozifanya huko kwa Baba Mungu, ni kutuombea, sasa ili leo tushirikiane naye katika huduma hii ndio maana akatuletea karama hii ya kunena kwa lugha ili tupate kuomba pamoja naye, kwani Huwezi kumtenganisha Roho Mtakatifu na Yesu, ikiwa hatuwezi kuwatenganisha basi fahamu Yesu ndiye anaye tuombea sisi akiwa ndani ya mioyo yetu, neno la Bwana lina sema hivi " Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa mwanawe mioyoni mwenu aliaye, aba, yaani, Baba." (GAL 4:6), Roho huyo aliyetumwa ndani yetu aliaye au atuombeye fahamu ni Roho wa Kristo Yesu, kwa lugha nzuri ni Yesu mwenyewe anayetulilia sisi mbele za Mungu, sasa ili tupate kushirikiana naye katika maombi yetu, akatuletea karama hii ya Lugha ili tupate kusema na kumwomba Bwana Mungu wetu.

Tatizo kubwa lililopo ndani ya kanisa ni kutokujua habari hizi za karama za rohoni, watoto wa Mungu wengi wamepewa Kipawa hiki, lakini hawakitumii vizuri, wengi wao hawana muda walioutenga iliwapate kuzungumza na Bwana kwa kutumia karama hii ya lugha, watoto wa Mungu wengi sana wamepewa karama hii lakini wengi pasipokufahamu hukwepa kunena kwa lugha wawapo ktika maombi yao na kukimbilia sana kuomba kwa akili, fahamu, akili zako na zangu haziwezi kuomba vema hata siku moja, Bali Roho mtakatifu ndiye anayeweza kuisaidia roho yako kuomba vema, na maombi hayo fahamu huwa yanamajibu, watoto wa Mungu wengi sana wamejikuta wamekwama katika sehemu hii ya maombi kwa sababu ya kutoitumia vema karama hii waliopewa na Bwana ili iwasaidiye katika maombi yao, wengi wamejikuta wanakata tamaa kwa sababu tokea walipo anza kumwomba Mungu awapatiye mahitaji yao hawajapata majibu kabisa, unafahamu ni kwanini? Ni kwa sababu hujui kuomba, ni mdhaifu wewe, na Mungu amekupatia karama hii ili unene kwa Lugha na umuombe vizuri huitumii karama hii, Waangalie watoto wa Mungu wengi sana walivyo, huwa wanaona aibu kunena kwa lugha, kwa sababu akili zao hazina matunda basi huona shida sana kuomba kitu wasichokifahamu, pia wengi wao wanaimani haba hawaamini kuwa lugha hiyo waliyonayo imetoka kwa Mungu, wengi wanajihisi uwepo wa shetani zaidi kuliko uwepo wa Mungu, sikia ndugu yangu Ikiwa umeokoka na kumpokea Bwana Yesu Maishani mwako fahamu Mungu yuko karibu nawewe kuliko shetani, Bwana anasema hivi **"Mimi ni Mungu aliyekaribu, asema Bwana, mimi si Mungu aliye mbali" (YER 23:23)**

Watoto wengi wa Mungu wamejaa hofu sana ndani ya mioyo yao, na hofu hiyo ndiyo inayo wasababishia wengi wasinene mara kwa mara, Huwa wanaikata hali ya kunena kwa lugha na kuanza kuomba kwa akili, Ebu, anza kuomba kwa kunena kwa lugha marakwa mara, tena angalau lisaa limoja, Yesu ali waagiza wanafunzi wake kuwa iliwapasa wakeshe kuomba angalau saa moja, **" Akawajia wale wanafunzi, akawakuta wamelala, akamwambia Petro, je! Hamkuweza kukesha pamoja nami hata saa moja?" (MATHAYO 26:40).** Kipimo hiki cha saa moja cha kukaa barazani pa Mungu na kusema naye au kumwomba Mungu, alikitoa Bwana wetu Yesu mwenyewe, kwa hiyo Ebu, weak jitiada au bidii ya kumwomba Mungu angalau kwa saa moja, ukiwa na bidii naamini kabisa utakuwa na mawasiliano na Mungu kila mara kama mtumishi wa Mungu Eliya, Neno la Bwana lina sema Eliya alikuwa kama sisi, alikuwa na tabia kama yako, lakini alipofanya bidii katika kumwomba Mungu Mungu alimsikia, (Yakobo 5:16-18); " Ungamaneni dhambi zenu nyinyi kwa nyinyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii. Eliya alikuwa

mwanadamu mwenye tabia kama sisi, akaomba kwa bidii mvua isinye;na mvua haikunya juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita. Akaomba tena, mbingu zikatoa mvua, nayo nchi ikazaa matunda yake

Fahamu Eliya alikuwa na tabia kama hiyo uliyonayo wewe, yaani alikuwa mwoga kama wewe, kumbuka alivyomwogopa sana Yezeberi na kumkimbia, pia wakati mwingine alijiona kuwa yeye ndiye mtakatifu kuliko wengine, kumbuka alimwambia Mungu kuwa yeye tu ndiye anaye mwabudu Mungu, na wengine wote wanaabudu miungu mingine, lakini Bwana alimjibu kuwa siyeye peke yake anaye mwabudu Mungu aliye hai, bali, wako watu wengine elfu saba wasioabudu miungu mingine, kwa hiyo utaona hapo kuwa Yakobo anapo sema Eliya alikuwa ni mtu mwenye tabia kama sisi alikuwa na maana kuwa Eliya, naye alikuwa na udhaifu kama huu tulio nao, ila alikuwa ni mtu mwenye bidii ya kusema na Mungu, fahamu pasipo bidii yako wewe mwenyewe, haiwezekani kabisa kumwomba Mungu, Bwana Yesu ana tufundisha kuwa roho zetu zinataka sana tumwombe na tuseme na Mungu wetu mara kwa mara, lakini miili hii yetu haitaki kabisa tuseme na tumuombe Mungu, **"Akawajia wale wanafunzi wake akawakuta wamelala, akamwambia Petro, je! Hamkuweza kukesha pamoja nami hata saa moja? Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho iradhi, lakini mwili ni dhaifu." (MATHAYO 26:40-41);** miili yetu imekataa kabisa kumtii Mungu "**Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti;bali nia ya roho ni uzima na amani; kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." (RUM 8:6-7);** roho yako inataka sana iseme na Mungu, na inataka sana imwombe Mungu, pia inataka sana ikaekatika maombi kila siku kwa Muda mlefu, yaani zaidi ya saa moja, lakini kizuizi chake kikubwa ni mwili, wala siyo shetani kama watu wengi wanavyo fikiri, mwili hautaki kabisa uupeleke kwa Mungu, kwani huo mwili wako una uadui na Mungu, hautaki kumtii Mungu na hautamtii Mungu, kinacho takiwa ni kuurazimisha tu, yaani wewe mwenyewe uhakikishe mwili haukutawali, yaani ufanye bidii mara kwa mara ya kuakikisha unafanya maombi tena kwa roho, yaani kwa kunena kwa lugha kwani hiyo ndiyo karama ya ambayo roho yako imepewa na Mungu ili ipate kuwasiliana na Mungu mojakwamoja bila hata mwili kujua jambo lolote lile ambalo roho imeliomba kwa Mungu, yaani roho inakuwa inajitegemea kabisa katika maombi na mwili unakuwa umenyamaza kimya ukiyawaza mambo mengine kabisa, au kwa lugha nyingine ni kwamba roho inakuwa imeipiga chenga mwili, Ebu, weka bidii ya kumwomba Mungu kwa lugha, utaona mabadiliko makubwa sana katika maisha yako ya kiroho, karama hii ya lugha za maombi Mungu aliitabiri katika kinywa cha Nabii Zekaria pale Bwana aliposema hivi 12:10A); Mungu alitoa taarifa ya kuwapatia watu wake roho ya Maombi na**"Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba;" (ZEKARIA** neema, sasa leo hii watu waliopewa roho ya neema ni sisi tuliookolewa kwa neema, na watu hao waliopewa neema na Bwana pia wamepewa na roho ya maombi, sasa fahamu ukienda kwa Mungu na kumwomba akufanye uwe mwombaji fahamu atakupatia roho ya maombi, na roho hiyo ya maombi ni hii ya kuomba kwa roho, yaani kunena kwa lugha, sasa watu wengi kila siku wana msumbua Mungu wakiomba wawe waombaji, wakati huo tayari wamepewa karama hii au roho hii ya maombi, ila hawataki wao kuichochea kwa kunena kwa lugha, Ebu, sikia ndugu yangu, ikiwa unayo karama hii ya kunena kwa lugha, hebu kila siku mwombe Mungu akujaze Roho wake Mtakatifu kama alivyo tuagiza kuwa **"Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho;" (WAEFESO5:18).**

Mungu anatutaka watoto wake kila siku tuhakikishe tuna jazwa Roho Mtakatifu, tatizo walilonalo watoto wa Mungu wengi lipo hapo, wengi hawafahamu kuwa Mungu anataka kila siku wajazwe Roho Mtakatifu, amabaye ndiye atupatiaye hata hiyo Lugha mpya, wengi hawafahamu kuwa Mungu anaouwezo wa kuwajaza Roho Mtakatifu kila siku, ilimladi wawe na uhitaji au kiu ya kujaa Roho Mtakatifu, neno la Bwana Yesu lina sema **" Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama;akapasza sauti yake akisema, mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa." (YOHANA 7:37-39)**

Mungu yuko tayari kumpatia mtu yeyote yulee amuaminiye Yesu Kristo Roho Mtakatifu, pia yuko tayari kumjaza mtu yoyote yulealiye na kiu ya kujaa Roho Mtakatifu, na anaweza kukuza ukiwa mahari popote pale hata chumbani kwako, si kwenye mkutano wa injili tu, au faraghani au kwenye semina Fulani, anaweza kukujaza wewe mwenyewe hata asipo kuwepo mtu wa kukuombea, neno la Bwana lina sema katika kitabu cha **(LUKA 11:9-13) " Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au samaki atampa nyoka? au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"**

Mungu yupo tayari kuwa zidishia au kuwa jaza watu wale watakaomwomba awazidishiye huyo Roho wake Mtakatifu, kwa hiyo ndugu yangu, ili kila mara unene kwa lugha bila kuchoka una takiwa uhakikishe unajaa Roho Mtakatifu kila wakati, Neno kujaa lina maana kuzidishiwa Roho Mtakatifu, si kuwa hauna Roho Mtakatifu, bali ni kuongezewa huyo Roho Mtakatifu, na fahamu, akizidi ndani yako ni lahisi sana akakupatia karama zake, na moja wapo ya hizo karama ni hii ya kunena kwa lugha, Ebu, kila siku uamkapo umwombe Mungu akujaze Roho Mtakatifu na uamini kuwa atakupatia Roho Mtakatifu, kama alivyo sema kuwa haiwezekani mtu muungwana mwanaye akimuomba samaki halafu ampe nyoka, sikia ukimwomba Mungu akupatie Roho Mtakatifu atakupatia Roho Mtakatifu, watoto wa Mungu wengi wamekuwa na hofu ya ajabu sana, wanakwenda mbele za Mungu na kumwomba awapatiye Roho Mtakatifu au awajaze Roho Mtakatifu, anapowapatia na kuanza kunena kwa lugha mpya hupata hofu kuwa huenda wana roho chafu, na kuacha kunena na wengine hukosa amani kabisa, sikia, Mungu hayuko hivyo, ukimwomba akupatiye Roho Mtakatifu atakupatiya Roho Mtakatifu, wala hata kutendea jamabo la kihuni kwa kuku patia roho chafu, watu wengi sana baada ya kuokoka tu, Mungu aliwapatia Roho Mtakatifu, na wengine wakapokea karama hii ya kunena kwa lugha, na baada ya kuipokea tu, wakaingiwa na hofu, na wengine wakaiacha kwa kujihisi kuwa wana mapepo, na wengine wakakimbilia kumbewa eti mapepo hayo yawatoke, fahamu, Mungu hawezi kukupatia pepo mchafu ukimwomba akupe Roho Mtakatifu, hilo ndilo tatizo kubwa linalo wazuia watu wengi wasinene kwa lugha, wanaogopa, na kukimbilia kuomba kwa akili zao walizo zizoea, Ebu, ondoa hofu, kila mara mwombe Mungu akujaze Roho Mtakatifu, na pia umwombe kila siku akupatiye nguvu zake, na utaona mabadiriko katika maisha yako ya kiroho, Mungu atakujaza na maendeleo yako ya kunena kwa lugha ya kuwa mazuri, pia ukifanya hivyo kila siku,

itakuwa ni lahisi siku moja utaanza kunena kwa lugha, kwani neno lina sema hivi Roho Mtakatifu alipomshukia Kolnelio na ndugu zake ndipo walipo anza kunena kwa lugha, sasa Ebu, weka bidii ya kumsihi Mungu akujaze Roho wake Mtakatifu kila siku, kasha upokee yaani uwe na uhakika kuwa kakupatia, na uanze kumshukuru, Yesu alikupatia huyo Roho mtakatifu, Mungu atakufungua ulimi wako na kuanza kunena kwa lugha.

JINSI YA KUFUNGULIA UNENAJI WA LUGHA MPYA

Nakumbuka mimi niliposoma maneno hayo ya kujaa Roho Mtakatifu katika Waefeso na Luka pamoja na kitabu cha Yohana hiyo sura ya saba ambayo Bwana alisema aliyena kiu, au haja na aende kwake akanywe maji ya uzima ambayo ni Roho Mtakatifu, kila siku, nilikuwa na bidii sana ya kumwomba Mungu anijaze sana Roho Mtakatifu wake, lakini sikuwahi kunena kwa lugha karibu miaka miwili na nusu hivi, lakini ilitokea siku moja nilipokuwa naendelea kumwomba Mungu anijaze Roho wake Mtakatifu, nikaambiwa, maneno haya na mtumishi mmoja wa Mungu alitoka mbali na eneo ninalo ishi, **"Mungu tayari kanijaza Roho wake Mtakatifu, ninachotakiwa ni mshukuru kwa kunijaza Roho Mtakatifu, nilitii sauti hiyo ya huyo mtumishi wa Mungu, nikaanza kumshukuru Mungu, kwa kusema "asante Yesu, kwa kunijaza Roho mtakatifu"**, baada ya kuendelea kumshukuru Mungu kwa dakika nyingi kidogo, ghafla, nikashangaa katika ulimi wangu nimenza kusema lugha tofauti na ile niliyokuwa namshukuru Mungu, nikaogopa kidogo, lakini nikaendelea, nikashangaa, ndani yangu yaani ya moyo wangu kunatokea chemichemi ya maneno mengi mageni kabisa, na kadili nilivyokuwa nayatamka ndivyo maneno mapya mengi nilipewa ulimini mwangu, niliendelea kuyatamka hivyo hivyo moja moja na kwa taratibu taratibu, na kadili nilivyo endelea kuyatamka ndivyo kasi ya kuyasema ilivyozidi, na nilipoikubali ile kasi ndipo nilipokuwa na uwezo wa kuyasema maneno mengi tena, nilipoondoa hofu iliyokuwa moyoni mwangu, ndipo nilipopata furaha sana ndani yangu, na cha ajabu, nilipo jiachia yaani kutoogopa kuyasema maneno hayo, ndipo, niliposhangaa badala ya kusema yale maneno nikaanza kuimba kwa hiyo lugha, na nilipoendelea kuimba nikashangaa, katika ulimi wangu ghafla kunatokea badiliko, nikaanza kushangaa maneno hayo nilianza kuyasema kwa kasi ya ajabu na maneno hayo yakapotea kabisa, na ulimi wangu ukaanza kusema **"Tatatatata……"**na niliyasema maneno hayo kwa kasi ya ajabu sana, yaani ulimi wangu ulikuwa kama cherehani ya kushonea inavyopanda juu na kushuka chini kwa kasi, na ilinichukua kama masaa manne niko katika hali hiyo, na tokea siku hiyo, ndipo nilipofunguliwa katika ulimi wangu kuanza kumwadhimisha Mungu kwa lugha na kuomba kwa Lugha, hivyo ndivyo ilivyotokea kwangu, lakini Mungu ana njia nyingi sana za kukufungua ili uanze kunena kwa lugha, Nakumbuka kipindi Furani nilikuwa katika huduma, na niliambiwa na Bwana katika semina hiyo, niwaombee watoto wa Mungu wajazwe Roho Mtakatifu, na wengi sana walipita mbele, wakiwa na kiu ya kujaa Roho Mtakatifu na kunena kwa Lugha mpya, na Nilipokuwa katika kumwomba Mungu, Mungu kwa uaminifu wake akawajaza watu wengi sana kipawa chake chema yaani Roho Mtakatifu, na wengi walianza kunena kwa lugha mpya, na wengine ilikuwa ni mara yao ya kwanza kabisa, lakini pale palikuwa na kijana mmoja ambaye alikuwa na kiu sana ya kunena kwa Lugha, na Bwana akaniongoza kwake, na akaniambia, mwambiye huyu, ashukuru, kwani tayari nimekwisha kumjaza Roho Mtakatifu ila yeye anaendelea kuniomba ni mjaze, nikamtii Bwana nikamfuata huyo kijana, na kumwambia kama Bwana akivyoniambia, akabadilisha wakati huohuo maombi yake, akaanza kumshukuru Mungu kwa **kusema "asante Yesu kwa kunijaza Roho Mtakatifu, ghafra akaanza kunena kwa Lugha mpya"**

Pia nakumbuka nilikuwa katika huduma sehemu fulani, na hapo pia Bwana aliniambia niwaombee wanae nguvu na ujazo wa Roho Mtakatifu, na kweli watu wengi sana waliitikia wito wa kupita mbele ili wapokee nguvu za Mungu na wajazwe Roho Mtakatifu, miongoni mwa waliopita mbele alikuwapo mtu mmoja mwanaume, akawa anamwomba Mungu kwa bidii sana, sikufahamu anaomba nini, Roho mtakatifu akaniambi mwambiye huyo ndugu anishukuru kwa kuwa nimemjaza Roho mtakatifu, na anataka anene kwa lugha mwambiye ashukuru nimempatia alichoomba, nikamfuata ndugu huyo, cha ajabu nilipomwambia afanye hivyo, akapata mashaka, hakufanya hivyo, aliendelea kuomba hivi "Bwana nakuomba unipatie karama ya kunena kwa lugha nk" nikamuacha, kesho yake akaja tena kwenye semina, na Bwana aliniambia wako watu wengi wana mahitaji mengi waombee, nikawaambia watu walio na mahitaji yao waje mbele ilitumwombe Bwana ayashughulikie, wakaja watu wengi sana, na miongoni mwao ni huyo Ndugu, aliyepita jana akiomba Mungu amjaze Roho Mtakatifu, basi, baada ya kuwaombe watu hao na wengi kuondoka pale mbele, ni kamfuata huyo ndugu, kwani yeye alichelewa kuondoka hapo mbele, nikamuuliza una shida gani ndugu, ambayo unataka Bwana akupe? Akasema nataka nijazwe Roho mtakatifu, na ninene kwa lugha, nika mwambia jana nilikuambia kuwa Bwana anasma unatakiwa ubadilishe maombi yako, na uanze kumshukuru Mungu, lakini hukutii, Ebu, mwombe Mungu msamaha, akakubali, akaomba msamaha, nikamuombea kwa Mungu amtiye Nguvu na ampe hitaji la moyo wake, nikamwambia anza sasa kumshukuru Mungu, akaanza kumshukuru Mungu, na ghafra Nguvu za Bwana zika mshukia, zikamtetemesha huyo mtu mwili wake wote, kama mtu aliyeshika waya wa umeme, kwali siku ile Mungu alituonyesha jambo la ajabu sana, alianza kutetemeka mikono yake aliyokuwa ameiinua juu pamoja na kichwa chake katika maungio ya shingo yake kilikuwa kina kwenda mbele na nyuma kwa kasi sana, na cha ajabu akawa kama anataka kuanguka, na alipokuwa anaanguka chini, hakugusa chini, aligandishwa hapohapo kama mti uliota siku nyingi, mimi na baadhi ya wahudumu tukajaribu kumsaidia ili adondokapo adondoke akiwa katika mikono yetu na tumlaze vizuri, lakini tulishindwa kushusha chini, wala hakuweza kupanda juu, nikamuacha, sasa kwa kitendo hicho kilicho mtokea ndugu huyo alipata hofu kubwa sana si yeye tu, bali na watu wengi waliokuwepo katika semina hiyo, basi, huyo ndugu, akaanza kupiga kelele sana za hofu, na hapo hapo akaanza kunena kwa lugha, na alikaa katika halihiyo ya kuganda hewani, kama dakika 50 hivi, tukimwangalia akitetemeshwa kiajabu kabisa, mikono ilikuwa inatetemeka kwa kasi ya ajabu, na imeinuka juu na haiwezi kushushwa chini, kichwa kilikuwa kina kwenda mbele na nyuma kwa kasi ya ajabu, na alinena kwa lugha dakika hiyo hiyo, na baadaye Mungu akamsimamisha na kwa kweli alishindwa kunena kwa lugha yake aliyo izoea, akaendelea kunena kwa lugha mpya tu.

Mungu ana njia nyingi sana za kumfanya mtu anene kwa lugha mpya, na Roho Mtakatifu alinifundisha kuwa, watu wengi sana, wamepewa karama hii, na ufunguo wa wao wa kuanza kunena kwa lugha uko kwao, sasa wengi wamekuwa na uonga na wengi hawajui namna ya kumfungulia Roho Mtakatifu mlango, yaani jinsi ya kupokea hiyo karama kivitendo, Mungu akiweka lugha hiyo kinywani mwako, wewe unatakiwa umfungulie mlango yaani uanze kunena, ufunguo wa kumfungulia unaujua? Ni, huu, Ebu, anza kumshukuru Yesu kwa Imani kuwa amekupatia tayari hiyo karama ya kunena kwa lugha, na pokea kila neno geni litakalo kuja ulimini kwako. Linene bila hofu, linaweza kuwa moja tamka hilohilo, kesho atakupa lingine, hivyohivyo na kuendelea, Usikate tamaa, taka kwa Mungu karama hii, ya lugha, na ichochee karama hii ya lugha katika maisha yako yote, kwani kupitia karama hii ya lugha, unaweza kujengwa ndani ya nafsi yako, pia utakuwa

unamwadhimisha Mungu au kumwabudu Mungu kwa uhalisi, pia itakusaidia katika maombi yako ya kila siku, Mungu akujalie karama hii na kukutia nguvu ya kuiochochea.

WANAWAKE KATIKAKUNENA KWA LUGHA

Neno la Bwana linatufundisha kuwa kwa Habari za karama za rohoni, kila mtu aliye mwana wa Mungu inatakiwa asikose kufahamu, yaani Mungu anataka watoto wake wote wahakishe kuwa wanazifahamu karama zote au zawadi zote walizopewa na Bwana, na katika habari hizi za karama za rohoni au katika suala zima la kumtumikia Mungu, Mungu hajatubagua kijinsia, yaani wanaume na wanawake, kama neno la Bwana linavyo sema katika **(MDO 2:17-18); "Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri;na vijana wenu wataona maono;na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri."**

Ukiyasoma maneno hayo ya Mungu utaona kuwa Mungu hajawatenga wanawake katika suala zima la kiutumishi wa kumtumikia Mungu kaika agano hili jipya, pia ukiya soma maneno hayo, utaona kuwa Mungu katika suala zima la kutumwagia kipawa chema cha Roho Mtakatifu, haja wabagua wanawake, kwani Bwana anasema atawamwagia watu wote wanaume na wanawake, na fahamu, ndani ya Roho Mtakatifu, ndimo karama zote za Mungu zilimo, sasa ikiwa Roho Mtakatifu yumo ndani ya mtu yeyote yule awe mwanamke au mwanaume, fahamu nilazima atampatia mtu huyo kipawa chochote kile, kama Roho Mwenyewe apendavyo, hatabagua langi, kabila au jinsia, atampa kila mmoja karama kama apendavyo yeye Roho mtakatifu, **"Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa apendavyo Roho yeye yule;" (2KOR12:8)**.

Roho Mtakatifu ndiye atupatiaye karama mbalimbali, sasa lazima ufahamu kuwa Roho Mtakatifu kamwagwa kwa watu wakike na wakiume, sasa, anao uweza wa kumgawia mtu wa kike karama ya aina yeyote ile, pia anao uweza wa kumgawia mtu yeyote wa kiume karama yeyote ile kama atakavyo yeye, Kwa maana hiyo basi, katika karama hii ya lugha Mungu Roho Mtakatifu ametugawia watu wa kike na wakiume kipawa hiki cha kusema lugha mpya, Wapo watu wengine wamekuwa na mashaka sana juu ya suala la wanawake kunena kwa lugha, kwani wamelishika neno hili lisemalo, **"Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena bali watii, kama vile inenavyo tolati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lolote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa, Au, je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? Au kuwafikia nyinyi peke yenu?(1KOR 14:34-36)**

Maneno hayo yamewachanganya watu wengi sana kiasi wengine wamewazuia wanawake wasiwe wananena kwa lugha kabisa katika vikundi vyao, au madhehebu yao, kwa kuwaambia neno la Mungu limewakataza wanawake wasinene kwa lugha, Fahamu ndugu yangu kuwa neno kunena lina tafsiri nyingi sana, mojawapo ya tafsiri hiyo ni kufundisha, kuamulisha, kuzungumza, nk, Sasa katika kanisa lililokuwepo Korintho wakati ule, kulitokea machafuko makubwa sana katika ndoa, wanawake wengi waliokuwa wamempokea Yesu kristo na kupewa karama mbalimbali hasa zilizo kuu, walijawa na kiburi kiasi cha kutowatii waume zao kama tolati ilivyo waamuru wafanye, kwani, neno la Mungu linasema wazi katika kitabu cha **(1KOR 11:3) " Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanaume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanaume, na**

kichwa cha Kristo ni Mungu". Hivyo ndivyo neno la Mungu linavyosema, sasa wanawake wa Korintho baada ya kumpokea Yesu na kuwa na karama za rohoni, wao wakajifanya kuwa ni vichwa vya waume zao, wakawa na sauti "unenaji"kwa waume zao, wakasahau agizo walilopewa na Bwana kuwa wanapaswa kuwatii waume zao, na ukisoma maneno yale siku ile Paulo alivyokuwa anawaonya alikuwa anawaonya wake za watu ambao walikuwa na kiburi kwa waume zao. Ana sema **"na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao"** pia ana sema **"Au, je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? Au kuwafikia nyinyi peke yenu?** Wanawake hawa walikuwa ni wake za watu walioolewa, wakawana sauti kwa waume zao baada ya kupata kulijua neno la Mungu, walijiona wao kuwa sasa ni zaidi ya waume zao, na wakataka kuwa juu ya waume zao, walijiona kuwa neno la Mungu liliwajia wao tu, wala si waume zao, Fahamu ndugu, Paulo alichokuwa anafanya ni kuwaonya wanawake waliokuwa ndani ya kanisa wawe na utii kwa waume zao wasioamini, na wasio na karama, ama wasiolifahamu neno la Mungu, na tatizo hilo lipo hata leo, hasa kwa akina mama walioolewa, baada ya kumpokea Bwana Yesu Kristo na kupewa karama mbalimbali si ya lugha tu, hata ya miujiza au kuponya, nk.wengi kwa kukosa mafundisho huwa hawawa heshimu waume zao, au hata kaka zao, na hata Baba zao, Nimewahi waona wanawake wengi waliopata karama ya kinabii, jinsi walivyoota kiburi na kuwadharau Baba zao na mama zao, pia hata waume zao, na zaidi ya hapo wanawadharau hata wachungaji wao, kisa, wana jiona kuwa nenola Mungu limewajia wao tu yaani wao ndio wajuaji sana kuliko waume zao ambao bado hawajaokoka, na wengi wao mwisho wao huwa mbaya, fahamu ukiwa ni mwanamke kuna maagizo maalum ambayo Mungu ameyatoa kwa wanawake wote wamchao wanatakiwa wayafanye, haijalishi ni mtumishi wa Mungu mwenye karama ya aina gani, au una elimu gani, unachotakiwa ni kumtii Mume wako, na uwaheshimu Baba yako na mama ili upate heri na siku zako zipate kuwa nyingi, kinyume cha hayo fahamu, huduma yako na karama zako mbele ya Mungu na wanadamu ni bure, nimewaona kina mama wengi waliona adabu kwa waume zao na ni watumishi wa Mungu, Mungu ameziinua sana huduma zao, na pia nimewaona mabinti wengi walio na heshima kwa wazazi wao na watu mbalimbali Mungu amewainua sana kwenye huduma zao, na nimewaona wanawake walio na dharau kwa waume zao, Mungu amewashusha katika hudumazao, hata mbele ya watu kwa kweli hawana ushuhuda mzuri kabisa, huduma zao au maisha yao kiroho ni mabaya, ingawa wanasema wameokoka.

Wanawake wengi baada ya kupata karama za rohoni au kupata elimu fulani, au kupandishwa cheo, au kuitwa kwenye utumishi wa kumtumikia Mungu, au baada ya kuokoka tu, au kupata mume nk, wamejikuta wamechomekewa dhambi ya dharau kwa waume zao na pia kwa wanaume wengine, na hilo ndilo tatizo kubwa linalo wasumbua wanawake wengi hata hivi leo, wanawake wengi baada ya kupata madaraka makazini mwao au hata kanisani, hutafuta kuwa vichwa katika ndoa zao, nakulipindua neno la Mungu lisemalo kuwa kichwa cha mwanamke ni mwanaume, na matokeo yake ndio ndoa nyingi zimevunjika, fahamu, Mungu, hatagombana na wewe ikiwa utamtii sana katika agizo hili la kutokuwa msemaji "mnenaji"katika ndoa yako au nyumbani kwako, ukimtii fahamu atakuinua na kukupatia karama nyingine ili ulijenge kanisa lake, Kwa hiyo, basi, usiogope kunena kwa lugha, bali uogope kuwa mnenaji kwa mume wako kama neno la Bwana linavyosema kuwa **"Ya kwamba wazee wawe wenye kiasi, wastahimilivu, wenye busara, wazima katika imani na katika upendo na saburi. Vivyo hivyo wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu;wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema;ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao; na kuwa wenye kiasi, kuwa**

safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe;ili neno la Mungu lisitukanwe."(TITO 2:2-5), Hivyo ndivyo Mungu anavyowaagiza wanawake wote wawe, na kinyume cha maagizohayo basi fahamu neno la Mungu litatukanwa tu, Kwani watu wengi huwa wanawaangalia na kuchunguza tabia za wanawake waliookoka na ni watumishi wa mungu, sasa usipo mtii na kumueshimu mume wako watasema unaona jinsi wanawake walokole walivyo? Basi anza kumtii mume wako leo, Fahamu Mungu hajamzuia mwanamke asinene kwa lugha, bali, amemzuia, mwanamke, asiwe juu ya mume wake asimtawale, Kama wewe ni mwanamke uliepewa karama hii, basi, ichochee, kwa kumwadhimisha Mungu kwa lugha, na itumie sana karama hii kwa kuomba kila siku ya maisha yako, Mungu akutie nguvu na kukujaza Roho wake Mtakatifu, siku zote za maisha yako.

KARAMA YA KUFASIRI LUGHA

Ebu, fungua kitabu cha (**1KOR 12:1); " Basi ndugu zangu kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu."**

Neno la Mungu linatutaka sisi kama watoto wa Mungu, tuhakikishe ya kuwa tunafahamu kwa upana habari zinazohusu karama mbalimbali za rohoni ambazo Baba Mungu ametupatia watumishi wake katika kulijenga kanisa la Mungu, Mungu ametupatia karama nyingi, na miongini mwa karama hizo mojawapo ni hii karama ya kufasiri lugha.

Karama hii ya kufasiri lugha Mungu ameiweka katika kundi lile la karama zilizo katika ulimi wa mwanadamu, na kundi hilo lina karama tatu, nazo ni, Karama ya kunena kwa lugha, Unabii, na hii karama ya kufasiri lugha, karama hizi tatu zipo katika ulimi wa mwanadamu ambaye ni mtoto wa Mungu, kwa ujumla karama hii ya kufasiri lugha huwa ina fanya kazi pamoja na karama nyingine hasa karama ya lugha na unabii pia ikibid, i na karama ya imani, neno lamaarifa, nk, Karama hii ya Kufasiri lugha kazi yake kubwa ni kufasiri lugha ile mpya iliyoletwa na Mungu katika kinywa cha mtu anenaye kwa lugha kwa kumwadhimisha Mungu au kwa kumuomba Mungu. Fahamu Neno la Mungu lina tuagiza kuwa kila mtu anenaye kwa lugha yampasa na aombe apewe kufasiri hiyo lugha mpya aliyoinena katika kinywa chake, Neno la Mungu linasema hivi, **"Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri." (1KOR 12: 13)**

Hivyo ndivyo kila anenaye kwa lugha yampasa aombe kwa Mungu apate kupewa karama hii ya kufasiri lugha mpya ambayo Mungu alikuletea katika kinywa chako na ukainena, Kwa maana hiyo utaona kuwa karama hii inafanya kazi pamoja na karama ya lugha, na kwa ujumla ni kwamba mtu aliye na karama ya kunena kwa lugha pia anatakiwa awe na karama ya kufasiri lugha, ila kwa watoto wa Mungu wengi sana hawajui au kufahamu kuwa karama hizi mbili zina kwenda pamoja, na wengi hawajui jinsi karama hii inavyofanya kazi Neno la Bwana linasema wazi kuwa, Anenaye kwa lugha anatakiwa pia aombe kufasiri lugha, watoto wa Mungu wengi sana, wamelidhika sana na karama ya kunena kwa lugha, wengi hawajaweka bidii ya kumuomba Mungu awape karama hii ya kufasiri lugha, utaona kuwa wengi kabla hawaja pewa karama ya kunena kwa lugha, walikuwa na bidii sana ya kumwomba sana Mungu ili awapatie karama ya kunena kwa lugha, na walipopewa karama ya kunena kwa lugha, wengi pasipo kufahamu hawaja mwomba Mungu awape pia karama ya kufasiri lugha, na wengine wanafahamu kuwa inatakiwa wamwombe Mungu ili awapatie karama ya kufasiri lugha, lakini, wameridhika na karama ya kunena kwa lugha kwa hiyo hawaja weka bidii ya

kumwomba Mungu awape karama ya kufasiri lugha, Namwamini sana Mungu katika jina la Bwana Yesu Kristo kwa uaminifu wake mkubwa, ambao ndio tabia yake, amesema anenaye kwa lugha na atake kufasiri, naamini ikiwa watoto wake waliona karama hii ya kunena kwa lugha watamuomba kwa bidii awapatie karama ya kufasiri lugha atawapatia tu, Kwanini watu wengi hawajapokea karama hii ya kufasiri lugha? Ni kwa sababu hawajataka kwa Bwana, na wengine tayari wanayo karama hii, ila hawajafahamu namna inavyofanya kazi, Ebu, tuone jinsi karama hii ilivyo na inavyofanya kazi, na Mungu Roho mtakatifu atufundishe kwa uzuri

ROHO MTAKATIFU NDIYE AFASILIYE MAFUMBO YA MUNGU

Neno la Mungu lina tufundisha kuwa mambo yote yaliyo mafumbo, au tusiyoyaelewa ya Mungu, anayeweza kuyafumbua ni Roho Mtakatifu tu, **(1KOR 2:10-11); " Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho.maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye, ila Roho wa Mungu."**

Fahamu ndugu yangu kuwa, mambo yote ya Mungu, anaye ya fahamu kwa usahihi, na kuyafumbua ni Roho Mtakatifu, sasa, basi, hata katika kufasiri mambo yatokayo kwa Mungu ambayo yametujia sisi watoto wake na tukayapoke lakini bila kuyafahamu anaye weza kutufasiria ni Roho Mtakatifu, Fahamu unaponena kwa Lugha, uwa unanena lugha ambayo hauifahamu kabisa, na lugha hiyo unayoinena umeipokea toka kwa Mungu, na anae weza kuifasiri hiyo lugha ya mbinguni ni Roho Mtakatifu tu, wala si kwa ufundi au kwa akili za kibinadamu, bali ni kwa uweza wa Mungu tu, ndiyo tunaweza kufasiriwa hiyo lugha.

Neno la Bwana linasema hivi, **"Ndipo Farao akapeleka watu, akamwita Yusufu, wakamleta upesi kutoka gerezani. Akanyoa, akabadili nguo zake, na kuingia kwa Farao. Farao akamwambia Yusufu, Nimeota ndoto, wala hakuna awezaye kunifasiria; nami nimesikia habari zako, ya kwamba, usikiapo ndoto, waweza kuifasiri.Yusufu akamjibu Farao, akisema. Si mimi; Mungu atampa Faraao majibu ya amani." (MWANZO 41:14-16).** Mfalme Farao, alikuwa ameonyeshwa ndoto na Bwana, na ndoto hiyo, Farao hakuifahamu kabisa, na akawa anatafuta sana kuifahamu ndoto hiyo, ambayo kwake ili kuwa ni fumbo asilolielewa kabisa, na alipomtafuta Yusufu iliaje amfasiliye hiyo ndoto, yeye alifikiri kuwa Yusufu yeye ndiye mfasiri, lakini Yusufu, akamwambia wazi kuwa anaye weza kufasiri ni Mungu, wala si, yeye Yusufu, fahamu ndugu yangu kuwa kufasiri mambo yote yaliyo toka kwa Mungu anaye yafasiri au kutuelewesha ni Mungu tu, Kwa maana hiyo fahamu kuwa suala zima la kufasiri hiyo lugha mapya unayoinena anaye weza kutufasiria ni Mungu tu, kwa Roho wake Mtakatifu, Neno la Bwana lina sema, **" Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni" (1KOR2:12-13).**

Roho Mtakatifu, tuliyenaye ndani yetu, yeye ndiye atupatiaye maneno yake ambayo tunayanena kwa Lugha, na fahamu yeye ndiye anayeweza kutufasiria hayo maneno yetu tuliyoyanena katika maombi yetu na sifa zetu tulizo msifu kwa lugha mpya, Kwa hiyo basi kila mtu anaye nena kwa lugha lazima afahamu kuwa lugha hiyo ainenayo

anayeifahamu ni Roho Mtakatifu, kwa hiyo ukimwomba aifasiri hiyo lugha, Roho Mtakatifu aliye ndani yako yuko tayari kukufasiria hayo uliyoyaomba kwa lugha na jinsi ulivyomwadhimisha Mungu kwa lugha, Na atakuletea fasiri hiyo kwa lugha unayoifahamu,

NAMNA TUNAVYO FASIRIWA

Neno la Bwana limetufundisha kuwa Mungu ndiye anayefasiri, na hakuna mtu mwingine awezaye kufasiri hiyo lugha kwa kutumia akili zake, na kuna njia mbalimbali ambazo Mungu huzitumia kutufasiria yale tuliyo mwomba Mungu kwa kunena kwa lugha, na njia hizo zote ambazo Mungu huzitumia kutufasiria tutazipata katika maandiko matakatifu,

Ebu, fungua kitabu cha (1KOR13:1), "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama….." Katika maneno hayo tunaona kuwa katika kunena kwa lugha, unaweza ukanena kwa lugha za kibinadamu, yaani lugha nyingine itumikayo na watu wa kabila au taifa Fulani, na lugha hiyo, mtu yule anaeinena mtu huyo huwa haifamu kabisa, pia unaweza ukanena kwa lugha za malaika, lugha ambayo inafahamika mbinguni, na pia lugha hiyo mtu yule ainenae huwa haifahamu kabisa, sasa basi fahamu, Mungu anaweza akakupatia lugha yeyote ile ya kibinadamu na ukainena na wakati huo unapoinena hiyo lugha Mungu anaweza kumleta mtu ambaye anaifahamu hiyo lugha na akaelewa kila neno linalosemwa, na mtu huyo anayeielewa hiyo lugha Mungu atamtumia kufasiri kila neno ambalo linatamkwa linasema nini, na nini maanayake, fahamu njia hiyo ya kufasiri lugha Mungu aliitumia siku ile ya pentekosti, siku ile Roho Mtakatifu alipokuwa amewashukia wanafunzi wa Bwana Yesu, mle chumbani, walitoka wote nje na kwenda mitaani na kila mtu alikuwa akinena kwa lugha mpya ambayo hakuifahamu kabisa na hakuwahi kuinena kabisa maishani mwake, Neno la Bwana linasema wazi kuwa watu wale waliokuwa wakiwasikiliza ndio waliokuwa wanaielewa lugha hiyo, hebu fungua kitabu cha **(MDO 2:4-12) " Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajaria kutamka. Na walikuwapo Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Warparthi na Wamedi na Wamedi, na Waelami nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, Frigia Rumi, Wayahudi na Waongofu, Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu.wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana Maana yake nini mambo haya?"**

Tukiyasoma maneno ya Mungu katika sehemu hii, tunaona kuwa siku ile wanafunzi wa Yesu Kristo wote walipokea karama hii ya kunena kwa lugha, na walianza kunena kila mmoja kwa kadiri Roho Mtakatifu alivyomjalia kutamka, na walipo kuwa wakinena kwa lugha mpya watu waliokuwa wakiwasikia hao ndio Mungu aliwatumia kufasiri lugha ile iliyokuwa ikinenwa na wanafunzi wa Bwana Yesu Kristo, Mungu ana weza kutufasiria lugha hiyo kwa njia hiyo, yaani, akifasiri lugha hiyo kwa kupitia wasikilizaji, ambao wanaifahamu hiyo lugha unayoinena, Fahamu unaweza ukanena kwa lugha za wanadamu, na fahamu Mungu anaweza kumtumia mtu yeyote yule anaeielewa hiyo lugha kwa kuifasiri, wanafunzi wa Yesu Kristo sikuile walipokuwa wakinena watu wa mataifa mbalimbali waliokuwepo Yerusalemu na walipokuwa wakiwasikiliza hao

wanafunzi wa Bwana Yesu, walisikia moja kwa moja na kuyaelewa yale yaliyo kuwa yananenwa, na watu hao ndio waliosema kuwa hawa wananena kwa lugha zetu, Kwa maana hiyo utaona kuwa Mungu anaweza akakufanya unene lugha yeyote ile ya kibinadamu, na akamleta mtu aifahamuye hiyo lugha na mtu huyo akamtumia kukufasiria yote uliyo kuwa unayanena.

MIFANO HAI YA JINSI MUNGU AWEZAVYO KUTUFASILIA

Kuna namna nyingi ambazo Mungu Roho Mtakatifu anazitumia katika kutufasilia lugha hizi mpya, ebu, tuangalie baadhi ya mifano hai, ambayo nimemwona Mungu akinifasilia na pia kuwafasilia watoto wake mbalimbali,

"Na kumbuka siku moja, Mama mmoja alifika nyumbani kwangu akiwa na tatizo katika maisha yake ya kiroho, na alihitaji msaada kwa Mungu, na alipofika nyumbani kwangu, Nilimwomba Mungu, amhudumie Mama huyo, na baada ya kukaanaye na kumweleza maneno ya Mungu, Mama huyo akalifahamu kosa lake, na akatubu, na nilipoanza kumwombea, kwa Mungu, ili amtiye nguvu, na amjaze Roho Mtakatifu, Mungu, alijibu kwa kumjaza Mama huyo Roho Mtakatifu, na pia Mungu alimshushia mama huyo nguvu zake toka mbinguni, na zikajidhihilisha kwa kumtetemesha mwili wa Mama huyo na kumfanya awechini sakafuni, na saa hiyohiyo mama huyo akaanza kunena kwa lugha mpya, na lugha aliyokuwa anainena ilikuwa ni lugha ya kiingeleza, na Mimi nilielewa maneno aliyokuwa akiyasema ya kiingeleza, na niliyaandika yote niliyoweza kuyaandika, na alipomaliza, nilimwambia alikuwa ananena kwa lugha ya kiingeleza, na kwa kweli mama huyo, alikuwa, amepata hofu sana kwa ajili ya tukio hilo, kwani alipoanza kunena kwa lugha, alitaka kuacha, nikamwambia asiogope aseme kila neno litakalo kuja kinywani mwake, kwani Neno la Bwana linasema wazi kuwa "Kwa hiyo nawaalifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu kusema, Yesu amelaaniwa;…." (1KOR:12-3A), Mama huyo aliendelea kunena kwa uoga na baadaye, akaondoa uoga huo, na akawaakiyatamka vema maneno yote, na alipomaliza, nilimuuliza, Mama unaweza kuongea kiingeleza? Akajibu hapana siwezi kuongea kabisa, akaniambia hajawahi hata siku moja kujifunza lugha hiyo ya kiingeleza, na nilipomwambia kuwa alikuwa akinena kwa lugha ya kiingeleza tena safi kabisa alishangaa sana, na nilimweleza tafsiri ya yale aliyokuwa akiyatamka, akashangaa sana, unajua! kwanini alishangaa?

Ni kwa sababu Mungu aliufunua moyo wa Mama huyo alivyo na namna Mama huyo anavyopaswa awe, Mimi mwenyewe nilishangaa sana, kwani kuna mambo ambayo Mama huyo aliyaficha na Mungu aliyafunua katika kunena kwake Mama huyo kuwa anatakiwa ayafanye na Mama huyo akakubali na kutubu, na alipoondoka nilimshangaa sana Mungu kwa tukio hilo, kwani alinipatia maarifa ya kufanya, kwa kupitia kinywa cha Mama huyo kwa kumfanya Mama huyo anene kwa lugha, na lugha yenyewe ilikuwa ni kiingeleza na katika kunena huko nikapata ufahamu kuwa kwanza ali mwadhimisha Mungu na kumwomba, na alicho kuwa anakiomba ni Upendo wa Mungu ujae ndani yake, na majibu ya yale aliyoyaomba, yalitoka kwa kusema kuwa mama huyo ahakikishe anaondoa chuki aliyokuwa nayo kwa jamaa zake, na alikubali kuwa kweli asemi na ndugu zake fulani, anawachukia sana, na akatubu, kwani Mungu aliliweka wazi jambo hilo"

Katika huduma hiyo utaona kuwa, Baba Mungu, alimpatia Mama huyo karama ya kunena kwa lugha, na akamfanya anene kwa lugha ambayo mimi naielewa, lakini mama huyo hakuielewa kabisa lugha hiyo, kwa hiyo, utaona hapo kuwa, Mungu anaweza kukufasiria kwa kutumia njia hiyo, akakufanya unene kwa lugha usiyoifahamu wewe, na hapohapo kati yenu akawepo mtu anaeifahamu lugha hiyo na akamtumia mtu huyo kufasiri maneno yote yaliyotamkwa, Na anaweza mtu huyo akafasiri neno kwa neno, au akayaandika yote, na akasubiri baada ya kumaliza kunena kwa mtu huyo anenaye, ndipo akayasema katika lugha iliyozoeleka yote yaliyo nenwa na huyo mtu.

MFANO WA PILI

Pia Mungu aliwahi kunionyesha njia nyingine anayoitumia katika kufasiri yale maneno mapya yaliyonenwa kutoka kinywani mwa mtu, kwa njia hii, **" Nakumbuka wakati mmoja nilikuwa sehemu moja nikifanya huduma ya kufundisha kanisa la Mungu, (semina), na Bwana aliniambia siku hiyo niwaombee watoto wake kipawa chema yaani Roho Mtakatifu, na kweli siku hiyo Mungu aliwaleta watu wengi sana katika semina hiyo, na watu wengi walikuwa na kiu ya kujaa Roho Mtakatifu, Miongoni mwao alikuwa ni dada mmoja, na Tulipomwimbia Mungu nyimbo za kumwabudu, Nikawaombea watu hao Mungu awajaze Roho wake Mtakatifu, na kweli, Mungu ni mwaminifu sana, akawashushia hao watu Roho wake Mtakatifu, na wengi wakaanza kunena kwa lugha, na Bwana akaniambia nimsogelee dada huyo nimsikilize kwa Makini ananena nini, Nikamtii Mungu, nikamsogelea dada huyo, na dada huyo alikuwa ananena kwa lugha, huku machozi mengi yakimtiririka toka machoni mwake, nikaanza kumsikiliza, yeye hakuniona, kwani alikuwa amefunga macho yake, na nilipoanza kumsikiliza, sikuyaelewa kwa haraka maneno aliyokuwa anayatamka, kwani alikuwa anayatamka harakaharaka, tena bila utulivu, nikamwambia tulia, yaseme maneno unayopewa na Bwana kwa utulivu, usiwe na haraka ya kuyatamka, tamka kama, kawaida yako, akanisikia, akaanza kuyatamka maneno hayo kwa utulivu, yaani bila papara, na hapo ndipo nilipogundua Roho Mtakatifu, anasema nini kwa kupitia kinywa cha dada huyo, alikuwa anatamka neno moja kwa lugha tatu, Alitamka neno moja kwa kihaya, na kiingeleza pia kwa kishwahili,**

Alipotulia katika kunena kwake, ndipo, tulipofahamu kuwa alikuwa anasema kwa lugha tatu, kwa wakati mmoja, kwa mfano, akisema Mungu, kwa kishwahili, basi, atasema tena kwa kiingeleza God, na atasema tena kwa kihaya, na alikuwa hafahamu kabisa kiingeleza, na kihaya, yeye ni myakyusa, kiswahili alikuwa anakifahamu vizuri sana, sasa alipokuwa akinena kwa harakaharaka ilikuwa nivigumu sana kufahamu kuwa alikuwa ananena kwa lugha hizo tatu, katika kila neno moja, yeye hakufahamu hilo, siku zote za maisha yake, na alikuwa anamwomba sana Mungu ampatie karama ya kufasiri lugha, hakujua kuwa Mungu alimpatia karama hiyo, kwani yeye alipokuwa ananena harakaharaka alikuwa anayaunganisha maneno hayo, kwa hiyo ilikuwa shida sana kutambua kuwa anasema nini.

Sasa baada ya kutambua hilo. Ndipo alipofahamu kuwa Mungu kumbe amempatia karama ya kufasiri hiyo lugha mpya aliyopewa na Bwana, na akafahamu kuwa ananena kwa lugha mpya mbili, akaanza kunena kwa lugha mpya, na akalitamka tena kwa lugha nyingine mpya hilo hilo neno, na akaendelea tena kulitamka kwa

kiswahili anacho kifahamu, tayari akawaamefasiriwa kile alichokitamka, Siku hiyo, Mungu alinifundisha kuwa watoto wake wengi wanamuomba awape karama ya kufasiri lugha, lakini wengi hawafahamu namna Mungu anavyofasiri hiyo lugha, kumbe inawezekana, ukawa unanena kwa lugha na hapohapo akakupatia karama ya kufasiri hiyo lugha katika kinywa chako wewe mwenyewe, wala si kwa kumtumia mtu mwingine, Kwa hiyo basi, ebu, jitahidi kutulia unapokuwa katika kunena kwa lugha, yasikilize yale maneno unayoyatamka kama kunaneno unalolifahamu ikiwa kuna neno unalolifahamu katika hayomaneno unayo yatamka, hebu fuatilia mtililiko wa hayomaneno, utaona, yamkini Roho Mtakatifu kakupatia neno jipya na neno la kukufasilia kwa wakati mmoja.

Tatizo lililopo kwa watoto wa Mungu wengi wanapokuwa katika maombi yao wanenapo kwa lugha huwa hawatulii, wengi hofu huwajaa, na huanza kutamka maneno hayo pasipo kutulia, na matokeo yake ni kukosa kumsikiliza Roho Mtakatifu, aliyendani yao, ambaye ndiye huwapatia karama ya kunena kwa lugha, na pia kufasiri hiyo lugha, kama neno linavyosema **" Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu makusudi tupate kuyajua tuliyokilimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni." (KOR 2: 12-13)** Ebu, badilika, anza kunena kwa utulivu, yaani, ukiwa, unasikiliza nini unacho kitamka kinywani mwako, Neno la Bwana lina sema hivi, **" Usiseme maneno ya ujinga kwa kinywa chako, wala moyo wako usiwe na haraka kunena mbele za Mungu;"(MHU 5:2A);**

Jitahidi kutulia, usiwe na haraka katika kuyatamka maneno mapya unayopewa, yatamke kwa uzuri bila papara, tena, usiwemjinga, bali, uyasikilize unayoyatamka, nimaneno gani?je! ni mapya? Au je! Yamejichanganya, yaani mapya na unayoyafahamu, nk, ukiwa na utulivu huo, nirahisi sana Mungu kukufasilia maneno mapya yote uyatamkayo

TULIA PIA UMALIZAPO KUOMBA

Wakati mwingine Mungu Roho Mtakatifu, anaweza kukufasiria lugha hiyo mpya uliyo inena kutoka kinywani mwako mwishoni mwa maombi yako, Kwa hiyo unatakiwa uhakikishe hufanyi haraka kutoka mbele za Mungu baada ya kumaliza kunena kwako kwa lugha, Neno la Bwana linasema, **" Usifanye haraka kutoka mbele za uso wake"; (MHU 8:3A)**, unaweza ukapoteza mtiririko mzima wa maombi yako utakapokosea katika kumalizia kwako, U kiisha kumaliza kuomba kwako kwa lugha, tulia mbele za Bwana, na ebu, msikilize ndani yako Roho Mtakatifu ana kuletea kitu gani, Fahamu anaweza kukuletea fasiri ya hiyo lugha mpya kwa kukupatia wimbo, ebu, uimbe huo wimbo, inawezekana ukawa unaufahamu sana wimbo huo, au ukawa ni wimbo mpya kabisa, ebu, uimbe, na utafakari huo wimbo, inawezekana kabisa fasiri ya maombi yako Mungu akakuletea kwa njia hiyo, Tatizo lilopo kwa watoto wa Mungu wengi nila kukosea wakati waanzapo kuomba kwa lugha, na wanapomalizia kuomba kwao kwa lugha, Fahamu, kabla haujaanza kuomba hitaji lako kwa lugha, ebu, Mwambie Roho Mtakatifu aliyendani yako akupatiye karama ya kufasiri hayo yote utakayoyanena kwa lugha, na amini, kuwa atafanya, anza kunena, na ikiwa umenena kila neno usilo lifahamu, yaani katika kunena kwako hukupewa fasiri ya neno kwa neno, umalizapo kuomba tulia, mshukuru kwa kukupatia karama ya kunena kwa lugha, na mwambie hitaji lako ulilo mwambia kwanza, kuwa unahitaji kufasiri hiyo lugha, Msubiri kwa kumshukuru na kumsifu, na kumwimbia nyimbo za kumwabudu, na itulize nafsi yako kwa kupokea neno lolote atakalo lileta kinywani mwako, anza kulitamka, kwa utaratibu mzuri, si kwapapara,

yaseme na uyatafakari kwa makini, kama unaweza kuyaandika hebu yaandike, Mungu roho Mtakatifu anaweza kutumia njia hiyo katika kukufasiria lugha mpya aliyokupa, kama nilivyosema mwazo kuwa Mungu ananjia nyingi sana za kutufasilia hiyo lugha, au mambo yake mbalimbali tusiyo ya fahamu, pia anaweza akakufasiria kwa kutumia njia hii katika kukufasilia maombi yako uliyoyanena kwa lugha.

MFANO WA TATU

Neno la Bwana pia linatufundisha kuwa, Mungu huwa anatufasiria mambo yale tusiyo yafahamu kwa kupitia maono ya usiku, au ndoto, (**AYUBU 33:14-16); " Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. Katika ndoto, katika maono ya usiku, usingizi mzito uwajiapo watu katika usingizi kitandani, Na kuyatia Muhuri mafunndisho yao"** Neno la Bwana lina tufundisha kuwa, Mungu anaweza akatufunulia sisi watoto wake mambo mbalimbali tulalapo usiku, kwa kutuonyesha njozi au kwa kuona maono, lnawezekana kabisa Mungu akakufasiria maombi yako yote uliyoyaomba kwa kunena kwa lugha kwa kutumia njia hii, Nakumbuka mara nyingi nilipomwomba Mungu kwa lugha na kukosa kufahamu wa kile nilicho mwomba Bwana, Mungu alinifasiria maombi hayo kwa kupitia maono aliyo niletea usiku, Mara ya kwanza ilinipa shida sana kufahamu maana ya maono mbalimbali niliyokuwa ninayaona, ndipo, siku moja Roho Mtakatifu akanifundisha kuwa ebu, kumbuka mchana wa leo ulikuwa umefanya nini, nikagunda mchana huo nilishinda katika maombi, tena nilinena kwa lugha sana, na sikufahamu kitu gani nilichosema na Mungu, na Mungu amesema na mimi kitu gani, kwani neno lina sema anenaye kwa lugha anasema na Mungu, sasa, Mungu akanifundisha kuwa ninatakiwa kuandika maono yale niyaonayao usiku, kwani wakati mwingine ndio fasiri ya hitaji langu nililo mwomba Mungu mchana kwa kunena kwa lugha, na pia kupokea majibu ya maombi yangu hayo.

Fahamu Mungu anaweza kukufasiri yale uliyomwomba kwa lugha mchana kwa kukuletea njozi au maono, Ukisoma maneno ya Mungu katika kitabu cha **(HABAKUKI 2:1-3); " Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniamabia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu, Bwana akajibu, akasema, iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji.maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamuriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake; wala haitasema uongo;ijapokawia, ingojee, kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia".**

Habakuki anasema atasimama katika zamu yake na kujiweka mahari pa juu ili apate kuona jambo ambalo Bwana atamuonyesha katika habari za kulalamika kwake, Habakuki alikuwa na jambo amabalo alimlalamikia Mungu, yaani, alimwomba Mungu, ukisoma sula ya kwanza ya kitabu hiki cha Habakuki iutagundua kuwa Habakuki alikuwa na maombi maalumu mbele za Mungu, na alimwomba Mungu kwa uchungu sana, na baada ya maombi yale, Habakuki anasema atasimama ili aangalie na aone lile atakaloambiwa na Mungu, yaani kutaka kujua kuwa Mungu atamjibu kitu gani, Mungu alimjibu Habakuki kuwa anatakiwa aiandike njozi ambayo Mungu atamletea, na aiandike vizuri ilikila aisomaye apate kuielewe, ukiyasoma maneno hayo hapo tunapata ufahamu kuwa Mungu anaweza kutufasiria yale tuliyomwomba kwa kusema nasi usiku katika njozi au ndoto, na kwa njia ya maono,

Nakumbuka siku moja nilimwimbia Mungu kwa muda mlefu sana kwa lugha, na nyimbo hizo nyingi zilikuwa ngeni kabisa, na siku hiyo sikupewa fasiri ya kuziimba kwa akili, lakini ilipofika usiku, Mungu alinionyesha jambo la ajabu sana, niliona nimechukuliwa na kupelekwa sehemu ambayo nilisikia sauti kama ya maji mengi, au sauti ya watu wengi sana sana, ambao walikuwa wanaimba, sikuwaona watu hao, ila niliwasikia wakiimba kwa sauti nzuri sana tena sana, na kwa mpangilio mnzuri mno, kwa kweli sijapatakusika uimbaji wa namna ile, na nilipopelekwa mahali hapo, nikashangaa, na mimi nikaanza kushilikiana nao katika kuimba wimbo huo mzuri, nikaimba nikiwa pamoja nao, lakini sikuwa nawaona, ila tuliimba pamoja, na wimbo huo ulikuwa ni wa kumsifu Baba Mungu, na baada ya kuimba sana, nikaludishwa hapa duniani, nikashangaa niko kitandani, nilikasirika sana, nilipenda niwepo mahali pale milele, na baada ya maono hayo, ndipo Mungu alipo nifundisha kuwa mchana nilimwomba Mungu anifasiliye yale niliyoyaimba na akanifasiria kwa kunionyesha kuwa nilimwimbia Mungu kwa kushirikiana na watakatifu wa Mungu katika ulimwengu wa roho, Kwa hiyo ndugu Mungu ana weza kukufasiria hayo uliyomwomba kwa lugha kwa kuitumia njia hii.

Hata Danieli Mungu alikuwa akimfasiria mambo mengi kwa kutumia njia hii ya maono na ndoto, Ukisoma maneno ya Mungu katika kitabu cha **(DANIELI 2:17-19) "Ndipo Danieli akaenda nyumbani kwake, akawapasha habari kina Hanania, na Mishaeli, na Azaria wenzake; ili waombe rehema kwa Mungu wa mbinguni kwa habari ya siri hiyo, ili kwamba Danieli na wenzake wasiangamizwe pamoja na wenye hekima wa Babeli, ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika njozi ya usiku. Basi Danieli akamhimidi Mungu wa mbinguni."** Katika maneno hayo, tunaona jinsi Mungu anavyoweza kutuambia au kutufasilia mambo ambayo hatuyafahamu, Danieli na wenzake, walikuwa na maombi maalum kwa Bwana ili awajulishe neno ambalo hawakuli fahamu, baada ya mfalme Nebukadreza kuota ndoto asiyoifahamu na pia alikuwa ameisahau ndoto hiyo, sasa Danieli alipomwomba Mungu amjulishe hiyo ndoto ilikuwaje, na pia alimwomba Mungu amfasilie hiyo ndoto maana yake nini, Neno la Bwana linasema kuwa Mungu alimjulisha Danieli maana ya ndoto hiyo kwa kumwotesha ndoto Danieli, kwa hiyo ndugu yangu, fahamu kuwa Bwana anaweza akakufasilia hata wew maombi yako uliyomwomba kwa lugha kwa kupitia maono au ndoto, Sasa unatakiwa uwe mwangalifu sana katika sehemu hii, kwani Bwana anaweza akawa ana kufasilia kila mara maombi yako uliyomwomba kwa lugha kwa kukuletea njozi au maono, Neno la Bwana linasema. **"Pasipo maono, watu huacha kujizuia" (MITHARI 29: 18A)**, Sasa ebu, uwe mwangalifu kwa kufuatilia kwa makini mambo mbalimbali ambayo unayaona katika ndoto au katika maono mbalimbali uyaonayo kwani kwa kupitia njia hiyo Bwana anaweza kukufasiria yale yote uliyomwomba kwa lugha mpya,

Katika njia hizo tulizoziona Mungu anaweza kuzitumia kukufasilia wewe maombi yako uyanenayo kwa lugha, pia hata kukufasilia jinsi ulivyomwadhimisha Mungu kwa lugha, basi ebu, anza kujifunza katika sehemu hizo tulizoziona ni sehemu gani Bwana anaitumia kukufasilia wewe, ukiiona ebu, ichojee bila kuwa na shaka. Na Mungu akusaidie.

KARAMA YA UNABII

“Namwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii;na mwingine kupambanua roho;na mwingine aina za lugha;na mwingine tafsiri za lugha;lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye” (1KOR12:10-11), Kama tulivyojifunza mwanzo kuwa Mungu ameziweka karama hizi tisa katika makundi matatu, yaani kundi la karama za rohoni zilizo ndani ya moyo wa mtu, zilizo katika ulimi wa mtu, na zilizo katika mwili wa mtu, na katika kila kundi kuna karama tatutatu, na tumeanza kujifunza kuhusu karama zile zilizo katika ulimi wa mtu, yaani karama ya Kinabii, karama ya Lugha na karama ya Kufasiri lugha. Na tayari kwa sehemu tumekwisha kujifunza habari za karama ya lugha, na kufasiri lugha.

Na sasa tuanze kujifunza habari za karama hii ya Unabii, karama hii ya unabii ni miongoni mwa karama tisa ambazo Mungu amewapatia watumishi wake ili kanisa lake Mungu lipate kujengwa kama atakavyo Mungu, fahamu kunatofauti ya huduma ya kinabii na karama ya kinabii, Neno la Bwana linatufundisha wazi kuwa wapo watumishi wa Mungu ambao Mungu amewaweka kuwa watendakazi wake katika ofisi au huduma ya unabii, **(EFE 4:11). “Naye alitoa wengine kuwa mitume;na wengine kuwa manabii;na wengine kuwa wainjilisti;na wengine kuwa wachungaji na waalimu.”** Fahamu kuwa wapo watumishi wa Mungu ambao huduma yao ni manabii, na unatakiwa usichanganye karama ya kinabii na huduma ya unabii, kama tulivyojifunza mwanzo wa somo hili kuwa karama za rohoni ni utendaji wa Mungu moja kwa moja kwa kupitia mwanadamu, ni pale tu, Mungu anapoamua kumtumia mtu yule aliye mchangua na kufanya jambo furani alitakalo Mungu, ambalo si la kawaida ya kibinadamu, sasa mtu aliye katika ofisi ya kinabii, yeye huduma yake iko kila saa, kapewa hiyo ndiyo ofisi yake, kwa hiyo utendaji wake katika kazi ya unabii ni tofauti na mtu yule aliye na karama ya kiunabii,

Fahamu unabii ni neno lile lililo toka kwa Mungu moja kwa moja, neno ambalo Mungu analitamka kwa lugha inayoeleweka kupitia mtu ambaye Mungu amemchagua, na mtu huyo anapolisema neno hilo ambalo si lake kwa watu, neno hilo ndilo liitwalo unabii, Fahamu Mungu si bubu, ni Mungu anayesema, na anapenda aseme sana na sisi watoto wake, ndio maana akaamua kutupatia watu wake karama hii, ili tupate kumsikia akisema nasi toka mbinguni, akitupatia maneno ya kutujenga, na kututia moyo, pia kutuonya, Neno la Bwana linasema katika **(EBR 12:25) “ Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale walio mkataa aliye waonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyae kutoka mbinguni”** Fahamu Mungu yuko mbinguni na huwa anatuonya sisi leo hii kutokea mbinguni, Fahamu Mungu ametupa neno lake yaani Biblia ilitupate kuyafahamu Mapenzi yake yote tuyasomapo maneno yake hayo, lakini, fahamu Mungu anaweza kutuonya sisi watoto wake leo kutokea mbinguni moja kwa moja, na anafanya hivyo kwa kuitumia karama hii ya unabii, kwa kuwatumia watoto wake aliowachagua yeye. Neno la Bwana linatufundisha kuwa Mungu alikuwa amewachagua watu wachache kuwa manabii katika Agano la kale, na walikuwepo manabii hao tokea zamani, Kama Ibrahimu, Musa, Miriamu nk, sikila mwamini kipindi kile alikuwa nanafasi ya kuwa nabii, lakini Mungu alikuwa anapenda watu wengi wawe manabii, ukisoma maandiko Matakatifu katika kitabu cha **(HES11:23-29) “ Bwana akamwambia Musa, je! Mkono wa Bwana umepungua urefu wake? Sasa utaona kwamba neno langu litatimizwa kwako, au sivyo? Musa akatoka, akawaambia watu maneno ya Bwana;akawakutanisha watu sabini miongoni mwa wazee wa watu, akawaweka kuizunguka Hema. Ndipo Bwana akashuka ndani ya wingu, akanena**

naye. akatwaa sehemu ya roho iliyokuwa juu ya Musa, akaitia juu ya wale wazee sabini, ikiwa roho hiyo ilipowashukia, wakatabiri, lakini hawakufanya hivyo tena. Lakini watu wawili walisalia kambini, jina la mmoja aliitwa Eldadi, na jina la wapili aliitwa Medadi;roho ile ikawashukia; nao walikuwa miongoni mwao walioandikwa, lakini walikuwa hawakutoka kwenda Hemani; nao wakatabiri kambini.mtu mmoja kijana akapiga mbio, akaenda akamwambia Musa, akasema, Eldadi na Medadi wanatoa unabii kambini. Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, tangu ujanawake, akajibu akasema, Ee bwana wangu Musa, uwakataze, Musa akamwambia, je! Umekuwa na wivu kwa ajiri yangu; ingekuwa heri kama watu wote wa Bwana wangekuwa manabii na kama Bwana angewatia roho yake;"

Ukiyasoma maneno hayo ya Mungu, utaona kuwa ni heri kila mtoto wa Mungu awe nabii na apewe Roho wa Bwana Yesu, na Mungu katika agano jipya aliamua kutupatia watoto wake karama hii ya kinabii ili iwe heri kwetu, wale wazee sabini walipokea karama hii, na walitoa unabii siku ile, na hii ilikuwa ni ishara kuu kuwa kuna siku Mungu atawapatia watoto wake karama hii ya kinabii, kwa hiyo lazima ufahamu kuwa Mungu katika Agano hili jipya katupatia karama hii ya kinabii ili kila atakaye apate kupewa ili kanisa la Mungu lipate kujengwa, watumishi wengi wa Mungu siku hizi wako kama Yoshua wana wakataza watu wasiwe manabii, au wasitoe unabii kwa sababu ya kuogopa unabii wa uongo, kufanya hivyo si vizuri, bali watu wanatakiwa wafundishwe habari hizi za karama za rohoni, na wajue unabii wa uongo ukoje na wakweli ukoje, kwani kunafaida nyingi sana kanisa likipata karama, hii na itatumika vema, kama mtumishi wa Mungu utakuwa na karama hii ya kinabii ikiwa labda wewe ni mwalilimi, mwinjilisti mchungaji, mtume, fahamu Huduma yako itakuwa bora sana, kwani utajua mambo mengi ambayo Mungu anataka uyafanye kwa wakati huo na huduma yako ya kujenga kanisa la Mungu itakuwa na mafanikio sana, ukisoma mandiko matakatifu katika kitabu cha **(1SAM30:7-8) "Daudi akauliza kwa Bwana, akasema, je! Nikiwafuata jeshi hili, nitawapata? Naye akajibu, Fuata;kwa kuwa hakika utawapata, nawe hukosi utawapokonya wote, "** katika maneno hayo ya Bwana tunapata ufahamu kuwa Mfalme Daudi alikuwa na mafanikio makubwa katika huduma yake kwa sababu ya karama hii ya kinabii, Mfalme Daudi alijua kuitumia sana karama hii katika maisha yake yote, ndio maana alifanikiwa sana, alikuwa hafanyi jambo lolote lile mpaka atakapopokea neno toka kwa Mungu, na neno hilo litokalo kwa Mungu ndiyo unabii, Mungu anataka watoto wake wote wawe na mawasiliano makubwa na Mungu, kwa kuitumia karama hii kanisa la Mungu linaweza kuongozwa vema katika mambo yote, Daudi aliitumia karama hii mara nyingi, ukisoma katika **(2SAMWELI 2:1) " Ikawa baada ya hayo, Daudi akauliza kwa Bwana, akasema, je! Niupandie mji wowote wa Yuda? Bwana akamwambia, Haya! Panda, Daudi akasema, niupandie mji upi? Akasema Hebroni, "**

Fahamu kunafaida kubwa sana katika karama hii ya unabii, katika karama hii tunaweza kupata muongozo moja kwa moja kutoka kwa Bwana akiwa juu mbinguni kwa wakati wowote, na Mungu anania hiyo ya kutaka kutufahamisha, kutujulisha, kutuongoza, nk, ndio maana akaamua kutupatia sisi kanisa lake karama hii ya unabii ili itusaidie katika utumishi wetu na katika maisha yetu ya wokovu, Mungu huitumia karama hii kutuimalisha, kutujenga na kutuongoza katika njia ile anayoitaka yeye, pia hata kutujulisha mambo mbalimbali ayatakayo tuyafahamu sisi kama watoto wake, Neno la Bwana linasema, **" Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake." (AMOSI 3:7)**

Ukiwa wewe ni mtumishi wa Mungu, fahamu, kuna mambo mengi ambayo Mungu anataka ayafanye katika kanisa lake, katika, nchi yako, pia katika huduma yako, katika maisha yako yote, nk, na mambo hayo Mungu anataka tuyajue, na akaona atupatiye karama hii ya unabii ili tupate kuyafahamu mambo hayo ambayo Mungu anataka kuyafanya, ndiyo maana leo hii, wapo manabii ambao ofisi yao kiutendaji ni hiyo, lakini pia akaamua kwa upendo wake awape hata watumishi wengine au waaminio wengine ambao si manabii kiofisi, karama hii ya kinabii, ili nao pia wapate kujua siri na mipango mbalimbali ya Bwana katika maisha yao na katika huduma zao, pia katika kanisa la Mungu, Ndio maana Musa alisema kuwa ingelikuwa heri kila mtu amchaye Mungu angelikuwa nabii, sasa leo hii katika agano hili jipya, Mungu kawapatia watu wengi Karama hii ya unabii, pia kawaweka watu wengine katika ofisi maalum ya kinabii, wanaitwa Manabii, fahamu, unaweza usiwe Nabii, lakini ukawa na karama ya kinabii. kwa mfano Mtume Paulo hakuwa Nabii, yeye mwenyewe anajieleza kuwa. **"Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume, (nasema kweli, sisemi uongo), mwalimu wa Mataifa katika Imani na kweli" (1TIM2:7)** Fahamu Mtume Paulo hakuwa nabii, bali alikuwa na karama ya unabii.na kwa kuitumia karama hiyo Mtume Paulo katika huduma yake alipata mafanikio sana, hebu ona mfano huu wajinsi karama hii ya unabii ilivyofanya kazi katika huduma ya Paulo, fungua kitabu cha **(MDO 16:910) " Paulo akatokewa na maono usiku;akamwona mtu wa Makedonia amesimama, akimsihi, na kumwambia, Vuka, uje Makedonia utusaidie.Basi alipokwisha kuyaona yale maono, mara tukataka kutoka kwenda Makedonia, kwa kuwa tuliona hakika ya kwamba Mungu ametuita tuwahubiri habari Njema"** Paulo alijaliwa kuwa na karama hii ya kinabii katika huduma yake, na alipata muongozo mzuri kutoka kwa Bwana katika huduma yake ya kuhubiri na kuwafundisha watu wa mataifa habari Njema za ufalme wa Mungu. Ndio maana Mungu anatutaka sisi watumishi wake tuzijue habari za karama tulizopewa na Mungu, ili huduma zetu na maisha yetu yawe katika usalama zaidi.na tutalijenga kanisa vizuri.

NINANI ANAYESTAHILI KUPEWA KARAMA HII YA UNABII

Watoto wa Mungu wengi wamekuwa na maswali mengi juu ya karama hii ya unabii, na watu wengi hawafahamu kuwa ni watu gani ambao Mungu anataka wawe na karama hii ya unabii, wengi wamefikilia kuwa, kuwa na karama hii ya unabii unatakiwa uwe umeokoka siku nyingi, au labda unasali dhehebu furani au uwe mkubwa kiumri, ndivyo watu wengi wanavyofikiri, Ebu, tuone maandiko matakatifu yanasemaje juu ya nani anastahili kuwa na karama hii au roho hii ya kinabii.

Fungua **(UFU19:9-10) " Naye akaniambia, andika, Heri walioalikwa karamu ya arusi ya mwana kondoo.akaniambia, maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu.Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie;akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu.msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya kinabii"**

Fahamu kuwa watu wanaostahili kuwa na karama hii ya unabii au roho ya kinabii, ni wale walio na ushuhuda wa Yesu Kristo, sasa ikiwa wewe umeokoka na Yesu yumo ndani yako basi fahamu tayari unayo sifa ya kuwa na roho ya kinabii au kwa lugha nzuri karama ya unabii, watoto wa Mungu wengi hawafahamu kuwa wanayo roho ya kinabii, wengi wanaushuhuda wa Yesu, lakini hawana karama ya kinabii, kwanini hawana wakati neno linasema ushuhuda wa Yesu ndio roho ya kinabii? Jibu, ni kwa sababu hawazijui habari

za karama za rohoni, kama wangezijua basi wangelikuwa na karama hii ya kinabii, Fahamu Mungu anataka watu wote wawe na karama hii ya kinabii, lakini sifa kuu anayotaka watu hao wawe nayo ni hii ya ushuhuda wa Yesu, sasa kama unao ushuhuda wa Yesu mwendee Mungu na kutaka karama hii ya kinabii, Neno la Mungu lina sema **" Takeni sana karama zilizo kuu….."(1KOR12:31A)** Katika habari za karama za rohoni, tumeluhusiwa kutaka, soma, **(1KOR 14:1) " Ufuateni upendo, na kutaka sana karama za rohoni…."** Bwana ametupa ruhusa ya kutaka Mungu atupe karama hii ya unabii, ikiwa tu, tunaushuhuda wa Yesu, fahamu neno kutaka linatofauti sana na kuomba, Bwana ana sema takeni, asemi ombeni, ukifahamu kuwa wewe unao ushuhuda wa Yesu, basi katake mbele zake Mungu akupatie roho hiyo ya kinabii, watoto wa Mungu wengi sana waliona ushuhuda wa Yesu Kristo, wanayo karama hii ya kinabii, tatizo hawajajijua kuwa wanayo karama hii, na jinsi karama hii inavyo fanya kazi ikiwa ndani yao. hebu tuone jinsi karama hii inavyo fanya kazi, na hapo utaona kuwa yamkini unayo karama hii, ila hukujua kuwa unayo karama hii ya unabii

JINSI KARAMA YA UNABII INAVYOFANYA KAZI

Unabii ni Neno au ujumbe uliotoka kwa Mungu, na Mungu atausema au kuuonyesha ujumbe huo kwa kumtumia mtu yeyote yule ambaye Mungu ataamua kumtumia, na Mungu anapokuwa anataka kutujulisha wanaadamu Neno lake huwa ana tumia njia nyingi sana, na kwa kuzitumia njia hizo ndipo watoto wa Mungu tunapopokea, Neno la kutuonya au kututia moyo pia hata kutufaliji, Sasa kuna njia nyingi sana ambazo Mungu husema na sisi, fahamu sizungumzii, njia ya mafundisho ya Biblia na waalimu, au kuhubiriwa Injili na wainjilisti, Nazungumzia kupokea ujumbe moja kwa moja kutoka mbinguni, yaani Kupokea neno la kuliimalisha kanisa au kulitia moyo, pia kupokea maonyo ya kukuongoza katika maisha yako au ya watu wengine, hilo ndilo ninalo lizungumzia, Watu wengi wanachanganya unabii na mafundisho yatolewayo na mwalimu katika kanisa la Mungu, wengi hufikilia kuwa ujumbe huo ndio unabii, fahamu, mwalimu amepewa upako na Mungu wa kulijua Neno la Mungu, na kulisoma kwa makini, na pia amepewe upako wa kulifundisha Neno hilo kwa kueleweka masikioni mwa wasikilizaji, na mwalimu mzuri akiisha kulifahamu Neno la Mungu hufanya maombi maalumu ili Mungu amwezeshe kulifundisha vema, hupanga atanamna atavyoanza na kulifundisha somo hilo, hujiandaa mapema kabisa, Sasa Neno la kinabii, huwa halipangwi na mtu, au mtu hajichagulii la kusema, bali ni neno lililoletwa na Roho Mtakatifu Moja kwa moja ndani ya moyo wa mtu, na linaweza kuwa nineno la kukujulisha yaliyokuwako au yaliyopo au yatakayo kuwapo, au nineno la kukuimalisha katika maisha yako ya kiroho, au katika huduma yako, pia katika kanisa, Ona mfano huu mzuri jinsi Mungu alivyo tumia neno la kinabii katika kuibolesha huduma ya Paulo na Barnaba. Fungua **(MDO 13: 1-2) " Na huko Antiokia katika kanisa lililokuwako palikuwa na manabii, na waalimu, nao ni Barnaba, na Simeoni aitwaye Nigeri, na Lukio mkirene, na Manaeni aliyekuwa ndugu wa kunyonya wa mafalme Herode, na Sauli. Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia."**

Fahamu Sauli au Paulo na Barnaba, na watumishi wengine waliokuwepo mahali pale siku zote tokea walipoanza kuamini hawakufahamu kazi ambayo Mungu alitaka kina Paulo na Barnaba waifanye, Mpaka ilipotokea Mungu alipoamua kuwaambia kwa kutumia unabii, ndipo wote walipopata ufahamu wa kitu kile Mungu anataka wakifanye Paulo na Barnaba, Sasa basi fahamu Neno la Mungu linalokuja moja kwa moja toka mbinguni hilo

ndilo liitwalo unabii. Sasa kuna namna nyingi Mungu anaweza kusema na kanisa lake kwa lugha nyepesi na watoto wake waliookoka. Ebu, tuangalie njia mbalimbali ambazo Mungu anazitumia kusema na sisi, na baada ya kuzijua hizo njia unaweza ukafahamu kuwa yamkini unayo karama ya kinabii ila hukufahamu.

NJIA YA KWANZA MAONO NA NDOTO

Fahamu neno nabii hapo zamani liliitwa mwonaji, **(1SAMWELI 9:9) "[Hapo zamani katika Israeli, mtu alipokwenda kuuliza neno kwa Mungu, husema hivi, Haya! Twende kwa mwonaji; maana mtu aitwaye sasa Nabii hapo zamani aliitwa mwonaji)"** Neno la Bwana linatufundisha kuwa neno nabii hapo zamani liliitwa mwonaji, kwa sababu manabii wengi walikuwa wanaona maono, yaani walikuwa wanapokea maneno au maagizo ya Mungu kwa kuonyeshwa maono maalum toka kwa Mungu, na walipoonyeshwa ndio walienda kuyasema maneno yote waliyoonyeshwa au waliyoambiwa na Bwana, fahamu manabii walikuwa wanaona maono au kuoteshwa ndoto maalum na Bwana, akiwapasha habari mbalimbali ambazo Mungu alitaka wazifahamu, ukisoma maandiko matakatifu utawaona manabii mbalimbali walipokea ujumbe toka kwa Bwana kwa kutumia maono au ndoto, ebu, ona maneno haya ya Bwana yanavyo sema, **" Kisha akawaambia Sikilizeni basi maneno yangu; Akiwapo nabii kati yenu, Mimi, Bwana, nitajifunua kwake katika maono, Nitasema naye katika ndoto." (HESABU 12:6)**

Maneno hayo ya Bwana yanatufundisha kuwa, Mungu hulituma neno lake kwa watu wake kwa kutumia njia hii ya maono na ndoto, Bwana anasema atasema na manabii wake kwa ndoto na kwa maono, Sasa basi ukiwa umepewa na Bwana karama hii ya kinabii, fahamu Mungu anaweza kusema na wewe kwa kuitumia njia hii ya maono au ndoto, Watoto wa Mungu wengi sana huota ndoto na kuona maono mbalimbali kutoka kwa Bwana, lakini wengi huwa hawatilii maanani maono au ndoto walizoziota, kwa sababu wengi hawajui habari za karama za rohoni, **"wengine utawasikia wakishuhudia wakisema niliona maono au niliota ndoto, na baadaye yale niliyo yaona au niliyoyaota yametukia vilevile, "** Fahamu lnawezekana Bwana kakupatia karama hii ya kinabii ndio maana anasema na wewe kwa kutumia njia hii ya kukuletea maono, au ndoto, lakini kwa kuwa hujajijua kuwa unayo karama hii ya kinabii, uonapo maono au uotapo ndoto zote alizokuonyesha Bwana huzifuatilii, unaziacha tu, Baada ya tukio au jambo Fulani kutokea ndipo wengi hukumbuka waliona maono hayo au waliota ndoto inayo fanana na hayo yaliyotokea wakati huo.Fahamu Mungu ana njia nyingi sana za kusema na sisi watoto wake, na fahamu anaweza kusema nasi kwa kutumia njia hii ya maono au ndoto, Manabii wengi kipindi kile Bwna alikuwa anasema nao kwa kutumia njia hii, aliwaletea maneno yake katika ndoto au maono, hebu tuone mifano iliyo hai katika Biblia inavyo tuonyesha jinsi Mungu alivyosema na manabii wengi kwa kuitumia njia hii ya ndoto na maono. Fungua **(MWANZO 15:1-3) " Baada ya mambo hayo neno la BWANA likamjia Abramu katika njozi, likinena, Usiogope, Abramu, mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana. Abramu akasema, Ee Bwana Mungu, utanipa nini nami naenda zangu hali sina mtoto, na atayeimiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, Mdameski? Abramu akasema, Tazama, hukunipa uzao, na mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu".** Ukisoma maneno hayo utaona kuwa Mazungumzo kati ya Mungu na Abrahamu yalifanyika katika njozi, Mungu alileta neno lake kwa Abrahamu akiwa amelala, na Abrahamu pia alisema maneno yake mbele za Mungu akiwa katika njozi, au ndoto, Fahamu ndugu yangu kuwa Mungu anaweza

kuhojiana na mtoto wake kwa kutumia njia hii ya ndoto na maono, Mungu alimwona mwanaye ambaye ni Abrahamu kuwa amefadhaika sana ndani ya moyo wake kwa sababu hakujariwa kuwa na mtoto wa kumrithi, alipata shida sana moyo mwake alipoona mtu mwingine ndiye atakayeridhi mali yake, wala si mtoto wake aliyemzaa, Mungu alipoona hivyo, akaamua kumletea Abrahamu neno la kinabii, la kumfaliji na kumjeanga pia la ufahamu, kuwa atampatia Abrahamu mtoto, na pia aliimarisha imani ya Abrahamu pale alipo mwambia kuwa mimi ndimi ngao yako na thawabu yako, Maneno hayo ni ya kutia moyo sana, ambayo Bwana alimwambia Abrahamu, Fahamu ikiwa wewe katika maisha yako Bwana anasema na wewe kwa kupitia njia hii, fahamu unayo karama ya kinabii, kwani Bwana katika agano hili jipya amesema ameamua kutumwagia Roho wake Mtakatifu, na Mungu amesema vijana wa kike na wakiume wataona maono, na wazee wataota ndoto, Fungua **(MDO 2:17-18) " Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri"** Fahamu kipindi alichokuwa anakitabiri Mungu kwa kupitia kinywa cha Yoeli, ni kipindi hiki tulichonacho sasa, kwani Mungu tayari amekwisha mmwaga Roho wake Mtakatifu tokea siku ile ya Pentekosti, na Mungu aliisha sema kipindi hicho Roho Mtakatifu akiisha kumwagwa atawafanya vijana waone maono na wazee waote ndoto, pia Bwana alisema kuwa watumishi wake Mungu watamwagiwa Roho Mtakatifu nao watatabiri, Fahamu, kitendo cha kutabiri ni kitendo cha kinabii, Manabii wengi kipindi kile cha agano la kale walikuwa wanatabiri, Neno la Bwana linasema **" Basi, walipofika Gibea, tazama, kikosi cha manabii wakakutana naye; kisha roho ya Mungu ikamjilia kwa nguvu, naye akatabiri kati yao. Ikawa wote waliomjua zamani walipoliona jambo hilo, kwamba, tazama, huyo anatabiri pamoja na manabii, ndipo watu wakasemezana, Ni nini hilo lililompata mwana wa Kishi? Je! Sauli pia yumo miongoni mwa manabii? Naye akajibu mtu mmoja wa mahari hapo, akasema, na Baba yao n'nani? Kwa hiyo ikawa mithari, je! Sauli pia yumo miongoni mwa manabii Naye alipokwisha kutabiri, alipafikia mahali pale pa juu" (1SAM 10:10-13)**

Ukiyasoma maneno hayo kwa makini utagundua kuwa manabii hutabiri, Sauli alipojiliwa na nguvu za Roho wa Mungu, alianza kutabiri, na watu wengi walimshangaa Sauli alipokuwa akitabiri kwani walifahamu wazi kuwa Sauli hakuwa nabii, walishangaa sana walipomwona akitabiri, kwani kazi ya kutabiri ilikuwa ni ya manabii, Sasa katika Agano jipya Maneno ya Bwana yana sema kuwa Mungu atawamwgia watumishi wake Roho Mtakatifu nao watatabiri, yaani watatoa unabii, ndio maana akaamua kuwapa watoto wake na watumishi wake karama ya kinabii, na ndio maana ana sema Wazee wataota ndoto, na vijana wataona maono, pia watumishi hao wakike na wakiume watatabiri, Ukiangalia kwa makini maneno hayo utagundua wazi kuwa Mungu alikuwa anazungumzia kuhusu habari za watumishi wake wakike na wakiume watapewa karama hii ya kinabii, kwa ajiri ya kulijenga kanisa lake kama atakavyo, Fahamu mtumishi wa Mungu inawezekana kabisa ukawa unayo karama hii ya kinabii ila hukufahamu namna inavyofanya kazi, Mungu amewamwagia watumishi wake wengi karama hii ila tatizo lao hawajui kuwa wanayo karama hii, fahamu, kupitia ndoto, na maono,, Mungu anaweza kukuletea neno lake kwa wakati wowote ule akiwa mbinguni.

Ukiangalia katika kitabu cha **(MWANZO 28: 10-15) "Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani. Akafika mahali Fulani akakaa huko usiku kucha, maana jua lilikuwa limekuchwa; akatwaa jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake,**

akalala usingizi pale pale.Akaota ndoto;na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni.Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake. Na tazama, Bwana amesimama juu yake, akasema mimi ni BWANA, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea upande wa magharibi, na mashariki, na kasikazini, na kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watajibarikia. Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia."

Bwana alisema na Yakobo maneno hayo mazito kwa kupitia ndoto, na Mungu alimweleza Yakobo kuwa asiwena hofu kwa sababu Mungu yupo pamoja naye, pia alimweleza kuhusu mpango wa maisha yote ya Yakobo ambayo yeye Mungu amempagia, Mungu hakumficha Yakobo mambo yote yatakayo kuja mbeleni katika maisha ya Yakobo, na fahamu maneno hayo yalikuwa ni maneno ya kinabii, na kweli Mungu alikwenda kuyatimiza katika maisha ya Yakobo, kwa hiyo ndugu yangu fahamu Mungu kwa kupitia karama hii ya kinabii anaweza kuzungumza na wewe mambo mbali mbali ya maisha yako binafsi, huduma aliyokupagia, na pia anaweza kukupasha habari yeyote ile aitakayo yeye akujulishe, na anaweza kukuletea neno lake hilo kwa njia ya ndoto, ona mfano huu, Yusufu alipokuwa amekusudia moyoni mwake kumwacha Mariamu mchumba wake kwa siri, Mungu aliamua kusema naye Yusufu na kumfahamisha mambo ambayo Yusufu hakuya fahamu kabisa, **" Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimia, kumwacha kwa siri. Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao." (MATHAYO 1:18-22)** Mungu kwa kuitumia karama hii ya kinabii, alisema na Yusufu habari hii ya kutokumwacha mke wake, fahamu Yusufu neno la Mungu halituambii kuwa alikuwa nabii, ila alipokea neno la kinabii toka kwa Mungu, Bwana aliamua kumwambia Yusufu ukweli wa jambo lililokuwa linamsumbua sana la mke wake kuwa na mimba nje ya ndoa yao.

Fahamu Baba Mungu leo anataka kuwaambia watu wengi habari mbalimbali zinazowasumbua, na pia Mungu yuko tayari kutuambia sisi watumishi wake mambo mbalimbali tutakayo mwomba atuambie, kwani ni mapezi yake kamili sisi watoto wake tumuulize habari yoyote ile tutakayo hitaji kuifahamu, na ametupa kibari sisi watot wake tumuulize yeye kitu chochote kile Bwana anasema hivi, **"BWANA, mtakatifu wa Israeli, na Muumba wake, asema hivi; Niulize habari za mambo yakayokuja;mambo ya wana wangu, na habari ya kazi ya mikono yangu; haya! Niagizeni" (ISAYA45:11),** Bwana katupa kibari sisi watoto wake tumuulize habari za mambo yatakayokuja, na habari za wana wake yaani kanisa, mtu binafsi, na habari za kazi zote za Mungu, na amesema kuwa atatuambia, sasa Mungu aliamua kuyadhibitisha maneno hayo ya nabii Isaya katika Agano hili jipya kwa kututumia karama hii ya rohoni ya kinabii, ilikila mtoto wake awe na mawasiliano na maongozi mazuri toka kwa Mungu, Petro hakuwa nabii, ila alikuwa na karama hii ya kinabii, na ilipotenda kazi karama hii katika huduma ya Petro, kila mtu alimwona Mungu akitenda kazi pamoja na Petro, ona mfano, huu siku moja Petro alipokuwa amekutana na Anania na Safira, Neno la Bwana linasema

“Lakini mtu mmoja jina lake Anania, pamoja na safira mkewe, aliuza mali, akazuia kwa siri sehemu ya thamani yake, mkewe naye akijua haya, akaleta fungu moja akaliweka miguuni pa mitume. Petro akasema Anania, kwa nini shetani amekuja moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? Kilipokuwa kwako, hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani haikuwa katika uwezo wako? Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu. Anania aliposikia maneno haya akaanguka, akafa.hofu nyingi ikawapata watu wote waliosikia maneno haya. Vijana wakaondoka, wakamtia katika sanda, wakamchukua nje, wakamzika” (MDO 5:1-6)

Kwa kupitia karama hii ya kinabii na karama ya kupambanua roho na karama ya miujiza, Petro alipata ufahamu kuwa Anania kasema maneno ya uongo, na baada ya tukio hilo kutokea Neno la Bwana linasema kuwa vijana wote au watu wote wakaogopa sana, kwa maana hiyo kanisa la Mungu likajengwa tokea siku hiyo lisiseme uongo, na huduma ya Petro ikawa nzuri sana na ya mafanikio sana. Kwa hiyo ndugu yangu fahamu Mungu anasema na sisi kwa kutumia njia nyingi sana, moja wapo ya njia hizo ni hii ya maono na ndoto, Watumishi wengi wa Mungu, Mungu alisema nao mambo mengi kwa kupitia njia hii ya maono na ndoto, ukimwangalia mtumishi wa Mungu Yusufu utaona kuwa Mungu alisema naye mambo mengi yatakayo mtokea mbeleni katika maisha yake, Neno la Bwana linasema kuwa, **(MWANZO 37: 5-11) “ Yusufu akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia; akawaambia, Tafadharini, sikieni ndoto hii niliyoiota Tazama, sisi tulikuwa tukifunga mikanda shambani, kumbe! Mganda wangu ukaondoka ukasimama, na tazama, miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu, Ndugu zake wakamwambia, je! Kweli wewe utatumiliki sisi? Nawe utatutawala sisi? Wakazidi kumchukia kwa ajiri yake, na kwa maneno yake. Akaota na ndoto nyingine, akawaambia ndugu zake, akasema, angalieni nimeota ndoto nyingine;na tazama, jua na mwezi na nyota kumi na moja zikaniinamia.akawaambia baba yake na ndugu zake;baba yake akamkemea akamwambia, Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je! Mimi na mama yako na ndugu tutakuja tukusujudie hata nchi? Ndugu zake wakamhusudu;bali baba yake akalihifadhi neno hili.** Yusufu hakujua kama Mungu alikuwa anasema naye, kwa kupitia ndoto hizo.aliziona kama ni ndoto za kawaida, kumbe Baba Mungu alikuwa anamtaarifu Yusufu habari za maisha yake jinsi yatakavyokuwa mbeleni, na kweli, Neno la Bwana linatufundisha kuwa wazazi wa Yusufu na nduguze walikuja kumsujudia Yusufu kama alivyoona kwenye ndoto, Kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa uwe mwangalifu sana katika eneo hili, yamkini Bwana anasema na wewe kila siku, na kukupasha habari ya mambo mengi sana, lakini kwa kuwa hujajijua kuwa Bwana kakupa roho au karama hii ya kinabii ndio maana hufuatilii maono au ndoto uzionazo mara kwa mara, anza sasa kufuatilia ndoto au maono mbalimbali unayoyaona Fahamu ukiwa wewe umeokoka na umejaa Roho Mtakatifu fahamu kabisa Bwana anaweza kusema na wewe kwa kupitia njia hii ya karama ya kinabii na atatumia maono au ndoto kusema na wewe. **“Ndipo ulipowaambia watakatifu wako kwa njozi”(ZABURI 89:19A).** Mungu yuko tayari kusema na wewe kwa kupitia njia hii, ilimladi uwe mtakatifu.na utakatifu tumeupata kwa kupitia Bwana Yesu Kristo.

KARAMA YA KUNENA KWA LUGHA + KARAMA YA KUFASIRI LUGHA = UNABII

Fahamu ndugu yangu kuwa ukiwa na karama ya kunena kwa lugha, na pia Mungu akakupatia karama ya kufasiri hiyo lugha, ujumbe utakao upokea katika kufasiriwa

kwako huo pia ni unabii, Fahamu umwombapo Mungu kwa lugha akujulishe habari fulani ambayo wewe hauifahamu, fahamu Mungu atakujulisha habari hiyo, kama alivyosema katika neno lake hivi, **" Bwana, mtakatifu wa Israeli, na muumba wake, asema hivi; Niulize habari za mambo yatakayokuja; mambo ya wana wangu, na habari ya kazi ya mikono yangu, haya niagizeni (ISAYA 45:11)** na anaweza kukujulisha kwa kutumia njia ya maono au ndoto au kwa sauti, na ujumbe huoutakaojulishwa unaitwa ni unabii.

Ona mfano huu wa mtumishi wa Mungu Danieli jinsi alikuwa akijulishwa mambo aliyomwomba Mungu amjulishe, Fungua **(DANIELI 2:17-23) " Ndipo Danieli akaenda nyumbani kwake, akawapasha habari kina Hanania, na Mishaeli na Azaria wenzake;iliwaombe rehema kwa Mungu wa Mbinguni kwa habari ya siri hiyo, ili kwamba Danieli na wenzake wasiangamizwe pamoja na wenye hekima wa Babeli. Ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika njozi ya usiku. Basi, Danieli akamhimidi Mungu wa mbinguni. Danieli akajibu, akasema, Na lihimidiwe jina la Mungu milele na milele;kwa kuwa hekima na uweza ni wake. Yeye hubadili majira na nyakati;huuzulu wafalme na kuwamilikisha wafalme; huwapa hekima wenye hekima;huwapa wenye ufahamu maarifa; yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo gizani, na nuru hukaa kwake. Nakushukuru, nakuhimidi, Ee Mungu wa baba zangu uliyenipa hekima na uwezo, ukanijulisha hayo tuliyo yataka kwako; maana umetujulisha neno lile la mfalme."** Ukiyasoma maneno hayo ya Mungu katika sura nzima hiyo ya tisa, utaonajinsi Mungu alivyo mjulisha Danieli mambo ya siri ambayo Danieli aliomba kwa Mungu ili amjulishe habari ya ndoto aliyo kuwa ameiota mfalme Nebukadreza, Mungu alimjulisha Danieli siri hiyo katika njozi au ndoto ya usiku, Na ukiyasoma maneno hayo ya Mungu utagundua kuwa Danieli alikuwa na maombi Maalum mbele za Mungu ili amjulishe siri hiyo iliyofichika ya ndoto ya mfalme, sasa utaona Danieli kabla hajapokea ujumbe huo kutoka kwa Mungu, alifanya kwanza maombi, na baada ya hayo maombi ndipo neno la kinabii toka kwa Mungu lilipomnjia usiku katika ndoto, hapo tunapata somo zuri kuwa ukiomba mbele za Mungu jambo lolote lile usilolifahamu na ukamuomba Mungu akujulishe, fahamu Mungu atakujulisha tu, na ana weza kukujulisha kwa kutumia maono au ndoto, Kwa maana hiyo unapoomba kwa lugha usiyo ifahamu, na utakapo muomba Mungu akufasirie yale uliyomwomba na jibu au fasiri utakayopokea ikiwa ni kwa njia ya maono, ndoto, sauti nk, ujumbe huo unaitwa ni unabii, kwani ni neno lililo toka kwa Bwana moja kwa moja.

Sasa hebu jiangalie katika maisha yako ya wokovu Bwana anasema na wewe kwa njia ya namna hii? Ikiwa ana sema na wewe kwa njia kama hii aliyo sema naye Danieli fahamu inawezekana kabisa ukawa na karama ya unabii, ikiwa unamwomba Mungu akujulishe jambo furani na ukaliombea jambo hilo kwa lugha, hebu anza kuwa makini kwa kufuatilia ndoto au maono utakayoyaona, yawezekana kabisa Bwana akakujulisha hilo unalo mwomba kwa kupitia njia hii ya maono au ndoto..na ujumbe huo utakaojulishwa unaitwa unabii. Neno la Bwana lina sema kuwa **"Maana, ni nani aliyesimama katika baraza la Bwana, hata akalifahamu neno lake na kulisikia? Ni nani aliyelitia moyoni neno langu, na kulisikia? (YEREMIA 23:18)** Ukiwa umesimama balazani au mbele za Mungu na kumwomba Mungu akupatiye ufahamu wa jambo Furani usilo lifahamu, fahamu Mungu atakujulisha neno hilo, atakuletea neno lake kwa ndoto au kwa maono, kitu kikubwa kinacho takiwa ni wewe uhakikishe unasimama balazani pake Mungu na kumwomba ili akupatiye neno lake la kweli, Na ndio maana tunajifunza kuwa ukiomba kwa lugha na ukaomba ufasiliwe hayo uliyoyaomba kwa lugha, jibu lake, utakalo pewa na Bwana ndio unabii, watoto wa Mungu wengi sana wamekuwa na maombi mengi sana

mbele za Mungu, wengi huwa wanaomuomba Mungu labda awaokoe ndugu zao, awaponye ndugu zao, au wanamuomba Mungu awaonyenye huduma anayoitaka Mungu waifanye, fahamu Mungu tunaye mwabudu siyo sanamu, ni Mungu aliye hai, anaye jibu, na kujulisha mambo mbalimbali tumuombayo na hata tusiyomwomba, na kwa kupitia karama hii ya kinabii, Mungu anaweza kukujulisha Mambo mengi sana unayo mwomba, na wengi majibu yao Mungu huwajibu kwa njia ya ndoto na maono.na ikiwa unapokea majibu yako au Mungu anasema na wewe kwa njia hii fahamu unayo karama ya kinabii, unatakiwa uichochee, kwa kumshukuru Mungu na kumhimidi, kama alivyo fanya Danieli, pia unatakiwa uyafanyie kazi au uyashike hayo aliyokuonyesha au aliyokujulisha, Fahamu unapokuwa katika kipindi cha maombi na ukawa unahitaji ufahamu furani mbele za Mungu Ufahamu huo utakaopewa na Mungu kwanjia yoyote ile unaitwa ni unabii, sasa ukiwafuatilia watoto wa Mungu katika kipindi hiki, Mungu husema nao sana, na wengi amewapa karama hii ya unabii, lakini, kwa kuwa hawazijui habari za karama za rohoni, ndio maana wengi huendelea kumuomba Mungu awape karama ya unabii wakati tayari wamepewa, ila hawajui kuwa wanayo, Ebu, leo hii jichunguze, je! Bwana anakuonyesha mambo mbalimbali kwa kupitia maono au ndoto? Ikiwa anasema na wewe kwa njia hii, na kukujulisha mambo yale uliyomwomba kwa kukuletea njozi na maono, au hata kwa sauti, fahamu, unayo karama ya kinabii, na umshukuru Mungu kwa kukupatia karama hii ya unabii,

Kwa sehemu tumejifunza namna Bwana anavyo weza kusema na sisi watoto wake kwa njia hii ya maono na ndoto, na kama tulivyojifunza mwanzo kuwa, Bwana anazo njia nyingi sana ambazo anaweza kuzitumia ili aseme na sisi watoto wake, na tumejifunza njia ya kwanza anayosema na sisi watoto wake kwa kutupasha habari anazotaka tuzifahamu au zile tulizomwomba atufahamishe, na ni kwa kutuletea maono au ndoto(njozi) mbalimbali, na tumeona kwa uwazi kuwa kumbe kwa kupitia karama hii ya unabii, Mungu ana weza kusema nasi kwa njia ya maono na ndoto atuleteazo, kama alivyosema wazi katika neno lake kuwa, **" Kisha akawaambia, Sikilizeni basi maneno yangu; Akiwapo nabii kati yenu, mimi, Bwana, nitajifunua kwake kati ka maono, Nitasema naye katika ndoto, " (HESABU12:6)**, Mwombe Mungu aseme na wewe kwa kupitia njia hii, kama alivyotuagiza katika neno lake kuwa **"Ufuateni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, …." (1KOR 14:1)**, Ebu, itakae karama hii mbele za Mungu, mwombe akupatiye karama hii nzuri ya unabii, Mwamini Mungu kuwa atakupa karama hii, na ataanza kusema nawewe kwa kupitia njia hii akipenda, Mungu akubariki na akusaidie katika kulifahamu somo hili kwa uzuri kabisa.

AINA ZA MAONO NDOTO

Katika karama hii ya unabii tumeona jinsi Mungu anavyoweza kusema na sisi watoto wake kwa kupitia maono na ndoto, Sasa basi hebu tuangalie maono na ndoto hizo jinsi zilivyo, Fahamu, kuna maono na ndoto zilizogawanyika katika makundi yafuatayo.

1. **Maono yaliyo dhahili (wazi)**
2. **Maono yasiyo dhahiri.**

Unaweza kujiuliza swali maono yaliyo dhahiri nini? na yasiyo dhahili pia nini?, Fahamu maono yaliyo dhahili ni maono yale ambayo Mungu anaweza kukuonyesha ukiwa macho, yaani waziwazi, na maono yasiyo dhahili niyale Mungu anaweza kukuonyesha ukiwa umelala au umezimia, Ebu, tuone Maono yaliyodhahili yalivyo, Fungua kitabu cha

(KUTOKA 3:1-3) " Basi huyo Musa alikuwa akilichunga kundi la Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani;akaliongoza kundi nyuma ya jangwa, akafika mpaka mlima wa Mungu, hata Horebu. Malaika wa Bwana akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti; akatazama, na kumbe! Kumbe kile kijiti kiliwaka moto, nacho kijiti hakikuteketea. Musa akasema, Nitageuka sasa, niyaone maono haya makubwa, na sababu kijiti hiki hakiteketei." Siku Mungu alipotaka kuongea na Musa, jambo la kwanza kabisa ambalo Mungu alilifanya lilikuwa ni kumletea Musa maono, na maono ambayo Mungu alimletea Musa yalikuwa ni maono ya dhahili yaani waziwazi, Musa alikiona kijiti hicho akiwa macho, yaani hakuwa amelala usingizi au hakuwa amezimia, aliyaona maono hayo kwa uwazi kabisa, kwa hiyo ndugu yangu lazima ufahamu kuwa Mungu anaweza kukuonyesha maono ya waziwazi kabisa, watu wengi sana wamekuwa na mashaka sana katika suala hili katika kipindi hiki, wengi wanajiuliza kuwa kweli inawezekana Mungu katika miaka hii anaweza kuwatokea watu kama vile alivyofanya katika kipindi cha agano la kale, fahamu Mungu ni yuleyule jana leo na hata milele, anaweza kabisa akakuonyesha maono yanamna hii, Katika agano hili jipya tunaona sehemu nyingi Mungu akiwaonyesha watumishi wake maono ya wazi wazi kabisa, Ukisoma maandiko katika kitabu cha **(LUKA 1:8-17). " Basi ikawa, alipokuwa akifanya kazi ya ukuhani katika taratibu ya zamu yake mbele za Mungu, kama ilivyokuwa desturi ya ukuhani, kura ilimwangukia kuingia katika hekalu la Bwana ilikufukiza uvumba. Na makutano yote ya watu walikuwa wakisali nje saa ya kufukiza uvumba, Akatokewa na malaika wa Bwana, amesimama upande wa kuume wa madhabahu ya kufukizia. Zakaria alipomwona alifadhaika, hofu ikamwingia. Lakini yule malaika akamwambiaUsiogope, Zakaria, maana dua yako imesikiwa na mkeo Elizabeti atakuzalia mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yohana. Nawe utakuwa na furaha na shangwe, na watu watakufurahia kuzaliwa kwake. Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye Na wengi katika Israeli atawalejeza kwa Bwana Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake kataka roho ya Eliya, na nguvu zake, ili ilikuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa".**

Maneno hayo yanatufundisha kuwa Mungu siku ile alipoamua kumtaalifu Zekaria mambo yale aliyokusudia kuyafanya hapa duniani, aliamua kumtumia ujumbe (Unabii) kwa njia ya maono, na maono aliyoyatumia yalikuwa ni maono ya waziwazi, Zekaria siku ile alikuwa hajalala usingizi, bali alikuwa macho, tena akiwa katika huduma madhabahuni, ndipo alipopokea maneno hayo ya kinabii, kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa Mungu anaweza kukuletea ujumbe wake kwa kupitia njia ya maono, na anaweza akakuletea maono ya waziwazi kabisa, kwa hiyo ukiwa unayo karama hii ya unabii, unatakiwa ufahamu kuwa anaweza kukuletea ujumbe kwa kukuletea maono ya waziwazi kama alivyomtokea Musa na Zekaria, kwa hiyo usimwekee Mungu mipaka, Ipo mifano mingi sana ambayo ipo kwenye Maandiko matakatifu ambayo ina tufundisha jinsi Mungu alivyosema na watu wake kwa kupitia njia hii ya maono yaliyo dhahili, kwa mfano alivyoamua kumpelekea ujumbe Kornelio, Mungu alimpelekea ujumbe huo kwa kuitumia njia hii ya maono ya waziwazi, kasome **(MDO 10:1-8);**

Pia ukisoma kitabu cha, **(DANIELI 5:2-6) " Belshaza, alipokuwa akionja ile divai, akaamuru wavilete vile vyombo vya dhahabu na fedha, ambavyo baba yake, Nebukadreza, alivitoa katika hekalu lililokuwako Yerusalemu; ni kwamba mfalme, na wakuu wake, na masuria wake, wapate kuvinywea.Basi wakavileta vile vyombo**

vya dhahabu, vilivyotolewa katika hekalu la nyumba ya Mungu lililokuwako Yerusalemu; na mfalme, na wakuu wake, na wake zake na masuria wake, wakavinywea.wakanywa divai, wakaisifu miungu ya dhahabu, na ya fedha, na ya shaba, na ya chuma, na ya miti, na ya mawe. Saa iyo hiyo vikatoea vidole vya mkono wa mwanadamu, vikaandika katika chokaa ya ukuta wa nyumba ya enzi ya mfalme, mahali palipokikabili kinara;naye mfalme akakiona kitanga cha ule mkono ulioandika. Ndipo uso wa mfalme ukambadilika;fikira zake zikamfadhaisha;viungo vyake vikalegea;magoti yake yakagongana." Mungu siku ile aliamua kusema na mfalme Belshaza kwa kutumia njia hii ya maono yaliyo wazi, kwa kumwonyesha wazi vidole vya mwanadamu vikiandika ujumbe ambao Mungu aliutoa wazi wazi kutoka Mbinguni, na fasiri ya maneno hayo yalipo tolewa na Mungu kwa kupitia Mtumishi Wake Danieli, mfalme na watu wote waliuelewa ujumbe huo kwa uzuri kabisa, Kwa hiyo ndugu yangu fahamu kuwa Mungu leo hii anaweza kuletea neno lake kwa njia ya maono yanamna hii yaani maono ya dhahili au ya waziwazi. Kwa hiyo ukiwa na karama hii ya kinabii, Bwana anaweza kukuletea ujumbe kwamtindo huu akipenda, watu wengi wanapoona maono ya namna hii, au wanapowasikia baadhi ya watu wakisema kuwa Bwana amenionyesha jambo furani, watoto wa Mungu wengi huingiwa na mashaka, Sikia ndugu, Mungu anataka kila mtoto wake apate kufahamu habari za karama za rohoni ulizopewa na Bwana, kipawa hiki ni kipawa kizuri sana ambacho kama watoto wa Mungu wengi watakuwa nacho, na wakakitumia vizuri, basi kanisa la Mungu litajengwa vizuri, hebu fikilia leo hii niviongozi wangapi wa kanisa ambao Mungu amewapima na wakaonekana wamepungua? Lakini bado wako katika uongozi, na hawafahamu kuwa uongozi wao hautambuliki mbele za Mungu, na hata watumishi wengine wa Mungu, Mungu aliisha wapiga ikabodi, siku nyingi, lakini bado wako kwenye huduma, hawajijui kuwa Mungu kawakataa,

Sasa basi kama karama hii ya kinabii ikifanaya kazi yake vema ndani ya kanisa kwa ujumla naamini Mungu aliyemtokea Belshaza hataleo hii anaweza kufanya zaidi ya alivyo mfanyia Belshaza, Ebu, itake karama hii kwa Mungu, ili kanisa lake lipate kujengwa, hebu acha kumwekea Mungu mipaka yakusema nawe, usitake maono ya kulala usingizi tu, jiachie kwake ili akuonyeshe maono ya wazi wazi, Fahamu inawezekana kabisa, tatizo liko kwetu, hofu na kutokuamini ndivyo vitu vinavyo waloga watoto waMungu wengi sana, Mungu akitaka kuwaonyesha jambo huwawengi hukimbia, au hukataa, kwa kuwa watoto wa Mungu wengi sana wana jihisi uwepo wa shetani zaidi kuliko kujihisi uwepo wa Mungu katika maisha yao, hebu yasilize maneno haya ya Mungu katika kitabu cha **(YEREMIA 23:23) " Mimi ni Mungu aliye karibu, asema Bwana, mimi si Mungu aliye mbali, "** Mungu wetu ni Mungu aliye karibu yetu sana kuliko kitu chochote kile kilicho karibu yetu, kwa hiyo sisi kama watoto wake tunatakiwa kila wakati tuhisi uwepo wake kuliko uwepo wa kitu kingine, Fahamu Roho Mtakatifu yu ndani yako, na wewe ukondani yake, sasa ondoa hofu, na ukiiondoa hiyo hofu, Mungu kusema nawewe kwa kukuonyesha Maono ya namna hii yaani ya waziwazi fahamu ni kitu rahisi kabisa, watoto wa Mungu wengi ni waoga sana, na kunawengine wamemwekea Mungu mpakawa kusema nao, wengine wamesema hawataki kuonyewsha jambo lolote lile, kwa sababu zao binafsi, fahamu Mungu ni Mungu anaechunguza mawazo na nia ya mwanadamu, akigundua nia yako wewe ni kama hii ya kutotaka kuonyeshwa jambo lolote lile la waziwazi, Basi fahamu hatakulazimisha, ukisoma maneno ya Mungu, utaona Musa alikuwa hajasema kuwa Mungu nataka nikuone, lakini Mungu aliigundua nia ya ndani ya Musa, ndio akamwambia kuwa **"Akasema, nakusihi unionyeshe utukufu wako. Akasema nitapitisha wema wangu wote mbele yako, nami nitalitangaza jina**

la Bwana mbele yako; nami nitamfadhili yeye nitakaye mfadhili;nitamrehemu yeye nitakayemrehemu, kisha akasema, Huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi, Bwana akasema, Tazama, hapa pana mahali karibu nami, nawe utasimama juu ya mwamba, kisha itakuwa wakati unapopita utukufu wangu, nitakutia katika ufa wa ule mwamba. Na kukufunika kwa mkono wangu, nawe utaniona nyuma yangu, bali uso wangu hautaonekana" (KUTOKA 33:18-23)

Mungu aliujua moyo wa Musa ulivyo kuwa, alikuwa na nia ya kumuona Mungu, na Mungu aliamua kumwonyesha Musa nyuma ya mgongo wake alivyo, na Musa alimwona Bwana, kwa hiyo ndugu yangu ikiwa weweni mwaminifu kwa Bwana, Bwana anaweza kukuonyesha maono mbalinbali, ondoa hofu, Tatizo hilila watumishi wa Mungu wengi kuwa na hofu ya kuonyeshwa maono ya wazi wazi lilianza tokea zamani, watumishi wengi siku zile waliokuwa wakionyeshwa maono ya namna hiyo waliogopa sana na kujihisi kuwa watakufa, ona mfano wa Gideoni, fungua, kitabu cha, **(WAAMUZI 6:22-23) "Gideoni akaona ya kuwa ni malaika wa Bwana; Gideoni akasema, Ole wangu, Ee Bwana Mungu! Kwa kuwa nimemwona Bwana uso kwa uso. Bwana akamwambia, Amani iwe pamoja nawe; usiogope; hutakufa.** Fahamu ndugu yangu kuwa Gideoni alikutana na malaika wa Bwana, na alikutananaye usokwa uso, na walizungumza kabisa, na malaika huyo wa Bwana alimletea Gideoni neno lililotoka kwa Mungu au unabii, baada ya kupokea ujumbe huotu, Gideoni, aliingiwa na hofu sana, alijihisi kuwa huenda atakufa kwa sababu ameona maono yaliyo waziwazi, Mungu alipouona moyo wa Gideoni ulivyojaa hofu, aliiamua kumtumia ujumbe mwingine wa kumtia moyo kuwa asiogope hata kufa, hata leo hii, watoto wa Mungu wengi sana wana hofu sana ya kuonyeshwa maono yaliyo ya dhahili, nataka nikutie Moyo ndugu yangu, usiogope, ikiwa Bwana amekupatia karama hii ya unabii, au amekupatia huduma [ofisi] ya unabii, unatakiwa usimwekee Mungu mipaka ya kusema nawewe, pia usiwe na mazoea ya kutegemea kuwa atasema nawewe kwa namna anayosema na wewe siku zote, fahamu, anaweza kusema nawewe kwa njia yoyote ile, kama ni kwa sauti, au kwa maono ya waziwazi au kwa maono na ndoto za usiku, usimwekee mipaka, watoto wa Mungu wengi sana huwa na maombi ya kumwomba Mungu asemenao, na wengi wanafikili kuwa atasema nao kwa kupitia Biblia tu, au kwa kumsikiliza mtumishi Fulani wa Mungu akimhubiria, lakini fahamu Mungu anaweza akasema na nawewe kwa njia ya maono ya waziwazi kabisa, Mungu anatakakutuonyesha mambo mbalimbali kama ya ulinzi wake kwetu, au maagizo maalumu anayotaka tuyajue ili tuyafanye katika maisha yetu ya wokovu, au ya kiutumishi, anaweza akasema na wewe kwa kutumia maono yaliyodhahili kabisa.

"Nakumbuka wakati Fulani siku chache tu baada ya mimi kumpokea Yesu Kristo moyoni mwangu, Mungu alinionyesha ono la waziwazi kabisa, nakumbuka nilikuwa nimekwenda nyumbani kwa Mama yangu mkumbwa, kumsaidia kutengeneza nyumba yake, kwa kupaka rangi, kazi tuliyoimaliza usiku wa manane, Baada ya kuimaliza ile kazi, ikanibidi nilale pale nyumbani kwa mama yangu mkubwa, kwa sababu safari ya kutoka pale nilipokuwepo kwenda nyumbani kwangu ilikuwa mbali kidogo, na usiku ulikuwa ndio umeingia, Basi, kabla sijalala nilimwomba Mungu anilinde usiku huo, na baada ya maombi nikalala, baada ya kulala, nikiwa usingizini, nilijisikia mwili wangu ukisisimka sana, nikaamka, na baada ya kuamka nikafanya maombi, nikizipinga nguvu za giza, baada ya kufanya hivyo, nikalala tena, hali hiyo ikaludia tena, nikaamka na kukemea sana, baada ya kukemea, nikalala tena, nikiwanimelala, hali hiyo ikatokea tena, safari hii ilitokea kwa nguvu sana, nikaita Yesu ni kiwa usingizini, na nikaamka toka usingizini, na nilipoamka tu,

nikashangaa sikuweza kutoa sauti, wala kuinuka, fahamu nilikuwa macho, naona kilakitu, nikaona mfano wa mtu, anaweza kwenda au kupita au kupenya ukutani, kama moshi vile ulivyo ndivyo alivyokuwa, mtu huyo alikuwa anania ya kunifuata pale nilipo lala, mimi nikawa namwangalia jinsi anavyoangaika kunifikia pale nilipolala, akinifuata ubavuni, kushoto na kulia, juu na chini, akaangaika hivyo kipindi kilefu sana, hawezi kunigusa ingawa alikuwa karibu sana na mimi, moyoni mwangu, niliogopa sana, lakini nilishindwa kuinuka au kupiga kelele, nikabaki naangalia tu, baadaye nikaona macho yangu yanafunguliwa, na kuanza kuona kitu kinacho mzuia huyo mtu asinikaribie, nilishangaa kuona kitu kama kioo, kimenizunguka kote, yaani niko ndani ya kioo hicho, na baada ya muda mlefu, huyo mtu akaondoka, na kioo hicho kikawepo tu nikikiona kwa uwazi kabisa nikiwa macho kipindi kilefu, na baada ya muda pia nacho kikapotea machoni pangu, na nikawa katik hali hiyo ya kutokusema na kutoamka pale kitandani kwa kipindi kilefu sana, ndipo baadaye, nikaona naweza kutanua kinywa changu, na kuweza kuinuka, nikainuka kitandani na kumshukuru Mungu, na kuomba ulinzi wake kwangu uendelee. Asubuhi kulivyokucha nikaondoka kwenda nyumbani, kwangu, siku hiyo yote nilikosa amani kabisa, nikiwaza nini hayo niliyoyaona?, jioni, ndipo, nilipopata jibu, kuwa Mungu alitaka kunionyesha jinsi alivyotuwekea ulinzi sisi watoto wake, kiasi ambacho adui, akija hawezi kutugusa kabisa, kwani Bwana ametuwekea ukingo kila mahali, kwani neno la Bwana lina sema hivi, " Ndipo, shetani akamjibu Bwana, na kusema, je ! huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? Wewe hukumzingira kwa ukingo pande zote, pamoja na nyumba yake na vitu vyote alivyo navyo?..." (AYUBU 1:9), Fahamu Bwana siku ile alitaka kunionyesha jinsi alivyoniwekea ulinzi mkubwa, ili nisiwe na woga wowote ule katika safari yangu ya kwenda mbinguni, inawezekana hata wewe ndugu yangu hujafahamu bado kuwa Mungu amekuwekea ulinzi mkubwa sana wewe na familia yako pamoja na mali yako yote kama alivyomuwekea Ayubu, fahamu, shetani aliifikia mali ya Ayubu, na mwili wa Ayubu kwa sababu ya ruhusa aliyopewa na Bwana, kabla yakupewa ruhusa hiyo alikuwa hana uwezo wa kumgusa Ayubu na mali yake yote, kwa hiyo ndugu yangu fahamu Mungu anaweza kutuonyesha maono ya waziwazi kabisa ili tupate kuyafahamu mambo yale aliyo tukilimia na yale anayotaka kutuagiza ilituyafanye, Basi karama hii ya unabii ikitumika kwa uzuri fahamu kanisa la Mungu litajengwa vizuri kabisa, Naamini Mungu amekufundisha vema kabisa katika sehemu hii ya maono yaliyo dhahili ambayo Bwana anaweza kumuonyesha mtu yeyote yule ili ujumbe wake upate kutufikia ipo mifano mingi katika Biblia inayo tuonyesha jinsi Mungu alivyo toa ujumbe kwa watu wale aliowakusudia wausikie kwa kuwa onyesha maono haya ya waziwazi au machomacho. Alisema na Kolnelio, alimtokea Joshua na kumwonyesha jemadari wa vita aliyenaye na kumtia moyo.

Ebu, tuendeelee mbele na tuone maono Yasiyo ya dhahili au yasiyo waziwazi, Maono ya namna hii ni yale ambayo Mungu anaweza kusema nawewe ukiwa umelala au umezimia, Ebu, tuangalie katika neno lake jinsi maono hayo yalivyo, Fungua **(MWANZO 15:8-21) "Akasema, Ee Bwana Mungu, nipateje kujua ya kwamba nitairithi? Akamwambia, Unipatie ndama wa miaka mitatu, na mbuzi mke wa miaka mitatu, na kondoo mume wa miaka mitatu, na hua, na mwana njiwa. Akampatia hao wote, akawapasua vipande viwili, akaweka kila kipande kuelekea mwenzake, ila ndege hakuwapasua. Hata tai walipotua juu ya mizoga Abramu akawafukuza. Na jua lilipokuwa likichwa uzingizi mzito ulimshika Abramu, hofu ya giza kuu ikamwangukia.Bwana akamwambia Abramu, ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo yake, watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia**

nne.Hata taifa lile, watakaowatumikia, nitawahukumu; baadaye nitawahukumu; baadaye watatoka na mali mengi.Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa amani, utazikwa katika uzee mwema.na kizazi cha nne kitarudi hapa, maana haujatimia uovu wa Waamori bado Ikawa jua lilipokuchwa likawa giza, tazama, tanuru ya moshi na mwenge unaowaka ulipita kati ya vile vipande vya nyama, siku ile Bwana akafanya agano na Abramu, akasema, uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huo mto mkubwa, mto frati, Mkeni, na mkenizi, na Mkadmoni na Mhiti, na mpelrezi, na Mlefai, na Mwamori, na Mkanaani, na Mgirgashi, na Myebusi."

Ukiyasoma maneno hayo ya Mungu utaona kuwa, Mungu aliamua kusema na Abrahamu kwa kutumia njia hii ya maono yaliyoletwa katika usingizi, Kumbuka, Abrahamu alikuwa na maombi maalumu kwa Mungu, akitaka kujua kwa uhakika maisha yake yeye na familia yake yatakuwaje, alimuuliza Mungu kuwa atapataje kujua kuwa ataairithi nchi hiyo ambayo Mungu amemwahidia kumpa, Mungu akasema naye kwa njia ya Neno lake moja kwa moja toka mbinguni, kuwa, Ibrahamu inampasa amtolee Mungu matoleo atakayomwagiza, na Ibrahamu, alimtii Mungu, akamtolea matoleo hayo, wakati amekwisha kumtolea, Mungu akaamua kusema na Ibrahamu, ili amjibu Ibrahamu swali lile alilokuwa amemuuliza, kuwa atajuwaje kuwa ataiirithi hiyo nchi, Mungu akamletea, Abrahamu usingizi mzito sana, na baada ya kumletea usingizi huo mzito sana, Mungu akaanza kumwonyesha na kumwambia Ibrahamu mambo yote yatakayo kuja mbele yake, alimwambia jinsi atakavyoirithi hiyo nchi, na alimwambia kuwa uzao wake ndio utakaoirithi hiyo nchi, na pia alimweleza jinsi uzao wake utakavyopata mateso mengi kutoka kwa taifa moja wapo, pia alimweleza jinsi atakavyo utoa uzao huo wa Ibrahimu katika hiyo nchi, pia alimweleza kuwa atawapa mali nyingi sana hao watoto wake, pia alimwonyesha jinsi mipaka ya hiyo nchi watakayoirithi hao wa uzao wa Ibrahimu, na Mungu akamweleza Ibrahimu mwisho wake yeye utakuwaje, na Mungu alimwonyesha Ibrahimu mwenge unaowaka na tanuru la moshi, na siku hiyo Mungu akafunga Agano na Ibrahimu la kuwapa uzao wake hiyo nchi, Mungu aliamua kusema siku ile na Ibrahimu kwa kutumia njia hii ya maono yasiyo ya waziwazi, bali alimletea Ibrahimu usingizi mzito sana, na baada ya kumletea usingizi huo ndipo alipoanza kusema naye na kumuonyesha mambo hayo makubwa sana, kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu wazi kuwa Mungu anaweza kusema na wewe kwa kutumia maono ya namna hii, ukaonyeshwa vitu ukiwa usingizini, haijalishi ni mchana au ni usiku, Ukisoma maneno ya Mungu katika Maandiko matakatifu, utaona wazi kuwa mara nyingi Mungu amesema na watumishi wake kwa kutumia njia hii, Ebu, Fungua **(DANIELI 10: 11) " Walakini nilisikia sauti ya maneno yake; nami niliposikia sauti ya maneno yake, ndipo nikashikwa na usingizi mzito, na uso wangu umeelekea nchi. Na tazama, mkono ukanigusa, ukaniweka juu ya magoti yangu, na vitanga vya mikono yangu, akaniambia Ee Danieli, mtu upendwaye sana, yafahamu maneno nikuambiayo, ukasimame kiwima –wima; maana nimetumwa sasa".** Danieli siku moja alikutana na Mungu akiwa katika mapumziko yake pamoja na jamaa zake katika mto wa Hidekeli, siku hiyo Danieli ghafla akashangaa anaona maono ya waziwazi kabisa, na alipoyaona maono hayo na kusikia sauti ya huyo aliyesema naye yaani Bwana, Danieli anasema alishangaa alipata usingizi mzito sana, na baada ya kupata huo usingizi, ndipo alipoambiwa maneno mengi na Bwana na baada ya hapo akasimama kiwima-wima, Kwa hiyo ndugu fahamu Mungu anaweza kusema au kukuonyesha wewe jambo lolote lile ukiwa usingizini, na usingizi huo Mungu ndiye anayekuletea.

Mara nyingi Mungu amekuwa akisema namimi kwa njia hii pia, Nakumbuka siku moja, nilikuwa na kipindi mimi binafsi cha maombi mbele za Mungu, na siku hiyo niliomba maombi mbalimbali, mojawapo ya maombi hayo, nilikuwa naliombea kanisa, yaani ndugu zangu wote waliookoka, sasa nilipo kuwa katika hayo maombi, Bwana siku hiyo alinishushia nguvu ya maombi sana, nikaanza kuomba kwa akili kwanza, na baadaye, Roho Mtakatifu akaanza kuugua ndani yangu, ni kaanza kuomba kwa lugha, nikaomba kwa muda mlefu kidogo ila kwa nguvu sana, nikashangaa, ghafla, usingizi mzito umenitokea, na nikashindwa kuustahimili, nikaangukia kitandani nikalala, nilipolala tu, nikashangaa sipo chumbani kwangu, bali nimepelekwa kwenye jengo moja kubwa la kanisa ninalo lifahamu, na nikaonyeshwa mle ndani, kuna mtu mmoja amekaa, kiti cha mbele kabisa, na huyo mtu nikashangaa, anainuka na kuanza kutoka humo ndani ya kanisa, naalipotoka nje tu, nikaludishwa chumbani kwangu nilipokuwepo, na usingizi nikawa sina kabisa, nikaanza kutafakari, nini Maana yake? Nikasikia sauti ya Roho Mtakatifu, ikisema simama mbele za Mungu na umwombe akujulishe maana yake, Nikanyanyuka pale nilipokuwa nimelala, na kuanza kumwomba Mungu anijulishe maana ya maono hayo, Mungu alisema na mimi maneno haya, “mtu huyo ninamtwaa”, na mimi nilikuwa na mfahamu ndugu huyo, kipindi hicho alikuwa ni mzima kabisa, basi, akili yangu harakaharaka ikataka kunifanya nianze kuipinga roho ya mauti juu ya mtu huyo, nilipokuwa nataka kuanza maombi hayo tu, nikaambiwa, omba hivi, “Baba Mungu katika jina la Bwana Yesu Kristo mapenzi yako ya timizwe katika suala hili”, ni katii, nikaomba hivyohivyo, nilipoomba hivyo, nikaambiwa tena, “ omba hivi Bwana unanitaka nifanye nini katika suala hili?), nikatii, nikaomba hivyo tena, Bwana akaniambia mwombee kila siku, nikaanza maombi juu yake siku ileile, na Bwana aliniongoza ni mwombee “toba” basi kila siku nikawa na mwombea huyo ndugu, na zaidi nikimwombe awena moyo wa kutengeneza na kutubu uovu wake wowote ule utakaomzuia asifike mbinguni, na mtu huyo alikuwa ni miongoni mwa watu waliompokea Yesu siku nyingi, na alikuwa anaheshimika sana, ndani ya kanisa, baadaya miezi miwili hivi, nikapata habari kuwa huyo ndugu anaumwa, na sikuwahi kumweleza mtu habari hii aliyoniambia Bwana, kwani Bwana hakunipa ruhusa ya kumwambia mtu yeyote yule, na siku moja nilikwenda kumtembelea mchungaji nyumbani kwake, na mchungaji aliponiona, akasema mwanangu afadhari umekuja, kwani kuna jambo lililoniuzunisha sana ndani ya moyo wangu, nikamwambia ni jambo gani hilo? Mchungaji akaniambia hivi, unamfahamu mtu Fulani, yaani huyo ndugu niyeambiwa habari zake na Bwana, nika sema ndio, akasema unahabari kuwa anaumwa sana, na watu wamefanya maombi sana lakini hajapona bado, mchungaji akaendelea kunieleza kuwa huyo mtu alimwita mchungaji, na akamwomba mchungaji amwombee kwa Mungu msamaha, kwani huyo mtu ingawa alikuwa amemkiri Yesu kuwa ni Bwana na mwokozi wa maisha yake lakini kuna dhambi moja alikuwa hajaitubia au kuiacha aliendelea kuitenda, nayo ni dhambi ya uchawi, na akasema mambo mengi sana mabaya aliyoyafanya, akiwa ndani ya ukristo, kwa kweli ilinishangaza sana habari hiyo, na mchungaji akasema kwa kweli habari hiyo imemsikitisha sana, hakutegemea kusikia maneno kama hayo kutoka kwa mtu huyo, jinsi alivyokuwa anaonekana ndani ya kanisa, baada ya kuondoka kwa mchungaji, Mungu alisema na mimi kuwa, ndio maana nilikuambia mwombee sana mtu huyo, kwani alikuwa na dhambi hiyo ingawa alikuwa na juhudi sana ya kufanya kazi yangu, nilimshangaa sana Mungu, na tokea siku hiyo nikajifunza sana kuwa kweli Mungu hapendi mtu yeyote yule apotee, bali kila mtu anataka afikilie toba, pia nikajifunza kuwa upendo alionao Mungu ni wa kipekee, kwani, alimuhurumia sana huyo mtu, na akanipa neno la kinabii mimi kwa njia ya maono ya kuletewa usingizi ili nifanye maombi maalumu ya kumwombea huyo mtu ili atubu, na mimi sikujua huyo mtu ana dhambi gani, na nikafahamu kuwa Mungu alinipeleka kwa

mchungaji kufahamu kuwa huduma aliyo nipa tayari imefanyika, kwani kitendo cha huyo mtu kutubu ndicho Mungu alicho kitaka huyo ndugu akifanye, na baada ya kama siku mbili baada ya huyo mtu kutubu, akafariki. Kumbuka alitubu

Fahamu Mungu anaweza kusema na wewe kwa kuitumia njia hii ya maono yasiyo ya waziwazi au machomacho, na anasema hivyo ili atujenge binafsi, au alijenge kanisa, nk, Mfano mwingine mzuri ni huu wa Petro fungua kitabu cha **(MDO 10 :9-10) "Hata siku ya pili, walipokuwa wakisafiri na kuukaribia mji, Petro alipanda juu darini, kwenda kuomba, yapata saa sita ya mchana; akaumwa na njaa sana, akataka kula;lakini walipokuwa wakiandaa, roho yake ikazimia akaona mbingu zimefunuka, na chombo kikishuka kama nguo kubwa, inatelemshwa kwa pembe zake nne hata nchi; ambayo ndani yake walikuwemo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na hao wataambaao, na ndege wa angani kisha sauti ikamjia, kusema, ondoka, Petro, uchinje ule. Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi.na sauti ikamjia mara ya pili, ikamwambia, vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi, jambo hili likatendeka mara tatu; kisha chombo kikapokewa tena mbinguni"**

Mungu alikuwa anataka kuzungumza na Petro siku hiyo, akamletea Petro njaa kali sana, kiasi ambacho Petro, akazimia, na alipokuwa amezimia tu, Mungu akamletea Petro maono na kusema naye kwa sauti, utaona hapo kuwa Mungu aliitumia njia hii ili aweze kusema na Petro habari muhimu sana ambayo alitaka Petro aijue, kwa hiyo basi, ikiwa wewe unayo karama hii ya unabii, Mungu anaweza kusema na wewe kwa kutumia njia hii, atakuletea Usingizi, mzito au utaweza kuzimia, na hapo Mungu akaamua kusema na wewe, **Nimewaona watu wengi sana Mungu akiwahudumia kwa kuwaletea usingizi, mzito, kama alivyo fanya kwa Adamu siku ile Bustanini, nakumbuka siku moja, Dada yangu ninaemfuata kwa kuzaliwa, alikuwa mjamzito, na ilionekana kuwa anauvimbe tumboni, na ma Daktari waliamua kumfanyia upasuaji, na kwa kweli walisema wazi kuwa kutakuwa na hatari sana kwa kiumbe kilicho tumboni, sasa baada ya mimi kuisikia habari hiyo, nikasikitika sana, nikamwomba Mungu auondoe uvimbe huo, na Mungu alinipatia neno lake kuwa alimfanyia upasuaji Adamu na kuuondoa ubavu wake, kwa hiyo inawezekana kabisa yeye Mungu kumfanyia Dada yangu upasuaji huo na kuondoa uvimbe huo, Basi kesho yake nika washirikisha ndugu zangu kuwa tutakuwa na maombi maalumu mbele za Mungu, ili amfanyie Dada yetu upasuaji, na kuuondoa uvimbe, na nikalisoma neno lile kuwa Mungu alimletea Adamu usingizi, na kumtoa ubavu, na nikawakumbusha kuwa Mungu yule aliyefanya huduma ile yuko hata leo, basi twendeni tuka mwite afanye huduma hiyo leo, Tulipokuwa katika maombi, na nilipomwekea mikono, ghafla, alilala usingizi mzito sana, na tukamuacha hapo, akiwa amelala tuka mshukuru Mungu, na tukaondoka na kuendelea na shughuli zingine, jioni nilipoludi ili nikamtake hari, nikamkuta ndio kwanza ametoka kuamka, akaniambia kuwa anajisikia tumboni sehemu ulipokuwepo uvimbe panamuwasha sana, na kwa sababu uvimbe huo ulikuwa ndani ya tumbo, alishindwa kujikuna, na baada ya masaa mengi kupita kuwasha huko kukakoma kabasa, na maumivu aliyokuwa nayo kabla hatujamuombe yakawa yametoweka, na baadaye alikwenda kuwaona madaktari wakamchunguza wakagundua hana tatizo tena, na alijifungua salama kabisa, na ni mzima mpaka leo hii, na akajariwa mtoto mwingine,** Kwa mfano huo, Mungu aliendelea kunifundisha kuwa, anaweza kutuhudumia, na hata kusema nasisi tukiwa usingizini.

Kwa hiyo ndugu yangu fahamu kuwa Bwana ana weza kulituma neno lake(unabii) kwa kutumia njia hii, akakuletea usingizi mzito na kukuonyesha au kusema na wewe jambo Fulani, nimatumaini yangu kuwa katika sehemu hii Mungu amekufundisha kwa uzuri kabisa na umepata kitu chema kabisa, Kwa hiyo ndugu yangu fahamu kuwa ukiwa na karama ya kinabii Mungu anaweza kusema nawewe kwa njia mbalimbali na njia mojawapo anayoweza kuitumia kukuletea neno lake ni hii njia ya maono na ndoto, basi unatakiwa uwe makini sana katika eneo hili, jifunze kuyaandika maono unayoyaona, na kuyachunguza kwa upana, uenda ukawa unapata majibu ya maombi yako au, ukawaunaletewa taarifa Fulani toka mbinguni, neno la Bwana lina sema hivi, **" Bwana akanijibu, akasema, iandike njozi, ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, iliaisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni wakati ulioamuriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake; bado niwakati ulioamuliwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake; wala haitasema uongo;ijapokawia, ingojee, kwa kuwa haina budi kuja haitakawia" (HABAKUKI 2:2)** Pia nawe ndugu yangu fanya hivi kila mara utagundua kuwa Mungu anasema na wewe na kukujulisha habari mbalimbali kila mara uwapo usingizini

YAHIFADHI MAONO UNAYOPEWA NA BWANA

Ili Mungu apate kukuonyesha maono mbalimbali katika maisha yako, unatakiwa, usiwe mlopokaji kwa kuyasema yale Mungu amekuonyesha kwa watu wengine, bila kibali cha Mungu, Mungu anapenda sana kutuambia na kutuonyesha mambo mbalimbali, lakini, kutokana na uchanga au udhaifu wa watoto wa Mungu wengi kutokuwa watunzaji wa siri za Mungu, Mungu anaacha kuwaambia na kuwaonyesha watu hao mambo mbalimbali aliyotaka kuwaambia au kuwaonyesha, Neno la Mungu linatufundisha hivi, **"Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu." (1KOR 4:1)**

Neno la Mungu linatufundisha hapo kuwa, tunatakiwa kuwa Mawakili wazuri wa siri za Mungu, fahamu, kila mtu aliyempokea Yesu Kristo ni mwakili wa siri za Mungu, sasa Mungu anatafuta watu ambao ni watunzaji wa siri zake, Sasa ili Mungu asikufiche jambo lolote wewe, au ili Mungu akutumie wewe kwa uzuri katika karama hii ya unabii, unatakiwa uhakikishe unakuwa mtunzaji mzuri wa siri zote za Mungu atakazokuonyesha au kukuambia wewe binafsi katika maisha yako au katia huduma yako, au katika kanisa lake, Watoto wa Mungu wengi kwa kutokuwa watunzaji wazuri wa siri za Mungu, wamejikuta wakiwa katika matatizo makubwa sana katika maisha yao ya wokovu, na hata pengine huduma ile ambayo Mungu alitaka kuifanya kwa kupitia wao ikawa ni ngumu mno kukubalika kwa sababu ya uzembe wa mpokea ujumbe kutoka kwa Bwana, hakuwa makini katika kuyatunza yale yote aliyoambiwa na Bwana, Ona mfano huu wa jinsi Yusufu alivyopata shida baada ya kuonyeshwa na Mungu habari za kuinuliwa kwake katika maisha yake ya mbeleni, Neno la Bwana lina sema **" Yusufu akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia; akawaambia, Tafadhalini, sikieni ndoto hii niliyoiota. Tazama, sisi tulikuwa tukifunga miganda shambani, kumbe! Mganda wangu ukaondoka ukasimama, tazama, miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu. Ndugu zake wakamwambia, Je! Kweli wewe utatumiliki sisi? Nawe utatutakawala sisi? Wakazidi kumchukia kwa ajili ya ndoto yake, na kwa maneno yake Akaota tena ndoto nyingine, akawaambia ndugu zake.akasema, Angalieni nimeota ndoto nyingine; na tazama, jua na mwezi na nyota**

kumi na moja zikaniinamia.Akamwambia baba yake na ndugu zake; baba yake akamkemea akamwambia, Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je! Mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi? Ndugu zake wamhusudu; bali baba yake akalihifadhi neno hili (MWANZO 37:5-11)

Yusufu alionyeshwa ndotoni jinsi Mungu alivyombariki katika maisha yake ya mbeleni, na Mungu alimuonyesha yeye Yusufu siri hiyo, lakini Yusufu, akashindwa kuitunza siri hiyo na kuanza kuwaambia ndugu zake na baba yake mambo yote aliyoonyeshwa na Bwana, na matokeo yake, akajikuta anakemewa na kuchukiwa na ndugu zake, fahamu, Mungu anaweza kukuonyesha wewe habari za mambo unayotakiwa uyafanye wewe, sasa usifikiri kila mtu anatakiwa ayajue mambo yote aliyokuambia Mungu, au leo hii Mungu kakuambia habari zinazomhusu mtu Fulani, hautakiwi wewe uende ukamwambie habari hizo mtu mwingine, fahamu, Mungu kakupa siri wewe na kakuamini wewe, na kakutuma wewe, ili labda ukamwonye mtu huyo, au ukamwambie habari zozote alizokuagiza Mungu ukamwambie mtu huyo, hautakiwi ukamwambie mtu mwingine habari hiyo, Watu wengi walio na karama hii ya unabii hawakubaliki mbele za watu kwa sababu wakiisha kuambiwa habari fulani na Bwana wana kwenda mbio kuyasema hayo walioambiwa kwa watu au sehemu ambayo Mungu hakutaka wakaseme, na matokeo yake karama hii ya unabii inaonekana kama ni mbaya na ya ufitini, au yakujifuna na kujionyesha, Nimewaona watu wengi sana wakisimama mbele za watu na kusema Mungu, kaniambia kuwa mwaka huu atanipa Gari, na fedha nyingi sana, nk, kwa Haraka –haraka utaona kuwa huyo ndugu ana upendo sana kwa hao ndugu zake, ndio maana kawaambia, fahamu, huyo mtu angelijua, akalihifadhi neno hilo moyoni mwake, na kulisuburi ingelikuwa ni bora sana, kuliko kulopoka hovyo kwa ndugu zake, Yusufu, alipoisema ndoto ile kwa ndugu zake, alitegemea kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa ndugu zake, matokeo yake, ndugu zake wakamchukia na kutafuta kumuua, mwishowe wakaamua kumuuza, kisa ni kwa sababu alishindwa kuhifadhi siri aliyopewa na Bwana, kwani hata sikuile nduguze walipomuuza walisema **" Yule mtu akasema, wametoka hapa, maana niliwasikia wakisema, twendeni Dothani. Basi Yusufu akawafuata ndugu zake akawakuta huko Dothani.Wakamwona toka mbali, na kabla hawajakaribia, wakafanya shauri juu yake ili wamwue.wakasemezana wao kwa wao, Tazama, yule bwana wa ndoto anakuja. Haya, twende, tukamwue na kumtupa katika birika mojawapo, nasi tutasema, mnyama mkali amemla; kasha tutaona zitakuwaje ndoto zake." (MWANZO 37: 17-20)**

Ndugu zake Yusufu walitaka kumuua ili wazikomeshe ndoto zake, kwa hiyo ndugu yangu ebu, jifunze kuanzia leo hii kuwa mtunzaji wa siri Zote Ambazo Mungu kakuonyesha iwe kwenye ndoto au kwenye maono au kwa sauti yake, ili kuzuia matatizo mengi yanayoweza kukukuta kutoka kwa watu wabaya wasiopenda maendeleo yako, fahamu unaweza kujicheleweshea baraka zako au hata kuihalibu huduma yako kwa kusema kwako yale Mungu aliyokuambia wewe kwa mtu yeyote yule pasipo kibari kutoka kwa Bwana, neno la Bwana lina sema **"Jihadhari kila mtu na jirani yake; wala msimtumaini ndugu awaye yote; maana kila mtu atachongea, na kila jirani atakwenda huko na huko na kusingizia. Nao watadanganya kila mtu jirani yake, wala hawatasema kweli…"(YEREMIA 9:4-5)**

Jihadhali sana ndugu yangu katika eneo hili, usimwamini kila mtu ukafiri ana kupenda na anakutakia mema, Bwana analifahamu sana jambo hili, ndio maana anaonya kuwa unatakiwa ujihadhari, fahamu unapomshirikisha maono yako uliyopewa na Bwana mtu

yeyote yule bila kibali cha Mungu, fahamu mtu huyo ibirisi anaweza kumtumia kukuharibia baraka zako au huduma yako, Watu wengi wameambiwa na Bwana kuhusu huduma zao zitakavyokuwa huko mbeleni, na wao bila hata ya kutulia au kuhifadhi siri hiyo, hukimbia mbio na kuwashirikisha wachungaji wao au rafiki zao, matokeo yake, wamejikuta wamepata upinzani mkali kutoka kwa hao watu waliowatumaini na kuwaeleza siri zote za Mungu alizowaambia. Fahamu hata mchungaji wako hapaswi kujua kila jambo alilokuambia Mungu kuhusu huduma yako ya mbeleni, Hivi hujaona leo hii watu wakigombana na wachungaji wao kwa sababu mchungaji anamfanyia mtu huyo fitina katika huduma yake? Fahamu inawezekana kabisa matatizo hayo yote yamekuja baada ya mchungaji kufahamu ndoto au maono ya mtumishi huyo, kuwa ni makubwa kuliko yake, anaamua kumfanyia fitina mtumishi huyo ili ndoto zake zisifanikiwe, kwa hiyo ndugu usiwe mwepesi wa kusema bali uwe mwepesi wa kusikia, sema pale unapokuwa umeruhusiwa kusema, watu wengi kwa sababu ya kusema mambo ya siri walizopewa na Mungu, hujikuta wanamzuia Mungu asifanye kazi ile aliyotaka aifanye kwa kuwatumia watu hao, Ona mfano huu, **" Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, Ukitaka, waweza kunitakasa, Naye akamhurumia, akanyoosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika. Na mara ukoma wake ukamtoka, akatakasika. Akamkataza kwa nguvu, akamwondoa mara, akamwambia, Angalia, usimwambie mtu neno lolote. Ila enenda zako ukajionyeshe kwa kuhani, ukatoe alivyoamuru Musa kwa kutakasika kwako, iwe ushuhuda kwao. Lakini akatoka, akaanza kuhubiri maneno mengi, na kulitangaza lile neno, hata Yesu asiweze tena kuingia mjini kwa wazi;bali alikuwako nje mahali pasipokuwa na watu, wakamwendea kutoka kila mahali." (MARKO 1l:40-45)**, Ikiwa wewe ndugu yangu unayo karama ya unabii, uhakikishe unatunza siri sana ya maneno aliyosema nawe Bwana katika maono au ndoto alizokupa Bwana, ikiwa ni kwa ajiri ya kupeleka ujumbe sehemu Fulani, basi peleka sehemu hiyo, wala usipeleke sehemu nyungine kama huyo mtu alivyofanya, Bwana alimwambia apeleke ujumbe kwa kuhani, yeye akaanza kuwaambia watu wengine, kwa kitendo hicho alimzuia Yesu asifanye huduma vizuri katika mji ule, inawezekana hata kwetu leo, tusipokuwa mawakili wazuri wa siri za Mungu, tutaiharibu huduma ambayo Bwana anataka kuifanya kupitia sisi. Pia unaweza ukajikuta unapata upinzani mkubwa wa kutokukubarika kwa sababu uliwaambia watu wasiostahili kufahamu mambo yote aliyokuambia Mungu kama Yusufu alivyofanya.

Nakumbuka siku moja Mungu aliniambia kuwa ninatakiwa nisiwashirikishe watu wengine habari zozote zinazohusu baraka zangu, ambazo Mungu ameniahidia kunipa, kweli baadaye ndipo nilipo kujakufahamu kwanini Mungu alinikataza nisiwashirikishe ovyoovyo watu wengine habari za baraka zangu alizoniahidi Bwana kunipa, baada ya wale niliowaambia habari hizo kuanza kunifanyia mambo mabaya sana kwa kutaka kuzuia baraka hizo, namshukuru Mungu ambaye, alikwenda kunipatia baraka hizo, lakini chamoto nilikiona kutoka kwa watu hao niliowashirisha habari hizo, ili waniombee, na nilifikili watanifurahia, kumbe nilikosea, wakaanza kunichukia sana, ndipo Bwana aliponiambia usimshilikishe kila mtu, habari za maono ninayo kuonyesha, bali mshirikishe mtu yule ntakaye kuambia mshirikishe, kwa hiyo ndugu yangu, peleka ujumbe mahali pale ulipoagizwa, hifadhi siri ile Mungu aliyokuonyesha, ikiwa ni habari zinazo Muhusu mtu fulani basi mpelekee mtu huyo, na usiitoe habari hiyo kwa mtu mwingine. Ukiyafanya hayo fahamu, Mungu atakuambia mambo mengi kwa ajiri ya kanisa lake, na kwa huduma yako na kwa maisha yako na familia yako, na atakujulisha vema habari za baraka zako. Mungu akujalie msaada ili uwe mtunza siri za Mungu.

UONAPO MAONO USIYO YAELEWA MWOMBE MUNGU AKUFAHAMISHE

Fahamu si kila wakati utaonyweshwa na Mungu maono au ndoto utakazozielewa kwa haraka sana, Fahamu, Mungu anaweza kukuonyesha maono ambayo ni vigumu sana kuyaelewa, kwani Mungu amesema katika neno lake kwetu kuwa **"Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyeha mambo makubwa, magumu usiyoyajua." (YEREMIA 33:3)** Huondio ujumbe atupao Bwana kwamba, lazima tufahamu kuwa ametuahidi tukimwita, au tukimwomba atatuitikia na kutupatia kile tulicho mwomba, na anatufahamisha kuwa atatonyesha mambo makubwa na Magumu ambayo hatuyajui. Kwa maana hiyo ndugu yangu unatakiwa ufahamu kuwa Mungu anaweza kukuonyesha mambo ambayo yatakuwa wazi kwako na ukayaelewa kwa haraka sana, yaani ndoto au maono yanayo eleweka, pia fahamu anaweza akakuonyesha maono magumu usiyo yaelewa kabisa, yaani ni kama mafumbo yaliyofichika sana, kwa mfano ebu, mwangalie Petro jinsi siku ile Bwana anamwonyesha maono ya kwenda kwa Kornelio, alimwonyesha Nguo iliyojaa wanyama mbalimbali, na Mungu akamwambia Petro achinje ale, Petro akakataa, kwa sababu wanyama hao aliwaona kuwa ni wanajisi, na Mungu akamwambia Petro kuwa, alichokiumba Mungu asikiite kuwa ni najisi, Baada ya maono hayo neno la Bwana linasema Petro akaanza kutafakari, nini maana ya maono haya?

Fungua, **(MDO10:17-23) "Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya nafsi yake, maana yake ni nini maono hayo aliyoyaona, wale watu waliotumwa na Kornelio, wakiiisha kuiulizia nyumba ya Simoni, wakasimama mbele ya mlango, wakaita; wakauliza kwamba Petro anakaa humo.Na Petro alikuwa akiyafikiri yale maono.Roho akamwambia, wako watu watatu wanakutafuta.Basi ondoka ushuke ufuatane nao, usione tashishwi, kwa maana ni mimi niliyewatuma.Petro akawashukia wale watu, akanena, Mimi ndiye mnayemtafuta.Mmekuja kwa sababu gani, wakasema, Kornelio akida, mtu mwenye haki, mchaji wa Mungu, aliye na sifa njema kwa taifa lote la Wayahudi, alionywa na malaika mtakatifu kutuma watu kwako, uende nyumbani kwake, apate kusikiza maneno kwako.akawakaribisha wawe wageni wake"** Petro alipoyaona maono yale alikuwa hayafahamu kabisa, yalikuwa na mafumbo ambayo Mungu alimfumbia Petro, na Petro alipokuwa akitafakari maana ya maono hayo, Roho mtakatifu akamwambia kunawatu watatu wanakutafuta, unatakiwa ufuatane nao, na watu hao ndio waliotumwa kutoka kwa Kornelio, na fahamu Kornelio alikuwa ni mtu wa mataifa, hakuwa Myahudi, na kipindikile mtu yeyote yule asiyekuwa Myahudi alihesabika kuwa ni mtu najisi, sasa Mungu alikuwa anataka kumtuma Petro aende kwa Mtu ambaye kisheria alihesabika kuwa ni najisi, na Mungu alijua kuwa Petro bila kupewa taarifa kuwa Mungu anataka aende kwa mtu huyo atakataa kwenda ndio maana akaamua kumletea maono hayo, na kweli Petro alikataa, na wakati anayatafakari maono hayo na kutaka kujua maana yake ni nini, Mungu akamwambia kunawatu wanaokutafuta, na watu hao walikuwa ni wamataifa, Baada ya hapo Petro akafahamu kuwa Mungu alitaka kumtuma kwa mtu ambaye katika utaratibu wa kiyahudi ni mtu najisi, akafahamu kuwa Bwana anataka Petro aende uko, na Petro akaenda na kuifanya kazi aliyotumwa na Bwana, soma kitabu hiki cha matendo ya mitume sura nzima ya kumi, utaelewa kwa uzuri sana habari hii.

Kwa hiyo ndugu yangu fahamu Mungu anaweza kukuonyesha Maono magumu usiyo yajua kabisa, na uyaonapo maono hayo au uotapo ndoto kama hizo, tafuta kuyafahamu, Neno la Bwana linatufundisha wazi kuwa Nabii Danieli, alipokuwa ameonyeshwa maono asiyo yajua alitafuta kuyafahamu mbele za Mungu, neno la Bwana linasema hivi, **"Ikawa**

mimi, naam, mimi Danieli, nilipoyaona maono hayo, nalitafuta kuyafahamu, na tazama, alisimama mbele yangu mmoja mfano wa mwanadamu., Nikasikia sauti ya mwanadamu katikati ya mto Ulai, iliyoita na kusema, Gabrieli, mfahamishe mtu huyu maono haya" (DANIELI 8:15-16). Danieli Alikuwa ameonyeshwa na Mungu maono Fulani, ambayo hakuyafahamu, Danieli anasema baada ya kutokuya fahamu maono hayo, alitafuta kuyafahamu, na kwa kuwa alitafuta kuyafahamu maono hayo, Mungu akamtuma malaika wake mtakatifu aitwaye Gabrieli ili amfahamishe Danieli maana ya maono hayo, fahamu hata kina Danieli manabii wazuri kabisa, walikuwa wanaonyeshwa maono magumu, ambayo hawakuwa wanayajua, Watoto wengi sana wa Mungu, waliona karama ya unabii, wanapata shida sana ndani ya mioyo yao kwa sababu ya ndoto au maono wanayoyaona, kwani yamekuwa magumu, hawayaelewi kabisa, na wengi kwa kuwa hawayafahamu huyaacha hivyo hivyo, na kupotea ujumbe waliopewa na Bwana,

Tatizo hili hata mimi nilikuwa nalo kabla Bwana hajanifundisha kuwa ninatakiwa nitafute kuyafahamu maono yale anayonionyesha Bwana, nilikuwa naona maono magumu sana Tena mengine waziwazi kabisa, lakini nilikuwa siyafahamu kabisa, nilikuwa nayaacha, lakini moyoni nilikuwa nakosa amani, kwa kujiuliza nini maana ya maono haya? Lakini sikuwa nachukua hatua ya kutafuta kuyafahamu kwa bidii, na kweli baada ya kuanza kutafuta kwa kuomba mbele za Mungu kwamba nifahamishwe maana ya Maono niliyoonyeshwa, Bwana alianza kunifundisha na kuniambia maana ya maono hayo, unatakiwa uwena bidii ya kutaka kufahamu maana ya maono yale uyaonayo yaliyo magumu yaani usiyoyafahamu, Mungu ni mwaminifu sana atakufahamisha tu, kwa kutumia njia Mbalimbali, anaweza akakufahamisha maana ya maono uliyo yaono kwa kukuletea maono mengine utakayo weza kuyafahamu, au anaweza kukufahamisha kwa kumtumia mtu aliye na Roho Mtakatifu, mfano mzuri upo kwenye kitabu cha **(Danieli 1:17) "Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima;Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto."**

Hata leo hii wapo watu waliojaliwa na Mungu kuwa na ufahamu kama huuo, na Mungu anaweza kuwatumia kukufahamisha maana ya ndoto au maono uliyopewa na Mungu, lakini nataka nikutie moyo, ikiwa Mungu anaweza kukuonyesha maono wewe au ndoto, fahamu anaweza pia kukufahamisha wewe mwenyewe maana halisi ya maono au ndoto alizokuonyesha, cha msingi uwena nia ya kutaka kuyajua, na unatakiwa utake kufahamishwa maana ya maono hayo kwa njia ya maombi kwa Mungu, Danieli alikuwa na tabia ya kufanya maombi ili Mungu amfahamishe maana ya maono aliyokuwa anayaona, **"Basi hapo nilipokuwa nikisema, na kuomba, na kuungama dhambi yangu, na dhambi ya watu wangu Israeli, na kuomba dua yangu mbele za Bwana, Mungu wangu, kwa ajili ya mlima mtakatifu wa Mungu wangu; naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza, akirushwa upesi, alinigusa panapo wakati wa dhabihu ya jioni. Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danieli, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu. Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari;maana wewe unapendwa sana;basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya." (DANIELI 9:20-23)**

Danieli alifahamishwa maana ya maono aliyoyaona baada ya kufanya maombi, Mungu akamtuma Gabrieli aende akampatie Danieli maana ya maono aliyoonyeshwa na Bwana, safari hii Gabrieli hakwenda kwa kupitia njozi, bali alikwenda ana kwa ana, na akamjulisha Danieli maana ya maono aliyokuwa ameonyeshwa.Basi ndugu yangu

unatakiwa uwe na tabia hii, hakikisha unatafuta kwa maombi kujua maana ya maono au ndoto usiyoijua ambayo Mungu amekuonyesha, unatakiwa pia uwe na subira ukiwa umemwomba Bwana akufahamishe maana ya maono uliyoyaona usiyoyafahamu, fahamu Mungu atakujibu kwa wakati wake, hakawii wala hachelewi, upo mfano mzuri sana kwenye neno la Mungu unao tufundisha sisi watoto wa Mungu kwamba tunatakiwa tuwe na subira, Mfano wenyewe ni huu, fungua kitabu cha. **(YEREMIA 42:1-7)"Ndipo maakida wote wa majeshi, na Yohana, mwana wa Karea, na Yezania, mwana wa Hoshaya, na watu wote tangu wadogo hata wakubwa, wakakaribia, wakamwambia Yeremia, nabii, Twakusihi, maombi yetu yakubaliwe mbele yako, utuombee kwa Bwana, Mungu wako, yaani, watu hawa wote waliosalia;maana tumesalia wachache tu katika watu wengi, kama macho yako yatuonavyo; ili kwamba Bwana, Mungu wako, atuonyeshe njia ambayo yatupasa tuiendee, na jambo litupasalo tulitende, Ndipo Yeremia nabiiakawaambia, Nimewasikia;tazama, nitamwomba Bwana, Mungu wenu sawasawa na maneno yenu; tena itakuwa, neno lolote ambalo Bwana atawajibu, nitawahubiri;sitawazuilia neno liwalo lote. Wakamwambia Yeremia, Bwana na awe shahidi wa kweli nauaminifu kati yetu;ikiwa hatufanyi sawasawa na neno lile, ambalo Bwana, Mungu wako, atakutuma, utuletee. Likiwa jema, au likiwa baya, sisi tutaitiii sauti ya Bwana, Mungu wetu, ambaye tunakutuma kwake;ipate kuwa faida yetu, tunapotii sauti ya Bwana, Mungu wetu.. Ikawa, baada ya siku kumi, neno la Bwana likamjia Yeremia"**

Yeremia nabii alimwomba Mungu awajulishe watu wake njia wanayotakiwa waipite na jambo lileambalo Mungu anataka walifanye, neno la Bwana linatufundisha kuwa, Yeremia alimwomba Mungu, na ilichukua siku kumi kupokea jibu toka kwa Bwana, Kwa hiyo ndugu fahamu kuwa hata leo hii unatakiwa uwe mvumilivu wa katika kusubiri kwako jibu kutoka kwa Bwana, fahamu, Bwana anaweza kukujibu siku ileile au anaweza kukujibu baada ya siku nyingi, kwa hiyo unatakiwa pia uwe na subira ya kusubiri majibu ya maombi yako utakayomwomba Mungu akufahamishe maono usiyo ya fahamu, Vumilia, endelea kumwomba mpaka atakapo kuwa amekujibu, fahamu Mungu ni mwaminifu sana, naamini atakufahamisha tu, natumaini, umeielewa vema sehemu hii ya kuomba ufahamishwena Mungu maono yote magumu usiyoyajua ambayo Mungu, amekuonyesha wewe, au ndugu yako, hebu tuendelee mbele tuyaone mambo mengine muhimu ambayo Roho Mtakatifu anataka tuyafahamu kuhusu habari za karama za rohoni katika sehemu hii ya karama ya unabii kwa kupitia njia ya maono na ndoto kwa lugha nyingine njozi.

NJIA YA PILI, KWA KUPITIA NENO LA SAUTI YA MOJA KWA MOJA

Kama tulivyojifunza mwanzo kuwa, Mungu anaweza kukuletea neno lake (unabii), kwa kutumia njia nyingi sana, na tumejifunza njia ya kwanza kuwa Mungu anaweza kukuletea neno lake kwa kutumia ndoto au njozi, na maono mbalimbali, pia lazima ufahamu kuwa ziko njia nyingine ambazo Mungu anaweza kabisa akazungumza na wewe na kukupatia ujumbe wake, hebu tuangalie njia nyingine ambayo Roho mtakatifu anaweza kusema na wewe, Fungua, kitabu cha **(MDO 22:14-15) " Akasema, Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake, na kumwona yule mwenye haki, na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake. Kwa maana utakuwa shahidi wake kwa watu wote, wa mambo hayo uliyoyaona na kuyasikia".** Tuyasomapo maneno hayo ya Bwana, tunajifunza hapo kuwa, Paulo, alipata neema mbele za Mungu na kupewa karama ya kumsikia Mungu, na pia alipata neema ya kuonyeshwa maono mbalimbali na Mungu, kwa hiyo ndugu yangu kuwa, Mungu, anaweza kusema na wewe kwa kupitia

maono, na pia anaweza kusema na wewe kwa kuisikia sauti yake moja kwa moja, yaani mdomo kwa mdomo, ukiwa na karama hii ya kinabii, ni jambo rahisi sana Mungu kusema na wewe kwa kuisikia sauti yake, Fahamu Mungu tunae mwabudu ni Mungu aliye hai, anayesema kabisa, ndio maana neno lake linasema, **" Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa mataifa, mlichukuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa." 1KOR 12:2-)**, Fahamu, kabla hatujampokea Yesu tulikuwa ni watu wa mataifa, na hatukuwa tuna Mungu anayesema, tuliifuata Miungu ya uongo, isiyo ya kweli, tena idanganyayo kabisa, sasa, Baada ya kumpokea Bwana Yesu Kristo tumekuwa na Mungu wa kweli aliye hai na anayenena au kwa lugha nyingine anayesema, Fahamu Mungu anayo sauti, kwanini nasema hivyo? Fahamu, ikiwa Mungu wetu yuko hai, basi anasema, na ndio maana alimwambia Paulo kuwa amechaguliwa na yeye na atamwezesha kuisikia sauti yake, mbali ya kumwonyesha mambo mbalimbali alimwambia atamwezesha kuisikia sauti itokayo kinywani mwake, Mungu anaweza kukuteua hata wewe ili uisikie sauti itokayo kinywani mwake, na ukawa shahidi wa yale yote atakayokuambia, yaani ukayasema yale yote aliyokuambia kwa kuisikia sauti yake.

Katika sehemu hii, watoto wa Mungu wengi sana wamekuwa na mashaka sana ndani ya mioyo yao, kuwa inakuwaje leo hii, mtu aseme Mungu, ameniambia maneno haya!, au tufanye hivi! Watoto wa Mungu wengi kwa kuwa hawazijui habari za karama za rohoni, wengi wamejikuta wakipinga au kutowaamini watumishi wa Mungu waliona karama hii ya unabii wawaambiapo kuwa Mungu ameniambia hivi, ukisoma maandiko matakatifu, kwa makini, utaonakuwa Mungu alisema na watumishi wake wengi sana kwa sauti yake, wakiwa macho kabisa, bila kuwa usingizini, na kunawengine Mungu alisema kuwa hao atazungumza nao mdomo kwa mdomo, **" Kisha akawaambia, Sikieni basi maneno yangu; akiwapo nabii kati yenu, Mimi, Bwana, nitajifunua kwake katika maono, nitasema naye katika ndoto. Sivyo kwa mtumishi wangu Musa; yeye ni mwaminifu katika nyumba yangu yote; kwake nitanena mdomo kwa mdomo, maana wazi wazi wala si kwa mafumbo; Na umbo la Bwana yeye ataliona……" (HESABU12:6-8)** Maneno hayo ya Bwana, alikuwa akimwambia kuhani mkuu Haruni, na nabii Miriamu, kuwa, atakavyokuwa anazungumza na manabii wengine wote, itakuwa ni tofauti na atakavyo kuwa akizungumza na Musa, Mungu alisema atakavyo kuwa anazungumza na Musa, atakuwa anazungumza naye waziwazi, wala si kwa maono au kwa ndoto za mafumbo, Bali atazungumza naye mdomo kwa mdomo, kwa hiyo ndugu yangu unatakiwa uelewe kuwa hata leo hii Mungu anaweza kuzungumza na wewe kwa njia hii ya kuisikia sauti yake waziwazi, Neno la Bwana linatufundisha kuwa Mtumishi wa Mungu Eliya Mtishibi, alisema na Mungu waziwazi mlimani Horebu, na walijibizana na kuongea kabisa, Fungua **(1FALME :19:11-14) " Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za Bwana.Na tazama, Bwana akapita; upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunjavunja miamba mbele za Bwana;lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi;lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto;lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu. Ikawa, Eliya alipoisikia, alijifunika uso wake katika mavazi yake, akatoka, akasimama mlangoni mwa pango.Na tazama sauti ikamjia, kusema, unafanya nini hapa, Eliya? Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajiri ya Bwana, Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwauwa manabii wako kwa upanga;nami nimesalia, mimi peke yangu;nao wanitafuta roho yangu waiondoe"**

Baba Mungu siku ile alizungumza waziwazi yaani mdomo kwa mdomo na Eliya, Eliya hakuwa usingizini, alikuwa macho kabisa, kwanza alizungumza na malaika wa Mungu, na Malaika akamwambia Eliya ajiandaye kuongea na Mungu, na baada ya maandalizi kukamilika ya Eliya kusimama mahali maalumu ili azungumze na Mungu, Mungu, alishuka na alizungumza na Eliya, Neno lina sema Eliya aliisikia sauti ya utulivu masikioni mwake na akaijibu ile sauti manenno yote aliyoyasikia, Fahamu Mungu, hajakaukiwa na sauti yake, anaweza kusema hata leo na hata milele, ndio maana neno la Bwana linasema **" Angalieni msimkataе yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyaye kutoka mbinguni;" (EBR 12:25);**

Fahamu Mungu anatuonya hata leo hii akiwa ameketi huko mbinguni kwenye kiti chake cha enzi, na atatuonya kwa Neno lake litokalo kinywani mwake, na kupenya masikioni mwetu na kusikika kabisa, Tatizo likokwetu, hatujui habari za karama za rohoni tulizopewa na Bwana, Ndio maana hata akionya kwa kutumia njia hii, watoto wa Mungu wengi huwa hawasikii, na wakisikia huwa hawatambui kuwa Bwana amesema nao, na ndipo linapotimia neno lile la nabii Isaya, asemalo **" Sikilizeni, enyi viziwi;tazameni, enyi vipofu, mpate kuona. Ni nani aliye kipofu, ila mtumishi wangu? Aliyekiziwi, kama mjumbe wangu nimtumaye? Ni nani aliye kipofu, kama yeye aliye na amani?naam, kipofu, kama mtumishi wa Bwana? Unaona mambo mengi, lakini huyatii moyoni;masikio yake ya wazi, lakini hasikii."(ISAYA 42:18-20).** Bwana anasema kuwa watumishi wake wengi ni watu wanamna hii, wengi masikio yao yako wazi kabisa, lakini hawasikii, kwanini Mungu anasema hivyo? Ni kwa sababu Mungu anapowaonya au kuwaelekeza watumishi wake mambo ya kufanya kwa njia ya maono huwa hawaelewi kabisa kuwa Bwana kawaonya jambo Fulani, na anapowaonya kwa kupitia njia hii ya kusikia sauti ya Mungu kutoka mbinguni, huwa hawayategi masikio yao ili wapate kumsikiliza, wengi hawafahamu kuwa Mungu anasema na hata kama wanafahamu ila hawaamini, ndio maana wengi wakisikia mtu anasema Mungu, amesema, au ameniambia, maneno haya, huwa wanapinga, hata kama Mungu alisema na huyo ndugu, Umewahi kujiuliza kwanini huduma yako au huduma za watumishi wa Mungu wengi zimedumaa? Jibu ni hili, wengi wanafanya huduma bila kusikiliza maonyo kutoka kwa Bwana, wanafanya kwa mazoea na uzoefu au elimu waliyonayo, na matokeo yake, huwa wanaachana na Bwana, kwa sababu ya kufanya mambo ambayo Bwana hakutaka wayafanye, ingawa wakiangalia kwa haraka haraka wanaona kama wanafanya kazi ya Mungu kisawasawa, lakini upako wa Mungu katika huduma zao huwa havonekani kabisa.

Mungu anataka watumishi wake wote wapate kufahamu kuwa Mungu anaweza kusema hataleo nao, ndio maana akaileta karama hii ya unabii, ili watoto wake wapate kusikiliza maagizo au maonyo kutoka kwa Bwana ili Huduma zao za kulijenga kanisa na maisha yao ya wokovu yapate mwongozo bora kutoka kwa Bwana, Tatizo lingine linalosababisha watoto wa Mungu wengi kutoifahamu vema na kuitaka karama hii, hili la kutojiamini, watoto wa Mungu wengi wanaamini kuwa Mungu alikuwa anasema kwa njia hii ya sauti ya moja kwa moja na watu maalumu tu, kama vile Musa, na Eliya na Paulotu, kwa kuwahebu kuwa watu hao walikuwa tofauti na wao, Fahamu Neno la Mungu linasema wazi kuwa, Eliya alikuwa ni mtu watabia ileile tuliyonayo sisi, Fungua **(YAKOBO 5:17-18) " Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi akaomba kwa bidii mvua isinye; na mvua haikunya juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita. Akaomba tena, mbingu zikatoa mvua, nayo nchi ikazaa**

matunda yake" Sikia ndugu yangu Eliya alikuwa ni mwanadamu mwenye tabia kama yako, lakini aliisikia sauti ya Mungu, na kuongea naye, na Mungu alimfundisha siku ile Eliya hata jambo analotakiwa alifanye nalo ni lile agizo alilompa la kumtia Elisha mafuta ili awe nabii badala ya Eliya, na Eliya akasikiliza onyo hilo na kufanya yote aliyoagizwa na Mungu, hata leo hii ndugu yangu Mungu anataka watoto wake wote wafahamu habari hizi za karama za rohoni, ili watakapo fahamu wamuombe Mungu awape karama hizi ili wayajue na kuyafanya mapenzi ya Mungu pia wapate kulijenga kanisa kwa uzuri kamaatakavyo Mungu, Fahamu Mungu anaposema na wewe, anakuwa anakufahamisha mapenzi yake au kukujulisha mambo ambayo anataka uyajue, pia Mungu anatakakila mara kuzungumza na sisi, kwa kutupatia majibu ya mswali yetu mengi tunayo muuliza, pia yuko tayari kutufahamisha sisi watoto wake habari mbalimbali, ona mfano huu mzuri jinsi Mungu alivyoamua kumweleza Musa jinsi dada yake, Miriam, na kuhani mkuu Haruni walivyokuwa wanamteta, Soma (**HESABU 12:1-15**), Musa alikuwa hajuijambo lolote lililo kuwa linasemwa na hao ndugu zake, Mungu alisikia maneno yote yaliyo semwa na hao ndugu zake Musa, Mungu akaamua kumpasha Mtumishi wake na hao ndugu zake kuwa watoke waende kwenye hema ya kukutania, huko Mungu aliamua kusema waziwazi kuwa hao ndugu walikuwa wanamteta Musa, na kila mtu aliisikia sauti ya Bwana, ukiyasoma maandiko hayo matakatifu utagundua kuwa, kumbe Mungu yupo tayari kutupasha habari ya aina yoyote ile kwa kuitumia sauti yake moja kwa moja toka mbinguni

Basi ndugu yangu naamini Bwana amekufundisha kwa uzuri sehemu hii ya unabii ujao kwa kusikia Neno la Mungu kwa kuisikia sauti ya Bwana katika masikio yako, au ndani ya moyo wako ukasikia sauti njema ya Bwana ikisema na ukazungumza nayo kabisa, watu wengi huwa na hofu sana katika sehemu hii, wakijiuliza swali hili, hivi hisauti ni ya Bwana au ni nafsi yangu? Nataka nikutie Moyo, ikiwa umempokea Bwana Moyoni mwako, na umejaa Roho Mtakatifu fahamu Mungu anaweza kusema na wewe, kwani ameahidi kukaa ndani yetu, kwa hiyo hebu jipe moyo, isikilize sauti hiyo, tafakari uliyoambiwa, yapime, fanya lile ulilolisikia lililo jema,

Nakumbuka siku Moja, nilikuwa na shida ya chakula nyumbani kwangu, na sikuwa na fedha ya kununulia hata mafuta ya taa, nilikuwa nimeishiwa kabisa, unga, mchele, na mboga, nikafanya maombi mbele za Mungu kuwa naomba anipatie chakula cha kula mimi na familia yangu, kama alivyoahidi kwenye neno lake kuwa anajua ya kuwa tunaitaji chakula na mavazi, basi, nilipofanya maombi hayo, nikashangaa muda ndio unakwenda na njaa inaniuma, na Muda wa kwenda kanisani umewadia, basi, nikaamua kwenda kanisanaibaada ya ibada, nilipotoka nje, nikamkumbusha Mungu kuwa, ninahitaji chakula nyumbani kwangu nilimwomba bila kutoa sauti, yaani kimoyomoyo, nikiwa katikati ya wapendwa waliookoka, nikasikia sauti, iliyopenya masikioni mwangu mpakandani ya roho yangu, ikasema, kwa utulivu, nenda nyumbani kwako, ntakupa chakula, nikashangaa sana, nikajiuliza swali!ninani aliyesema nami?, nikatambua si mtu aliyesema nami, nikaamua kuondoka na kwenda nyumbani kwangu, nikiwa na mawazo kuwa nikifika nyumbani ntakuta muujiza wowote toka kwa Bwana wa kutumiwa chakula au fedha toka kwa Bwana kwa kumtumia mtu yoyote yule, nilipofika nyumbani kwangu, na nilipoufungua mlango nikakuta hakuna chakula wala majilani zangu hawaniambii habari yoyote ile ya mtu yeyote yule kuw amewaachia mzingo wangu, basi, nikaamua nimwambie Mungu kuwa nimetii agizo lake tayari nipo nyumbani kama alivyoniambia kuwa niende nyumbani kwangu huko ntapewa mahitaji yangu yote, baada ya maombi hayo, niliisikia tena sauti, ikasema chukua karamu na karatasi na Bibilia yako ilinikupe chakula, nikasema, mimi naomba unipatie chakula cha kuulisha mwili wangu na familia

yangu iweje tena nichukue karamu na karatasi na Bibilia? Nikaisikia tena hiyo sauti ikisema, chukua karamu na karatasi na Biblia ukae hapo kwenye kiti nikupe chakula, nikakubari, unajua, siku hiyo Bwana alinifundisha mambo mengi sana ndani ya maandiko yake matakatifu, baada ya kumaliza darasa hilo, nikaisikia hiyo sauti, ikasema, nimekupa chakula cha rohoni, na sasa inuka uende mjini, katika banda la wauzao nafaka, utamkuta mtu furani, (namwifadhi jina lake), atakupa kila kitu ulichoniomba, haya Inuka, nenda, Bila, hofu, nikainuka nikaenda mpaka mahari pale nilipoelekezwa, na kweli, nilimkuta mtu huyo humo ndani, na nikamsalimia, nilipokuwa nikimsalimia tu, watu wengine wanao nifahamu waliokuwemo mle, wakaniita, nikawaitikia nikaenda, wakaniuliza maswali mengi sana yakuhusu safari ya kwenda mbinguni, wakiwa wanahitaji kufahamu baadhi ya mambo, na nilikuwa naendelea kuwaeleza akili yangu ikakumbuka kuwa nimefuata hapa hitaji langu nililo muomba Mungu, na nimeambiwa nije humu ndani ya banda la wauzaji wa nafaka na Bwana amemwandaa mtu furani kunipa hitaji langu hilo, nilipokuwa nageuka ilinimtizame huyo mtu kama ameondoka baada ya mimi kuitwa na hao ndugu, nika shangaa huyo mtu yupo mgongoni kwangu anasubili nimalize kuongea na anipe mzingo wangu, nilipomaliza, akaniamba " Haloo! Chukua mzingo huu na uendenao nyumbani" nikamshukuru, nikaondoka kwenda nyumbani, unajua, nilipofika nyumbani, na kuufungua, nikakuta amenipatia mchele wa kula siku nyingi, mboga, nyanya na vitunguu, na fedha niliyonunulia mafuta ya kupikia na ya taa, nikamshukuru Mungu kwa tendo hilo.

Siku hiyonilijifunza kuwa Mungu anasema, na hana ubaguzi ni Mungu anaeweza kusema na watu wa umri wa aina yeyote, na watu wa kabila lolote lile waliopo katika kizazi hiki katika Agano hili jipya tulilopewa na Bwana, kwani watu wengi wanaamini kuwa Mungu alisema na akina Eliya tu, kuhusu habari mbalimbali, kama za kwenda kwenye kile kijito ili akapewe chakula na Bwana kupitia kunguru, naza kwenda Sarepta kwa mwanamke mjane iliakatunzwe huko, hawaamini kuwa hata leo hii Mungu anaweza kutuelekeza twende sehemu gani ambayo Mungu ametuwekea baraka zetu huko, Basi taka kwa Mungu ili akupekarama hii ya unabii, iliazungumze nawewe kwa kupitia njia hii, itake karama hii kwa moyo wa upendo, sio ule wa majivuno, kutakakuonekana mbele za watu, na umwamwamini Mungu kuwa atakupa

USHIRIKIANO NA KARAMA NYINGINE

Karama hii ya Unabii, pia hufanyakazi kwa kushirikiana na karama nyingine, Mungu anaweza kuitumia karama hii ya unabii ikashirikiana na karama nyingine ili kanisa lake lipate kujengwa na kuongozwa vema katika mapenzi ya Mungu, Mara nyingi utaona kuwa karama ya unabii imekuwa ikishirikiana sana na karama ya neno la maarifa na karama ya neno la hekima, Kwa mfano, ukisoma maneno ya Mungu kutoka kitabu cha **(KUTOKA 14:15-16) " Bwana akamwambia Musa, mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israeli waendelee mbele.Nawe inua fimbo yako, ukanyoshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya; nao wana wa Israeli watapita kati ya bahari katika nchi kavu"**

Tukiyasoma maneno hayo ya Bwana Mungu, tunaona kuwa siku ile Mungu alimpatia Musa neno (unabii), ambalo ndani yake kulikuwa na neno la maarifa toka kwa Mungu, lililomtaka Musa ainue fimbo na kupiga maji, pia alimpatia Musa maarifa ya namna wana wana wa Israeli wanavyotakiwa watende watakapokuwa wakivuka baharini, alimwambia awaambie wapiti katika sehemu itakayokuwa kavu baharini, Katika kifungu hicho tunaona jinsi Mungu anavyoweza kumpatia mtu yeyote yule Maarifa maalumu ya

namna mtu huyo anavyotakiwa afanye, Ukiyasoma maandiko hayo matakatifu utaona kuwa Musa hakuwa na maarifa yeyote ya kuwavusha hao wana wa Israeli katika bahari ya Shamu, alikuwa analia tu, ndipo, Mungu akatuma neno lake yaani unabii, ambao ndani yake kulikuwa na ujumbe maalumu wa kumpatia Musa maarifa ya namna anavyotakiwa afanye, Pia utaona kuwa neno hilo la kinabii toka kwa Mungu, lilikwenda kushirikiana na karama ya miujiza, Fahamu, tendo la kuigawa bahari siku ile lilikuwa ni tendo la kimiujiza, siyo tendo la kawaida, nitendo la kustaajabisha kabisa, Pia utaona hapo karama ya Imani ilihusika katika huduma hiyo, Fahamu Mungu alimwona Musa amekwisha kukata tamaa, kwani alimuona Musa akilia, ndipo Mungu alipoamua kumsaidia, na alimsaidia kwa kumletea neno maalumu kutoka mbinguni, na fahamu, kitendo cha Musa kuamini neno lile na kulikubari, kwenda kuwaambia wana wa Israeli songeni mbele yaani waingie ndani ya maji, hakikuwa kitendo cha kawaida, Kulikuwa na Imani maalumu, yaani karama ya Imani ilitumika siku ile, sasa utaona hapo kuwa karama hii ya kinabii ilifanya kazi pamoja na karama ya neno la maarifa, karama ya miujiza na karama ya imani, zote nne zilifanya kazi pamoja.

Kwa hiyo ndugu fahamu kuwa Mungu anaweza kukupatia maarifa kwa kuitumia karama hii ya kinabii, Bibilia ina sema kuwa Mfalme Yehoshafati, alipokuwa anakwenda vitani kupigana na maadui zake, Mungu alimpa maarifa ya namna anavyotakiwa apigane kwa kumtumia unabii, uliotolewa na nabii mmoja kipindi kile, maneno ya Bwana yanasema hivi, **(2NYA 20:10-18), "Na sasa, tazama, wana wa Amoni, Moabu, na mlima Seiri, ambao hukuwaacha Israeli waingie katika nchi yao, walipotoka nchi ya Misri; lakini wakawageukia mbali, wasiwaharibu;tazama, jinsi wanavyotulipa, wakija katutupa toka milki yako, uliyoturithisha. Ee Mungu wetu, je! Hutawahukumu? Maana sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu;wala hatujui tufanyeje; lakini macho yetu yatazama kwako. Wakasimama Yuda wote mbele za Bwana pamoja na wadogo wao, na wake zao, na watoto wao. Ndipo Yahazieli mwana wa Zekaria, mwna wa Benaya, mwana wa Yeieli, mwana wa Matania, Mlawi, wa wana wa Asafu, akajiliwa na roho ya Bwana, katikati ya kusanyiko;akasema, Sikieni, Yuda wote, nanyi mkaao Yerusalemu, na wewe Mfalme Yehoshafati; Bwana awaambia hivi, Msiogope, wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu. Kesho shukeni juu yao; tazameni, wanakwea kwa kupandia sisi; nanyi mtawapata penye mwisho wa bonde, mbele ya jangwa la Yerueli. Hamtahitaji kupigana vita, jipangeni, simameni, mkauone wokovu wa Bwana ulio pamoja nanyi, enyi Yuda na Yerusalemu;msiogope, wala msifadhaike;kesho tokeni juu yao; kwa kuwa Bwana yu pamoja nanyi.Yehoshafati akainama kichwa, kifulifuli;wakaanguka mbele za Bwana Yuda wote na wakaao Yerusalemu, wakimsujudia Bwana".**

Pia katika maneno hayo tunaona jinsi Baba Mungu, alivyotumia unabii kwa kuwaletea maarifa ya kufanya hao wana wa Israeli siku ile walipovamiwa na maadui zao, Mungu alilituma neno lake(unabii)kutoka katika kiti chake cha enzi mojakwamoja, na neno hilo lilimfikia Yahazieli nabii, na Yahazieli akalisema mbele ya Mfalme Yehoshafati na wana wa Yuda wote walilisikia, Mungu aliutumi unabii kwa kuwapalekea maarifa ya kufanya hao ndugu, kwani walimwomba Mungu wakisema hawajui la kufanya, ndipo Mungu akawajibu na kuwapa maarifa ya kufanya, utaona hapo, kuwa karama ya unabii ilifanyakazi pamoja na karama ya neno la maarifa, ipo mifano mingi sana ndani ya maandiko matakatifu inayoonyesha jinsi karama ya unabii inavyoweza kufanya kazi pamoja na karama nyingine, Ebu, tumalizie kwa kuangalia mfano jinsi Mungu alivyoitumia karama hii ya unabii kwa kumpatia mfalmeDaudi maarifa ya kupigana na Wafilisti **(2**

SAM 5:22-25) "Lakini wakapanda hao Wafilisti tena mara ya pili, wakajitawanya bondeni mwa Walefai. Naye Daudi alipouliza kwa Bwana, akasema, Usipande;zunguka nyuma yao, ukawajie huko mbele ya miforsadi. Kisha itakuwa, hapo utakapoisikia sauti ya kwenda katika vilele vya miforsadi, ndipo nawe ujitahidi; kwa maana ndipo Bwana ametoka mbele yako awapige jeshi la Wafilisti. Ndivyo alivyotenda Daudi, vile vile kama Bwana alivyomwagiza;naye akawapiga Wafilisti toka Geba hata ujapo Gezeri".

Mfalme Daudi alimwomba Mungu ampatie ufahamu wa namna ya kupigana na Wafilisti, na Mungu alimjibu kwa kumletea neno lililotoka mbinguni yaani unabii, na Mungu alimwambia Daudi kuwa inampasa asiwapandie Wafilisti bali awazungukie kwa nyuma, na Mungu alimpatia Mfalme Daudi maarifa ya kufanya katika vita hiyo, Na Daudi alifanya kila jambo, aliloambiwa akashinda vita hiyo, Kwa hiyo ndugu yangu utaona wazi kuwa karama hii ya unabii inaweza kufanya kazi na karama nyingine za rohoni, Fahamu, Ikiwa una karama ya unabii, Mungu anaweza kuitumia karama hiyo kwa kukupatia maarifa mbalimbali ya kulijenga kanisa na hata katika maisha yako ya wokovu au katika huduma yako, ikiwa wewe ni mtumishi wa Mungu, fahamu, unahitaji sana maarifa toka kwa Mungu, na Mungu anaweza kukupatia hayp maarifa kwa kuitumia karama hii ya unabii, basi, Ebu, ona jinsi karama hii ilivyo ya muhimu katika kanisa la Mungu, ikitumika vema naamini kanisa la Mungu litajengwa kwa uzuri sana, tena kwa usahihi kabisa, pia ukiwa na karama hii, na ukaitumia kwa uzuri, fahamu huduma yako itakuwa nzuri sana, kwani utafanya kila jambo kwa maelekezo mazuri toka kwa Mungu Baba, na utafanikiwa sana, umewahi jiuliza swali, kwanini watumishi wengi wa Mungu hawafanikiwi? Na kwa nini kondoo wa Mungu wametawanyika? Jibu ni hili, **"Kwa sababu wachungaji wamekuwa kama wanyama, wala hawakuuliza kwa Bwana; basi hawakufanikiwa na makundi yao yote yametawanyika" (YEREMIA 10:21);** Fahamu mnyama hana akili, hana maarifa yeyote yale, ndivyo hata leo kwetu sisi kama watumishi wa Mungu ambao tumepewa dhamana ya kuliongoza kundi la Mungu, kulifundisha nk, pasipo kuwa na akili, fahamu hatutafanikiwa na kanisa halitajengwa, sasa kumbe tunatakiwa tuka muulize Mungu jambo lolote lile tulilokusudia kulifanya kwa ajiri yake atupe maarifa ya namna tunavyotakiwa tulifanye, na Mungu atatupatia hayo maarifa kwa kwanjia nyingi, moja wapo ya njia hizo ni hii karama ya unabii, kwa hiyo ebu, itake kwa Mungu karama hii, na ikiwa unayo hebu ichochee. Mungu awe pamoja nawe.

USIUTWEZE UNABII

(1 THE 5:20-21) " Msitweze unabii; jaribuni mambo yote;lishikeni lililojema"
Ukiyasoma maneno hayo ya Mungu, utaona kuwa Mungu anatuonya sisi watoto wake akisema kuwa tunatakiwa tuhakikishe kuwa hatuutwezi unabii, au kwa lugha nyingine, hatuupingi au kuupuuzia, ama kuukataa unabii wowote ule, bali tumeambiwa kuwa tunatakiwa tuuujaribu, na baada ya kuujaribu au kuupima ndipo tuukubali au tuukatae.

Biblia inatupa agizo la kuupima unabii wowote ule, uwe umekuja kwa njia ya maono, au kwa njia ya ndoto, au kwa kusikia sauti katika ulimwengu wa roho, au unabii utakaotolewa na mtu yoyote yule haijarishi ni nani, Neno la Mungu linasema hivi, **" Na manabii wanene wawili au watatu, na wengine wapambanue" (1KOR 14:29)** ; Kila mtu aliye na karama hii ya unabii anatakiwa afahamu kuwa anatakiwa akubari kupimwa, na hata yeye mwenyewe anatakiwa ahakikishe anaupima unabii au neno

alilolipokea kabla hajalisema au kulifanyia kazi, pia hata yule asiye na karama hii ya unabii, anatakiwa afahamu kuwa ana takiwa aupime kila unabii anaoambiwa na hao waliona karama ya unabii.

Kwa nini Neno la Mungu lina tuagiza hivyo? Jibu ni kwa sababu, ya kutuokoa na unabii wa uongo, fahamu sikila mtu akuambiae Mungu amesema, anakuwa kweli Mungu amemwambia hilo neno, Biblia ina sema wapo watu wengine wasemao Mungu ametutuma tusema jambo Fulani lakini ni waongo, **(YEREMIA23: 16) Bwana wa majeshi asema hivi, msisikilize maneno ya manabii wakiwatabiria; huwafundisha ubatili;hunena maono ya mioyo yao wenyewe; hayakutoka katika katika kinywa cha Bwana"** Fahamu unabii ni lile neno lililo toka katika kinywa cha Bwana mojakwa moja, na kumjulisha mtu aliyemchagua ili alifikishe kwa watu wake, sasa ukiyasoma maneno hayo, utaona kuwa, Mungu anawaonya watu wake wasiwasikilize manabii ambao wanaowajia na kuwaambia, Mungu, ametuambia maneno haya, Mungu aliwaonya hivyo watoto wake kipindi kile kwa sababu, manabii wengi walikuwa hawasemi ukweli, walikuwa wanawaambia wana wa Israeli maneno ambayo Mungu hakuwatuma, yalikuwa ni maneno yalitoka kwenye mioyo yao wenyewe, hakupokea neno lolote kutoka kwa Bwana, wakasimama mbele ya wana wa Israeli na kuwaambia Bwana amesema hivi, wakati hawajamsikia Bwana akisema nao, Ebu, angalia mstali wa 18, Unasema hivi, **" Maana ni nani aliyesimama katika baraza la Bwana, na hata akalifahamu neno lake na kulisikia? Ni nani aliyelitia moyoni neno langu, na kulisikia? (YEREMIA 23:18)** Fahamu Mungu aliyasema maneno hayo kwa sababu, manabii hao waliosimama mbele ya watu na kusema kuwa Mungu amesema, hawakusimama barazani pake Mungu na kumsika Mungu akisema maneno hayo waliyoyasema kuwa Mungu amewaambia walikuwa ni waongo kabisa, yaani manabii hao waliyatunga maneno hayo mioyoni mwao, na kumsingizia Mungu kuwa amewatuma kumbe hata kumsikia hawakumsikia, fahamu wapo watu ambao wamepewa karama ya unabii, na kwa sababu zao binafsi, wanaweza kusema maneno ya uongo ili kuwatumainisha watu au ili wapate utukufu kwa hao watu, fahamu watu wengi sana ndani ya mioyo yao huwa wanatafuta utukufu au kuonekana kuwa wao ni watumishi wa Mungu, na watu wanamna hiyo ni rahisi sana kusema uongo kuwa Mungu asema hivi, lakini kumbe Mungu wala hakusema nao, Bwana anasema hivi, **"Nimesikia waliyoyasema manabii wanaotabiri uongo kwa jina langu, wakisema, Nimeota ndoto;nimeota ndoto. Je! Mambo hayo yatakuwa katika mioyo ya manabii wanaotabiri uongo hata lini, manabii hao wenye udanganyifu katika mioyo yao wenyewe wanaodhani ya kuwa watawasahaulisha watu wangu jina langu kwa ndoto zao, wanazomhadithia kila mtu jirani yake, kama vile baba zao walivyolisahau jina langu, kwa ajili ya baali. Nabii aliye na ndoto, na aseme ndoto yake;na aliye na neno langu, na aseme neno langu kwa uaminifu…."(YEREMIA 23:25-28)**

Bwana anajua kuwa wapo watu watakaokuwa si waaminifu katika eneo hili, ndio maana anasema kuwa tunatakiwa tuupime unabii, au kwa lugha nyingine tuupambanue kama kweli umetokana na Bwana, bila kupambanua nilahisi sana kupokea unabii wa uongo kutoka kwa watu wasio waaminifu, ambao nia yao ni kupata faida yao wenyewe, ipo mifano mingi sana kwenye maandiko matakatifu inayotufundisha au kutuonya dhidi ya unabii wa uongo toka kwa watu wanaosema Bwana asema, wakati hajasema nao, kunahadithi moja nzuri kutoka kitabu cha (1FALME 13:1-34)Ukiisoma surahii yote utapata fundisho zuri sana la jinsi baadhi ya watu wanavyo weza kutoa unabii wa uongo na kuwapotosha watu wa Mungu, hebu tuiangalie baadhi ya mistari, angalia mstari wa **(1-**

3), " Na tazama, akatoka mtu wa Mungu katika Yuda kwa neno la Bwana, akafika Betheli naye Yeroboamu alikuwa akisimama penye madhabahu, afukize uvumba, Basi mtu huyo akapigakelele juu ya madhabahu, kwa neno la Bwana, akasema, Ee madhabahu, Bwana asema hivi, Angalia, mtoto atazaliwa katika nyumba ya Daudi, jina lake Yosia; na juu yako atawachinja makuhani wa mahali pa juu, wanaofukiza uvumba juu yako, na mifupa ya watu itateketezwa juu yako.aktoa ishara siku ile ile, akasema, Hii ndio ishara aliyoinena Bwana, tazama, madhabahu itapasuka, na majivu yaliyo juu yake yatamwagika"

Maneno hayo yanatufundisha kuwa Mungu ndiye aliyemtuma nabii huyo kusema na kufanya hayo aliyomwagiza, kwani neno lina sema alisema kwa neno la Bwana, hakusema kwa neno lake, sasa utaona mbeleni nabii huyo alipewa maagizo maalu na Bwana iliayafanye, nayo yanapatikana katika mistari ya (**9-10) " Maana ndivyo nilivyoagizwa na kwa neno la Bwana, kusema, usile chakula chochote wala kunywa maji, wala usirudi kwa njia nyingine, wala hakurudi kwa njia ile aliyoijilia Betheli**" Mungu alimpa maagizo huyo mtumishi wake kuwa asile chakula wala asinywe maji katika mji huo, pia alimpa agizo la kutoiludia njia ile aliyokuja nayo, ilaapite katika njia nyinginea, itakayomludisha nyumbani kwake, ni kweli mtumishi huyo alimtii Mungu, baada ya huduma akafanya kama alivyo agizwa na Bwana, sasa baadaye Neno la Mungu lina tufundisha akatoke mtu mmoja ambaye alikuwa ni nabii, akamfuata mtu huyo na kwenda kumwambia maneno ya uongo, Ebu, angalia mistari ya, **(14-19) " Akamfuata mtu wa Mungu, akamkuta ameketi chini ya mwaloni, akamwambia, je! Wewe ndiwe yule mtu wa Mungu aliyetoka Yuda? Akamwambia, Mimi ndiye. Akamwambia, karibu kwangu nyumbani, ule chakula naye akamwambia siwezi kurudi pamoja nawe, wala kuingia pamoja nawe;wala sili chakula wal sinywi maji pamoja nawe hapa; kwani nimeambiwa kwa neno la Bwana, Usile chakula walausiywe maji huko, wala usirudi kwa njia ile uliyoijia. Akamwambia, Mimi nami ni nabii kama wewe, na malaika akaniambia kwa neno la Bwana, kusema mludishe pamoja nawe nyumbani kwako, ale chakula, akanywe maji.Lakini alisema uongo, Basi mtu yule akarudi pamoja naye, akala chakula, akanywa maji nyumbani mwake"**

Fahamu ndugu yangu kuwa, huyo mtu aliyesema maneno hayo ya uongo alikuwa ni nabii kweli, lakini alisema maneno hayo ya uongo kuwa amekutana na malaika wakati hajakutana na malaika, nalifahamu kabisa kuwa anasema uongo, na akafanikiwa kumdanganya huyo mtu wa Mungu, na matokeo yake huyo mtu wa Mungu baada ya kulachakula tu, laana ikamfikia, alikufa kwa kuliwa na simba, fahamu ndugu yangu kuwa watumishi wanamna hii wapo hata leo hii, ambao wakotayari kutunga maneno ya uongo ili kuwadanganya watu, na hata kuwapoteza kabisa kwa huo uongo wao, kwa hiyo basi iliusiushike au kuukubari unabii wa uongo unatakiwa uhakikishe unaubambanua, au unaupima kwanza ndipo uupokee au uukatae, sikila mtu asemaye Bwana amemtuma inakuwa ni kweli Mungu amemtuma, nimewaona watu wengi sana hasa kina Mama na kina Dada, wakiwa katika maisha magumu sana au huduma ngumu sana, kwa sababu ya kudanganywa na watu wenye mafunuo ya uongo, wengi leo hii wamejikuta wamekwama kuolewa, kwa sababu ya unabii wa uongo, wengi wameacha kazi zao kwa sababu ya unabii wa uongo, wengi wamewaacha wake zao kwa sababu ya unabii wa uongo, wengi wamefanya uzinzi kwa sababu ya unabii wa uongo.

Niliwahi zamani kukutana na Dada mmoja ambaye naamini alidanganywa na mtumishi mmoja kuwa, Eti, Mungu amemwambia mtumishi huyo kuwa Dada huyo ndiye mke wake,

wakati huo huyo mtumishi anamke aliye hai na watoto, na Dada huyo aliamini, kabisa na kupokea unabii huo, na nilikutana na huyo mtumishi, nika mwambia kuwa Dada huyo siyo mke wake. Kwa kweli inasikitisha sana, na baada ya kumwambia Ndugu huyo, nilishangaa sana, Ndugu huyo alikasilika sana, na alisema hata mwacha Dada huyo, na alikwenda kumwambia kuwa mimi nimemwambia kuwa huyo Dada si mke wake, huo ni mfano mmjoja tu, ipo mifano mingi sana, ambayo watu wengi wamemsingizia Mungu kuwa amewatuma wakati Mungu hajawatuma.

VINYAGO AU MAWAZO YAKO

Kwa hiyo basi unatakiwa uhakikishe katika maisha yako yote, hauutwezi au kwa lugha nzuri hauupingi unabii, lakini unatakiwa uupime unabii, kama kweli umetokana na Mungu, au umetoka kwa mtu yeyote yule au kutoka katika roho zile zidanganyazo mapepo nk, ama kutoka katika mawazo yako au kwalugha nzuri ya kibiblia ni vinyago vyako, Fahamu, ikiwa ndani ya moyo wako umeweka jambo Fulani na ukaenda mbele za Mungu kumuomba au kumuuliza, fahamu atakujibu sawasawa na jinsi ulivyo moyoni mwako, ona mfano huu, Fungua kitabu cha **(EZEKIELI 14:1-7) " Ndipo baadhi ya wazee wa Israeli wakanijia, wakaketi mbele yangu, Ndipo neno la Bwana likanijia, kusema, mwanadamu, watu hawa wametwaa vinyago vyao na kuvitia mioyoni mwao, nao wameweka kwazo la uovu wao mbele ya nyuso zao.je! ni laiki yangu niulizwe na wao katika neno lolote? Basi sema nao, uwaambie, Bwana Mungu asema hivi; kila mtu wa nyumba ya Israeli atwaaye vinyago vyake na kuvitia moyoni mwake, na kuliweka kwazo la uovu wake mbele ya uso wake, na kumwendea nabii;mimi Bwana nitamjibu neno lake sawasawa na wingi wa sanamu zake, ili niwakamate nyumba ya Israeli kwa mioyo yao wenyewe, kwa sababu wamefarakana nami kwa vinyago vyao."**

Neno la Bwana linatufundisha kuwa, Mungu alimpatia agizo Mtumishi wake Ezekieli kuwa, awaambie wana wa Israeli ambao wanakuja mbele za Bwana ilikumuuliza jambo lolote lile, kuwa ikiwa watakuja mbele zake huko ndani ya mioyo yao wameweka sanamu au vinyango vyao, basi Mungu atawajibu sawasawa na hivyo vinyago vyao walivyoviweka moyoni mwao, unaweza ukajiuliza swali, sanamu au vinyago vinavyo weza kukaa mioyoni mwa watu nini? Jibu zuri linapatikana katika kitabu cha, **(WAKOLOSAI 3:5) " Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu."** Fahamu mawazo mabaya na, tamaa mbaya na kutamani, hivyo ndivyo vinyago vinavyoweza kukaa ndani ya moyo wako, ona mfano, leo hii vijana wengi sana, na mabinti wengi sana ambao bado hawajaoa, wakifika katika kipindi cha kuhitaji mume au mke, wengi wanajikuta wako katika kipindi kigumu sana cha kufahamu ninani aliye mke au mume wake, unajua ni kwanini? Ni kwa sababu, katika mioyo yao inawezekana kukawa na mabinti wawili au watatu ambao wako mawazoni, sasa inapofika kipindi cha kwenda mbele za Mungu kumuomba ampatie mke, ikiwa hakuwaondoa hao mabinti moyoni mwake fahamu, Mungu atamjibu sawasawa na jinsi awazavyo, ndio hapo wengi wanajikuta wanachanganyikiwa kwani, leo, wataambiwa binti Fulani, kesho ataambiwa binti mwingine, keshokutwa binti mwingine, itakuwa hivyo hivyo, mpaka atakapo waondoa wote katika mawazo yake, natumaini kwa mfano huo umenielewa, fahamu, watu wengi wamejikuta wamekwenda mbele za Mungu huku ndani yao wakiwa wamenia kufanya jambo fulani kwa tamaa zao, na Mungu fahamu atawajibu sawasawa na tamaa zao, sasa huko mbeleni watakapo kwama, wengi wanafikiri shetani kawazuia wataomba na kukemea sana, lakini hawapati jibu, wala

mafanikio mpaka watakapo pata ufahamu kuwa wamekosea, ndipo, Mungu atakapo sema nao vizuri na kuwaonyesha jambo la kufanya, kwa hiyo ndugu yangu, unatakiwa pia uwemchunguzaji wa kila ndoto, au ono utakaloliona, kuwa je? Ni ono la mawazo yangu? au ni Bwana amesema nami, Pia hata sauti, lazima upime je! Sauti hii iliyoniambia maneno haya ni ya Bwana au si ya Bwana? Kwani neno la Bwana linasema hivi **(AYUBU4:12-19) " Basi, nililetewa neno la siri, sikio langu likasikia manong'ono yake.katika mawazo yaliyotokana katika maono ya usiku, hapo usingizi mzito uwaangukiapo wanadamu. Hofu ikaniangukia na kutetema iliyoitetemesha mifupa yangu yote.ndipo pepo ilipita mbele ya uso wangu; na nywele za mwili wangu zilisimama. Hiyo pepo ilipita mbele ya macho yangu;kulikuwa kimya, nami nilisikia sauti ikinena, je! Binadamu atakuwa na haki kuliko Mungu wake?je! mtu atakuwa safi kuliko muumba wake?Tazama yeye hawategemei watumishi wake, na malaika zake huwahesabia upuuzi."**

Ukiyasoma maneno hayo utaona yakuwa, kumbe, sikila neno utalolisikia ukiwa usingizini au katika maono ya usiku, ama katika ndoto, ni neno lililotoka kwa Mungu, Ayubu, anasema pepo, alisimama mbele zake na mwili wa Ayubu ulitetemeka sana, na nywele zake zilimsimama, na Ayubu, anasema alisikia sauti ikisema maneno hayo aliyoyaeleza, na sauti hiyo ilitoka kwa yule pepo, Kwamaana hiyo Neno la Mungu linatufundisha kuwa hata pepo wachafu wanaweza kusema, na usipopapanua unaweza kuupokea ujumbe uliotoka katika pepo wachafu, Watoto wa Mungu wengi sana wamejikuta wamepokea ujumbe kutoka kwa pepo na wakaushika kwa sababu hawapimi kila neno wanalolisikia kama limetoka wapi.

Ona mfano huu utaonajinsi watu wengi wanavyopokea ujumbe au unabii uliotokana na mapepo na wakauamini na wakaushika, **"Siku moja kuna Dada mmoja alikuw amepagawa na mapepo, na kikundi cha watu waliookoka wakaenda kumfanyia huduma, walipofika pale, wakaanza huduma, walipokuwa wanalikemea pepo hilo kwa kipindi kirefu, pepo hilo likaanza kusema haliondoki kwa sababu dada huyo alikuwa ametengeneza nywele, kwa sababu hiyo haliwezi kutoka mpaka watakapo mkata hizo nywele, na hao ndugu, wakakubali, na wakamkata nywele dada huyo, baada ya kumkata nywele wakaliamuru limtoke huyo dada, likawaambia haliwezi kutoka mpaka wamvue hereni dada huyo, wakakubali wakamvua hereni dada huyo, baadaye likasema halitoki kwa sababu dada huyo ana bangili, wakamvua bangili dada huyo, na walipoendelea kukemea likawaambia sitoki, wakaliuliza mbona tumetoa vyote ulivyosema? Likawaambia sitoki."** Umeona mfano huo? Ipo mifano mingi sana ya namna watu wanavyo sikia unabii kutoka kwa mapepo, na wakaukubari, wakifili ni Mungu, ona mfano huu uliokatika maandiko matakatifu, jinsi Paulo alivyo kutana na mtu aliyekuwa na pepo ambaye alikuwa akiwatambulisha kina Paulo kuwa ni watumishi wa Mungu, **"Ikawa tulipokuwa tukienda mahali pale pa kusali, kijakazi kimoja aliyekuwa na pepo wa uaguzi akatukuta, aliyewapatia bwana zake faida nyingi kwa kuagua.akamfuata Paulo na sisi akipiga kelele, akisema, Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu Akafanya hayo siku nyingi, lakiniPulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu kristo, mtoke huyu.akamtoka saa ile ile.(MDO 16:16-18)**, Kijakazi huyo alikuwa anasema habari zinazoonekana kama za kweli, kweli kina Paulo walikuwa ni watumishi wa Mungu aliye juu, lakini fahamu, maneno hayo hayakutokana na Roho Mtakatifu, bali yalitokana na pepo aliyekuwa ndani ya huyo kijakazi, sasa kama Paulo

asingeipima hiyo roho inayoyatamka hayo maneno kama kweli imetokana na Mungu, fahamu angeisikiliza hiyo roho, na kuupokea ujumbe wake, lakini Paulo alikuwa ni mtumishi anayepima kila neno kwamba limetokana na nini, ndio maana akagundua kuwa huyo anayetoa maneno hayo ni pepo, akamkemea na kumwamuru amtoke huyo kijakazi na akamtoka, Ndugu, mpendwa unatakiwa upime kila neno utakalokuwa unalipokea, kama kweli limetoka kwa Mungu au kwa roho nyingine fahamu, Mungu anaposema tunatakiwa tuupime unabii, anajua wazi kuwa inawezekana ukasikia au kuona maono ya moyo wako, au ukasikia sauti ya mapepo, kwa hiyo unatakiwa uhakikishe au upime kila unabii, usikurupuke na kuanza kufanyia kazi jambo ambalo umelisikia.Wapo leo hii watu waliowachawi ambao wanaweza kukuambia neno ukafikiri kweli limetoka kwa Mungu, kumbe siyo, na wakaja kama malaika wa nuru, Ngoja nikupe mfano huu, ili uelewe zaidi.

“Nakumbuka siku moja nilikuwa nyumbani kwangu, na Mungu akasema nami usiku kwanjia ya maono, akanionyesha, mama mmoja ninaemfahamu, anaumwa, na akatoke mtu mmoja kama daktari kimpatia dawa, na nilipomwangalia kwa makini mtu huyo, nikaonyeshwa siyo daktari, bali ni mgaga wa kienyeji aliyejifika mavazi ya kidaktari meupe kabisa, na mama huyo ikaonekana akadanganyika, akaipokea hiyo dawa, na Bwana akaniambia mwambie mama huyo aiache kuitumia hiyo dawa, kwani mtu huyo aliyempa hiyo dawa si mtu mwema, nikaamka, na nikaelewa kuwa Bwana amenipa ujumbe maalumu kwaajiri ya mama huyo, na mama huyo alikuwa anaishi mbali kidogo na sehemu ile niliyokuwa ninaishi mimi, ni kama maili sabini, basi nikaondoka na kwenda kumwona, kweli nilipofika nilimkuta anaumwa sana, na nikamwambia jambo alilonionyesha Bwana, na lile alilioniambia Baada ya maongezi hayo mama huyo, alikubali, akasema, nikweli, kunaNdugu, mmoja ambaye pia ni muumini mwenzetu anaye mwamini Yesu kuwa ni Bwana na mwokozi, aliposikia kuwa mimi naumwa, madawa yote niliyo yatumia hayakunipatia unafuu, basi ndio maanaakaja kwangu na kuniambia kuwa zamani Bwana alimtokea na kumwonyesha mizizi Fulani na kumwa mbia aichanganye na vitu Fulani ni dawa kwa ajiri ya magonjwa mbalimbali, na akanipa nieanza kuyatumia jana, na baada ya kuyatumia hali yangu ndio imezidi kuwa mbaya, basi akanionyesha sefulia aliyokuwa anachemshia hayo madawa, na ndani yake mlikuwa na mizizi mingi sana, basi, tukayachukua hayo madawa na kuyachoma, na mama huyo, akatubu mbele za Mungu, na tukafanya maombi, na baada ya maombi, Mungu akamponya mama huyo ugonjwa uliokuwa unamsumbua, akawamzima kabisa”, baada ya huduma hiyo, nilipata ufahamu kuwa sikila mtu, atakaye kuambia Mungu amemtuma afanye jambo Fulani, ni kweli Mungu amemtuma, yatupasa tuwe makini katika suala hili ili tusije kudanganywa

NAMNA YA KUPIMA UNABII

Watu wengi wamekuwa na maswali mengi juu ya karama hii ya unabii, na moja la swali wanalojiuliza ni hili, lanamna ya kupambanua au kuupima unabii, Fahamu Mungu anatufundisha katika neno lake kuwa tunatakiwa tuupime unabii kama umetokana Mungu, na fahamu neno unabii maana yake ni neno lililotoka kwa Mungu moja kwa moja na kumjia mtu ambaye Mungu amemchagua, kwa njia mbalimbali kama tulivyo jifunza, sasa ili upate kujua kuwa neno hilo limetoka kwa Mungu kuna mambo yafuatayo unatakiwa uweunayafanya.

JAMBO LA KWANZA HAKIKI KWENYE NENO LA MUNGU

Unatakiwa uhakikishe kuwa, kila neno utakalolisikia au kuliona unalipima katika neno la Mungu yaani Biblia, Neno la Mungu linatufundisha hivi **"Wapenzi, msiiamini kila roho bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetoka na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani".(1YOHANA 4:1)** Ukiyasoma maneno hayo tunaoana kuwa Mungu anatuambia tuhakikishe tunazipima kila roho zinazotuletea unabii, kwamba zimetokana na Mungu, sasa hebu tuangalia tutazipimaje hizo roho, Ukisoma maneno ya Mungu kutoka kitabu cha (YOHANA 6:63) "**Roho ndio itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyo waambia ni roho, tena ni uzima."** Bwana Yesu anatufundisha kuwa maneno aliyotuambia ndiyo roho, kwa maana hiyo tunapoambiwa tuzipime hizo roho, anamaakuwa tulipime neno la Mungu, Fahamu, mtu atoapo unabii huwa anasema neno la Mungu, sasa ili kujua kuwa neno hili limetokana na Mungu unatakiwa uhakikishe unahakikisha katika Biblia kama kunamapatano ya neno ulilo lisikia na maneno yale yaliyomo ndani ya Biblia, fahamu Mungu hawezi kukuambia kitu ambacho kitapingana na neno lake lililomo katika Biblia, ona mfano huu mzuri.Ukiyasikiliza maneno ambayo Ayubu aliyasikia kutoka kwa pepo, **(AYUBU 4:12-19**)na ukayapima katika neno la Mungu, utagundua yako tofauti, kabisa, pepo alisema, " je! Mtu atakuwa na haki kuliko Mungu wake? Ukiyasikiliza maneno hayo kwa haraka haraka utaona kuwa mtu hawezi kuwa na haki kuliko Mungu wake, lakini hebu chunguza neno la Mungu katika Biblia linavyosema, **(RUM 3:21-26) " Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihilika pasipo sheria;inashuhuduwa na torati na manabii;ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio.maana hakuna tofauti; kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa; apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu"**

Fahamu kuwa leo hii Mungu ametupatia haki yake kamili kabisa, kupitia Yesu Kristo, na haki hiyo aliyotupatia ni haki yake iliyokamili, kwa kila mtu anayemwamini Yesu Kristo, na haki ya Mungu tuliyopewa sisi ni Yesu Kristo, hebu angalia **(1KOR 1 :30) "Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi"** Fahamu ukiwa ndani ya Yesu Kristo unayo haki ya Mungu, na pia umtakatifu kabisa, kwani Mungu Yesu Kristo aliye haki yumo ndani yako na wewe uko ndani yake, kwa hiyo unayohaki ileile ya Mungu, na fahamu haki hiyo ya Mungu haiongezeki wala haipungui, ni haki ya Mungu aliyotupatia bure, kwa hiyo tunayo haki. Sasa pepo ana weza kukunong'oneza kuwa Je! Unayo haki kuliko Mungu wewe? Jibu ni ndiyo, ninayo, kwani haki yake Mungu ametupa kupitia Bwana wetu Yesu Kristo.Kwa haraka haraka utaona hapo unabii ule aliyoletewa Ayubu katika maono ya usiku haukutokana na Mungu, kwa sababu ulitofautiana na maneno ya Mungu, fahamu hata Ayubu alikuwa na haki ya Mungu, kwani Mungu alimwesabia haki, neno la Bwana lina sema hivi, **"Kisha Bwana akamwuliza shetani, je! Umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na mwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu." (AYUBU 1:8)** Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi kuwa Mungu alimwona Ayubu kuwa ni mtu mwenye haki mbele zake, alimshuhudia mbele za shetani vizuri kwa matendo ya haki aliyokuwa anayatenda Ayubu, Kwa hiyo ndugu unatakiwa uhakikishe kila unabii unaopewa kama ni

kwenye maono ndoto, au kwanjia ya sauti, au kutoka kwa mtu yeyote yule uuhakikishe kama unapatana na neno la Mungu lililoko kwenye Biblia, ikiwa unapatana ushike, ukiwa haupatani uache.Tatizo liloko kwa watoto wa Mungu wengi la kushindwa kupambanua unabii kama ni mwema au si mwema linatokana na uvivu wa kusoma neno la Mungu, fahamu, ukiwa umejaa neno la Mungu ndani ya moyo wako, itakuwa ni rahisi sana kupambanua kila unabii, kwani akili zako zitakuwa zimezoezwa kujua lililo la Mungu na lisilo la Mungu " Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake;na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia. Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, **(maana wakati mwingi umepita), manahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu;ninyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga.lakini chakula kigumu ni cha watu wazima ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupamabanua mema na mabaya" (EBR 5:11-14)** Ili upate kupambanua unabii kama umetokana na Mungu au la, ni lazima akili zako ziwezimeshiba sana Neno la Mungu, kwani ukiwa mtoto, ni lahisi sana kusikia kila aina ya sauti ukafikili ni sauti njema, lakini ukiwa ni mtu mzima ni lahisi sana kupambanua unabii mwema na unabii wa mbaya, na ukaukataa uliombaya, na ukaushika uliomwema, Neno la Mungu ndilo linaloweza kutambua Maono ya mawazo yako au ya moyo wako, ndilo linaloweza kutambua kila roho kama imetokana na Mungu, **" Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena ili jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo, wala hakuna kiumbe kisicho kuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu"(EBR 4:12-13)** Fahamu Neno la Mungu linaweza kukupambanulia kila neno kuwa limetokana na nani, linaweza kukupambanulia kuwa unabii huu unaousikia ni wa kutunga yaani wamtu huyo anayekuambia unabii huo ni mwongo yaani unabii wa kutunga haupatani na neno la Mungu hata siku moja, pia hata ukiwa ni unabii wa moyo wako wewe mwenyewe, fahamu Neno la Mungu litakujulisha wazi kuwa unajidanganya mwenyewe, yaani maono uyaonayo ni maono yasiyo patana na neno la Mungu.

Kwa mfano, Neno la Mungu lina sema wazi kuhusu namna kila mtu aiheshimu ndoa **"Ndoa na iheshimiwe na watu wote.." (EBR 13:4)** Ikiwa utasikia unabii kutoka kwa mtu yeyote yule akisema Mungu amemtuma usimweshimu mkeo, ila umuheshimu yeye au usimweshimu mumeo ila umuheshimu yeye, au usii heshimu ndoa ya mwenzio, fahamu unabii huo unawalakini, watoto wa Mungu wengi sana leo hii wengine wanajuta kwa kudanganywa na maono ya mioyo yao wenyewe pale walipoona waume wa wenzao ndio waume zao, na wakajiachia na kutafuta kuolewa nao na kufanya kila jambo la kuwavuta hao wanaume ili wawaoe wao.na matokeo yake wakaambiwa "mbona nina mke"mwisho wa huzuni yao huwa wanamsingizia Mungu, kuwa mbona ulituonyesha Maono kama huyo ndio mume wangu, kumbe mtu huyo ameoa kwanini Mungu imekuwa hivyo? Jibu liko wazi, hukuchunguza neno linasemaje, ulijuakabisa kuwa mtu huyo kaoa, ukashindwa kuiheshimu ndoa ya huyo mtu kama Mungu alivyo agiza, kwa hiyo maono hayo hayakutokana na Mungu, Mungu hawezi kujichanganya au kutuchanganya, Kwa hiyo ndugu unatakiwa uupime unabii kwa kutumia Neno la Mungu, si kwa akili zako, bali ni kwa Neno la Mungu, si kwa macho yako, bali ni kwa Neno la Mungu, ukifanya hayo utajikuta kila mara unaishi katika furaha na ushindi mwingi, na utaipenda karama hii ya unabii, na Mungu atalijenga kanisa lake kwa uzuri sana. Anza sasa kupima unabii ili usiwe mjinga na ukawa mtumwa wa watu.

JAMBO LA PILI NI MATOKEO

Watu wengi wamekuwa na swali je! Nitajuaje neno asilolinena Bwana? Jibu la swali hili Mungu amelijibu katika neno lake akisema, **"Nawe ukisema moyoni mwako, tutajuaje neno asilolinena Bwana? Atakaponena nabii kwa jina la Bwana, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena Bwana; kwa kujikinai amelinena huyo nabii usimwogope" (KUMB 18:21-22) .** Kipimo kingine cha kuhakiki unabii kama ulitokana na Mungu, ni hicho, ikiwa umepokea unabii kutoka kwa Mtu au wewe mwenyewe katika maono ya usiku nk, Mungu akikuonyesha au kukupasha habari ya jambo litakalo tokea au atakalolifanya, na jambo hilo lisitokee, fahamu unabii huo haukutoka kwa Mungu, Unabii unaotoka kwa Mungu huwa ni lazima utokee, kwa hiyo kipimo cha kujua kuwa unabii huu umetoka kwa Mungu au haukutoka kwa Mungu ni pale jambo alilolisema huyo mtu kuwa Mungu amemtuma lisipotokea, Watu wengi huwa wasikiapo unabii huwa wanaupokea hapohapo na kuuamini, lakini siku sinapokwenda na jambo hilo halijatokea badala ya kutambua kuwa Mungu hakumtuma nabii huyo ndio kwanza wanafanya maombi Mungu alidhibitishe neno alilolisema nabii yule, fahamu, Mungu akilituma neno lake kuwa atafanya jambo fulani, fahamu, atafanya, asipolifanya, basi fahamu hakuwa Mungu, lnawezekana uliambiwa Mungu amesema mwaka huu utapakata mtoto wa kiume, na mwaka umekwisha na mtoto huna, fahamu, Mungu hakusema na huyo aliyekuambia ujumbe huo, Pia watu wengi wamepokea ujumbe mkali wakiambiwa Mungu amesema lazima wafanye jambo Fulani, wasipolifanya watakufa, na ukalikataa jambo hilo usilifanye, na usife, fahamu mtu huyo aliye lisema neno hilo ali Mungu hakumtuma, .

Neno la Mungu linatufundisha kuwa mtu yeyote yule atoaye unabii, ikiwa ni kweli Mungu alimtuma nilazima nenolile alilomtuma lifuatie, hebu ona kisa hiki, kilichotokea kati ya manabii wawili hawa wa Mungu. **(YEREMIA 28:1-9) "Ikawa, katika mwaka ule ule mwanzo wa kutawala kwake Sedekia, mfalme wa Yuda, mwaka wa nne, mwezi wa tano, Hanania, mwana wa Azuri, nabii, wa Gibeoni, akasema nami ndani ya nyumba ya Bwana, mbele ya makuhani na watu wote, akisema, Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema hivi, Nimeivunja nira ya mfalme wa Babeli.kabla haujatimia muda wa miaka miwili mizima, nitavirudisha mahali hapa vyombo vyote vya nyumba ya Bwana, ambavyo Nebukadreza, mfalme wa Babeli aliviondoa katika mahali hapa, akavichukua mpaka Babeli, nami nitamludisha hapa Yekonia, mwana wa Yehoyakimu, mfalme wa Yuda pamoja na mateka waote wa Yuda, waliokwenda Babeli, asema Bwana; maana nitaivunja nira ya mfalme wa Babeli.Ndipo nabii Yeremia akamwambia nabii Hanania, mbele ya makuhani, na mbele ya nyumba ya Bwana, naam, nabii Yeremia akasema, Amina, Bwana na atende hivi; Bwana ayatimize maneno yako uliyotabiri, kuvirudisha hapa vyombo vya nyumba ya Bwana na watu wote waliofungwa, toka Babeli, hata mahali hapa. Lakini lisikilize sasa neno hili lisemalo, masikioni mwako, na masikioni mwa watu wote, manabii waliokuwako kabla ya zamani zangu, na zamani zako, walitabiri juu ya nchi nyingi, na juu ya falme kubwa, habari ya vita, na mabaya na tauni.Nabii atabiriye habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa Bwana amemtuma kweli."**

Manabii hao wawili walikuwa ni manabii wa Bwana, ambao kila mmoja alikwenda mbele za wana wa Yuda na kutoa unabii uliotofautiana, Yeremia alitoa unabii kuwa Bwana amemtuma aseme kuwa, wana wa Yuda, watakaa utumwani huko Babeli kwa kipindi cha

miaka sabini, na Hanania yeye alikuja baadaye kusema Mungu amemtuma kusema ataivunja nira ya mfalme wa Babeli kwa kipindi kisicho zidi miaka miwili mizima baada tu ya kuchukuliwa wana wa Israeli utumwani Babeli. Sasa kukatokea ubishi hapokati ya manabii hao wawili ninani aliyetumwa kweli na Mungu, nabii Yeremia, akasema, maneno yaliyojaa hekima sana, kuwa tokea zamani nabii yeyote yule aliye toa unabii kwa jina la Bwana, alijulikana kuwa Mungu alimtuma ni baada tu ya lile alilo litabili kutokea, ikiwa halikutokea basi nabii huyo ilijulikana kuwa Mungu hakumtuma, Katika maneno hayo tunapata mafundisho mazuri sana kuwa kumbe, ikiwa mtu amekupa unabii kuwa Mungu amesema mwakani ataleta njaa kwa sababu ya maovu ya watu, na watu hao kama hawakutubu kama walivyofanya wale watu wa Ninawi, na mwaka huo ukafika na njaa isitokee kama alivuo sema huyo nabii fahamu nabii huyo hakutumwa na Mungu, Nabii Hanania ilikuja kujulikana baadaye kuwa Mungu hakumtuma kwa sababu wana wa Israeli walikaa utumwani kwa kipindi cha miaka sabini kama alivyotabiri Yeremia, pia nabii huyo Hanania alikufa kweli kama alivyotabiri Yeremia, neno la Mungu linatufundisha kuwa, Baada ya Hanania kutoa unabii ule, Mungu alimwambia Yeremia kuwa hakumtuma Hanania kusema maneno hayo aliyomsingizia Mungu kuwa amemtuma, neno la Bwna linasema hivi, **"Kisha nabii Yeremia akamwambia nabii Hanania, Sikia sasa, Ee Hanania; Bwana hakukutuma;lakini unawatumainisha watu hawa maneno ya uongo.Basi Bwana asema hivi, Tazama, nakutuma uende zako toka juu ya uso wa nchi; mwaka huu utakufa, kwa sababu umenena maneno ya uasi juu ya Bwana.Basi nabii Hanania akafa, mwaka uo huo, mwezi wa saba." (YEREMIA 28:15-17)** katika maneno hayo utaona ninani aliyetoa unabii wa kutoka kwa Mungu, na ni nabii Yeremia, kwani kila neno alilolisema kuwa Mungu amemtuma kuwa wana wa Israeli watakwenda utumani miaka sani, na kuwa nabii Hanania atakufa mwaka huu, yalitokea hayo yote.

Ndivyo ilivyo, hata leo hii wapo watumishi wa Mungu wengi wenye tabia kama ya Hanania, wanatabia ya kutaka kuwatumainisha watu, na hapo ndipo wanapotunga uongo wakisema sikiliza Bwana asema, atakubariki sana mwaka huu, lakini kumbe Bwana hakusema naye neno hilo, na wewe unatakiwa uhakikishe je!mwaka huo uliotabiriwa kubarikiwa umebarikiwa kweli?utaona watotot wa Mungu wengi sana wanautumainia uongo waliotabiriwa na hao watu wajiitao watumishi wa Mungu, watumiao akili ili wawatumainishe watoto wa Mungu kwa kuwa danganya kuwa Mungu asema atawabariki lakini baraka hizo hazionekani, ama Bwana asema mwaka huu utaolewa, lakini mwaka huo utapita ujapata hata mchumba nk, ukiona mwaka umepita na huja pewa hicho ulicho tabiriwa na huyo mtu mwenye karama ya unabii, fahamu mtu huyo Mungu hakumtuma, alisema uongo.Kwa maana hiyo tayali utakuwa umempima kuwa hakukuambia ukweli yaani haukuwa unabii uliotoka kwa Mungu. Unabii uliotoka kwa Mungu kweli ni lasima ukamilike, ona mfano huu wa unabii ambao Bwana Yesu Kristo aliutoa kabla ya kifo chake cha msalabani, **(MARKO10:32-34) "Nao walikuwako njiani huku wakipanda kwenda Yerusalemu;na Yesu alikuwa akiwatangulia, wakashangaa, nao katika kufuata wakaogopa Akawatwaa tena wale Thenashara, akaanza kuwaambia habari za mambo yatakayompata, akisema, Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalemu;na mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa mataifa, nao watamdhihaki, na kumtemea mate, na kumpiga mijeledi, na kumuua;na baada ya siku tatu atafufuka."**

Bwana Yesu alitoa unabii kuwa huko anakokwenda Yerusalemu kutatokea nini, aliwaambia kuwa atakamatwa na atateswa na kuuwawa, na siku ya tatu atafufuka, na

kweli maneno hayo yote yalitimia alipofika Yerusalemu, na kweli siku ya tatu akafufuka, hopo tunaona kuwa Kipimo cha kuwa unabii huu ulitoka kwa Mungu ni pale tunapoona lile neno lililotabiliwa limetokea,

Kwa hiyo ndugu yangu kipimo kingine cha kufahamu au kujua unabii uliotoka kwa Mungu au usiotoka kwa Mungu, tunaweza kuupima kwa kutumia njia hii, kila uliloambiwa kama litatokea, ikiwa limetokea Basi fahamu Mungu ndiye aliyesema, ikiwa halikutokea, basi fahamu Mungu hakusema usiogope. Ebu, tuangalie jambo lingine tunalotakiwa tulifanye ili tupate kupambanua unabii.

JAMBO LINGINE LA TATU NI MAOMBI

(ISAYA 45:11) " Bwana, Mtakatifu wa Israeli, na Muuumba wake asema hivi;niulize habari za mambo yatakayokuja;mambo ya wana wangu, na habari ya kazi ya mikono yangu;haya niagizeni." Baba Mungu ametuagiza sisi watoto wake tumuulize au tumuombe atujulishe habari za mambo mbalimbali, kwa hiyo hata ukitaka kujua mbele za Mungu kuhusu unabii uliotolewa na mtu yeyote yule, au unabii uliokujia wewe mwemyewe katika maono au kwa njia ya sauti, unatakiwa umwombe Mungu akujulishe, fahamu Mungu anaweza kabisa kukujulisha kama kweli amemtuma huyo mtu au kama hakumtuma huyo mtu, Fahamu Mungu ametupatia kibali sisi watoto wake cha kumwomba jambo lolote lile, na ametuahidi kuwa tukimwomba atatupa kile tumwombacho, kwa hiyo basi ili mimi na wewe tupate kuupima unabii kama umetokana na Mungu tunatakiwa tumwombe Bwana atufahamishe, tusimwekee mipaka katika kumwomba kwetu, nimemwona Mungu katika maisha yangu akinijulisha habari kuhusu, maono mablimbali ninayoyaona mimi mwenyewe, pia akinijulisha kuhusu unabii wowote ule uletwao na mtu yeyote yule kama umetoka kwa Mungu au kama haukutoka kwa Mungu.

Kwa mfano "**Siku moja nilikuwa nyumbani kwangu, na Dada mmoja alinijia na akaniambia kuwa, Mungu amemwambia kuwa, aje kwangu na kuniambia kwamba, ninatakiwa niache kazi, kwa sababu kazi hiyo ninayo ifanya ni kubwa kuliko uwezo wangu nilionao, kielimu na hata kiumri, kwani kazi hiyo ni kazi inayotakiwa waifanye watu waliona wasomina wenye umri mkubwa, sasa wewe kiumri bado ni mdogo, na kielimu pia haustahiri uifanye wewe. Basi, Bwana amenituma nikuambie uiache hiyo kazi na ukubari kuwa chini ya mtu mwingine kiofisi, "** Basi sikuutweza unabii huo ulioletwa na dada huyo ambaye kwa kweli Mungu alikuwa anamtumia sana katika karama hii ya unabii, na alikuwa anakubarika sana na hata manabii wengine walikuwa wana mheshimu sana, Basi nika mwambia sawa, nimepokea ujumbe huo, na nitaufanyia kazi. Akaondoka kwenda nyumbani kwao, basi mimi nikaenda mbele za Mungu aliye hai, nikamwomba anifahamishe kuhusu ujumbe huo kama kweli ni yeye Mungu aliyemtuma dada huyo, Unajua ni kwa nini ilinibidi nimuulize Mungu juu ya ujumbe huo?, ni kwa sababu kabla haijatokea nafasi ya kazi hiyo, Mungu alikuwa amesema nami kuwa, kuna kazi iko mbele yangu na yeye Mungu ndiye aliyeileta kazi hiyo, na anataka mimi nikaifanye, na alinionyesha mazingila ya kazi nzima itakavyo kuwa, na alinitaka nisiende kufanya kazi nyingine sehemu yeyote ile, bali niisubiri kazi hiyo aliyonionyesha, Baada ya miezi sita hivi, ikatokea shilika lile alilonionyesha Bwana likawa linafunguliwa katika nchi hii, na kwa kweli kwa Mijiza ya Mungu nika pata nafasi ya kufanya kazi kwenye shirika hilo, na nikapata neema ya ajabu sana, nikachaguliwa kuwa msimamizi wa shirika hilo katika mojawapo ya mkoa wetu, sasa nilipopokea huo unabii kutoka kwa huyo dada kuwa Mungu amemtuma, ilinibidi niludi kwake Mungu, aliyesema nami kwanza

kuhusu habari zote za kazi hiyo anayotaka niifanye, na kunionyesha wazi kuhusu mazingira mazima ya hiyo kazi, niliamua kufanya maombi ya kutaka Mungu anijulishe ukweli wa jambo hilo, ili nilishike lililojema, Na baada ya mombi yale. Bwana alinijibu kuwa sikumtuma dada huyo, nikamuuliza, mbona amesema wewe ndiye uliyemtuma? Akanijibu hivi, nitakujulisha ninani aliyemtuma, Bwana akaniambia kesho nenda kamuulize huyo dada hivi, Mungu amekuonyesha nini usiku wa leo? Basi kweli kesho yake ilipofika nikaonana na dad huyo, nika muuliza kama vile nilivyoagizwa na Bwana kuwa Usiku wa kuamkia leo Mungu amekuonyesha nii? Akanijibu kuwa, kwa kweli usiku wa kuamkia leo Mungu amenionyesha ono la kutisha sana, nikamuuliza amekuonyesha nini, akaniambia Bwana amenionyesha hivi, alikuwa amesimama sehemu na nyoka mkubwa sana, akamjia na alipomkalibia, nyoka huyo, akageuka kuwa mtu, na dada huyo akaogopa sana, na mtu huyo akamfuata huyodada na kumuuliza, je! Umeifanya kazi ile niliyokuagiza? Dada huyo akajibu ndio tayari nimeishaifanya, basi nyoka mtu huyo, akaondoka na kwenda mbele kidogo ambako kulikuwa na shamba, basi dada huyo akakimbia kwa kumuogopa nyoka huyo, na alipokuwa anakimbia akakutana na kijana mmoja aitwae Gabrieli, akamwambia kuwa anamwogopa huyo nyoka, na yule kijana akamjibu usimwogope huyo nyoka, bali unatakiwa umuue huyo nyoka, na dada huyo akasema yeye hawezi kumuua huyo nyoka, basi Gabrieli akaenda kumuua huyo nyoka, na akaludi akampasha habari kuwa asiogope kwani yule nyoka tayari ameisha kufa, na baada ya maono hayo akaamka toka usingizini.

Mimi nikamuuliza kuwa, unafiri nini maana ya maono hayo?akasema sijui, basi, nikamuuliza umefanya kazi gani ambayo unahisi shetani alikupa? Akasema sijui, nikamwambia niambie ukweli, ninani alikutuma uje jana kuniambia kuwa Mungu anataka mimi niache kazi? Akasema, kweli naomba unisamehe, Sio Mungu aliyenituma, bali ni Fulani ndiye aliye nituma, aliambia kuwa yeye aliogopa kuja kuniambia, na akasema Mungu amemwambia kuwa aje kwangu (kwa huyo dada) kwani ndiye anaefaa kutoa ujumbe huo kwa sababu ni mtumishi ambaye anaweza kusikilizwa, basi nikamwambia ukweli huyo dada kuwa Mungu aliniambia kuwa hakumtuma ila kunamtu aliyemtuma na Mungu atanijulisha ninani, na jinsi Mungu aliyo niambia kuwa nije ni Muulize ono ambalo Mungu amemwonyesha usiku, Huyo dada aliogopa sana, akalia na kuomba msamaha mbele za Mungu kwa kufanya kazi ya shetani pasipo kujua, na mtu huyo aliyemtuma alikuwa ni mfanyakazi mwenzangu tena ni mtu aliyesemaameokoka, na aliyekuwa anaelimu kubwa kuliko mimi na umri mkubwa kuliko mimi, kwa kweli nilishangaa sana kusikia habari hiyo.

Basi nikaondoka na kwenda Mbele za Mungu na kumshukuru kwa kunijulisha huyo mtu aliyemtuma dada huyo, na ndipo nilipo pata somo zuri kuwa, ukimwomba Mungu akupambanulie au akujulishe kuhusu unabii wowote ule umetoka wapi, kama ni kwa Mungu au ni kwa mtu ama kwa shetani, Mungu yuko tayari kutujulisha, na fahamu nisingeupima unabii huo kwa njia ya maombi, yamkini ningelikuwa niukubari na kuacha kazi ambayo Mungu amenipa, kwa hiyo ndugu yangu upatapo unabii kabla haujaanza kuutendea kazi unatakiwa uupime kwa njia ya maombi, Mungu atakujulisha kila kitu. Fahamu kuna baadhi ya watumishi wa Mungu wamejikuta wakimsingizia Mungu kuwa amewatuma waseme jambo Fulani kumbe si Mungu aliye watuma, bali ni watu waliomtuma, labda ni viogozi wake, au niyeye mwenyewe kwa kutafuta kuheshimiwa na kuonekana mbele za watu anaamua kusema Mungu asema hivi, wakati Mungu hakusema, na ikiwa wewe hupimi unabii huo kwa kuufanyia maombi, unaweza kudanganyika kabisa

na ukapotea katika njia ambayo Bwana anataka uipite, anza kuupima unabii wowote ule kwa maombi maalumu mbele za Mungu, na Mungu atakujulisha kilakitu.

Basi ndugu mpendwa ukiwa unahitaji kuubima unabii unatakiwa uyafanye mambo hayo matatu, ukiupima unabii katika sehemu hizo tatu fahamu Mungu atakujulisha kuwa unabii huo umetokea wapi, katika hatua hizo tatu lazima hatua mojawapo Mungu ataitumia kukudhibitishia neno lake, au kukutaadharisha na neno hilo ulilo lisikia kuwa limetoka kwa mwanadamu, au kwa shetani, ebu, anza kufanya hivyo kuanzia sasa, pima unabii kama Mungu anavyo tuambia kuwa **" msiitweze unabii;jaribuni mambo yote;lishikeni lililo jema" (1THE 5:20-21).** Usiogope kukataa jambo lolote utakalo akikishiwa kuwa si la Mungu, pia usisite kulishika jambo lolote utakalo akikishiwa kuwa limetoka kwa Mungu, hapo ndipo maisha yako ya wokovu au ya kiutumishi yatakapo fanikiwa sana.Mungu akusaidie katika kuyafanya mambo hayo.

NAMNA YA KUUWAKILISHA UNABII

Kama kuna jambo la msingi sana ambalo kila mwana wa Mungu ambaye amepewa karama hii ya unabii anapaswa alijue ni namna anavyo paswa kuutoa unabii aliopewa na Bwana kwa kanisa la Mungu au kwa mtu binafsi, Watu wengi kwa kushindwa kuuwakilisha vema unabii toka kwa Mungu wamejikuta wakikataliwa na kupingwa hata kutengwa na jamii, kwa sababu ya kutoliwakilisha neno la Mungu vema kwa wahusika, Fahamu ni kweli Bwana Yesu alisema kuwa **" Akasema, Amini, nawaambia ya kwamba, Hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe" (LUKA 4: 24)** ni kweli Bwana Yesu alisema wazi kuwa nabii hapati kukubaliwa katika nchi yake au sehemu anayoishi kwa urahisi, Na kwa neno hilo watumishi wa Mungu wengi walio na karama ya unabii wanapo kataliwa au kutokukubaliwa watoapo unabii waliopewa na Bwana, huwa wanasema Bwana alisema kuwa tutakataliwa, lakini fahamu, inawezekana kabisa ukikosea kuuwakilisha vema unabii uliopewa na Bwana unabii huo hata kama ni wa kweli, walengwa hawata upokea kabisa, watakuona wewe ni mwongo.

Fahamu ndugu yangu kabla ya kuutoa unabii, unatakiwa umwombe Mungu akupe hekima ya namna utakavyo uwakilisha unabii huo kwa watu au kwa mtu yeyote yule, Watu wengi wamejikuta wakiumizwa vibaya katika nafsi zao baada ya kuuwakilisha unabii waliopewa na Mungu kwa watu au kwa kanisa la Mungu, si kwa sababu unabii walioutoa ulikuwa ni wa uongo, bali ni kwa sababu ya kukosa hekima ya namna ya kuuwakilisha tu, Ebu, Mfano huu wa jinsi nabii Nathani alivyo uwakilisha unabii aliopewa na Bwana mbele ya mfalme Daudi, neno la Bwana linasema hivi, **"Ndipo Bwana akamtuma Nathani aende kwa Daudi. Naye akamwendea, akamwambia, Palikuwa na watu wawili katika mji mmoja; mmoja wao alikuwa tajiri, na wapili maskini. Yule tajiri alikuwa na kondoo na ng'ombe wengi sana;bali yule maskini hakuwa na kitu, ila mwana kondoo mmoja, mdogo, ambaye amemnunua na kumlea;naye akakua pamoja naye, na pamoja na wanawe;hula sehemu ya posho lake, na kukinywea kikombe chake, na kulala kifuani mwake akawa kwake kama binti. Hata msafiri mmoja akamfikilia yule tajiri, naye akaacha kutwaa mmoja wa kondoo zake mwenyewe au mmoja wa ng'ombe zake mwenyewe, ili kumwandalia yule msafiri aliye mfikilia, bali akamyang'anya yule maskini mwana- kondoo wake, akamwandalia yula aliyemfilia.Ndipo hasira ya Daudi okawaka sana juu ya mtu yule; akamwambia Nathani, aishivyo Bwana, mtu huyo aliye tenda jambao hili, hakika yake astahili kufa; naye atamrudishia yule mwana –kondoo mara nne, kwa sababu ametenda**

neno hili, na kwa sababu hakuwa na huruma. Basi Nathani akamwmbia Daudi, Wewe ndiwe mtu huyo. Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Nalikutia mafuta, uwe mfalme juu ya Israeli, nikakuokoa na mkono wa Sauli; nami nikakupa nyumba ya Bwana wako, na wake wa bwana wako kifuani mwako;nikakupa nyumba ya Israeli na ya Yuda;na kama hayo yangalikuwa machache, ningalikuongezea mambo kadha wa kadha. Kwa nini umelidharau neno la Bwana, na kufanya yaliyo mabaya machoni pake?umempiga Uria, Mhiti, kwa upanga nawe umemtwaa mkewe awe mke nawe umemuua huyo kwa upanga wa wana wa Amoni" (2SAMWELI 12:1-9); Ukiangalia kisa hiki kizima, utaona hapo yakuwa nabii Nathani kama asingelikuwa na hekima ya namna ya kuuwakilisha ujumbe aliopewa na Bwana Mungu ili ampelekee mfalme Daudi, sidhani kama ujumbe huo ungelipokelewa na hata yeye kuwa salama. Fahamu Mungu alimpatia Nathani hekima itakayo msaidia kuuwakilisha vema ujumbe aliompa kwa mfalme Daudi, kama Nathani angelikwenda hovyo hovyo kwa mfalme na kuanza kumwambia tena kwa kumfokea kuwa " Daudi wewe umemuua Uria na umemjukua mkewake na Mungu amesema utakufa", unafikiri nabii Nathani angelifanya hivyo kungelitokea nini? Nionavyo mimi Mfalme Daudi angelikasirika sana na wala asingelitubu, pia nionavyo mimi mfalme Daudi angeliamuru Nathani auawe haraka sana, Fahamu, ikiwa wewe umepewa karama hii ya unabii, unatakiwa uhakikishe uwakilishaji wako wa ujumbe wowote toka kwa Bwana unauwakilisha kwa hekima na maarifa toka mbinguni, ukienda kichwa kichwa, ujumbe wako utakataliwa na uhuduma yako itakuwa hatarini, Nathanieli, alianza kuuwakilisha ujumbe huo aliopewa na Bwana kwa kumletea Daudi fumbo, ambalo Daudi yeye mwenyewe akalifumbua, na likambana yeye mwenyewe, ndipo kwa upole na unyenyekevu mkubwa Nathani akamwambia Daudi mambo yote, na matokeo yake mfalme Daudi akasema hivi, **"Daudi akamwambia Nathani, Nimemfanyia Bwana dhambi. Nathani akamwambia Daudi, Bwana naye ameiondoa dhambi yako, hutakufa." (2SAMWELI 12:13);** Hayo ndiyo matokeo mazuri ambayo huduma ya kinabii inatakiwa iyapate, na yatapatikana tu iwapo mtumishi wa Mungu aliyepewa neno la kinabii akiliwakilisha vema kwa hekima na unyenyekevu.

Nimewaona watu wengi waliona karama hii ya kinabii, wakiingia katika matatizo makubwa sana baada ya wao kuuwakilisha ujumbe waliopewa bila hekima, ona mifano hii ambayo watu wengi walio na karama hii ya kinabii wamejikuta wakiwa katika wakati mgumu baada ya kuuwakilisha ujumbe wa Mungu pasipo hekima, mfano, **"leo hii Mungu kakuambia habari zinazo muhusu kiongozi wako Fulani, labda ni mchungaji, au kiongozi wa faragha, au askofu wako au mtu yeyote yule, kwamba amechukua mke wa mtu, na amemfanya kimada wake, na Mungu anasema nenda ukamuonye aiache tabia hiyo mbaya, la asipo iacha tabia hiyo atakufa, halafu wewe, unakwenda nyumbani kwake, na unamwita yeye na mke wake, na watoto wake, na jamaa zake walionyumbani mwake, na bila unyenyekevu, unaanza kumwambia kuwa Mungu amenituma nije nikuonye kuwa wewe ni mzinzi, unazini na Mungu amesema hakika utakufa, na baada ya kuutoa ujumbe huo, ukaanza kumwambia piga magoti sasa hivi utubu, na nikuongoze sala ya toba, ukikataa mimi naenda kumwa mbia Mungu kuwa umekataa, "** Unafikiri mtu huyo atapiga magoti? Fahamu hata piga magoti wala hatakukubalia kuwa kweli Mungu amekutuma atakuambia wewe ni mwongo, unaye taka kwanza, kuivunja ndoa yake, pia ata sema umekuja kwake ili udhalilishe, na kitakacho tokea ni kesi, ambayo naamini itakushinda na inawezekana ukakabiliwa na kutengwa, au kulipa faini, kwanini unajua? Ni kwa sababu hukwenda kwa hekima mbele za huyo mtu, kitendo cha kumwita yeye mbele za mke wake na watoto wake na hao jamaa zake, si kitendo cha hekima, na kwa kitendo hicho tayari utakuwa umempa ibirisi nafasi ya

kumfanya ndugu huyo awe na moyo mgumu, asikubali kutubu, hatakama kweli amefanya kitendo hicho, na anakijutia, hatataka kukuonyesha kabisa kuwa wewe ni mkweli, lazima ujue namna utakavyo kaanaye, nafahamu lazima ujue kuwa Mungu kakupa ujumbe huo kwa ajiri ya huyo ndugu tu, si wakifamilia, kwa hiyo unatakiwa ukaenae yeyetu, wala mtu mwingine asisikie, labda yeye aanze kuwaambia hao ndugu zake, Watumishi wengi wa Mungu waliopewa karama hii huwa wanakosea kuiwakilisha vema kwa sababu ya kukosa hekima, **Ona mfano mwingine, Inawezekana kabisa ukawa ni binti uliye na karama hii, na Mungu kakupa ujumbe wa kuwapelekea vingozi wako, ambao ni sawa na baba zako kiumri, na ukawaendea kwa kiburi, na kwa kuongea nao kwa sauti ya juu, tena kwa ukali, sana, kuwa Mungu kakutuma uwaambie neno hilo, fahamu hata kama ujumbe huo ulikuwa kweli umeupata kwa Mungu, viongozi wako hao hawataupokea kwa sababu ya wewe kukosa heshima mbele yao**, Paulo alilifahamu jambo hilo, ndio maana alimwagiza Timotheo kuwa, **"Mzee usimkemee, bali umwonye kama baba; na vijana kama ndugu; wanawake wazee kama mama; wanawake vijana kama ndugu wa kike; katika usafi wote." (1TIMOTHEO 5: 1-2)**, Fahamu ukiwa kinyume cha maagizo hayo, huwezi kuwaonya watu na wakaonyeka, kila siku utawaona kama ni watu wenye kiburi wasiotmtii Mungu, kumbe tatizo si kwa hao watu bali ni la kwako wewe, Watu wengi wameukataa unabii si kwa sababu ya kiburi chao, bali ni kwa sababu ya mtu aliyepewa dhamana ya kuupeleka huo unabii kwa wau, ona mfano huu mwingine mzuri na wa kueleweka, **" Mungu amesema na wewe, na kakuonyesha na kakutuma ukamuonye nduguyo wakiroho, au mtu yeyote yule ayaache mabaya Fulani au kakupa neno la maarifa lililo kuja kwa njia yakinabii, na wewe usimpelekee huyo mtu ujumbe huo mapema, ukawaambia watu wengine na habari hizo zikavuja na kumfikia mlengwa, halafu ukaenda kumpelekea ujumbe hup kuwa Mungu asema hivi, unafikili mtu huyo ataupokea ujumbe huo, ataukataa, na atakuambia kuwa mbona nimeanza kusisikia habari hizi kwa watu wengine, naona hata wewe umezisikia kwa watu wengine na ukanijia na kumsingizia Mungu kuwa kakutuma wewe, sikweli kuwa Mungu kakutuma ila habari hizi umezisikia mitaani ondoka hapa"** Fahamu mtu huyo atakuwa ameukataa ujumbe huo ni kwa sababu ya mwakilishi aliyepewa ujumbe huo kutokuwa na hekima, kauvujisha ujumbe wa Mungu, na matokeo yake ni kukataliwa, Basi ndugu yangu iliuwakilishi wako uwe mzuri unatakiwa uhakikishe unamwomba Mungu kila mara akupe hekima yake. Na ukitaka upate hekima toka kwa Bwana ni lazima uwe msomaji wa Biblia sana, neno lina sema **(MITHARI 2:6) "Kwa kuwa Bwana huwapa watu hekima;kinywani mwake hutoa maarifa na ufahamu"**

Fahamu hekima hutoka katika kinywa cha Bwana, kwa maana nyingine nzuri hekima hutopatikana katika neno la Bwana, sasa neno la Bwana tunaweza kulipata katika neno lililoko katika Biblia, au kwa kulisikia kutoka kwa watumishi wake, waalimu, manabii, nk. Ikiwa unahitaji hekima basi weak bidii katika kulisikia neno la Bwana kwa kujiwekea utaratibu mzuri wa kusoma maandiko matakatifu, pia usisite kusoma vitabu mbalimbali vilivyoandikwa na watumishi wa Mungu, pia unatakiwa uweke bidii katika kusikiliza kanda za mafundisho ya neno la Bwana, nk, Mungu akusaidie sana ndugu yangu mpendwa. Katika sehemu hii ya kwanza naamini ndugu kuna kitu Mungu amekufundisha Mungu akujarie ndugu kuyatendeakazi haya aliyokufundisha, pia Taka kwa Mungu hizo karama zilizo kuu, neno la Bwana linasema **"Ufuateni Upendo na kutaka sana karama za rohoni..." (1KOR 14:1)** Takaleo karama hizo za Aina za Lugha, Tafsiri za Lugha, na Unabii, Taka sana Mungu atakakupa, akikupa chochea karama utakayopewa kwa maombi na kuitendea kazi bila hofu.Amani ya Bwana Yesu iwe na wewe Amen.

Ukitaka maombi au ushauri wa kiroho pia masomo mbalimbali basi wasiliana nasi kwa anwani hii.

Mr Steven & Mrs Bett Steven Mwakatwila
P.O.Box 3613
Mbeya
Simu 0756 849924
0756715222
E-Mail: stevenmwakatwila@yahoo.com